# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Sita – Tarehe 12 Aprili, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Kwa siku ya leo swali la kwanza linaelekezwa kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI na linaulizwa na Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Mwakang'ata.

Na. 45

**Posho kwa ajili ya Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Serikali inatambua uwepo wa Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji ambao wanatekeleza majukumu yao moja kwa moja na wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa posho viongozi hao kama inavyofanya kwa Madiwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia kila Halmashauri imeweka utaratibu wa kuwalipa posho Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani ya Halmashauri. Katika makusanyo ya mapato kupitia vyanzo vya ndani kila Halmashauri hupeleka asilimia 20 kwenye vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa fedha hizo ni kwamba 3% hutumika kwa ajili ya maendeleo na 17% hutumika kwa ajili ya utawala ikiwemo kuwalipa posho za Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa. Viwango vya kulipa posho hizo hutofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine kulingana na makusanyo ya mapato ya ndani katika vyanzo vilivyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha usimamizi na upatikanaji wa fedha hizo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imependekeza kulifanya suala la asilimia 20 kuwa la kisheria katika marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Maandalizi ya sheria hii yako katika hatua za mwisho na Muswada huo utawasilishwa na kujadiliwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mwakang'ata.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, sote tunajua kazi za Wenyeviti, wamekuwa wanafanya kazi nzuri sana katika mitaa na vijiji vyetu, lakini hakuna hata siku moja wamelipwa posho. Nataka Serikali iniambie leo ni lini itapanga kiwango cha kuwalipa Wenyeviti hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Wenyeviti hawa wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana, wakati huo hawa ndio wasimamizi namba moja wa usalama katika vijiji na vitongoji vyetu, wanatatua migogoro kila siku, watoto wa mitaani wakipotea, wanapelekwa kwenye Wenyeviti, tukigombana usiku *break* ya kwanza kwa Wenyeviti, sote tunajua kazi za Wenyeviti. Je, Serikali ipo tayari kuwapa hata usafiri angalau baiskeli za kuwasaidia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Bupe, Wenyeviti wetu wanafanya kazi kubwa sana katika vijiji, hili jambo halipingiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema lini? Naomba nizungumze wazi, kwa sababu tulikuwa na changamoto kubwa hapa nyuma, hata ukija kuangalia Halmashauri zetu, hata kupeleka zile fedha, Halmashauri nyingine ilikuwa inaonekana kama ni hisani. Ndiyo maana sasa hivi tunafanya haya marekebisho na muswada huu utaingia Bungeni wakati wowote. Hivi sasa umeshaiva na wadau wameshiriki vya kutosha. Katika Sura ya 290 kifungu cha 54 kinafanyiwa marekebisho na Waziri mwenye dhamana sasa atapewa utaratibu wa kuweka kama misingi ya kisheria, kuzielekeza Halmashauri sasa kupeleka zile fedha. Mwisho wa siku ni kwamba aidha, Halmshauri wataweza kupata hasa Wenyeviti wetu wa vijiji ambao tunatambua kwamba wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la usafiri, ni kweli kama nilivyosema ni kwamba utakuta sehemu nyingine Mwenyekiti wa Kijiji anatoka kitongoji kimoja anakwenda kitongoji kingine, changamoto yake ni kubwa. Vilevile kwa sababu kama tutaweka utaratibu mzuri wa kisheria na hata ukiangalia sheria, sehemu inayozungumza mambo ya *expenditure* pale, inazungumza kama kuna matumizi ya

fedha nyingine zinazoweza kutumika kwa maslahi mapana ya kujenga eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu huo tukishafanikiwa vizuri, basi tutatoa maelekezo ya kutosha kuona jinsi gani tutafanya, tutaangalia na rasilimali fedha zilizopatikana angalau kama itawezekana baadhi ya vipando hasa baiskeli, lakini maelekezo hayo yatakuja baada ya kurekebisha sheria yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge jambo, lako ni la msingi na Serikali tunalifanyia kazi kama nilivyozungumza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chegeni na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Paresso.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Halmashauri nyingi zina mapato kidogo na kwa vile baadhi ya vyanzo vya mapato Serikali Kuu imevichukua, kwa hiyo, ina maana kwamba baadhi ya Halmashauri hazitaweza kulipa Wenyeviti kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Waziri alivyosema hapa. *(Makofi)*

Je, Serikali ina mpango gani mbadala kuhakikisha kwamba Wenyeviti wote, *regardless* wanatoka kwenye Halmashauri ipi na wenyewe waweze kupata malipo kama haya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna wakati mwingine marejesho yanakuwa siyo rafiki sana, ndiyo maana katika utaratibu wa sasa inawezekana Wabunge wengine watauliza kwamba *property tax* imechukuliwa imeenda Serikali Kuu, tunafanyaje na haijaridi? Hili hata Waziri wa Fedha baadaye akija ku-*table* bajeti yake hapa katika

mjadala mpana baadaye, itaonekana ni jinsi gani tutafanya. Lengo letu ni kuziwezesha Halmashauri zetu cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu changamoto hii hata Waheshimiwa Wabunge wengine wanaweza wakasimama baadaye wakasema hata Madiwani wengine wamekopeshwa kwenye mabenki, wanataka kupelekewa mahakamani, ndiyo maana nasema katika mchakato huu mpana, mara baada ya kurekebisha sheria, kwa sababu sheria ile itakuja hapa mtaona kwamba Waziri mwenye dhamana atakuwa anapata fursa ya kuhakikisha Halmashauri zinaenda vizuri, kwa sababu zimewekwa kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 145 na utelekezaji wake Ibara ya 146.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waziri mwenye dhamana amepewa mamlaka hiyo kwa utaratibu wa sheria za nchi Sura namba 287 na 288 ile ya vijijini na ile ya miji. Kwa hiyo, katika kurekebisha Sheria ya Fedha, itamsaidia sana Waziri mwenye dhamana kufanya maamuzi hayo mwisho wa siku kwa kuangalia jiografia ya Halmashauri hizi ambapo zenyewe zinatofautiana katika nguvu ya kimapato. Halmashauri ya Ilala huwezi ukafananisha na Halmashauri ya Kakonko kwa mwalimu wangu pale, hizi zinatofautiana.

Kwa hiyo, Waziri mwenye dhamana atakuwa anapata nafasi nzuri kuiangalia nchi kwa upana wake na kuangalia hizi Halmashauri, Madiwani na Wenyeviti ili kazi iende vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha Madiwani nchini kutokupata nyongeza ya posho kwa muda mrefu. Ni ukweli usiopingika kwamba Madiwani hawa wamekuwa wakifanya kazi kubwa hasa kutusaidia sisi Wabunge tukiwa huku Bungeni muda mrefu,

lakini Madiwani hawa wamekuwa wanasimamia fedha nyingi sana zinazopelekwa katika Halmashauri zetu, lakini wameachwa hawana mafunzo, hawana vitendea kazi na posho zao haziongezeki.

Je, Serikali sasa iko tayari kumaliza kilio cha Madiwani cha muda mrefu katika nchi hii?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Paresso na tukifanya *reference* ya mwaka 2002 kulikuwa na Tume iliyokuwa inaitwa Tume ya Lubeleje ambaye ni Mbunge *senior* yuko hapa. Tume hiyo iliundwa na iliweza kubaini mambo hayo. Bahati nzuri katika mikitano yetu ya *ALART* miwili tuliyofanyia hapa Dodoma na Musoma, jambo hilo vilevile lilijitokeza. Serikali hivi hatuwezi kutoa kauli hapa haraka haraka kwa sababu mchakato huu wa bajeti tutakuja ku-*table* bajeti na mambo mengine tutajadili kwa pamoja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kazi ya Madiwani ni kubwa na Serikali inaona hilo, lakini tutajadiliana kwa upana katika mchakato wa bajeti tuone ni nini tunafanya, *way forward* katika suala zima la Madiwani wetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo ni namba 46, linaulizwa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini.

Na. 46

**Kuifanya Haydom kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Wananchi wa Mji wa Haydom wamekuwa wakiomba Haydom iwe Mamlaka ya Mji Mdogo.

Je, ni lini Serikali itaupa Mji wa Haydom hadhi hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya kuwa na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Haydom yamejadiliwa katika vikao vya awali vya Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira tarehe 25/09/2012, Baraza la Madiwani katika kikao cha tarehe 19/10/2012 na Kamati ya Huduma za Uchumi katika kikao cha tarehe 13/06/2014. Kimsingi, vikao vyote hivyo vimekubaliana na wazo la kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Haydom.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri mapendekezo hayo sasa yawasilishwe katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC)* na Mkoa *(RCC)* ili hatimaye yawasilishwe kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kupata kibali. Hivyo, taratibu hizo zikikamilika na kuonekana mamlaka hiyo imekidhi vigezo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, haitasita kuanzisha mamlaka hiyo kisheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumeleta maombi haya muda mrefu; na vikao hivi vimekaa muda mrefu; na tuna miji miwili ya Dongobesh na Haydom; na kwa kuwa muda umepita, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kutuma wataalamu wake kutoka TAMISEMI ili kushirikiana na wataalamu walioko Wilayani kusaidia vigezo hivi kutimia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri yuko tayari, je, ni lini sasa atawatuma wataalamu hawa ili kiu ya wananchi wa Mbulu Vijijini itimie?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama nilivyosema pale, kwanza elekezo langu ni kwamba naomba niwasihi ndugu zetu wa Mbulu kwamba kwa sababu kazi kubwa na Mbunge umekuwa ukipigania jambo hili sana kwa wakati wote kwamba zile taarifa zipite katika vikao vile vya kisheria sasa zije huku kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwatuma hili jambo, siyo tatizo kubwa sana, kwa sababu hata Mheshimiwa Flatei kama atakumbuka, kuna *team* mara ya kwanza ilikuja kule kwa maombi yake vilevile na taarifa tunazo kuhusu Mji huu wa Haydom.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Mbunge amesema na suala zima la Mji wa Dogobesh. Kama nilivyosema mwanzo ni kwamba hata Mji wa Dogobesh wakati unataka upandishwe, lazima taratibu hizi za kisheria ziweze kufuatwa ambapo mamlaka haya kuanzishwa kwake, yanatuletea utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Flatei naomba nikutoe hofu kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI, cha kufanya ni kwamba tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo kukupa ushirikiano wote. Ninachokiomba ni kwamba vile vikao vya kisheria viweze kutimiza wajibu wake, tukipata taarifa hizo katika ofisi yetu, nitakupa ushirikiano wote kuhakikisha Halmashauri yako katika maeneo yako ya Mamlaka Mji Mdogo, basi yaweze kupitiwa na kuweza kupewa hadhi kama tulivyozungumza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya, swali moja la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa matatizo yaliyoko huko Mbulu yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo Itigi katika Jimbo la Manyoni Magharibi, ni kwamba Itigi ni eneo kubwa sana, lipo katika Wilaya ya Manyoni. Kutoka mwanzo wa Tarafa ya Itigi hadi mwisho kuna zaidi ya kilometa 200 na ni Tarafa moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuigawa Tarafa hii ya Itigi kuwa Tarafa nyingi kwa sababu ya eneo na jiografia ni eneo kubwa sana?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi tu, uko tayari kuigawa? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuko tayari, lakini kwanza lazima mchakato huu uanze katika suala zima la vijiji, itakuja katika vikao vya *Ward Council,* vitakuja katika vikao vya *full council*, vitakuja *DCC*, *RCC* vitafika kwetu, *then* Waziri mwenye dhamana, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 287 kifungu cha 10 ambacho kinafanya *variation* ya haya maeneo, atachukua jukumu hilo la kufanya hivyo.

Kwa hiyo, ndugu yangu wa Itigi wala usiwe na hofu katika hilo, anzeni mchakato, sisi Serikali tuko kwa ajili ya kutekeleza hayo ambayo mtayafanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nampongeza ndugu yangu Naibu Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya na hasa ya kushughulikia matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tatizo la kule Mbulu hasa kule Haydom, inalingana kabisa na Korogwe Vijijini katika Mji Mdogo wa Hale na wewe mwenyewe umeshafika

pale; je, Serikali Serikali ina mpango gani wa kupandisha hadhi Kijiji cha Hale kuwa Mji mdogo kule Korogwe Vijijini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuliweza kufika pale kwa sababu walikuwa na *concern* ya Mji wa Mombo. Hayo yote, hata timu yetu tuliituma, waliweza kufika kule na kufanya *assessment* na wataalamu wameshafanya jukumu lao, iko katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI sasa inafanyiwa kazi. Kwa hiyo, mchakato ukikamilika, basi mtapata mrejesho nini kimepatikana katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea. Swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 47

**Mradi wa Upandaji Miti Kwenye Maeneo Makame Mkalama**

**MHE. ALLAN J. KIULA** aliuliza:-

Baadhi ya maeneo ya Halmashauri ya Mkalama ni kame sana.

Je, Serikali ipo tayari kusaidia mradi wa upandaji miti katika maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali hilo litajibiwa na Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Namwona Naibu Waziri, Mheshimiwa Mpina.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau wengine ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Mkakati wa Taifa wa Miaka Mitano wa Kupanda Miti (2016/2017 hadi 2020/2021). Kiasi cha shilingi bilioni 105 zinahitajika ambapo kila mwaka imependekezwa zitengwe shilingi bilioni 20 kutoka vyanzo mbalimbali vya Serikali na wadau wa maendeleo kwa ajili ya kutekeleza mkakati huu ambao unaelekeza kila mwananchi, taasisi za Serikali, taasisi za madhehebu, asasi zisizokuwa za kiserikali, kambi za majeshi, magereza, shule, makampuni na kadhalika kupanda na kutunza miti katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na miaka mingine iliyopita, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini, itahakikisha kwamba miti inayopandwa inatunzwa na kukua. Aidha, visababishi vinavyochangia miti kutokuwa vimeainishwa na mikakati ya kudhibiti imeandaliwa ikiwa ni pamoja na upandaji wa aina ya miti kulingana na maeneo na utunzaji wa miti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Allan Joseph Kiula kuwa Serikali imekuwa ikitekeleza zoezi la upandaji miti kote nchini kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Wakala wa Misitu Tanzania na Halmashauri zote ikiwemo Halmashauri ya Mkalama ambapo kila Halmashauri inatakiwa kupanda miti 1,500,000 kila mwaka na kuhakikisha inatunzwa.

Aidha, pale itakapoonekana inafaa, Halmashauri zihakikishe maeneo ya wazi yanahifadhiwa ili kuruhusu uoto

wa asili ulegee au kutumia mbinu zijulikanazo kama kisiki hai ambapo visiki vilivyo hai hutunzwa hadi kuwa miti mikubwa. Iwapo Mheshimiwa Mbunge ana maombi mahususi awasilishe Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushauri na hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itasimamia utekelezaji wa mkakati wa taifa wa kupanda na kutunza miti na kuendeleza kuhimiza utekelezaji wa kampeni za upandaji miti na mikakati mingine inayolenga kupanda na kutunza miti nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri yalitolewa na Naibu Waziri, lakini ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Ulansoni, Nyalelembo Mkalama ambayo yanazalisha sana chakula, yameathirika sana na mmomonyoko wa ardhi. Je, Serikali ipo tayari kupeleka wataalamu kutoka Wizarani na kutoa ushauri namna ya kudhibiti hali hayo kupitia program maalum ya upandaji miti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa tupo katika mkakati wa upandaji miti kama ilivyoelezwa na Wilaya ya Mkalama imeathiriwa na ukame, kutokana na kutokuwa na miti na mvua kutokunyesha, maeneo kama ya Mwangeza, Ibada na Mpambala yatapata uhaba mkubwa wa chakula.

Je, Serikali iko tayari kuwasaidia wananchi hao ambao baadhi yao leo wamefika Bungeni kuweza kufuatilia suala hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza la nyongeza ambalo anaomba kupeleka wataalamu katika maeneo hayo, namhakikishia

kwamba kama Mheshimiwa alivyoomba, tutapeleka wataalam waliobobea katika mazingira, wataalam waliobobea katika masuala ya misitu kwa maana ya waliopo ofisi yetu na wengine walioko Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la kusema kuwasaidia kuhusu suala zima ambalo linajitokeza sasa hivi la mmomonyoko mkubwa wa udongo, lakini ukame kutokana na miti imekatwa na uharibifu wa mazingira, hilo kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi, kama kuna ombi mahususi, basi atuletee tutalishughulikia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ni suala mtambuka na watu wote wanahitajika kulinda mazingira. Juzi au jana nafikiri, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alitoa taarifa kwamba ni marufuku kuanzia Julai kusafirisha mkaa kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine, lakini tukumbuke kwamba miti ni nishati ambayo inatumika na watu wote, hasa mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni je, si muda muafaka sasa kwa Serikali kutoa ruzuku au tuseme ku-*subsidize* gesi asilia kusudi watu wengi waweze kutumia gesi badala ya kutumia nishati ya mkaa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mollel, ambaye kwa kweli ndiye alikuwa Katibu Mkuu wa Ofisi hii ya Makamu wa Rais katika miaka ya nyuma iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba sasa ni muda muafaka kwa Serikali kutoa ruzuku, ndivyo tunavyofanya na ndiyo maana mnaona mambo mengi ambayo tunayafanya sasa hivi ni kuhakikisha kwamba gesi hii asilia pamoja na gesi *imported* zinakuwa na bei ambayo wananchi wanaweza ku-*afford* pamoja na jitihada nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoweza kusema tu kwamba, ni muda muafaka sasa wa Serikali kuendelea. Kwa hiyo, tutaendelea hivyo. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuhakikisha tunafanya bidii kadiri inavyowezekana. Kwanza kuhakikisha kwamba, gesi asilia inasambaa nchini, lakini vilevile kuhakikisha kwamba, *imported gas* inauzwa kwa bei nafuu ili wananchi wengi waweze kuitumia, waweze kuachana na nishati ambayo inapelekea uharibifu mkubwa wa mazingira kwa maana ya ukataji wa miti hovyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 48

**Wawekezaji Kuanzisha Viwanda vya Alizeti - Singida**

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE** aliuliza:-

Alizeti ndiyo zao kubwa la biashara na limekuwa kimbilio kubwa kwa maisha ya wananchi wa Mkoa wa Singida. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Singida ilipatiwa mashine ndogo tisa za kukamulia alizeti ambazo hazikidhi matarajio ya wakulima katika kujikwamua kiuchumi na alizeti inayozalishwa mkoani humo ambayo ni bora Afrika ya Mashariki na Kati haijapatiwa soko la uhakika kwa maana ya kuwa na viwanda vya kutosha ili wakulima waweze kuuza zao hilo kwa urahisi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuanzisha viwanda vya kisasa vya kukamulia mafuta ya alizeti Mkoani Singida?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mkakati wa Fungamanisho la Maendeleo ya Viwanda la mpaka mwaka 2025, mkakati uliozinduliwa Desemba, 2011 na Mkakati Maalum wa Kuendeleza Sekta ya Alizeti, 2016 mpaka 2020 uliozinduliwa mwaka 2016, tunaendelea na uhamasishaji wa zao la alizeti nchini. Moja ya mpango wa kuendeleza sekta hii ni kuhamasisha uongezaji wa thamani hapa nchini kwa kutumia viwanda vya aina zote. Kwa Mkoa wa Singida, mpaka Desemba, 2016 tulikuwa na viwanda vidogo 126, viwanda vya kati viwili na kiwanda kimoja kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada nyingine za Serikali ni kuuweka Mkoa wa Singida katika kundi la mikoa inayonufaika na Mfuko wa *SME Credit Guarantee Scheme* unaoendeshwa kwa ubia kati ya *SIDO* na Benki ya CRDB. Pia ubunifu wa Shirika la *TEMDO* wa kuchonga vipuri vya mashine za kukamua alizeti na *business-re-engineering* ya mashine za alizeti unalenga kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya viwanda vya alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii ya swali hili kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kukamua na kuchuja alizeti. Kiwanda kidogo sana kinakadiriwa kuwa na gharama kati ya shilingi milioni 10 mpaka shilingi milioni 15; kiwanda kidogo kati ya shilingi milioni 16 mpaka 200 ambacho kina uwezo wa kukamua na kuchuja kwa kiwango kidogo. Kiwanda cha kati kinachoweza kukamua na kuchuja mara mbili *(double refinery)* kinagharimu kati ya shilingi milioni 200 mpaka milioni 500.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Matembe.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imejikita katika uanzishwaji wa viwanda ili kuzalisha ajira za kutosha kwa vijana, je, Serikali ipo tayari sasa kuupa Mkoa wa Singida kipaumbele cha kwanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili. kwa kuwa Tanzania tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda: Je, ni lini sasa Mfuko huu wa *SME Credit Guarantee Scheme* utaletwa Singida ili vikundi vya wanawake na vijana viweze kunufaika na mfuko huo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mhesimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Aisharose maswali yake mawili ya nyongeza na nianze na hili la pili ambalo ni rahisi. Mfuko wa *SME Guarantee Scheme* umeshafika Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema kwa sababu yeye anashughulika na akina mama na vijana, namuagiza Meneja wa Singida awasiliane na Mheshimiwa Mbunge, halafu namuagiza Mkurugenzi Mkuu wa *TEMDO* wawasiliane, zile mashine zinazotengenezwa na *TEMDO* huyu mama ndiye awe mhamasishaji wa kuwaonesha watu namna gani wakope. Tumeshusha riba mpaka 17%. Mashine ya kwanza Singida uanze nayo wewe, utembee kijiji kwa kijiji ukiwalenga vijana na akina mama. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi ni kwamba Singida tayari wako kwenye uchumi wa viwanda. Tumeshatenga maeneo ya kujenga viwanda na Mbunge wa Singida, Mheshimiwa Kingu,

anajasiria kupitia *e-scheme,* mradi wa kiwanda cha maziwa. Kwa hiyo, Singida viwanda siyo jambo geni, tunahangaika Singida kwenye viwanda kuona ile malighafi ya saruji kama tunaweza kutengeneza kiwanda angalau cha ku-*blend* saruji kutafuta *crinker* na kuchanganya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tuwe wote, Singida wako kwenye viwanda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nape na mwisho Mheshimiwa Sokombi. *(Makofi)*

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa niaba ya wananchi wangu wa Mtama na Mkoa wa Lindi kwa wakulima wa ufuta. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ongezeko la uzalishaji wa zao la alizeti kasi yake inafanana sana na ongezeko la uzalishaji wa ufuta katika Mkoa wa Lindi na hasa katika Jimbo la Mtama na kwa kuwa ubora wa mafuta ya ufuta ni mzuri kuliko yale ya alizeti. Sasa Serikali ina mpango gani wa kusaidia uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo vya kukamua mafuta ya ufuta kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wangu wa Mtama na Mkoa wa Lindi ambao wanalima ufuta na kuinua uchumi wao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jibu langu, napenda niseme mafuta yote ya alizeti na yale ya ufuta yote ni mazuri. Kwa hiyo, wananchi waende kuyatumia, ilimradi yazalishwe Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vidogo vidogo, namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na *SIDO.* Nina Meneja mzuri wa *SIDO,* Lindi na kwa sababu hili liko kwenye mamlaka yangu, mradi wa *SME Guarantee Scheme* unahusisha na Mkoa wa Lindi.

Kwa hiyo, Mkurugenzi wangu anayeshughulikia mpango huu, ahakikishe na Lindi inakwenda kule kwa sababu Tanzania tunaagiza mafuta mengi ya kula. Tuna-*consume* tani 400,000 kwa mwaka, lakini karibu 70% tunaagiza nje. Mafuta ya kula ni *commodity* ambayo inachukua pesa za kigeni ikiwa ni namba mbili baada ya mafuta jamii ya petroli.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, unalisaidia Taifa lako, tukamue mafuta hapa, tujitosheleze, tuokoe pesa za kigeni.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sokombi.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Mara kulikuwa na takribani viwanda saba, lakini sasa hivi viwanda vyote vimekufa, kimebakia kiwanda kimoja tu cha samaki cha *Mara Fish.*

Je, ni lini Serikali itafufua viwanda hivyo kwa sababu sasa hivi ni kipindi cha viwanda tu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya maagizo niliyopewa katika Wizara yangu pamoja na *Treasurer Registrar* ni kuhakikisha vile viwanda vilivyobinafsishwa au ambavyo havifanyi kazi vinafanya kazi. Zoezi hilo linaendelea.

Mhesimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba nashindwa kusema ni lini kwa tarehe, napenda nimhamasishe Mbunge na yeye akimbilie kwenye viwanda vidogo, kwa sababu viwanda vidogo kulingana na taratibu za Bunge, pesa mnazonipa za *NEDF,* zinaniwezesha mimi kuweza kutoa

vile viwanda vya shilingi milioni 10, shilingi milioni 80 na shilingi milioni 200. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, twende kwenye viwanda vidogo kwa sababu vinaweza kufanya kazi kuanzia ngazi ya familia na vinajenga utamaduni wa Watanzania kumiliki. Hivyo viwanda vingine ni vya watu ambao ni wa kupita.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini.

Na. 49

**Fidia Kwa Ajili ya Kupisha Shughuli za Mgodi wa Dhahabu wa *GGM***

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Wananchi wa Mtaa wa Katoma na Magema katika Kata za Mtakuja na Kalangalula kwa muda mrefu wamezuiwa kuendeleza ardhi zao kwa sababu Mgodi wa *GGM* ulipima na kuweka vigingi vya mpaka ndani ya makazi yao.

Je, ni lini mgodi huo utawalipa fidia ili kupisha shughuli za mgodi huo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mhesimiwa Dkt. Kalemani.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 huwataka wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini kuzingatia umbali uliowekwa kisheria kutoka sehemu

ambako shughuli nyingine za kijamii zinaendelea. Kwa kuzingatia sheria hiyo, mgodi hulazimika kuwalipa fidia na kuhamisha wananchi wanaoishi ndani ya umbali wa mita 200 kutoka katika shughuli za uchimbaji ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kutokana na uchimbaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa *GGM* mwaka 2007, 2010, 2013 na 2014 ulilipa fidia ya jumla ya shilingi bilioni 9.67 kwa wananchi 733 wanaoishi ndani ya mita 570 katika maeneo ya Katoma na Nyamalembo. Hata hivyo, kwa kuwa mgodi haujaanza kutumia eneo hilo kwa shughuli za uchimbaji, baadhi ya wananchi waliopata fidia pamoja na wengine wapya, wamejenga tena katika maeneo hayo kwa ajili ya kudai fidia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa eneo la Magema, mgodi hauzuii wananchi kuendesha shughuli za kilimo na kuendesha shughuli za kimaisha kwa sababu eneo hilo halihitajiki na mgodi kwa sasa. Mgodi utalazimika kulipa fidia kwa kuzingatia sheria husika iwapo mgodi utahitaji kuendeleza eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini katika jibu lake naomba nifanye marekebisho kidogo kwamba kwanza haiwezekani watu wakalipwa halafu wakadai, kwa sababu wanaolipwa wanalipwa kwa *coordinates* na eneo linajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa miaka 17 wananchi wa maeneo ya Mizingamo, Ikumbiyaga, Compound pamoja na Mtakuja wako ndani ya eneo ambalo ni leseni ya mgodi, lakini hawaruhusiwi kujenga, hawaruhusiwi kupima, hawaruhusiwi kuuza, lakini mgodi haujajiandaa kulitumia eneo hilo sasa wala kesho. Sasa ni nini hatima ya wananchi wa eneo hilo, kama mgodi sheria inasema utalipa tu fidia pale ambapo

watataka kulitumia, lakini hawaruhusiwi kufanya chochote kwa miaka 17? Swali langu la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa muda tofauti, Serikali kupitia Waziri wa Wizara husika, Naibu Waziri wa Mazingira, wamekuja na wameshuhudia aina ya uchimbaji wa madini wa Mgodi wa *GGM* ukiwa na madhara makubwa kwa wananchi wa Kata ya Kalangalala, Mjini Geita. Matokeo ya uchimbaji mbovu ni mipasuko ya nyumba inayotokana na mitetemo mikubwa, watu wengi wamezimia, lakini maji machafu yanatoka kwenye eneo la kuchimba na Mkurugenzi wa Mgodi aliyekuwepo ambaye alitaka kuleta suluhisho la migogoro hiyo, mgodi ulipoona anataka kuchukua hatua, ukamfukuza. Maagizo yote yaliyotolewa na Serikali hayajawahi kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Serikali itahakikisha mgodi unawalipa fidia wananchi ambao nyumba zao zimepasuka kutokana na mitetemo ya uchimbaji wa dhahabu Geita? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Kanyasu jinsi ambavyo anapambana na kuhangaikia maendeleo ya wananchi wa Geita Mjini. Hongera sana Mheshimiwa Kanyasu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la kwanza, ni kweli kabisa maeneo ya Compaund, Nyakabale, Katoma pamoja na eneo lingine la Kagema, yako katika maeneo ya *beacon.* Kama ambavyo nilieleza kwenye jibu langu la msingi, wananchi hawa ambao mgodi unahitaji eneo lile, tutakapolihitaji wakati wa uchimbaji, tutawalipa fidia kwa wale ambao hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa wako wananchi wachache ambao baada ya kulipwa fidia, pia

walirejea katika maeneo yale. Kama haitoshi, mgodi ulilipa fidia ya umbali wa mita 570 badala ya mita 200 ili kuhakikisha kwamba hakuna mwananchi ambaye anabaki bila fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Kanyasu kwamba suala hilo tumelipokea, tutaendelea kulifanyia kazi. Kama kuna wananchi hawajafidiwa, basi itabidi wafidiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la pili, kuhusu mipasuko. Kwanza kabisa niendelee kumpongeza Mheshimiwa Kanyasu na Wabunge wote wa Geita, wakiwemo Mheshimiwa Mbunge wa Busanda na Waheshimiwa wengine, pamoja na Mheshimiwa dada yangu yule wa Chama cha Upinzani wa Mkoa, waliita Mkutano, nilifika kule mwenyewe nikaangalia taarifa ya kampuni. Taarifa ya kampuni ya awali ilionesha kwamba mpasuko hausababishwi na kampuni. Tuliunda tume, ikaleta matokeo, ikaonesha baadhi ya maeneo kwa kweli yanasababishwa na mpasuko wa kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, tuliunda tume nyingine kwenda kutathmini majengo yaliyoharibika. Nimhakikishie Mheshimiwa Kanyasu, ilionekana nyumba takribani 890 zilisababishwa kwa kiasi fulani na mlipuko wa Mgodi wa *GGM.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Kanyasu alitaka kujua ni lini sasa Serikali itatoa tamko? Tarehe 20 mwezi huu wa Aprili, timu ya wataalamu saba wakishirikiana na uongozi wa Wilaya pamoja na Jimbo lako Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mheshimiwa Mbunge na *GGM* watakwenda sasa kuangalia nyumba ngapi zinahitaji fidia ili fidia sasa itakapothibitika waweze kulipwa fidia wale ambao itaonekana kuwa halali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Katika Jimbo langu la Bunda kuna vijiji vya Nyabuzume na Nyaburundu. Kuna wachimbaji wadogo wenye *PL* wa muda mrefu sana. Tatizo wale wachimbaji wanachimba, madini yanapatikana, lakini pale wanaambiwa kwamba wana leseni za utafiti. Serikali ya kijiji iliwaomba kutoa huduma za maendeleo katika maeneo hayo ya Nyabuzuma na Nyaburundu, hawataki kutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni sheria ipi inawataka hawa wachimbaji ambao wanapata madini, hawataki kusaidia vijiji hivyo vinavyohusika?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa hakuna sheria inayowakataza wachimbaji wadogo au wachimbaji wakubwa wasilipe *levy* au mapato yoyote yanayotokana na uchimbaji wao. Sheria ya Madini pamoja na Sheria ya Fedha inawataka walipe.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Getere kama kuna shida, wasiliana na sisi tukusaidie ili Halmashauri yako iweze kupata fedha hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Anna Gidarya.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgodi wa Tanzanite uliopo Mkoa wa Manyara ni mgodi ambao unachukua idadi kubwa ya vijana, lakini kumekuwa na vifo mfululizo miaka tisa sasa ambavyo havijawahi kufanyiwa utafiti wa kina ni kwa nini vifo hivi vinatokea.

Je, ni lini sasa Serikali itakaa na hawa wawekezaji wa vitalu husika ili kuanzisha utaratibu wa kifuta jasho kwa familia zile ambazo zinapata maafa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa yapo madhara yanayotokana na uchimbaji, siyo katika mgodi wa *Tanzanite One* peke yake, hata katika migodi mingine. Sheria zinataka kama kuna mtu ameathirika na uchimbaji au na dhuluma yoyote, taratibu za kisheria lazima zifuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tumelichukua kwa muda mrefu, tunashirikiana na Wizara ya Kazi pamoja na Kitengo cha Maafa ili kutathmini ukubwa wa tatizo la namna hiyo ili hatua zifuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili, tumeunda timu inayojumuisha Wizara yetu, Wizara ya Kazi pamoja na Halmashauri husika ili mwezi wa tano tuanze kuyatathmini madhara hayo. Baada ya tathmini itakapofanyika Mheshimiwa Mbunge, tutakujulisha hatua kamili zitakazochukuliwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Muda hauko rafiki. Swali linalofuata namba 50 linaelekezwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; na linaulizwa na Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini.

Na. 50

**Ujenzi wa Barabara Kuu ya Zambia - Mbeya**

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI** aliuliza:-

Nyumba nyingi katika barabara kuu ya Zambia Jijini Mbeya kuanzia maeneo ya Uyole mpaka Lwambi ziliwekwa alama ya “X” kuashiria kuvunjwa ili kupisha upanuzi wa barabara hiyo muhimu na wapo wananchi waliowekewa alama nyekundu walivunja nyumba zao wenyewe na

wananchi waliowekewa alama ya "X" za kijani bado wanasubiri fidia.

(a) Je, mradi huo umefikia wapi na ni lini upanuzi huo utaanza?

(b) Je, upanuzi huo umezingatia ushauri wangu wa kuweka njia nne *(four lines)* toka Uyole mpaka *Songwe Airport* ili kuondoa kabisa tatizo la foleni ambalo linakua siku hadi siku Jijini Mbeya?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekaji wa alama za 'X' katika majengo yaliyopo ndani ya hifadhi ya barabara kuu ya *TANZAM* Jijini Mbeya pamoja na maeneo mengine mengi nchini ni utekelezaji wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na kanuni zake za mwaka 2013. Kutokana na sheria hiyo, mapendekezo yote yaliyopo ndani ya mita 22.5 kutoka katikati ya barabara kwenda kila upande yanapaswa kuondolewa bila fidia, hivyo wamiliki wote wa mali zilizokuwepo ndani ya eneo hilo waliwekewa alama za 'X' nyekundu na kupewa *notice* za kubomoa nyumba zao bila fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wote waliokuwa na maendelezo kati ya mita 22.5 na mita 30 kutoka katikati ya barabara kila upande wa barabara, kabla Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 haijaanza kutumika waliwekewa alama za 'X' za kijani na kupewa *notice* za kutofanya maendelezo mapya kwa kuwa maendelezo yaliyopo yatalipwa fidia wakati eneo hilo litakapohitajika kwa ajili ya upanuzi wa barabara ili kujiweka tayari na kuzuia ucheleweshaji wa kuanza kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi wa barabara ya kutoka Mbeya kwenda Zambia hususan kuanzia Uyole kwenda Songwe utaanza pale upembuzi yakinifu na usanifu wa kina utakapokamilika na kuonesha viwango vya upanuzi vinavyohitajika na Serikali tutakapopata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inakusudia kujenga barabara ya mchepuo wa Mbeya *(Mbeya Bypass)* yenye urefu wa kilometa 40 inayoanzia Uyole hadi Songwe ambapo mradi huu upo kwenye hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na unatekelezwa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua sahihi ya kuondoa msongamano na magari kwenye Jiji la Mbeya itatokana na mapendekezo yatakayotolewa baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaoendelea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili limerudi mara ya pili, lililetwa mwaka 2016 na majibu yalikuwa tofauti. Mwaka 2016 waliniambia fedha ziko tayari kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya Uyole ya *TANZAM,* lakini leo wananiambia upanuzi utaanza pale upembuzi yakinifu na usanifu utakapopatikana na kuonesha viwango vya upanuzi vinavyohitajika na Serikali itakapopata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 waliniambia fedha tayari ipo. Sasa hili ni tatizo, mara wanahama kutoka *project* hii ambayo tulikuwa tumeshaizungumzia, wanarukia *project* nyingine wakati wameshasema fedha hakuna. Kwa nini upembuzi unafanywa na TAMISEMI badala ya *TANROADS?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape ushauri kwamba *efforts* ziwekwe kwenye kupanua barabara kuu inayopita Mwanjelwa ya *TANZAM* iwe ya *four lanes* kwa sababu mchakato wake umeshaanza, nyumba za wananchi

zimeshavunjwa, wengine wamevunja kwa hiyari na wengine wanasubiri fidia huu ukiwa mwaka wa pili sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, mtachukua ushauri wangu kurudisha *efforts* kwenye barabara kuu ya *TANZAM* kwa sababu tayari mchakato wake ni kama umeshaanza na ule mchakato mwingine ni kama kuanza upya?

**MWENYEKITI:** Hilo ni la pili bwana.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Mheshimiwa Naibu Waziri kila anapokuja kujibu swali lililoulizwa na Mbunge wa Upinzani hasa CHADEMA huwa anapenda kusema hata Mbunge fulani wa Viti Maalum wa CCM aliuliza hilo swali? Mfano, akiuliza Msigwa utamtaja Mheshimiwa Ritta Kabati, nikiuliza mimi utamtaja Mheshimiwa Mary Mwanjelwa? Kwa nini unapenda ku-*undermine* shughuli za Wabunge wa Upinzani ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano? *(Makofi/ Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi tu. Jibu maswali mawili tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambaye yupo katika sherehe ya uzinduzi wa ujenzi wa reli ya *standard gauge,* naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie kwamba Wizara hii inachapa kazi na Serikali hii kila inachoamua kutekeleza na inachokisema inamaanisha hicho. Naomba nirudie kwenye jibu langu la msingi kwamba kazi ya usanifu pamoja na upembuzi itakapokamilika, suala la fedha litashughulikiwa na kazi hiyo itaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nimhakikishie kwamba ushauri wake umefika, tutawasilisha kwa wataalam wakaufanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyongeza tu, mimi bahati mbaya huwa nasema ukweli. Sasa kama Mbunge wa Viti Maalum amelishughulikia hilo hilo, nadhani ni sahihi naye kusema kwa sababu ninachokisema ni ukweli. *(Makofi/ Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa na mimi ni lazima nitende haki, maana ni lazima uyajue maeneo haya. Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Ni kweli kabisa hili suala nimekuwa nikilifuatilia na kuliulizia kwa miaka mingi. Nakumbuka hata Mheshimiwa Rais alipokuwa Waziri wa Ujenzi, hili suala nimekuwa nikilizungumza hususan katika barabara ya mchepuko wa Uyole hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kama ifuatavyo; pamoja na maswali mazuri ya Mheshimiwa Mbilinyi, nilitaka kujua ni lini barabara ya mchepuko kutoka Uyole hadi Uwanja wa Ndege itakamalika pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri? Kwa sababu kwenye kikao chetu cha *Road Board* tulikubaliana kwa pamoja kwamba barabara ya mchepuko lazima itiliwe mkazo, vinginevyo nitakamata shilingi kwenye bajeti yake. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi, muda siyo rafiki.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali Mheshimiwa Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa

Viti Maalum, swali ambalo huwa linafuatiliwa sana na Mheshimiwa Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini kama ifuatavyo:- *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mwanjelwa kwamba kazi hii inayofanyika sasa ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inafanyika kwa umakini na watu makini. Nikuhakikishie, mara itakapokamilika mchepuko huu tutaujenga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mtayasema kwenye Wizara wakati itakapofika.

Swali linalofuata namba 51 litaulizwa na Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini.

Na. 51

**Magari ya Zimamoto Mkoa wa Kilimanjaro**

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL** aliuliza:-

Mkoa wa Kilimanjaro una tatizo la uhaba wa magari ya zimamoto; gari linalofanya kazi mpaka sasa ni moja tu, hivyo kufanya huduma ya zimamoto kuwa duni sana.

(a) Je, ni lini Serikali itaongeza magari mengine mawili ili kusaidia shughuli za zimamoto na kuepusha hasara zinazowakabili wananchi wanaopata majanga ya moto?

(b) Je, Serikali haioni kwamba uamuzi wa kuhamishia Kitengo cha Zimamoto Wizara ya Mambo ya Ndani umeiongezea mzigo Wizara hiyo na kupunguza ufanisi wa shughuli za zimamoto?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mkoa wa Kilimanjaro una gari moja kubwa la kuzima moto ambalo lina uwezo wa kubeba maji lita 7,000 na dawa za kuzimia moto wa mafuta lita 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa sasa kuna magari mawili madogo ya kuzimia moto yasiyo na matanki ya kubeba maji na madawa. Pamoja na magari haya, hufanya kazi kwa kupata maji kutoka gari lingine au kutoka katika vituo maalum vya maji ya kuzimia moto *(fire hydrant).* Hata hivyo, kwa sasa ni gari moja tu linalofanya kazi na lingine linahitaji matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kununua magari ya zimamoto na uokoaji kwa ajili ya Mkoa wa Kilimanjaro pamoja na mikoa mingine. Katika kutekeleza mpango huo, Serikali inafanya mazungumzo na taasisi mbalimbali za nje ya nchi ambazo zimeonyesha nia ya kutukopesha fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya zimamoto pamoja na uokoaji na mazungumzo yatakapokamilika mkataba utasainiwa na kuanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhamishwa kwa Kitengo cha Zimamoto kutoka katika mamlaka mbalimbali na kuwekwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kulifanyika baada ya tathmini hususan ya utendaji kazi za kila siku, ambapo ilibainika kuwa utendaji kazi wa Vikosi vya Zimamoto katika Halmashauri ulikuwa dhaifu kutokana na vikosi hivyo kuwa chini ya Wahandisi wa Majiji, Manispaa na Miji ambapo hawakuwa na utaalam wa masuala ya Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ilibainika pia kuwa vikosi vikiwa chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vihamishiwe Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kuleta ufanisi zaidi wa kazi na viwe chini ya kamandi moja ili viweze kupokea amri kutoka kwa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba uamuzi huo uliongeza ufanisi na siyo mzigo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali nilikuwa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kitengo cha Zimamoto kikiwa kipo kwenye Mamlaka za Halmashauri za Miji na Manispaa, Manispaa ya Moshi ilikuwa ina uwezo wa kuhudumia magari makubwa mawili na gari moja dogo ambalo tuliazima kutoka Japan. Tangu magari yale yachukuliwe na Kitengo cha Zimamoto Mkoa wa Kilimanjaro, leo tunahudumia gari moja tena tunahudumia kwa taabu na hicho kigari kimoja tulichokiomba Japan ndicho kinachofanywa kama ndiyo gari wanalotembelea Maafisa wa Zimamoto.

Je, Serikali imetumia kigezo gani kuonesha kwamba ufanisi umeongezeka baada ya kuhamisha kitengo hiki kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani tofauti na kilivyokuwa Halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, naomba kama Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kusaidia Mkoa wa Kilimanjaro kwa kuazima gari moja ya zimamoto kutoka *KIA* kwa sababu *KIA* wanaonekana wana magari ya ziada ili iweze kusaidiana na gari lililopo sasa hivi Mkoa wa Kilimanjaro ili kutoa huduma ya zimamoto kwa watu wa Mkoa wa Kilimanjaro? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa kifupi tu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa jambo hili. Niseme tu kwamba vigezo vilivyotumika kwa sasa, moja tofauti na ilivyokuwa katika ngazi za Halmashauri, sasa hivi vipo *dedicated* kwa ajili ya masuala haya ya zimamoto na kutokuhudumia gari mbili ni kwa sababu tu gari yenyewe imeenda kwenye uchakavu. Ukipima

kwa ujumla wake, ni kwamba ufanisi umeongezeka na utaona kwamba sasa kikosi kipo *dedicated* kwenye masuala ya zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la kuazima gari; gari za zimamoto zipo kwa ajili ya matukio na mara zote katika maeneo yote panapotokea tukio la moto, gari zilizo karibu za kuzimia moto huwa zinaenda kutumika. Kwa hiyo, hilo hatuna tatizo nalo, lakini tunapanga kuimarisha hasa katika Miji ikiwemo hiyo ya Moshi kwa ajili ya ukubwa wa miji pamoja na uwepo wa uwanja wa ndege. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuzingatia umuhimu wa magari ya zimamoto katika Mikoa yetu, lakini mikoa mingi mipya hususan Mkoa wa Songwe unakabiliwa na ukosefu wa magari ya zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata kauli ya Serikali kwamba je, Serikali ina mpango gani wa kutuletea magari ya zimamoto katika Mkoa mpya wa Songwe? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, lini watapata hiyo gari ya zimamoto?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake na siyo tu jambo la zimamoto, bali masuala mazima yanayohusu idara zilizopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ikiwemo Makao Makuu ya Polisi katika Mkoa mpya wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu Songwe ni moja ya mikoa mipya, lakini una bahati ya kuwa karibu na uwanja wa ndege. Tutaupa kipaumbele kama Mkoa mpya lakini pia kama mahitaji ya Mji ambao upo karibu na Mji wa Tunduma ambao unakua kwa kasi, ambao mara nyingi sana

Mheshimiwa Juliana Shonza amekuwa akitetea masuala ya maendeleo ya mkoa huo na miji hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Murad.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mkoa wa Kilimanjaro matatizo yake yanafanana kabisa na Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Morogoro unakua sana na viwanda vipo vingi na vingine vinaendelea kujengwa, lakini Kikosi cha Zimamoto katika Manispaa ya Morogoro kinafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, kutokana na uchakavu wa magari katika Manispaa ya Morogoro, je, Serikali iko tayari kushirikiana na Manispaa ya Morogoro kupata magari mapya katika Manispaa ya Morogoro?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alichosema Mheshimiwa Murald na nimpongeze sana kwamba maeneo ambayo yana viwanda gharama za bima huwa zinakuwa juu sana kama magari ya zimamoto ama huduma za zimamoto zisipokuwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *nature* ya Mkoa wa Morogoro Serikali iko tayari kushirikiana na Mkoa na Mji wa Morogoro kuweza kupata magari mapya. Kwenye taratibu hizi tunazoendelea nazo za upatikanaji wa magari mapya, tutazingatia maombi na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama kutaka kuuliza maswali la nyongeza)*

**MWENYEKITI:** Muda, muda. Swali namba 52 litaulizwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 52

**Hitaji la Kiwanda cha Kutengenezea *ARV***

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Baadhi ya nchi za Afrika kama Uganda na Zimbabwe zimejenga viwanda vyao kwa ajili ya kutengeneza dawa za kupunguza makali ya VVU *(Generic* za *HIV)* na hivyo kupunguza gharama za kusaidiwa dawa hizo ambazo zinabadilishwa kila baada ya miaka kadhaa na hivyo kutengeneza usugu kwa baadhi ya magonjwa.

(a) Je, Serikali ina mpango wowote wa kujenga kiwanda cha kutengeneza *ARVs* za watu wazima pamoja na watoto?

(b) Kwa dawa zinazoletwa hapa nchini, je, kuna *ARVs* za watoto?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahamasisha mashirika, taasisi, wafanyabiashara wakubwa na wawekezaji kuwekeza kwenye viwanda vya kuzalisha dawa mbalimbali zikiwemo dawa za kupunguza makali ya UKIMWI *(ARVs).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kuna kiwanda kimoja Mkoani Arusha *TPI ARV Limited* ambacho kimepewa leseni ya kutengeneza *ARVs.* Kiwanda hicho bado hakijaanza uzalishaji. Wizara inatarajia kuwa kiwanda hicho kitaanza uzalishaji wa *ARVs* hivi karibuni.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dawa za *ARV* zinazoingizwa nchini, kuna dawa za watoto ambazo ni pamoja na *Nevirapine Syrup, Lopinavir/Ritonavir Syrup,* dawa nyingine ni pamoja na mchanganyiko wa dawa za vidonge mfano *Lamivudine/Atazanavir* zenye nguvu ya miligaramu 30 na miligramu 60 pamoja na *Lamivudine* zenye nguvu ya miligramu 30 na miligramu 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote kwa ujumla kwamba nchi yetu haina tatizo la upungufu wa dawa za *ARV* kwa watoto.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fatma, maswali ya nyongeza au swali moja la nyongeza.

**MHE FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imeanzisha Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI na imetenga kiasi cha shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya mfuko huo, je, Serikali haioni umuhimu wa kutumia sehemu ya pesa za mfuko huo kwa kutoa ruzuku kwa kiwanda hicho?

Swali la pili, je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kuwa uzalishaji unaanza mapema zaidi ili kupunguza gharama za kuagiza dawa za *ARV* kutoka nje? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye Mfuko huu wa UKIMWI kwa mujibu wa sheria uko chini ya Ofisi hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambaye ni mdau mkubwa tunayefanya naye kazi kwa pamoja kushughulikia masuala haya ya tatizo la UKIMWI nchini kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu ambao unashughulikia matatizo ya UKIMWI *(ATF)* umeanzishwa kwa mujibu wa sheria na sheria imeweka mamlaka kwa bodi inayosimamia mfuko huo kutoa miongozo na kuangalia ni kwa namna gani fedha zitakazopatikana kwenye mfuko zitatumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali zinazoendana na tatizo la UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi imeshagawa utaratibu wa matumizi ya fedha hizo kwa asilimia 60 kutumika kwenye matibabu, dawa na vitendea kazi na asilimia nyingine 25 na 15 kwa kazi nyingine.

Kwa hiyo, kwa utaratibu ama ushauri ambao ameutoa Mheshimiwa Mbunge, tutarudi kuwasiliana na bodi kuona kama katika zile asilimia 60 zinaweza pia zikatumika katika kusaidia utengenezaji wa dawa kwenye nchi yetu ya Tanzania kama mfuko utakuwa umeshajitosheleza kwa kiasi kikubwa na kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kupokea ushauri wa kuboresha matumizi ya fedha ya mfuko huo kadiri inavyoonekana inafaa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Jenista kwa kujibu sehemu ya kwanza ya swali hili, kati ya maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fatma Toufiq.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha tunawekeza katika uzalishaji wa dawa za *ARV* nchini Tanzania? Nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hadi sasa tuna viwanda vitano, wawekezaji watano ambao wameonesha nia ya kutaka kuwekeza katika uzalishaji wa viwanda vya dawa nchini na wiki iliyopita tulikuwa pale Bagamoyo, *Zinga Phamaceutical Company* na moja ya dawa ambayo watazalisha ni pamoja na dawa za kupunguza makali ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka tu kumthibitishia tunafanya kazi pia pamoja na Mheshimiwa Charles Mwijage kuhakikisha kwamba tunazalisha dawa zetu zote ndani ya nchi badala ya kununua dawa nje ya nchi kama tunavyofanya sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde.

Na. 53

## Ongezeko la Watoto wa Mitaani

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wa mitaani hasa katika Miji Mikuu ya nchi yetu.

Je, Serikali inachukua hatua gani kupunguza tatizo hilo ili watoto hao walelewe katika mazingira salama na maadili halisi ya Kitanzania?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa sana, kaka yangu Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kumekuwa na ongezeko la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani hasa katika miji mikubwa. Kwa mujibu wa takwimu zilizofanyika katika Majiji ya Dar es Salaam na Mwanza mwaka 2012 zilionesha kuwa Jiji la Dar es Salaam lilikuwa na watoto 5,600 kutoka mikoa kumi ya Tanzania ambayo ni Dar es Salaam yenyewe 28%, Dodoma 9%, Mwanza 7%, Morogoro 7%, Tanga 6%, Lindi 6%, Iringa 5%, Pwani 5%, Kilimanjaro 5% na Arusha 4%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inalo jukumu la msingi kuhakikisha ulinzi na usalama wa mtoto. Katika kutekeleza wajibu huu, Serikali kwa kushirikiana na wadau, inatekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuwezesha jamii kuwa na mipango shirikishi ya kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wa mitaani. Hadi sasa mpango huu unatekelezwa katika Halmashauri 111 nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imeanzisha mpango wa kuimarisha ulinzi na usalama kwa watoto ambapo Halmashauri 51 zimewezeshwa kuunda timu za ulinzi wa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kueneza mpango huu katika Halmashauri nyingine nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Haji umeridhika? Tunaendelea. Umeridhika na majibu!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeridhika, lakini nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi iliyoridhia Mikataba ya Kimataifa ya Haki na Ustawi wa Mtoto. Kuna Mkataba wa *Convention of the Right of the Child (CRC)* wa mwaka 1989 na pia kuna mkataba wa Itifaki ya Nyongeza wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto *(African Charter of the Rights and Welfare of the Child)* wa mwaka 1990. Mikataba yote hii inatutaka nchi wanachama kuhakikisha kwamba watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi

wanapatiwa maisha bora na haki zao za msingi za kuishi kwa mujibu wa mikataba hii.

Je, ongezeko hili la watoto wa mitaani katika nchi yetu, ni jibu tosha kwamba Tanzania imeshindwa kuifanyia kazi mikataba hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sheria za nchi yetu, Sheria Na. 15 ya mwaka 1984 Ibara ya (6) inasema; "Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata hifadhi kutoka kwa jamii kwa maisha yake kwa mujibu wa sheria."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria za nchi yetu zinakataza, Sheria za Kazi; Ajira kwa Watoto. Jamii inayopelekea wimbi kubwa la watoto wa mtaani ni kwamba imewasusa watoto, wazazi wameshindwa kuwahudumia watoto na Serikali inakataza ajira kwa watoto. Sasa watoto hawa wanafanya kazi, siyo kwamba wanapenda, bali kwa kukidhi haki ya kupata maisha yao.

Je, Serikali inatoa jibu gani la miujiza, watoto hawa waweze kuishi huku ikitambua kwamba Sheria za Kazi zinakataza kupata ajira na huku Serikali imeshindwa kuwahudumia watoto hawa? Je, waishi kwa miujiza gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kaka yangu, Mheshimiwa Khatib Haji kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, Serikali imeshindwa kufanyia kazi mikataba hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijashindwa kufanyia kazi Mikataba ya Kimataifa inayohusu haki za watoto. Kwa taarifa tu, taarifa zetu zote ambazo tunaziwasilisha kwenye Kamati inayoshughulikia masuala ya haki za watoto katika ngazi ya Umoja wa Mataifa na ngazi ya Afrika, tunapongezwa kwa

kazi nzuri ambayo tunafanya katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa mtoto ikiwemo uamuzi wa Mheshimiwa Rais kutoa elimu bure, maana yake imewezesha watoto wa kike na wa kiume kupata elimu kuliko zamani. Haki kubwa ya msingi ya mtoto katika kuendelea ni pamoja na haki ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu ajira kwa watoto, kwamba tuna mikakati gani? Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009, jukumu la kwanza la kutoa chakula, malazi na mavazi kwa mtoto ni kwa wazazi. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwataka Maafisa Ustawi wa Jamii wote kuwafikisha katika vyombo vya sheria wazazi na walezi wote ambao hawatimizi wajibu wao wa kuwatunza na kuwalea watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mtoto imesema, pale ambapo mtoto huyo hana mlezi au mzazi, basi ni jukumu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kifungu cha 94. Sisi hapa wote ni Madiwani, tunao wajibu wa kuhakikisha Halmashauri zetu zinaweka mikakati madhubuti ya kutoa malazi, chakula, kwa watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu. Kwa hiyo, hilo suala tutaendelea kulihamasisha na kulisisitiza kwa Serikali za Mitaa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali letu la mwisho kwa siku ya leo ni swali namba 54 linaulizwa na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake linaulizwa na Mheshimiwa Mwamoto.

Na. 54

**Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. RITTA E. KABATI)** aliuliza:-

Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 imekuwa ya muda mrefu na hivyo kupitwa na wakati.

Je, ni lini sheria hii itafanyiwa marekebisho ili iendane na mahitaji na kuondoa upungufu uliopo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ni matokeo ya mjadala mpana na shirikishi kupitia Waraka wa Serikali Na.1 ya mwaka 1969. Lengo la mjadala huo lilikuwa kupata muafaka kuhusu maudhui ya sheria hiyo ambayo yaligusa imani, mila na desturi za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya miaka zaidi ya 20 kupita tangu Sheria hiyo ya Ndoa itungwe, Serikali kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria iliifanyia mapitio sheria hiyo na kubaini maeneo kadhaa yenye udhaifu na hivyo kuhitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa mwenyekiti, kutokana na maoni hayo ya tume, mwaka 2008 Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria iliandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri uliokuwa na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mnamo Desemba, 2010 kabla ya waraka huo kujadiliwa na kuridhiwa na Baraza la Mawaziri, mchakato wa mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukaanza na kulilazimu baraza kusitisha kwa muda mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikuwa na matarajio kuwa wakati Tume ya Mabadiliko ya Katiba inakusanya maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya Katiba, wananchi wangetoa maoni kuhusu Sheria ya Ndoa pamoja na sheria nyingine zinazofanana na hiyo. Hata hivyo, maoni

yaliyotolewa wakati wa mchakato huo kuhusu Sheria ya Ndoa yalikuwa machache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na muda kupita na mabadiliko kadhaa yaliyotokea kuhusu Sheria ya Ndoa, Wizara yangu imeendelea na mchakato wa ndani wa kuifanyia mapendekezo ya marekebisho sheria hiyo. Wakati muafaka utakapofika, tutawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo Bungeni ili iweze kuendana na wakati kwa kuondoa upungufu uliopo kwa maslahi mapana ya nchi yetu na kuhuisha na kuimarisha maeneo yaliyo mazuri ndani ya sheria hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyokiri Mheshimiwa Waziri, sheria hii ni ya muda mrefu lakini imekuwa ikikinzana sana na baadhi ya mila, desturi za makabila na baadhi ya sheria za dini ambazo baadhi ya makabila na sheria za dini zinatambua mtoto wa kike hata akiwa na miaka kumi akishavunja ungo ni mtu mzima. Hivyo, haioni sasa hiyo pia ilikuwa ni kichocheo kikubwa cha watoto wadogo kuolewa kabla ya wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa sheria hii ya ndoa imechelewa na kusababisha ongezeko kubwa la ndoa nyingi kuvunjika na kusababisha watoto wa mitaani kuongezeka, sasa Serikali haioni kwa kuwa Katiba bado itachukua muda, sheria hiyo iletwe hapa ili tuifanyie marekebisho? *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Moja, kuhusu suala la umri wa msichana au mvulana kuoa pamoja na suala la imani, dini na desturi. Kwa wale ambao wametabahari (wame-*specialize*) katika eneo hili la Sheria za Ndoa watafahamu kwamba hili ni moja ya maeneo ambayo yanahitaji umakini mkubwa sana ili kufikia muafaka wa nini kifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bara la Afrika Tanzania ndiyo ilikuwa nchi ya kwanza kufanikiwa kutunga Sheria ya Ndoa. Uganda toka mwaka 1966 chini ya Ripoti ya Kalema mpaka leo wameshindwa kuwa na Sheria ya Ndoa, kwa sababu ya mambo hayo ya mila, desturi na imani. Kenya ambao mwaka 1968 waliunda Tume ya Spry, wameweza kutunga sheria mpya ya ndoa ambayo haifanani na ya kwetu kwa maana ya kwetu ni bora zaidi baada ya Katiba yao mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ya ndoa ilipotungwa mwaka 1971 ili kuweza kuvuka, yalikuwepo maarugu *(rationale).* Maarugu hayo yaliyosababisha baadhi ya vipengele ambavyo leo vina upungufu, ndiyo yaliyowezesha sheria hii kupita na moja lilikuwa ni umri wa mtoto kuolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka wa Serikali Na.1 wa mwaka 1969, Ibara ya 7 inaeleza kinagaubaga kwamba huo ndiyo ulikuwa umri pia uliopitishwa na Umoja wa Mataifa. Sasa kwa kuzingatia muktadha wa leo, mazingira ya leo, ni dhahiri kabisa kwamba eneo hilo linahitaji kufanyiwa marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwa mtoto wa kike; ukisoma kifungu cha 15(2) kinaruhusu mtoto wa kike lakini hata mtoto wa kiume kuoa chini ya umri wa miaka 14 na hiyo ilikuwa kukubaliana na mazingira ya wakati ule, kwa sababu makundi mawili mwaka 1971 yaliikataa Sheria ya Ndoa, ilikuwa ni Baraza la Maaskofi Katoliki na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania na ilikuwa ni vyema baadhi ya maoni hayo kuyachukua ili tuvuke, lakini baadhi ya mambo hayo sasa kwa muktadha wa leo yamebadilika, tutayafanyia kazi

na yanahitaji uangalifu mkubwa ili tusikwame kama walivyokwama Uganda na Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masuala yanayohitaji afua mbalimbali *(interventions)* ili kuweza kuyavusha. *(Kicheko/ Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, si ndio Profesa, anatuhutubisha. Endelea bwana! *(Kicheko)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Sambamba na Sheria ya Ndoa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Sera ya Wazee tangu mwaka 2003. Ni lini Serikali italeta sheria kamili ya wazee ili waweze kutambuliwa katika nchi yetu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunayo Sera ya Wazee na sasa hivi tayari tumeshapeleka kwenye Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri mapendekezo ya kutengeneza Sheria ya Wazee ili kuhakikisha kwamba yale ambayo tumeyaweka katika Sera ya Wazee basi yanapewa nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni lini? Ni mara tu baada ya kumaliza taratibu za kutengeneza Sheria hiyo katika Baraza la Mawaziri tutaleta Bungeni tukiwa tayari.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tumevuka kipindi chetu cha maswali na mnaelewa kwa nini, sitaki kurudia.

Matangazo, kwanza tuanze na wageni wetu waliopo hapa. Tuna wageni mbalimbali Waheshimiwa Wabunge, sijatolewa *breakdown* ya makundi hayo, lakini tunao. Karibuni sana wageni wetu mliopo hapa kufuatilia shughuli za Bunge.

Nina matangazo ya kazi, lakini nianze na moja kwa sababu hayo matangazo ya kazi wataamua wao sasa wafanye lini, lakini nianze na hili ambalo tulijulishwa mapema leo tarehe 12 Aprili, tangazo la semina.

Niwatangazie kuwa, leo Jumatano tarehe 12 Aprili, 2017 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu masuala ya hisa *(shares)* na *securities in general*. Semina hiyo ambayo itaratibiwa na Taasisi ya Vodacom pamoja na *Dar es Salaam Stock Exchange* na *Capital Market Security Authority* itafanyika katika ukumbi huu wa Bunge kuanzia saa saba mchana.

Aidha, baada ya semina hiyo, *CRDB, NMB, Solomon Brokers* watakuwepo nje ya jengo la habari kwa ajili ya kuwauzia hisa kwa wanaotaka kununua. Ukishaona *CRDB, NMB* na *Solomon Brokers* unajua maana yake. Kwa hiyo, mnahamasishwa mfike kule. Ni tangazo muhimu sana na semina hii muhimu sana hasa kwa vijana. Sisi ambao tumenufaika na haya tukawezeshwa na Serikali, tunaelewa faida ya kuwa na hisa. Vijana kwa sababu mnaanza mapema, wekeza mapema ili inapofika saa 12 kasoro robo, mambo yamekaa vizuri. *(Makofi)*

Sasa matangazo ya kazi. Kikao cha Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii tafadhali nimeambiwa niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa leo tarehe 12 Aprili, 2017 saa 7.00 mchana, ndiyo nilikuwa nasema sasa mtapima wenyewe, kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi wa 229 Jengo la Utawala. Imetolewa na Mheshimiwa *Engineer* Nditiye, Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyoletewa mezani. Sasa niketi kidogo halafu tuone tunaendaje.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Nilitegemea tu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Makatibu nyie fanyeni kazi ya kuchukua majina, siyo kazi yangu kuchukua majina. Nyuma huko, Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Sixtus Mapunda, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Dkt. Mollel, Mheshimiwa Nassari umerudi?Haya.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Haonga.

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Eeh, Haonga.

**MWENYEKITI:** Mnajua muda, lakini nawapeni. Mheshimiwa Haonga. Tuanze na Mheshimiwa Haonga.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) jambo ambalo limetokea hapa Bungeni. Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Juma Nkamia jana wakati anachangia alijaribu kuhoji kwamba ndugu yetu Mheshimiwa Mwakyembe, Waziri alikuwa anafanya nini kwenye ile *press conference* ya Roma?

Sasa kwa sababu Mheshimiwa Mwakyembe jana hakuwepo, nadhani labda tuweze kujua Mheshimiwa Mwakyembe alikwenda kufanya nini kwenye *press conference* ya Roma maana suala hili limeleta kidogo sintofahamu na Watanzania wengi wanajiuliza sana kwenye mitandao mbalimbali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Mwakyembe yuko hapa, atatusaidia kama alialikwa atuambie alialikwa na nani? Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nimeuliza swali la nyongeza kuhusu eneo la Mgodi wa *GGM* na wananchi kulipwa fidia, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yalikuwa mazuri sana, lakini nilitaka tuweke kumbukumbu vizuri.

Kwa kuwa wananchi wale kwa miaka 17 hawana maji, hawana barabara, hawaruhusiwi kujenga wala kufanya chochote; na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba mgodi utawalipa tu pale utakapohitaji eneo lile.

Je, kwa kauli hiyo sasa kuanzia leo wanaruhusiwa kupimiwa, kujenga, kupitisha barabara na kufanya maendeleo ya aina yoyote pamoja na kwamba wako ndani ya leseni ya mgodi? Nilitaka kuweka kumbukumbu vizuri ili wananchi wangu waweze kunisikia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Mapunda.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7); na kwa ajili ya muda naomba nisiisome. Jana kipindi cha Maswali na Majibu, Mheshimiwa Felister Bura aliuliza swali la nyongeza kuhusu kupitika kwa barabara inayounganisha *Area D* inayokatiza *Airport.* Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kipindi analijibu lile swali, alisema hakuna namna yoyote ambapo ile barabara inaweza ikatumika isipokuwa Serikali ina mpango wa kutengeneza barabara nyingine kwa gharama nyingine ili kutatua hilo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wangu, Tanzania siyo nchi ya kwanza kutumia *airport* na barabara kwa wakati mmoja. Kuna *Gibralta International Airport* iliyoko

*Spain,* iko *busy* kuliko hiyo *airport* yetu, magari yanapita na ndege zinapita. Kwenda kutengeneza barabara nyingine kunaitia Serikali hasara kubwa na gharama kubwa badala ya kutumia gharama ndogo. Kwa utafiti wangu, ile barabara inaweza ikapitika kwa shilingi 259,740.23 tu katika mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itahitaji bomba mbili tu na *bolt* zake na makopo mawili ya rangi, aidha nyeupe au nyeusi kuweka alama ambayo itagharimu shilingi 68,220.12. Vilevile Serikali itahitaji watu wawili tu wa kufunga geti na kufungua geti ambao watahitaji *uniform*, kirungu na tochi na gharama yake itakuwa shilingi 72,421. Serikali vilevile itahitaji mifuko miwili ya saruji...

**MWENYEKITI:** Nisaidie unataka mwongozo gani? *(Kicheko)*

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itahitaji mifuko ya saruji miwili yenye gharama za shilingi 26,700; itahitaji kokoto, mchanga na nondo vyenye jumla ya shilingi 92,400. Jumla yake inakuwa shilingi 259,740.23 iki-*include* ufundi na dharura. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwenye hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kuniona, ahsante kwa kutambua kwamba nimerudi na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68(7), naomba nisiisome, lakini nikisoma pamoja na Kanuni ya 47(1), (2), (3) na (4), lakini pia nikisoma pamoja na Kanuni ya 48 na vipengele vyake vyote, nitavirudia baada ya kuzungumza lile ambalo limenifanya kusimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni mbili za mwisho nilizozisoma zinazungumzia masuala ya dharura na kuahirisha shughuli za Bunge. Ukisoma vyombo vya habari leo, magazeti karibia yote, taarifa za habari za vituo karibia vyote vya *television*, redio, mijadala iliyoko mitaani inazungumzia habari ambayo imekuwa ikijadiliwa kwenye Bunge hili, imekuwa ikitajwa tajwa kwenye Bunge hili inayohusu masuala ya utekaji ambayo yameshamiri kwenye Taifa letu kwa siku za usoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Bunge hili amezungumza Mbunge mmoja na akaelezea kupewa taarifa kabisa tena kutoka kwa watu ambao ni *credible* kwamba kuna Wabunge 11 ambao wapo kwenye *target*. Hatujui ni wewe, hatujui ni mimi na imezungumzwa hapa jana na Mheshimiwa Msigwa kama siyo juzi kwamba Wabunge hatuna ulinzi na hatujui hatima yetu. Mimi nataka kwenda Arusha kesho kwa ajili ya Pasaka, lakini nina mashaka sijui nakwendaje. Sijui kama ni mmojawapo kati ya Wabunge 11 au la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ametekwa msanii wa muziki, amevamiwa ambaye ni Mbunge na alikuwa Waziri saa 24 kabla ya tukio lile na wanaodaiwa kwamba ni watu wa usalama kutoka Kitengo cha Usalama wa Taifa na amezungumza Mheshimiwa Zitto jana hapa na akasema anao ushahidi ni kwa namna gani ambavyo watu wanaohusika na matendo ya utekaji kwenye nchi sasa hivi wanatumia Taasisi ya *TISS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia sasa, ni kwa nini naomba shughuli za Bunge ziahirishwe kwa kutumia Kanuni ya 47 ambapo naomba vipengele vyake visomwe; sitaki kupoteza wakati, lakini Kanuni zaidi ya 48 ambayo imezungumzia masharti ya jumla yafuatayo kwamba yatatumika kwenye hili na kwa nini nasema kwamba ni suala la dharura.

Kanuni ya ya 48(1)(a) inasema; "Hoja hiyo haitaruhusiwa iwapo inahusu jambo ambalo kwa taarifa ya

hoja imekwisha.” Suala hili halijajadiliwa ndani ya Bunge na taarifa yake haijatolewa. Kwa hiyo, hoja hii bado haijakwisha.

Vilevile kifungu (c) kinasema: “Jambo ambalo litakuwa limejediliwa katika hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii halitaletwa tena Bungeni katika Mkutano ule ule kwa kutumia kanuni hii.” Suala hili bado halijajadiliwa, kwa hiyo, kwa msingi huo haliathiriwi na kanuni hii.

Pia kanuni ndogo ya (2) ya hiyo hiyo 48...

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ninaomba sasa kwamba shughuli za Bunge ziahirishwe, na mimi nipewe nafasi ya kuzungumza kwa dakika tano kwa mujibu wa kanuni, halafu tuone kama kuna haja ya kujadili au shughuli za Bunge ziendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu mniunge mkono kwa sababau hatujui *who is next.* Naomba kutoa hoja.

**MBUNGE FULANI:** *Caucus* hiyo, *caucus* ya jana. *Caucus* eeh!

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kimsingi nilikuwa naomba kutumia Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja, kama alivyosoma Mheshimiwa Joshua Nassari 47 na 48. Niongeze kidogo kwamba jana karibu tangu tumekuja Bungeni hapa ndiyo mjadala uliopo katika mitandao ya kijamii na maeneo mbalimbali kama ambavyo imezungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nikiwa hapo nje, mimi nilipokea *message* ikitaja Wabunge ambao ni

*target* na mtoa taarifa anasema, imeundwa timu ya watu watatu, yaani timu mbili tofauti za watu wa utaalam wa Usalama Taifa sita; wana majina ya Waheshimiwa Wabunge wanaotafutwa. Majina ambayo yanatajwa ni Mheshimiwa Nape Nnauye, anatajwa Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Msigwa, ameingizwa mle na Mheshimiwa Waitara na wengine. Hao watu nimeambiwa kuna timu iko Bagamoyo, kuna nyingine imesogea Morogoro na nyingine ilikuwa Loliondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitashangaa sana, kwa sababu kwanza mazungumzo na taarifa zilizopo zinaichafua sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Nawashangaa Wabunge wa CCM na Mawaziri hawataki jambo hili lijadiliwe. Hawataki kutoa kauli, wanafikiri wanatukomoa sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili hatuwezi kuwa watu wa ajabu sana kiasi hicho, kwa kuzungumza maisha ya watu yatapotea. Kwa kuzungumza, Mtanzania mwenzetu, kijana mwenzetu, Ben Sanane hajulikani alipo. Sasa nilikuwa naomba, kwa kutumia kanuni maalum ambazo zimetajwa; shughuli ziahirishwe, jambo hili lijadiliwe ili tupate muafaka tuweze kutoka hapa. Hatuwezi kufunga masikio kwamba hatuelewi na hatusikii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima yako kubwa...

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo hili lijadiliwe na Bunge liahirishwe, baada ya hapo ndiyo...

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu muunge mkono hoja hiyo.

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea. Mheshimiwa Jenista!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba mwongozo wako. Kanuni zetu zinatuelekeza kwamba kama jambo lolote likishatolewa Bungeni na maamuzi yake yakishafanyika, jambo hilo halitarudishwa tena Bungeni kwa namna yoyote na linakuwa limefungwa...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Jambo hilo halijatolewa maamuzi hapa Bungeni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mpaka...

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu kuongea Mheshimiwa Waitara. Naomba uzingatie kanuni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mpaka litakapoletwa kwa utaratibu mwingine wa kikanuni. Naomba hawa wenzetu wawe wavumilivu, wanaposema tunawasikiliza, nao wajifunze *listening skills. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilishafanyiwa maamuzi na Mheshimiwa Naibu Spika alipokalia kiti hicho na akatolea maelekezo kuhusu jambo hilo wiki hii siku ya Jumatatu. Sasa naomba mwongozo, hivi ni kwa nini jambo hili liendelee kurudi huku likivunja kanuni na Wabunge wakiendelea kulileta huku wakijua wanavunja kanuni kwa makusudi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sasa kiti chako kingetupa mwongozo wa kuzingatia utaratibu wa kanuni na hasa kama hoja inakuwa ilishafanyiwa maamuzi na utaratibu wa kuirudisha tena hoja hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba sana. Mheshimiwa Bulaya.

Nimeombwa mwongozo na Waheshimiwa wafuatao, Mheshimiwa Haonga, Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Mapunda, Mheshimiwa Nassari, Mheshimiwa Waitara na mwisho Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI***: Ooh, I am sorry, I am sorry!* Mheshimiwa *Doctor*.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenisahau.

**MWENYEKITI:** Basi, niwie radhi ngoja niketi tumalize. *Doctor*.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia kanuni zilizotajwa na Mheshimiwa Nassari pamoja na Mheshimiwa Waitara, ili kuokoa muda naomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala hilo hilo la utekaji. Nazungumzia kwa sababu tatu, kwamba ni suala ambalo linahitaji Bunge lijadili na lifanyiwe maamuzi. Kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alienda na kikosi kwenye *studio* za *Clouds,* lakini kukawepo na tetesi kwamba ni polisi; polisi wakasema sio wao. Kukawepo na tetesi za *TISS, TISS* wakasema sio wao. Kwa maana nyingine bila kusema Serikali inatuambia Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ana jeshi lake ambalo hatulijui.

Kwa hiyo, kuna umuhimu wa sisi kujiridhisha na Bunge hili kuridhishwa kwamba katika nchi hii kuna majeshi mangapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili; Waziri, Mheshimiwa Nape alitishiwa na bastola, Polisi wakasema sio wao, *TISS* wamesema sio wao. Tunataka kujua ni kikosi gani kiko kwa ajili ya kutishia viongozi na kutaka kuwaua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya tatu, leo Usalama wa Taifa wa Marekani wanawaza kwenye *International Space Station,* wanapataje sehemu ambazo wanaweza wakapitisha *information* bila Urusi kuona au nchi nyingine yoyote? Usalama wa Taifa ni uchumi, leo ukienda kwa Usalama wa Taifa wa Marekani, inawezekana hata wanajua chini ya ardhi hapa kuna mali gani tunakokalia sisi. Maana yake ni nini? Usalama wa Taifa ni tanuru la fikra la nchi. Leo usalama wetu wa nchi unatuhumiwa kama tanuru la unyanyasaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima kama nchi tusimame tutafute ni nini? Kama ni tuhuma siyo za kweli, tunatakiwa tufike mahali tujadili, tusafishe usalama wetu wa Taifa kwa sababu ni nchi yetu. Kama ni kweli, sisi tuna busara, ni viongozi, ni lazima tufike mahali tunajua jinsi ya ku-*handle* kiuongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, naomba suala hili lijadiliwe kwa dharura.

**MWENYEKITI:** Haya. Nawashukuru sana Waheshimiwa kwa maombi yenu ya mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68(7).

Waheshimiwa Wabunge, niseme wazi na nirudie; Mwongozo unapoombwa unaomba sahihi kabisa kupitia Kanuni ya 68(7), lakini Kanuni hiyo huwezi ukaiunganisha kama tishari na Kanuni ya 47 na 48. Kama unataka kuingilia Kanuni ya 47, ikisomwa pamoja na Kanuni ya 48 wewe simama usemee hapo hapo, lakini huwezi ukachanganya hayo kupitia mlango wa Kanuni ya 67(8).

Nasema hivyo kwa sababu nitayajibu haya mengine kwa kutumia Kanuni zetu tu. Kanuni hiyo wote mmeisoma

na wote mnaifahamu, ni kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema siku hiyo ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge. Siku hiyo tumeshaiingiza kwenye maamuzi ya kiti. Tumeshaliamulia na msinirudishe nyuma, nasema kiti kimejaa, tumeshaliamulia mapema siku hiyo. Sasa naendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa mengine hayo sio lazima niyasome. Niimalizie kabisa, ukienda kwenye Kanuni ya 47, wote mnayo hapa, iko wazi. Inasema; "Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zinavyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja ina hatua mbili; kwanza wewe uombe, Kiti kiridhie, halafu kikiridhia, kikuruhusu useme kwa ufupi tu, hoja yako uitoe na iungwe mkono. Huwezi kuwahisha kama mlivyokuwa mnachangia. Kwa maana hiyo, nasema wote mliosimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 mkaiunganisha na Kanuni ya 47 na 48 hamjazingatia taratibu. Kwa hiyo, sina mwongozo unaoombwa kwa masuala hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Dkt. Mollel, Mheshimiwa Nassari, huo ndiyo mwongozo wangu kwa hayo.

Mheshimiwa Haonga, nipo pale pale kwenye Kanuni ya 68(7). Mambo ya jana mimi siyajui. Mimi nataka tuzingatie Kanuni, yaliyotokea mapema leo. Sasa tafuta njia nyingine. Kama Mheshimiwa Haonga unadhani kuna kitu ambacho unataka kifahamike vizuri, tumia tu Kanuni, utapata njia ya kuweza kufikisha ujumbe wako. Huo ndiyo Mwongozo wangu Mheshimiwa Haonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kanyasu, mwongozo wangu ulioombwa, maana Serikali imo humu, kama wewe unataka *assurance* kwamba wananchi wa maeneo hayo sasa wanaweza kuendelea na shughuli zao, nadhani ungelipata

tu kutoka kwa Serikali, uelewa wa jibu la nyongeza ambalo umepewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini. Kwa sababu Serikali imo Bungeni humu, lakini pia tunataka wananchi katika shughuli zinazoendelea za madini na wenyewe wajue hatma yao ni nini. Sasa nadhani mwongozo wangu kwa hilo suala lako litakuwa ni hilo kwa sababu wahusika wako hapa, mnaweza ukapata maelezo mazuri ya kuwafikishia wananchi wetu wa maeneo husika katika Jimbo lako la Geita.

Mheshimiwa Mapunda, nakushukuru kwa *effort* yako *for your industry,* lakini narudi tena kwenye Kanuni. Jibu lilitolewa jana, halijatolewa leo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mapunda Serikali imesikia. Kama kuna utaalam wa namna hiyo kama ulivyoeleza, mimi siyo mtaalam wa mambo ya zege na nini, lakini Serikali inaweza ikaona jinsi gani wanavyoweza kuchukua utaalam wako huo na kama teknolojia hiyo ipo, lakini narudi tu kwenye Kanuni ya 68(7) kwamba suala hilo halijatokea hapa Bungeni. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwongozo wangu kwa suala lako ni hivi, suala lolote likishaamuliwa na Kiti ni uamuzi na huwezi tena mkaanza kuhoji au kutafuta njia ya kurejesha kwa maneno tofauti tofauti. Ni uamuzi umechukuliwa na kama Mbunge aliyeuliza au aliyetaka apate mwongozo hakuridhika na majibu ambayo yametolewa na Kiti, Kanuni ya (5) inaweka utaratibu wa nini cha kufanya kama huridhiki na hiyo. Sasa haya yote yamo ndani ya uwezo wetu, lakini hatuwezi kuwa tunahoji maamuzi ya Kiti. Kiti ndiyo siyo *infallible,* wanaweza wakakosea; lakini ndiyo maana kuna Kamati ya Kanuni za Bunge kwenda wakalinyooshe kule.

Sasa huo ndiyo mwongozo wangu kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba suala likishaamuliwa, huwezi ukalirejesha kwa mlango wa nyuma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumechukua muda wetu mwingi sana kwa masuala haya. Ni masuala mazito na

mazuri ambayo mlitaka mpate mwongozo, lakini narudia, tumieni vizuri Kanuni hizi ili tuweze kufanikisha shughuli za Bunge letu vizuri na kwa ufanisi.

Sasa baada ya kusema hayo, Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI**:

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hamjaanza nina wasemaji ambao nimeletewa hapa, lakini niwatangazie tu mapema mlifahamu hili kwamba hoja iliyo mbele ya Bunge itahitimishwa leo hii mchana. Kwa hiyo, naomba mfahamu kwa upande wa vyama vyote vinavyowakilishwa Bungeni kwamba hali ndiyo hiyo.

Ukweli ni kwamba, ukifuatilia michango ya Bungeni hapa *(discussion)* unaona tunaanza kurudia yale yale. Ni afadhali tukatumia muda huu vizuri hoja hii ikahitimishwa leo. Naomba hilo mlifahamu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza kwa wachangiaji ambao tunao hapa. Nianze na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillah Rahman Rahim.*Nakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwanzo katika siku ya leo katika hotuba iliyo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama walivyotangulia wenzangu na mimi napenda nikukumbushe kwamba kama ambavyo tuliagizwa kwamba tukumbushe hakika ya ukumbusho unawafaa wanaoamini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ulipoapa kuwa Mbunge ulishika Msahafu na kauli yako ya mwisho ukamwomba Mwenyezi Mungu akusaidie na ulipoapishwa kuwa Waziri Mkuu ulishika tena Msahafu na kauli yako ya mwisho ikawa unamwomba Mwenyezi Mungu akusaidie. Na sisi tunamwomba Mwenyezi Mungu akusaidie *inshaallah. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yako ukurasa wa 52 na 53 umezungumzia suala la amani, lakini amani haiwezi kuwa amani ya kweli kama haijasimama kwenye nguzo zake na nguzo kubwa ya amani ni haki, Katiba na kufuata sheria. Ni dhahiri Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ambayo sasa wewe ndiye Kiongozi Mkuu wa Serikali hiyo kwa maana ya Mtendaji Mkuu wa Serikali, Serikali yako au nchi yako unayoisimamia sasa hivi, siyo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya mipaka yetu hatuna vita, lakini ndani ya nchi yetu wananchi hawaishi kwa amani kabisa. Kila mmoja wetu ana hofu ya nini kitatokea baadaye? Kuanzia Mawaziri na watendaji wote wa Serikali hakuna mmoja anayefanya kazi yake akiwa na amani ndani ya nafsi yake akiamini kwamba jua litatua hajatumbuliwa. Wafanyabiashara kuanzia wakubwa na wadogo, hawana amani na biashara zao wakiona kwamba wakati wowote biashara zao zitapotea. Wafanyabiashara wakubwa, wamachinga wenye vibanda vidogo vidogo, anaweza akaamka asubuhi, biashara yake haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomoa bomoa za nyumba, mtu ana nyumba yake amejenga kwa miaka 20, 30 anaishi inakuja kubomolewa ndani ya dakika tano. Watanzania hawaishi kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vifo vinavyotokana na watu wenyewe kupigana, wakulima na wafugaji, wanyama

kufa kwa kukatwa mapanga ama sumu, vimezidi kuendelea katika nchi yetu, lakini njaa inayoendelea kwa sababu mbalimbali za ukame, mafuriko ama wanyama waharibifu na ndege, inazidi kuendelea katika nchi yetu na wananchi wakisema wana njaa majibu ya Serikali yanakuwa hayaeleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi sana, nchi hii siyo salama. Baya zaidi hivi sasa kinachotia hofu ni hii kamata kamata, utekaji na uuaji unaoendelea katika nchi yetu. Wilaya za Mkuranga na Rufiji sasa hivi watu wanapigwa risasi, viongozi wa Chama cha Mapinduzi ambao ni Wenyeviti wa Vijiji wanapigwa risasi, hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanishangaza sana kuona polisi wanatumia nguvu kubwa kuondoa mashamba ya bangi huko, lakini watu wanakufa kwa risasi ndani ya nchi hii. Kwa umri wangu wa miaka 54 sasa sishangai suala la utekaji, wala uwekwaji ndani wa watu, wala kupotea watu wasionekane kama Ben Sanane, sishangai na sitashangaa.

Waheshimiwa Wabunge, haya yalianza Zanzibar. Miaka ya 1964 mwanzoni, akina Abdallah Kassim Hanga, Mlungi Ussi, Abdulaziz Twala, Othman Sharrif na Twaha Ubwa walipotea katika mazingira ya kutatanisha na hadi leo hawajaonekana.

Mwaka 1972 mwasisi wa Jamhuri ya Muungano Abeid Aman Karume amepigwa risasi, akauawa. Kesi ikawa inaoneshwa *live* katika televisheni ya Zanzibar wakati huo ndiyo televisheni ya mwanzo kwa Afrika, ikionesha kesi ile. Mshtakiwa *Mr. 'X'* hajulikani ni nani, kesi ile ikaishia. Wanaotuhumiwa kuwa wauaji wakahifadhiwa na Jamhuri ya Muungano hadi kufa kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeshuhudia kifo cha Edward Sokoine kimeacha maswali mengi sana. Kifo cha Imran Kombe aliyekuwa Mkuu wa Usalama wa Taifa, kapigwa risasi kama ngedere katika shamba lake, lakini pia Horace Kolimba alipotea katika mazingira ambayo yameacha maswali mengi; Balali aliyekuwa Gavana Mkuu wa Serikali kapotea, lakini Wazanzibari hadi leo tunajiuliza kifo cha Dkt. Omar Ali Juma kupotea kule na familia yake imetelekezwa hadi leo.

Kwa hiyo, sishangai Ben Sanane, sishangai kukamatwa kwa Wabunge na watu wengine kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haya ni mazoea! Naona ni utamaduni, kwa hiyo, hili silishangai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninayasema haya kukwambia kwamba Serikali yako pamoja na kwamba unazungumzishwa hapo hunisikilizi, lakini sishangai na napenda tu nikwambie kwamba Serikali yako unayoisimamia ndani ya mwaka mmoja na nusu, haina amani ndani ya nchi yako na ujue kama wewe ukiwa Mtendaji Mkuu wa Serikali iko siku utaulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mtihani, uongozi ulionao ni mtihani; uzima ni mtihani; watoto ni mtihani; madaraka ni mtihani; na iko siko utaulizwa juu ya neema hii aliyokupa Mwenyezi Mungu umeitumia vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadithi fupi tu; Nabii Nuhu aliishi katika dunia kwa miaka 950. Siku anakufa, Mwenyezi Mungu anampelekea malaika wawili kuzungumza naye, anaulizwa, Yaa Nuhu, hebu tupe habari za duniani? Nuhu akasema yeye asiulizwe mambo ya duniani, kwa sababu hakika ya dunia ni kama nyumba, ameingia kwa mlango wa mbele akatoka kwa mlango wa nyuma. Hajui kilichomo ndani. Miaka 950, seuze sisi wenye miaka 60 na 70. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nizungumzie suala hili linaloitwa mgogoro wa Chama cha Wananchi CUF. Chama cha Wananchi CUF hakina mgogoro. Mimi ni kiongozi ndani ya Chama cha Wananchi *CUF*, naingia katika vikao vyote vya Chama cha Wananchi CUF, Chama cha Wananchi CUF kinaendesha vikao na shughuli zake kama kawaida. Unaoitwa mgogoro ambao umepandikizwa na *system* kwa kutumiwa Msajili wa Vyama vya Siasa na Profesa Ibrahim Lipumba, huu sisi hatuuiti mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lake kubwa huu unaoitwa mgogoro kwa kutumia watu hao ni kuzuia haki ya Wazanzibari ya tarehe 25/10/2015. Hawawezi kuzuia haki hii Profesa Ibrahim Lipumba na Msajili wa Vyama na mwingine yeyote kwa sababu ni haki na maamuzi halali ya wananchi wa Zanzibar na haki ya WazanzibarI itapatikana muda mfupi unaokuja. Msijidanganye wala wasijidanganye katika hili, hamuwezi kuzuia haki ya Wanzibari ya tarehe 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kumwambia bosi wangu, keshakimbia eeh, Mheshimiwa Magdalena Sakaya juzi wakati anachangia hapa alisema anawashangaa Wabunge kwamba ni wanafiki. Nataka nimuulize na kwa sababu kakimbia lakini yupo kibaraka mwenzie atamfikishia huu ujumbe, ni nani mnafiki? Yeye akikaa na Profesa Ibrahim Lipumba anasema kwamba...

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, ndiyo Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 68(1) kuomba Kuhusu Utaratibu nikijielekeza kwenye Kanuni ya 64(1) ambayo inamtaka Mheshimiwa Mbunge anapochangia ndani ya

Bunge kuhakikisha kwamba hatumii lugha ya kuudhi wala ya kumdhalilisha Mbunge mwenzake yeyote anapochangia ndani ya Bunge.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utusaidie Mheshimiwa Mbunge anayechangia ikiwezekana afute kauli yake ya kumwita Mbunge mwenzake ni kibaraka ndani ya Bunge hili kwa sababu lugha hiyo inakinzana na Kanuni ya 64(1)(g) ambayo inamtaka Mbunge kutumia lugha yenye staha anapochangia ndani ya ukumbi wa Bunge.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee nashangaa sana pilipili...

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa, nimeombwa kuhusu utaratibu. Kuhusu utaratibu inachukua kipaumbele cha kwanza kwa sababu ndiyo kanuni zinazotuongoza humu.

Waheshimiwa Wabunge, alichosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mhagama kikanuni ni sahihi. Naomba Mheshimiwa Mbunge unayechangia tumia lugha ya staha na usirudie hayo uliyoyasema. Tunaendelea, endelea, maliza muda wako. *(Makofi)*

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mwongozo wako. Ninachotaka kusema, hii pilipili usiyoila sijui yakuwashia nini Mheshimiwa Jenista. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, anapokaa na Profesa Ibrahim Lipumba anasema kwamba Profesa Ibrahimu

Lipumba anamuunga mkono na wako pamoja. Akiondoka Profesa Ibrahim Lipumba anawaita Wachungaji anawaambia nimechoka kutumia pesa yangu, Mwenyekiti akija hapa akiondoka analeta masuala mengine. Nawaomba Wachungaji mwende mkaongee na Seif Sharif suala hili limalizike ili mimi nisitumie pesa zangu, mnafiki ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magdalena Sakaya huyu kaandika barua ya kuomba kukata rufaa baada ya kusimamishwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, kwa sababu anajua taratibu za chama, si mjinga. Kaandika barua ya rufaa, kikao hicho hakijakaa kumjadili leo anakuja hapa *anatutumisha kiuno* kwamba yeye ni Kaimu Katibu Mkuu, kwa Katiba ipi? Lazima ajue kwamba yeye ndiyo mnafiki na suala hili liishie hapa. *(Makofi)* ***[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]***

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nawaambia tena Msajili wa Vyama vya Siasa, mpango wake alioupanga taarifa tunazo asitegemee kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, lakini kuna dakika zangu walizichukua, namalizia kwa kusema kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Kuhusu Utaratibu

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Naomba nimalizie.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Kuhusu Utaratibu. Nasimama kwa Kanuni ya 68(1)...

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Taarifa.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mbunge anayezungumza, amezungumza lugha ya kuudhi, amemkashifu Mbunge aliyemzungumzia Mama Magdalena Sakaya...

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nia yako ni njema lakini sijakuruhusu. Sasa endelea na Kuhusu Utaratibu. *(Makofi)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, kwa kweli kwanza naomba radhi kwa kusimama bila kuniruhusu...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Kuhusu Utaratibu...

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Kwa sababu ni hoja yenyewe iliyotolewa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Kuhusu Utaratibu.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Kwa sababu Mbunge aliyekuwa anazungumza amezungumza lugha ya udhalilishaji. Mheshimiwa Sakaya ni Mbunge na hayuko hapa kwa ajili ya kutingisha hicho alichokuwa anazungumza. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba afute kauli yake mara moja, ni kauli mbaya...

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Inadhalilisha na haifai kuzungumzwa na kiongozi anayewakilisha wananchi. Ahsante.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Usinipe taarifa mimi. *(Kicheko)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Nampa yule.

**MWENYEKITI:** Huwezi kukipa Kiti taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, mimi naendelea kuwasihi turudi kwenye Kanuni tu. Kanuni ya 63 inakataza uongo kabisa, Kanuni ya 64 inasiliba vizuri yale ambayo yanakatazwa ikiwemo la uongo lakini pia kumsema vibaya Mbunge mwenzako. Haya yako ndani ya kanuni zetu sasa Kiti na ninyi lazima mziheshimu kanuni hizi.

Waheshimiwa Wabunge, uamuzi wangu kwa hili, kuanzia sasa mimi ndiyo nimekalia Kiti, Mbunge yeyote ambaye hatapenda kuzingatia Kanuni ya 64 na 63 ninyi kwanza mnisaidie haraka haraka lakini na mimi nitakuwa makini sana kuzisimamia kanuni hizi. Nawasihi sana tutumie lugha ya staha katika kuchangia. Tunaendelea. *(Makofi)*

Mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, naomba nichukue nafasi hii kuwatakia Wakristo wote walio hapa Bungeni na kote Tanzania kila la kheri katika siku hizi kuu za Juma kuu zitakazoanza kesho ili ziwe kwao baraka na neema katika maisha na kazi zao. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kusema kwamba, mimi ni Mbunge wa Rombo na katika siku mbili, tatu zilizopita jina la Ben Sanane limetajwa sana hapa Bungeni. Ben Sanane ni mpiga kura wangu, amezaliwa Tarafa ya Mashati, Kata ya Katangara Mrere, Kijiji cha Mrere na Kitongoji cha Kilosanjo. Baba yake ni Mzee Focus Benard Sanane na mama yake ni mama Arinata Ben Sanane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Rombo tuna uchungu wa hali ya juu sana kwa sababu tangu jambo hili liliporipotiwa watu wa Rombo hususan familia na ukoo wa Mzee Focus Ben Sanane umetahayari, hawajui wafanye matanga, hawajui wafanye nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea kusema ninachokusudia kusema kuhusu jambo hili, nichukue nafasi hii kwa niaba ya Mzee Focus Benard Sanane na Mama Arinata Benard Sanane kutoa shukrani za dhati kwa Wabunge wote, vyombo vya habari, viongozi wote na wote wenye mapenzi mema ambao kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakiomba, wakishinikiza, wakishauri kwamba jambo hili lifanyiwe kazi na Serikali ili tujue mwisho wake. Waheshimiwa Wabunge sisi wote ni wazazi, akinamama mlio Wabunge mnajua uchungu wa uzazi...

**WABUNGE FULANI:** Sana.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mnajua uchungu ambao mama Arinata Benard Sanane anaupata. Mheshimiwa Jenista Mhagama dada yangu, fikiria kwa mfano yule mwanangu Victor angekuwa amekumbwa na sakata kama

hili, ungekuwa katika hali gani, unatikisa kichwa kwa uchungu kwa sababu huu ndiyo uchungu ambao watu wa Rombo wanao, huu ndiyo uchungu ambao mama Arinata anao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Oktoba mwaka jana, kuna mtu aliyejitambulisha kama Joackim, Afisa wa Takwimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo. Alikwenda kwenye Ofisi za CHADEMA pale Wilayani. Baada ya kujitambulisha, akaomba kujua kama Ben Sanane ni mwanachama wa CHADEMA. Akaomba kujua kama Ben Sanane huwa anafika maramara katika Ofisi za CHADEMA. Akaomba kujua nyumbani kwa Ben Sanane na baada kukusanya taarifa alizozitaka mwezi wa Novemba tukasikia kupotea kwake, tupo katika lindi kubwa la mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, niishie tu kusema nawaomba Wabunge, naiomba Serikali, nawaomba na Watanzania wote msifanye jambo hili kuwa jambo la siasa. Jambo hili linaumiza watu, jambo hili lina machungu makubwa miongoni mwa mioyo ya watu.

**MBUNGE FULANI:** Sana.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Nawaomba na nawasihi na Warombo wenzangu wananisikia na familia ya Ben, Mzee Focus na Mama Arinata wananisikia, tunaomba sisi watu wa Rombo Serikali tuambieni chochote ambacho mnacho. Tuambieni kama mmeshindwa tulie, yaishe. Tuambieni kwamba amekufa ili tujue tufanye matanga. Haiwezekani tukakaa kama familia kwenye *suspense* tu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudi kwa Warombo wenzangu katika mambo mengine ya maendeleo yanayowahusu. Katika kipindi hiki cha mwaka, tulipata bahati ya kutembelewa na Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na Naibu wake, waliutembelea mpaka wa Rombo pamoja na shughuli zinazohusu Wizara ya Mambo ya Ndani. Nataka niwashukuru kwa sababu tuumeendelea kutekeleza yale waliyoshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu ya urefu wa mpaka wa Rombo na Kenya, watu wa Rombo wameamua kujenga kwa namna ya kujitolea vituo vya polisi. Kituo cha Ngoyoni, Mahida, Mengwe, Useri na Kirongo Chini. Wamejenga na wanaendelea kujenga kwa kuchangia ili waweze kukaa katika hali ya usalama kwa sababu mpaka unaingiza mambo mengi na unawahusu sana katika usalama wao. Naiomba Serikali katika bajeti hii iangalie namna ya kusaidia hizi nguvu za wananchi ili hivi vituo viweze kukamilika tuweze kupata huo msaada au tuweze kupata hiyo huduma kutoka polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo pia alitembelea Rombo na tunamshukuru. Alitembelea miradi kadhaa, kati ya mradi uliotembelewa ni ujenzi wa jengo la halmashauri. Nimesikia Wabunge wenzangu ambao halmashauri zao ni mpya wakiomba majengo ya halmashauri yajengwe na yakamilike. Rombo ni halmashauri ambayo ina umri zaidi ya miaka 30 lakini haina jengo la halmashauri. Jengo wanalotumia lilitaifishwa kutoka kwa Masista wa Shirika la Masista Kilimanjaro. Ujenzi unaendelea lakini umekwama kwa sababu mkandarasi amekosa fedha. Tunaomba fedha zipelekwe ili kuweza kukwamua ujenzi ambao unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni Hospitali ya Wilaya. Vilevile hatuna Hospitali ya Wilaya. Hospitali ya Huruma ni Hospitali ya Kanisa Katoliki Jimbo la Moshi. Kituo cha afya cha Karume tuliamua kwa makusudi ijengwe hapo Hospitali ya Wilaya, ujenzi unaendelea nao umekwama kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Naomba sana jitihada zifanyike ili jengo hilo liweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji. Waziri wa Maji ametusaidia kuifuta *Kill Water*. Namshukuru Waziri na nimpe taarifa tu kwamba wataalam kwa ajili ya kutusaidia kuanzisha mamlaka wameshafika Rombo wanaendelea na kazi. Naomba msukumo uweze kufanyika ili tupate hiyo mamlaka, kwa Rombo kuna shida kubwa sana ya maji hasa ukanda wa chini. Mamlaka itatusaidia kwa sababu kuna

chanzo cha Ziwa Chala, kuna vyanzo vingine kule Rongai ambavyo tunaambiwa vinapeleka maji Kenya ili kuweza kutatua tatizo la maji katika halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya, ni wataalam katika vituo vya afya. Kwa sababu wananchi wa Rombo wamejitahidi kujenga zahanati na kadhalika tunaomba sana waungwe mkono katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, tuna uhaba mkubwa sana wa walimu wa sayansi. Rombo tuna shule za kata karibu 41 lakini tangu tumeanza shule za kata hatuwahi kupata mwalimu hata mmoja wa sayansi katika baadhi ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maliasili, tunavamiwa sana na nyani, ukanda wa juu. Nimesikia kuna utaratibu wa kuhamisha nyani na kuwapeleka mahali pengine. Tunaomba Serikali ione uwezekano wa kuwasaidia hawa wananchi ambao wanapambana na nyani kila kukicha, wanashindwa kufanya kazi zao kwa sababu ya kupambana na nyani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la njaa. Rombo kwa kawaida tunapata chakula kutokana na mvua za vuli lakini mvua za vuli mwaka huu hazijanyesha. Kwa hiyo, ukanda wa chini wa Rombo sio siri wananchi wana shida kubwa sana ya chakula. Mimi sijatembelea mikoa mingine Serikali inasema nchi ina chakula, naomba ufanyike utaratibu chakula kilicho katika maeneo mengine ya nchi kiweze kusambazwa ili kusaidia wananchi wa maeneo mengine hususan katika Jimbo langu la Rombo. Watu wa Rombo siyo wavivu, akinamama wanalima kila wanapopata fursa lakini jambo ambalo limetufanya tukaingia katika hali hiyo kwa Ukanda wa Chini ni kwa sababu ya hali ya ukame, mvua hazikunyesha tukapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni zao la kahawa ambalo lilikuwa zao la biashara katika Wilaya ya Rombo. Chama cha Ushirika *KNCU* kilitusaidia sana, lakini

kimeingiliwa na mafisadi, wanauza mali za *KNCU*, wameuza magari, nyumba na rasilimali zote za *KNCU* hatimaye wameshindwa kulisaidia zao lile. Matokeo yake gharama za uzalishaji wa zao lile zimekuwa kubwa, kodi imekuwa kubwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba sana Serikali itusaidie katika hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge nimelazimika kusimama, Mheshimiwa Makilagi aliposimama kuomba Kuhusu Utaratibu hakusema maneno fulani, nadhani ametumia busara lakini kisheria ndivyo vizuri alivyofanya, hakuyarudia maneno yaliyosemwa na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein wakati anachangia kuhusiana na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

Niliomba watu wa meza wanitafutie kwa haraka maneno yaliyosemwa, wameniletea, kasema, Mheshimiwa Magdalena Sakaya amekuja kutingisha kiuno Bungeni. Nadhani mimi yalinipita kwa haraka sana. Mheshimiwa upo, mimi nakutaka sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 73(2) ufute kauli yako hiyo ya maneno hayo. Tulimalize vizuri, futa kauli yako, uombe radhi kwa hayo twende mbele. Mheshimiwa! *(Makofi)*

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi uliyonipa. Napenda watu wa *Hansard* kama hawajui Kiswahili basi wajue na hilo neno sijasema...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Hebu nyamazeni, hashuo la nini? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema 'kututumisha', hilo ndilo neno nililosema mie, iangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mimi ni Muislam nikisema naamini ninachokisema, kwa sababu kiongozi wangu umenitaka niondoe hiyo kauli naondoa lakini nililotamka ni neno hilo, wajue Kiswahili vizuri na wasitulishie maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru kwa hilo. Tunaendelea na tunahamia upande wa Chama cha Mapinduzi kwa kufuata orodha mliyonipa. Waheshimiwa mjue kwa sababu ya muda wengi hamtapata nafasi. Kwa hiyo, anayefuata ni Mheshimiwa Amina Makilagi, atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Silanga na Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Vilevile nimshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote, aliyenipa fursa na mimi kuweza kusimama kutoa mchango wangu katika hoja yetu hii iliyo muhimu ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuunga mkono hoja na sababu ninazo. Sababu ya kwanza ni kwamba, tangu Serikali imeingia madarakani imefanya kazi kubwa sana yenye kutukuka. Kama kura zingepigwa leo, ushindi wa CCM ungekuwa 99.999%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kama tutamaliza miaka 10 na Rais huyu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, makofi tuliyompigia juzi Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Wabunge tutasimama juu ya meza kwa kazi anazozifanya. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana unayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa mwaka mmoja Rais umethubutu kutununulia ndege. Ni Bunge hilihili na Wabunge hawahawa walikuwa wanasema na ndiyo maana mimi wakati mwingine huwa nashangaa watu wanakuwa na ndimi mbili; leo wanasema Tanzania haina ndege tunazidiwa na Rwanda, Rais ananunua ndege wanabeza. Waswahili wanasema akutukanaye hakuchagulii tusi na ukiwa kwenye maji unaoga akija mwendawazimu haumkimbizi. Mheshimiwa Rais chapa kazi, tuko pamoja, kazi ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Rais huyuhuyu Mheshimiwa Dkt. John Magufuli amefanya uamuzi wa busara akasema elimu iwe bila malipo kwa watoto wetu. Ni ukweli usiopingika watoto walioandikishwa wamevuka kiwango cha miaka yote iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Rais huyuhuyu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, amethubutu. Kwa miaka mingi tangu nchi yetu imeanza, dhamira ya kuhamia Dodoma ilikuwepo, lakini Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ndiyo ameweza. Hongera sana Rais wetu, chapa kazi, panga Mji wetu wa Dodoma, maendeleo yaendelee na Watanzania wanakuthamini, endelea baba na usiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Rais wetu huyuhuyu aliyesikiliza kilio cha Wabunge cha muda mrefu kwamba, mapato mengi ya Tanzania yanapotea, akaziba mianya yote ya upotevu wa mapato. Si Rais mwingine ni Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Rais huyuhuyu ambaye Wabunge na wengine nawaona wako humu ndani, tulipaza sauti tukasema Rais apunguze safari za kwenda nje ya nchi. Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amepunguza, Wabunge hatuendi nje ya nchi, Rais haendi nje ya nchi, watumishi tuko humu ndani, gharama za kuendesha Serikali

zimepungua. Ni Wabunge ndio tulioshauri ndio maana mimi wakati mwingine nashangaa kuona watu wenye ndimi mbili. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana unayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Rais huyuhuyu ambaye tulimtaka aangalie mishahara hewa. Amedhibiti na leo tunashuhudia jinsi anavyokabiliana na mishahara hewa, wakiwemo watumishi hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kueleza mafanikio ya Serikali hii ya Awamu ya Tano tutalala hapa. Kama tungeanza kuandika kitabu, Mheshimiwa Rais kwa mwaka huu mmoja ameshafanya mengi ambayo kwa kweli Watanzania na hasa wanawake ambao mimi nawawakilisha, zaidi ya milioni 50 wanawake walioko hapa wamenituma nije kusema wanamshukuru sana Rais, achape kazi na timu yake akiwemo Makamu wa Rais Mheshimiwa Mama Samia, kijana Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu, Mheshimiwa Jenista na Baraza lote la Mawaziri na Watendaji wote wa Serikali msirudi nyuma, songeni mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli unabaki palepale ndiyo maana watu sasa wamekosa hoja, tunaanza sasa kuzungumza watu, hatuna cha kusema. Ndiyo maana kila mtu anayesimama anazungumza mtu badala ya kuzungumza maendeleo ya wananchi kwa sababu Mheshimwa Dkt. John Magufuli amefuta na hakuna mtu mwenye swali kwa Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapoona Wabunge sasa wanaacha kujadili matatizo ya wananchi, binafsi nafurahia kwamba Serikali sasa inasonga mbele, kero zimeisha na ndiyo maana tunaanza kuzungumza mtu mmoja-mmoja badala ya kuzungumzia matatizo ya wananchi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee na mchango wangu, nizungumze mambo machache ambayo nimejielekeza kuyachangia kama ifuatavyo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makilagi, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Msemaji anayesema, amepongeza kwamba Rais amenunua ndege, tunashukuru kwa hilo. Naomba zifanyiwe marekebisho kwa sababu wakati wanaenda kumzika Mzee Sitta, kweli tumeona *Bombadier* ndege mpya lakini zahitaji kuwekewa *television,* kwa hiyo, tutaishauri Serikali iweke *television. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makilagi, taarifa!

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa taarifa nzuri, ndege zinahitaji *television*. Si jambo baya, ndege zijazo tutakazozinunua miaka ijayo tutaweka *television* ili Wabunge mfurahie matunda yenu. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zile nyingine zinazokuja tutaweka *television* mtembee raha mustarehe kwa sababu Mheshimiwa Dkt. John Magufuli amedhamiria. Ahsante sana kwa taarifa nzuri.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze katika mchango wangu...

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu, Kanuni gani?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Kanuni ya 68(1).

**MWENYEKITI:** Kinasema nini?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinasema:-

*"Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno "kuhusu utaratibu", ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atampa Mbunge aliyedai Utaratibu kwa kutaja Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa."*

**MWENYEKITI:** Kanuni iliyokiukwa ni ipi?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Kanuni ya 64(1)(d) inasema: "Hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala, au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani".

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri umenielewa ninachokisema. *It is whether in a negative way or in a positive way.*

**WABUNGE FULANI:** Aha aha.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mchangaiji anachokifanya hapa anatumia jina la Rais kushawishi ili Wabunge waunge mkono bajeti hata kama walikuwa na mpango wa kuipinga.

**MBUNGE FULANI:** *Yes.*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Anadanganya Bunge kwa sababu hoja anazozitoa hajaanza yeye, wamekuwepo Marais wengine. Hoja ya elimu bure imeanza na Mheshimiwa

Jakaya Mrisho Kikwete, sio yeye Rais Magufuli, watu tunafahamu sera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kama mchangiaji anachangia achangie *in a way* kutokutumia jina la Rais...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anatupotezea muda huyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Makilagi amechangia kuelezea hali halisi ya mambo yaliyofanywa kutekeleza Ilani. Huwezi ukasema anataka kushawishi Bunge.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Anashawishi.

**MWENYEKITI:** Hapana! Huo ndiyo uamuzi wangu, endelea Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ndio maana mimi nasema watu wenye ndimi mbili. Ni Mheshimiwa Kikwete huyuhuyu walisema alikuwa hafanyi kitu, leo hapa mtu anasema haya yalifanywa na Mheshimiwa Kikwete. Ahsante sana kwa kutambua kwamba na Mheshimiwa Kikwete alitoa hayo mawazo ya elimu bure. Ahsante Mheshimiwa Waitara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze katika mambo matatu ambayo nimeyapanga kuyatilia mkazo. La kwanza, nimejipanga kuelezea uwezeshaji wa wananchi na la pili, masuala ya maji, sekta ya afya na kama muda utaniruhusu nitazungumzia kidogo elimu na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 15 - 17 Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kwa kina jinsi ambavyo Serikali ya CCM ina dhamira nzuri sana ya kuwawezesha wananchi. Hapa naomba nishauri katika maeneo machache ambayo nimeyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika kuwawezesha uchumi wanawake na vijana. Naomba nitoe ushauri kwa Serikali, nimejaribu kupekua kwenye hivi vitabu, sijaona ile milioni 50 katika kila kijiji. Ningependa kumwomba Waziri Mkuu, atakapokuja kusimama hapa mbele yetu hebu atuambie hii milioni 50 iko wapi? Maana Bunge lililopita tulipitisha zaidi ya bilioni 50 kwa ajili ya kupeleka kwenye vikundi vya wananchi vya kiuchumi. Napenda Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja hapa atuambie ziko wapi na zinatoka lini na utaratibu wa kutoa mikopo hii utakuwa ni nini na wanawake na vijana na wananchi kwa ujumla waweze kushiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimepekua katika vitabu vyote ambavyo tumepewa, sijaona ule Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Ni ukweli usiopingika kwamba wanawake ndiyo wazalishaji wa Taifa hili, ndiyo nguvu kazi, ndiyo wenye vikundi, ndiyo walezi wa familia, ndiyo wajasiriamali, lakini kwa bahati mbaya sana ule mfuko ambao ulikuwa ndiyo ukombozi kwa wanawake siuoni katika vitabu hivi. Napenda kumwomba Waziri Mkuu atakapokuja atuambie hivi mpango ni nini katika suala zima la kuwakomboa wanawake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama mfuko haujawekwa, hatujachelewa. Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itakuja. Turejee Mheshimiwa na Kamati ya Bajeti itusaidie fedha hizi ziingie kwa ajili ya wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni 5% ya Vijana na Wanawake inayotokana na Halmashauri zetu. Kwa bahati njema mimi niko kwenye Kamati ya *LAAC,* nimejionea kwamba Halmashauri nyingi hazitengi fedha. Nimefanya utafiti nimegundua kwamba hawatengi fedha kwa sababu, hakuna sheria. Wanatekeleza Waraka wa Waziri Mkuu tena wakati ule alikuwa Mheshimiwa Sumaye, ni muda mrefu sana. Naishauri Serikali, hebu ilete sheria hapa Bungeni tutunge sheria itakayoweka masharti ya kutenga fedha hizi kwa ajili ya halmashauri ziende kuwakomboa wanawake na vijana

kwa sababu wameanzisha vikundi vingi sana, hawana uwezo wa kufikia vyombo vya fedha na huu mfuko peke yake ndiyo ukombozi kwa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie masharti ya vyombo vya fedha. Kuna taasisi za *FINCA, PRIDE* na mabenki mengine wanatoa mikopo, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri wanayofanya. Naiomba Serikali iweke riba elekezi kwa sababu baadhi ya taasisi zinatoza riba kuanzia 1% - 35%. Hawa wanawake na vijana wanashindwa kurudisha huo mkopo matokeo yake wananyang'anywa magodoro na vitu vyao vya ndani. Badala ya mkopo kumsaidia yeye unamsaidia yule aliyemkopesha fedha. Hebu Serikali chukueni ushauri wangu, wekeni riba elekezi ili wanawake na vijana waweze kunufaika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Njalu Silanga atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Joseph Mhagama ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri wanayoifanya. Watanzania tunaamini na tunaotoka vijijini, Awamu ya Tano ni awamu ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika sekta ya uwezeshaji, ukurasa wa 19. Niipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu kwa jinsi walivyobainisha kuhakikisha viwanda vinafanikishwa katika nchi yetu hii. Kuna mashirika sita ambayo yameorodheshwa hapa na huu utakuwa muarobaini wenye kuleta ajira kwa vijana wetu nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la viwanda linahitaji malighafi. Nitaenda katika ukurasa wa 21, sekta ya kilimo. Sisi tunaotoka Simiyu na Mkoa wa Shinyanga na Kanda ya Ziwa kwa ujumla ni wakulima wa pamba, alizeti, mahindi na vitu vingine. Katika viwanda hivi ili viweze kuendelea, naiomba Serikali iweze kutumia kila njia inayowezekana kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wakati ili hivi viwanda viweze kufanya kazi vizuri kwa muda mrefu na vijana wetu waweze kupata ajira kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na mwenzangu aliyemaliza kuzungumza kwamba Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa sana. Ukienda kwenye Idara ya Maji, *target* ya mwaka 2015/2016 tulikuwa tumejiwekea malengo ya kukamilisha miradi 1,301 lakini hivi sasa tuna miradi 1,801 na bado miradi 509. Mungu atupe nini Chama cha Mapinduzi kwa mambo mazuri yanayofanyika haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi wa kutoka Ziwa Viktoria ambao utahudumia vijiji takribani 253. Niiombe Serikali iendelee kuharakisha kwa maana ya Mji wa Gangabilili pamoja na Bariadi ambako unatoka Mheshimiwa Mtemi Chenge ili wananchi hao waweze kupata maji safi na salama kwa sababu, mji wetu unakua kwa kasi na mahitaji ni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yoyote utakayoyafanya mazuri lazima ukosolewe tu. Serikali ya Awamu ya Tano inafanya mambo makubwa sana, leo hapo Morogoro keshokutwa kuna reli inaenda kuzinduliwa ya kilometa 160 kwa saa moja. Ni maajabu ya nchi hii lakini bado watu tunalalamika. Mungu atupe nini ili tujue Serikali inapiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujifunze Waheshimiwa Wabunge kuishauri Serikali kwa maana ya maendeleo na pale inapokosea tuiambie. Mimi ninakotoka Wilayani kwangu Itilima kuna bwawa lilikuwa limejengwa tangu mwaka 2002, hela zinakwenda na zinapotea. Leo hii Serikali ya Awamu ya

Tano bwawa lile limejengwa kwa miezi minne, ni maajabu! Serikali ifanye nini na maji yanaendelea kupatikana katika maeneo haya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kwenye shule za sekondari na shule za msingi, ukifika maeneo ya kule utadhani umeingia Chuo Kikuu cha *UDOM,* wakati ni kijijini. Serikali ya Awamu ya Tano imeungwa mkono na Watanzania wote na tuendelee kutia moyo pale Mheshimiwa Rais anapotoa maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anaungwa mkono na Watanzania. Kulikuwa na tatizo la madawati, amezungumza, wananchi wote wa Tanzania wameitikia na wametengeneza madawati ya kutosha na watoto wetu sasa migongo haiugui. Ni kwa sababu wanapata elimu iliyo safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme. Sisi sote ni mashahidi tunakotoka umeme sasa hivi unamulika mpaka mafisi, hata uchawi utaanza kupungua. Ni kwa sababu ya maendeleo hayahaya katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Silanga. Tunaendelea na Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama na Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kipekee namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai kwetu sote tulio hapa, ambao tunaweza kushiriki katika mjadala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imetupa dira ya nchi yetu inakoelekea kwa

kazi zilizofanyika pia mwaka mmoja katika awamu hii ya uongozi wa Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Natoa pongezi kwa uongozi mzima na namshukuru Mungu kwamba nchi yetu iko salama na tuko tayari sasa katika kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kuzungumzia suala zima la ajira. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ametueleza kwamba vijana wapo wengi na wamepelekwa mafunzo lakini katika hao vijana aliotueleza wamepelekwa kwenye mafunzo hatukuambiwa lengo lilikuwa ni kiasi gani. Tumeweza kupewa takwimu pale kwamba vijana waliopelekwa mafunzo katika kipindi hiki walikuwa wawe vijana ambao watarudi ili waweze kuwa wameandaliwa vizuri, lakini je, lengo lilikuwa ni vijana wangapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata hofu kwa kasi ya maendeleo. Naona kwamba kwa *speed* tunayoenda siamini kama endapo hatutaongeza kasi tutaweza kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Nasema hivyo nikiwa na maana kwamba, pamoja na kuwa na rasilimali nyingi katika nchi yetu, rasilimali kubwa sana ni rasilimali watu lakini watu hawa lazima waandaliwe na waandaliwe vizuri ili wanapohitajika watumike vizuri. Kwa hiyo, naomba au nashauri Halmashauri zote ziweze kujua hawa vijana walio katika umri wa kufanya kazi wameandaliwa kiasi gani? Nikifika hapo nataka nisisitize tu kwamba tuwe na takwimu sahihi za kuweza kujua ni wangapi na wanapelekwa vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni bei kupanda hasa za vyakula. Muhimu zaidi nikienda kwenye ukurasa wa 21 inapozungumziwa kilimo, sikuona walipozungumzia kilimo au upatikanaji wa sukari katika nchi yetu. Sukari ni bidhaa ambayo imekuwa ikipanda bei kila mwaka. Sukari ni bidhaa ambayo inatumika kila siku kwenye nyumba na kwenye familia. Sukari ni kitu ambacho tunaita ni kifungua kinywa, maeneo mengine kama ninakotoka ukitaka baraka, basi unampelekea bibi

au babu sukari na anakubariki. Sukari imekuwa ni tatizo inapopanda bei na hasa tunapoelekea kwenye kipindi cha mfungo wa Ramadhani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kama huu mwaka jana sukari ilianza kuadimika na mpaka sasa sijui kama Serikali imeshapata ufumbuzi kwamba mwaka huu sasa ifikapo mwezi Mei wakati wenzetu watakuwa wanafunga, sukari hiyo itabakia na bei ileile ili kila mtu afuturu kwa raha. Mara nyingi unakuta familia ambazo ni duni, wanafuturu kwa uji wa chumvi. Kwa kweli, katika nchi kama Tanzania haipendezi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, kipindi kama hiki, kabla hatujafikia ule wakati ambapo, nadhani sasa hivi viwanda vimefungwa tayari lakini Serikali iwe imefanya mpango mahsusi wa kuona kwamba, akiba ipo, wamewakutanisha wenye viwanda, waagizaji na wale wafanyabiashara wakubwa. Jukumu la kuagiza sukari litolewe kwa wale wenye viwanda. Hii inayokuja ghafla, sukari inaagizwa na watu ambao wapo tu, wafanyabiashara wamekaa tu wanangojea ili watupige bei siyo jambo zuri kabisa. Naomba hilo liangaliwe kwa sababu kila mtu ana haki ya kupata kifungua kinywa katika nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mbegu za mazao mbalimbali kwa wakulima wadogo. Hapa ndani ukizungumzia mbegu zinazozungumziwa sana ni korosho, kahawa, mahindi na mtama yaani zile *cereals.* Hata hivyo, sasa hivi tunazungumzia pia kilimo cha mihogo na viazi, sijasikia wala sikuona katika hotuba ya Waziri Mkuu akizungumzia tutapataje sasa mbegu ya viazi vitamu na mbegu nzuri ya mihogo katika Halmashauri zetu. Kwa sababu haya ni mazao mbadala na yote ni ya wanga lakini ikipatikana mbegu nzuri basi tutakuwa katika hali nzuri sana ya kuweza kuwa na mazao mengi ya kutosha na tutaweza kusahau hayo mambo mengine ya njaa. *(Makofi)*

Naomba nizungumzie jambo lingine kuhusu wanawake wetu na inavyozungumzwa katika Ilani ya CCM

kwenye ule ukurasa wa 117, ibara ya 61, 62 na 63(a),(b), (c), (d) na (e), kuwawezesha wanawake kiuchumi. Imewekwa vizuri sana katika Ilani na imezungumzwa jinsi gani watasaidiwa au wataelekezwa kuwa na vikundi kama *VICOBA* na *SACCOS* lakini inapokuja kuwapa elimu wanaachiwa. Unakuta wanawake wako kwenye *VICOBA* lakini mwanamke mmoja anakuwa kwenye *VICOBA* zaidi ya kimoja akiamini kwamba nikivunja mzunguko hapa nitapokea mwingine na mwingine, hiyo ni dhana potofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwasiliane na vyuo au watu wanaotoa elimu ili wanawake wetu waweze kupatiwa elimu ya ujasiliamali na uwekezaji. Ukimuelimisha mwanamke umeelimisha familia nzima. Mwanamke akiwa na elimu ya kufanya ujasiriamali ambao unaeleweka, akiwa na elimu ya kuwekeza na hivi leo umetueleza hapa kwamba tutapata semina ya hisa na mwanamke huyo huyo akiwa na elimu ya hisa basi atakuwa amefungua milango ya kupata kipato ambacho kitakuwepo siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu sikivu na Tukufu itoe fursa kwa wanawake kupatiwa elimu na wasimamiwe na Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum. Wabunge hawa wa Viti Maalum wana muda wa kuzunguka mikoani na kwenye Taifa zima kuona kwamba wanawake hawa wanapata elimu. Tunaomba Serikali iweze kuzungumza na taasisi na vyuo mbalimbali, wanawake hawa wapatiwe elimu ambayo ina muendelezo, elimu ambayo kila leo watajua nikiwekeza hivi ni benki au kwenye hisa naweza nikasimama na nikawa nimeimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niseme kwamba jambo hili la elimu bila malipo limeleta faraja kwa wazazi wengi. Kuna wazazi ambao walikuwa hawawezi kupeleka watoto wao shule lakini sasa mtoto akiandikishwa akienda shule ana uhakika wa kusoma kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ninayoiona hapa wadau wengine wa elimu wamerudi nyuma, hilo neno bure limeleta shida. Maana yake ni kwamba mpeleke mtoto wako shule atapatiwa elimu bila malipo lakini haikutoi wewe mzazi kutokununua *uniform*, kumlisha mtoto wako na kutokuangalia uhakika wa vitabu vya mtoto wako, madaftari na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni jinsi gani tutaelimisha wananchi wetu waondoe hiyo dhana potofu kwamba elimu ni bure basi mtoto akishaandikishwa wewe mzazi usiangalie tena, hivi kweli? Hata mbwa anazaa mtoto wake anamtunza, anamtafutia maziwa, anajua saa za kunyonyesha sembuse mwanadamu mwenye utashi, akili na anayetawala vyote, anashindwaje kujua kuwa mwanangu anatakiwa kula? Hii ni dhana potofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba itolewe elimu kumwambia mtu sawa Serikali itakupa mwalimu, itatoa vitabu vya kufundishia na itahakikisha mwanafunzi anafika shuleni na anasimamiwa lakini wewe ukiwa kama mdau unatakiwa uchangie mambo yafuatayo na usikwepe majukumu. Hakuna mzazi anayezaa mtoto wake amuache hivi hivi. Naomba sana nyie Waheshimiwa Wabunge tushirikiane pamoja kutoa elimu hiyo lakini pia na Serikali iendelee kuelimisha kila wakati ili wajue kwamba wanawajibika na wanatakiwa kuendelea kutoa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba nizungumzie suala la ajira. Vijana wengi wanamaliza vyuo na kuhitimu lakini wanatarajia kupata *white collar jobs* na kweli siyo wote wanaweza kwenda kulima. Pia wale wanaotaka kulima kama wanatokea eneo ninalotokea mimi Kilimanjaro wala hakuna ardhi ya kilimo. Niombe kama Serikali imejipanga vizuri iko tayari sasa kufungua maeneo mapya kwa vijana ambao wanamaliza vyuo waweze kupatiwa ekari za kwenda kufungua mashamba darasa ambapo pia yatakuwa ndiyo maeneo yao ya kuishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya kugawa vihamba yamekwisha, vihamba havipo tena na vijana ni wengi, nchi hii ilikuwa na watu wachache sasa hivi tupo karibu milioni 50. Nashauri na napenda sana watu wapate baraka wazae watoto wengi tu lakini na nchi yetu ihakikishe kwamba watoto hao wanapatiwa mahali pa kukaa na mahali pa kujiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema ni mwisho lakini sitaitendea nafsi yangu haki kama sitazungumzia suala hili la tabia nchi na jinsi ya kuboresha mazingira. Naomba sana wote tuwe tayari sasa kuotesha miti.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru wewe lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja kati ya Wabunge waliobahatika kuwa katika Kamati ya Katiba na Sheria, Kamati ambayo inafanya kazi kwa karibu sana na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara zote zilizopo chini yake. Tumebahatika kujua mambo mengi na kujifunza mengi na nikuthibitishie kabisa kwamba Ofisi hii na Wizara zake zote wapo vizuri sana katika kuwatumikia Watanzania. Nikuombe wewe na Bunge zima kuunga mkono jitihada za Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa kuzingatia muda naomba nijikite kwenye eneo moja muhimu sana ambalo linagusa asilimia 90 ya Watanzania ambalo liko katika ukurasa wa 21 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu kulimo. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya 2012 asilimia 85 - 90 ya Watanzania tunaishi kwa kutegemea kilimo au moja kwa moja, kibiashara au kwa namna nyingine lakini asilimia 90 ya Watanzania tunategemea kilimo. Kwa mujibu wa sensa ya kilimo na mifugo ya hivi karibuni inatupa takwimu hizo za asilimia 85 - 90 lakini sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 inatueleza idadi ya Watanzania ambao tupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 21 kwa taarifa tulizonazo, uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa mwaka 2015/2016 ukijumuisha mazao ya nafaka na yasiyo ya nafaka tumezalisha jumla ya tani milioni 16. Tani hizi milioni 16 maana yake zimezalishwa na asilimia 85 ya Watanzania kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012. Kama hivyo ndivyo maana yake kila Mtanzania anayetegemea kilimo amezalisha tani 0.34 au sawa na gunia nne tu za mahindi kwa mwaka mzima wa 2015/2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunaambiwa ziada ya mazao ya nafaka na yasiyo ya nafaka ni tani milioni tatu. Tukizigawa kwa idadi ya Watanzania wanaotegemea kilimo ambao ni asilimia 85 tunapata ziada ya tani 0.07 ambayo sawa na gunia moja tu la ziada. Kwa hiyo, ukiangalia kwa takwimu hizi maana yake Watanzania tunaotegemea kilimo asilimia 85 - 90 kila kaya au kila mtu amezalisha gunia nne za mahindi na ametumia gunia tatu kwa chakula na amebaki na ziada ya gunia moja. Tanzania ya viwanda hatutaweza kuifikia kwa kasi hiyo ndogo kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kwa nini asilimia kubwa ya Watanzania hatuna pesa mifukoni ni kwa sababu ziada yetu ni ndogo sana tani 0.07 kwa maana ya gunia moja tu la mahindi kwa mwaka mzima sawa na Sh.35,000 – Sh.50,000. Ziada hii ni ndogo maana yake kilimo katika Taifa letu kinakua taratibu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tumefika hapo? Kwa nini uzalishaji wetu uwe mdogo kiasi hicho? Tani milioni 16 za chakula siyo jambo la kujivunia. Tumefika hapo kwa sababu kubwa mbili. Moja, kilimo chetu hakina dira. Watanzania na taifa hatujui kwenye sekta ya kilimo tunatafuta nini. Tuna maneno ya jumla ya kusema kwamba tunataka ku-*address food security, very good.* Kwenye *food security* tumefaulu, Tanzania hakuna njaa mgawanyo wa chakula ukiwa vizuri kila kaya ina uwezo wa kujilisha, kwa hiyo, kwenye hilo tumefaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini malengo yetu kwenye sekta ya kilimo siyo ku-*address food security* pekee. Sekta ya kilimo pamoja na kuwa inakwenda ku-*address food security* kwa maana ya uhakika wa chakula, sekta hii ya kilimo inawaajiri Watanzania asilimia 90. Kwa hiyo, lazima tutoke hapo kwenye *food security* twende sasa kukifanya kilimo chetu kiwe biashara na kiwe chanzo cha mapato kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Serikali tumefanya vizuri kwenye suala zima la uhakika wa chakula lakini bado tuna kazi sasa ya kuwafanya asilimia 85 - 90 ya Watanzania wanaotegemea kilimo waweze kujiajiri katika sekta hiyo. Kwa hiyo, ni vizuri sasa Wizara ya Kilimo itoe dira ni nini kama Taifa tunataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni kwamba kilimo chetu siyo *demand driven,* hatulimi kwa kuzingatia mahitaji ya soko. Kama tunataka kujitosheleza kwa chakula tulime mazao gani na kwa kiwango gani, uwezo wetu wa ndani wa ku-*consume* kile ambacho tunazalisha ni upi na ziada tunaipeleka wapi. Tumeona sekta ya kilimo inayumba sana kwenye eneo la masoko. Mara tunafunga mipaka tusipeleke mazao nje, mara tunafungua mipaka, hatuna uwezo wa ku-*forecast production* zetu katika sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni tatizo na napenda sana Wizara inayohusika ichukue muda wa kutosha

kufanya *consultation* na wataalam mbalimbali lakini hasa na Wabunge wa Bunge hili kwa sababu Wabunge hawa ndiyo wanaoishi na wananchi, ndiyo wanaojua matatizo ya wananchi na sisi ndiyo tunaolima mahindi, maharage, mpunga, soya na kadhalika. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Na tangawizi.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pili kwenye sekta ya kilimo ni uwezeshaji katika sekta hii umekuwa mdogo sana na uwezeshaji huu wakati mwingine umekuwa holela usiozingatia mahitaji halisi. Serikali imebeba mzigo mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba Watanzania tunapata pembejeo zenye ubora ikiwemo mbolea na kadhalika na zinakwenda kusaidia kuzalisha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia mwelekeo wa bajeti kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianzie alipoishia Mheshimiwa Mhagama kwenye suala zima la kilimo. Naanzia hapo kwa sababu huyu ni pacha mwenzangu naye anaendesha kilimo cha tangawizi kama ambavyo mama yetu Mheshimiwa Anne Kilango amesema sasa ni zamu ya tangawizi. Napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba kule Mlalo, Kata ya Mbaramo, Lunguza, Mnazi na lakini kule katika Jimbo la Madaba na Jimbo la Same Mashariki na

Same Magharibi kule ndiko tangawizi inalimwa kwa kiasi kikubwa. Tena sisi tunalima ile tangawizi ambayo ni kilimo hai, tunatumia mbolea ya samadi ambayo inakubalika hata kimataifa. Kwa hiyo, kwa kuungana pamoja na mama yetu Mheshimiwa Anne Kilango naamini jambo hili litapiga hatua kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa hatuwezi tukawa na kilimo endelevu kama hatutawekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo ni kwamba ni asilimia moja tu ya ardhi yote ya Tanzania ambayo ni kilimo cha umwagiliaji. Ina maana Serikali inapaswa kuja na mikakati madhubuti kuhakikisha kwamba sasa kilimo chetu kisitegemee mvua. Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi mvua zetu zimekuwa sio za uhakika tena. Kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba tunawekeza miundombinu ya mabwawa katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri zetu ili kilimo hiki kiende kutoa ajira iwasaidie Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo wakati mwingine namshangaa Waziri wa Viwanda na Biashara kwa sababu viwanda anavyozungumza bado haviendi kutatua tatizo kubwa la ajira. Tunahitaji tupate viwanda ambavyo ni shirikishi, viwanda ambavyo vitasaidia kunyanyua soko la bidhaa za mazao. Tukiwa na viwanda vya vigae na malighafi hizi za ujenzi pekee bado wananchi hawa hawatakuwa na uwezo wa kununua hivyo vitu lakini bado hatutatatua tatizo la ajira. Kilimo pekee... *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie tu Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Shangazi...

**MWENYEKITI:** Keti Mheshimiwa, endelea.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie kwamba hivi viwanda anavyovitaja ikiwemo kiwanda cha vigae, kile kilichopo pale Mkuranga kinatumia zaidi ya asilimia 95 ya malighafi ya ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Malighafi hiyo inatoka Kisarawe, Kilindi kwa Mheshimiwa Kigua na nyingine inatoka palepale Mkuranga. Ni aina ya udongo unaopatikana ndani ya nchi yetu wenyewe, wanauza Watanzania wenyewe na ajira ni za Watanzania wenyewe. Atafute maneno mazuri zaidi ya kumhamasisha Mheshimiwa Waziri wa Viwanda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi unasemaje kuhusu taarifa hiyo?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo ni nzuri lakini mimi sikuwa nazungumzia kiwanda kimoja *specific,* nilikuwa nazungumzia kwa maana ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninavyozungumza pale Tanga pana kiwanda kinaitwa *AFRITEX* kilikuwa kinatengeneza nguo, ni mwaka wa pili sasa kimefungwa. Mheshimiwa Waziri kila anaposimama anazungumzia viwanda vipya, hivi vya zamani vinavyokufa anavisimamia kwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia Kiwanda cha Nguo tunamaanisha kwamba wakulima wa pamba ndiyo watakaoweza kulisha pamoja na kupata soko kupitia viwanda hivi. Kiwanda cha *AFRITEX* pale Tanga kilikuwa kimeajiri watu zaidi ya 2,000 sasa hivi watu wale hawana ajira. Kwa hiyo, lengo langu ni kusema kwamba, pamoja na ajira za viwandani lakini pia ajira hizi zitokane na mazao yanayozalishwa na wananchi katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Kiwanda cha *Rhino Cement* palepale Tanga kina tatizo la kupata malighafi.

Tatizo lile ambalo alikuwa anakumbana nalo Dangote, *Tanga Rhino Cement* pia wana shida hiyohiyo. Malighafi wanayopata kutoka kwenye makaa ya mawe kule haitoshi. Uwezo wa kiwanda ni mahitaji ya malighafi tani 20,000 kwa mwezi lakini hawana uwezo wa kupata tani hizo wanaendesha kiwanda mara moja kwa wiki na kiwanda kile wakisimamisha uzalishaji kwa siku moja ina maana ajira zaidi ya watu 700 zitatetereka. Kwa hiyo, pamoja na hiyo nia nzuri lakini tunaomba kwamba viwanda vilivyopo pia viweze kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Chai Mponde, ni mwaka wa tano sasa hakifanyi kazi kiko kule Bumbuli. Kwa taarifa yako Jimbo la Bumbuli lina kata 18, kata 15 zote wanalima chai lakini ni mwaka wa tano sasa kiwanda kimefungwa, wananchi hawana shughuli zozote za uzalishaji kule. Maana yake ni kwamba hata Halmashauri sasa haiwezi kupata mapato kwa sababu ndani ya Halmashauri yenye kata 15 zinazolima chai, leo chai ile haina soko kwa sababu kiwanda kimefungwa. Mheshimiwa Mwijage anafahamu, Ofisi ya Waziri Mkuu hili wanalifahamu, kwa sababu *PPF* na *NSSF* wamekwenda kule lakini mpaka sasa hivi hakuna matumaini. Mheshimiwa Mwijage, sisi ni wajomba zako kule, tunakuomba utunusuru katika hili, Kiwanda cha Chai Mponde kifunguliwe ili wananchi wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Kiwanda cha Sabuni cha Foma pale Tanga. Kiwanda hiki kimenunuliwa na mwekezaji Haruna Zakaria lakini amekifunga, kimepoteza ajira zisizopungua watu 1,000. Tunaomba Serikali ikae na mwekezaji huyu kujua kwa nini amekinunua kiwanda na amekifunga, kwa sababu mitambo ipo pamoja na nyenzo nyingine zote zipo pale lakini amefunga. Sasa inawezekana wakati mwingine ni mambo haya ya kodi lakini ni vizuri sasa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana akaenda kukutana na watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niongelee suala la miundombinu ya barabara katika Mkoa wetu wa Tanga. Mkoa wa Tanga, Wilaya za Pangani na Handeni ni

sehemu ambayo Mbuga ya Saadani pia inapatikana, siyo kwamba Saadani inapatikana kwa Wilaya ya Bagamoyo pekee. Ili tuweze kuimarisha utalii katika Mkoa wa Tanga, ambapo pia kuna Mbuga ya Hifadhi ya Mkomazi iliyopo katika Wilaya za Kilindi na Lushoto kwa upande wa Tanga, ni lazima sasa ile barabara ya kutoka Pwani - Pangani - Tanga iunganishwe na barabara ya kwenda Maramba – Bombomtoni – Mlalo - Same Mashariki iweze kunyanyuliwa. Hii barabara iko chini ya Wakala wa Barabara wa Mkoa, tunaomba sasa ianze kufikiriwa kuingizwa katika mpango wa kuwekewa lami. Sambamba na hilo, barabara ya kutoka Lushoto - Mlalo – Mnazi - Same kule Ndungu kwa mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango pia lazima na yenyewe ifikiriwe kwanza kuwekwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayazungumza haya kwa sababu uzalishaji mkubwa wa mazao ya mbogamboga na matunda katika Wilaya ya Lushoto unategemea sana barabara. Inawezekana kabisa kwamba kama kutanyesha mvua barabara ikasumbua ndani ya siku moja unaweza ukamtia mtu hasara kubwa sana kwa sababu mazao haya yanaharibika kwa haraka. Kwa hiyo, mpango pekee ni kuhakikisha kwamba barabara hii inawekewa lami ili iweze kuwa na uhakika wa kufikisha mazao ya wananchi masokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niongelee suala la *MIVAF*. Tumetembelea miradi mbalimbali iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kule Pemba na Unguja. Nishukuru kwamba *MIVAF* ni mradi ambao umesaidia sana lakini unakwisha mwaka huu mwezi Desemba. Niiombe Serikali, kuna tetesi kwamba andiko la miradi hii lipo kwenye Ofisi ya Wizara ya Fedha, tunaomba sasa wasisite waweze kuhakikisha kwamba wanasaini hii mikataba ili angalau tuweze kupata na *MIVAF II*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kule Jimboni Mlalo, tulipata mradi mmoja wa soko kupitia *MIVAF* lakini nasikitika kusema kwamba soko lile ni dogo sana. Sisi uzalishaji wetu wa viazi, Mheshimiwa Mhagama ni mkubwa

sana, tunazungumzia takribani fuso 40 kwa kila wiki zinaingia Dar es Salaam. Bila Lushoto Dar es Salaam chipsi zitakuwa ni adimu sana. Kwa hiyo, tunaomba pamoja na mambo mengine lakini soko lile pale kwenye Kata ya Malindi ambalo limejengwa kwa fedha za MIVAF liongezewe uwezo liwe kubwa zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nachuma.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia makadirio haya ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia kuwa na afya njema na leo hii naweza kuchangia bajeti hii ipasavyo na siyo matusi kama wanavyofanya wachangiaji wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza moja kwa moja na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa…

*(Hapa baadhi ya Wabunge wa Chama cha Wananchi - CUF wanaomuunga mkono Maalim Seif walitoka nje ya ukumbi wa Bunge)*

**TAARIFA**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona wenzetu waliokuwa wanachangia sasa hivi ameanza

Mheshimiwa Maftaha wanatoka nje, tunaomba warudi wamsikilize kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa hiyo, wasubiri wasiondoke...

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu Mheshimiwa.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Nimeipokea kwa mikono miwili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Naam!

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu kuongea humu, tafadhali.

**MWENYEKITI:** Unasemaje taarifa hiyo Mheshimiwa?

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa, wasubiri, wasikilize kwa sababu sichomi sindano nazungumza maneno tu ya kawaida. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati niko mwaka wa kwanza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nilikuwa napitia kitabu kimoja kimeandikwa na Ishumi na Nyirenda cha saikolojia. Kuna kipengele kimoja amekieleza kwa kiasi kikubwa sana, kwamba *philosophy is the study of fundamental questions.* Wakati anaeleza Mheshimiwa huyu Ishumi na Nyirenda akaliweka neno moja kwamba falsafa maana yake wewe unayesoma lazima uweze kujiuliza swali kwamba hiki unachoelezwa maana yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima uweke swali, *why,* kwamba umeelezwa nenda Bungeni, kamtukane Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Profesa Lipumba, Mheshimiwa Maftaha na Msajili wa Vyama vya Siasa halafu unabeba kama mbuzi, umebeba kama mzigo kwenye gunia unakuja Bungeni na wewe unakuja kutukana. Hii ni kukosa weledi na kukosa ufahamu wa kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi kama nimesoma shule nimeelimishwa, siwezi kufanya haya. Kila unalotumwa na mtu kwamba kalifanye hili, lazima nijiulize kwa nini eti unanituma niende nikamtukane Mwenyekiti wa Chama Taifa, siwezi kufanya haya kwa sababu nina uelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala hapa limepotoshwa kwa kiasi kikubwa sana. Waheshimiwa Wabunge hapa wamekuwa wakizungumza na hawapo wamekimbia nje, kwamba eti Msajili wa Vyama vya Siasa amemrudisha Mwenyekiti wa Chama Taifa, Profesa Ibarahim Lipumba kuwa Mwenyekiti wa Chama, hili naomba nikanushe na Watanzania na Bunge hili liweze kufahamu sio kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Wananchi *CUF* mwaka jana 2016 mwezi Agosti, tarehe 21, tulikuwa na Mkutano Mkuu wa Chama Taifa. Naomba nizungumze haya ili Watanzania waweze kufahamu kwamba ni nini kinaendelea ndani ya Chama cha Wananchi *CUF* badala ya kumbebesha mzigo Msajili wa Vyama vya Siasa. Tarehe 21 Agosti 2016 tulipofanya Mkutano Mkuu Chama cha Wananchi *CUF* kulikuwa na mambo ambayo hayakufanywa sawasawa na Katibu wa Chama kwa makusudi kabisa eti kwa sababu hamuhitaji Profesa Lipumba kuwa Mwenyekiti wa Chama wakati Katiba ya Chama cha Wananchi *CUF,* Ibara ya 117(1)(2) kinaonesha kabisa kwamba Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi *CUF* ni Profesa Ibrahim Haruna Lipumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa katika mkutano wetu wa ndani ya chama tuliweza kuona mambo ambayo kimsingi siyo mambo ambayo yanaweza yakafanywa na kiongozi mkubwa kama Katibu Mkuu wetu wa Chama cha Wananchi *CUF.* Mambo yaliyotokea, kwa sababu tunazungumza suala la utawala bora hapa na utawala bora pamoja na vyama viendeshe taratibu zao sawasawa. Naipongeza Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kusimamia vyama vyetu vya siasa sawasawa kwa sababu watu wanatumia kama *SACCOS* zao binafsi.

**WABUNGE FULANI:** Haya haya haya.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyoingia kwenye ukumbi wa mkutano upande wa Katibu Mkuu wa Chama, Maalim Seif Shariff Hamad alileta wajumbe 116 kutoka Zanzibar kinyume na taratibu za Katiba ya *CUF* eti waje kupiga kura ya hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa miongoni mwa watu waliouliza maswali ndani ya ukumbi ule, nikahoji kwamba hawa wajumbe 116 ambao wameongezwa kutoka upande wa Zanzibar wapo kwa mujibu wa Katiba na kama wameongezwa mbona upande wa Bara hawapo? Majibu yalikuwa ni kwamba hao wameongezwa ni wajumbe maalum. Tukamuuliza wajumbe maalum mbona huku Bara haukuwateua wajumbe maalum, wakawa hawana majibu wakasema tutawafukuzeni chama, hivi vyama lazima viangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusema kwamba eti Msajili kazi yake ni kusajili tu vyama vya siasa na baadaye kuvifuta, Sheria Na. 5 ya mwaka 1992 ilivyoanzisha vyama vya siasa inampa mamlaka Msajili wa Vyama vya Siasa kusajili pamoja na kuvilea. Naomba niulize swali, hivi unavyosema kuvilea maana yake ni nini, ni kwamba kumchukua mtoto kumweka pale na wewe ukatembea zako, si lazima umwangalie mwenendo wake na takwimu zake ziko vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa wa Chama cha Wananchi *CUF* tarehe 21, Agosti, 2016 tulivyoona kwamba yanafanyika mambo ambayo ni kinyume na taratibu za uendeshaji wa vikao vyote duniani tukasema kwamba hatuwezi kukubaliana na haya. Wajumbe asilimia 99 kutoka upande wa Tanzania Bara tulikuwa tunataka marekebisho na utaratibu uendeshwe sawasawa likiwemo suala la kuondolewa wajumbe 116 walioletwa kinyume na taratibu za Katiba ya *CUF. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyomueleza Mheshimiwa Katibu akasema hapana hatutakubaliana na hilo. Pia tukamhoji kwamba kuna watu wameongezwa tunaambiwa wanatoka vyama vingine wameongezwa kama wajumbe waje kupiga kura humu ndani tunaomba tufanye uhakiki wa kila wilaya, akakataa akasema hatufanyi uhakiki, mimi ndio Katibu Mkuu, mimi ndiyo mwenye chama. Sisi tulichofanya tukasema hatuwezi kuendelea na mjadala huu mpaka haya yarekebishwe, kama Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa tuna uhalali wa kuyarekebisha haya. Wakaenda juu wakaleta vyombo vya habari wakasema kwamba tunakwenda kulazimisha kupiga kura wakati wajumbe zaidi ya 400 tulikataa kwamba tusipige kura kwa sababu hoja ya Kujiuzulu kwa Mwenyekiti ni lazima sisi Wajumbe wa Mkutano Mkuu tukubali sasa Mheshimiwa umejaza wajumbe kutoka Zanzibar ambao sio halali ili kuongeza namba, hatuwezi kukubaliana na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi sana, wakaingia wakaita vyombo vya habari wakasema Mkutano Mkuu umeridhia kujiuzulu kwake kitu ambacho siyo sahihi kabisa. Sisi ndani ya ukumbi tukasajili majina yetu, zaidi ya 324 tukaenda kwa Msajili wa Vyama vya Siasa tukilalamika kwamba taratibu za uendeshaji wa vikao vya Chama hiki cha Siasa cha *CUF* zimekiukwa kwa makusudi, tunaomba utupe tafsiri. Msajili wa Vyama vya Siasa alituita sisi wote, upande wa walalamikaji sisi Wajumbe wa Mkutano Mkuu zaidi ya 320, upande wa Katibu Mkuu, tukaitwa tukakaa wote tukawa tumepewa miongozo zaidi ya mara nne, mara tano

na mwisho wa siku Msajili wa Vyama vya Siasa akatoa mwongozo kwamba kwa mujibu wa Katiba ya *CUF* Profesa Ibrahim Lipumba ndio Mwenyekiti halali wa Chama cha Wananchi *CUF* Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nazungumza haya kwa sababu yameelezwa sana, kuna upotoshwaji unaofanywa kwa makusudi eti kwa sababu ya kuwahadaa Watanzania kwa sababu ya kutafuta huruma kupitia Bunge hili wanakuja wanasema uongo eti kwa sababu wametumwa na mtu mmoja. Chama ni taasisi, chama sio mtu mmoja, chama ni uamuzi wa wanachama ndugu zangu na tunasema tutasimamia hili mpaka mwisho wetu na Profesa Lipumba ndiyo Mwenyekiti halali wa Chama cha Wananchi *CUF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hapa limezungumzwa kwamba Msajili wa Vyama vya Siasa eti ametoa ruzuku akishirikiana na wahuni wake. Naomba nizungumze tu kwamba ruzuku ya Chama cha Wananchi *CUF* imeletwa kwa mujibu wa Sheria ya Ruzuku za Vyama vya Siasa na hivi ninavyozungumza baada ya ruzuku kuletwa kwenye chama, Mheshimiwa Mwenyekiti na Kamati Tendaji Taifa, hata mimi ni mjumbe pia, ni Mkurugenzi wa Mambo ya Nje ya Chama cha Wananchi *CUF,* tulikaa tukapeleka ruzuku wilayani. Tulivyopeleka ruzuku Wilayani ili ziweze kujenga chama na kulipia posho, Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi *CUF* akaandika barua kwa Meneja wa Benki Kuu kwamba afungie ruzuku akaunti za wilaya ambazo hata yeye hana mamlaka nazo na tunashangaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu ilishughulikie hili suala kwamba kwa nini Meneja wa *NMB Tanzania* ameandikia barua akaunti zote za wilaya za Chama cha Wananchi *CUF* ambazo wao ndiyo wamefungua akaunti, hazikufunguliwa na Katibu Mkuu Maalim Seif Shariff Hamad lakini hivi ninavyozungumza zimefungiwa na zile pesa hazifanyi kazi ya chama, ziko kwenye akaunti za *NMB* Tanzania nzima.

Tunaomba sana huyu Meneja wa *NMB* Taifa achukuliwe hatua kwa nini anaingilia akaunti za Chama cha Wananchi *CUF* ngazi ya wilaya. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujifunze heshima kidogo...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Kwa sababu tuna mengi sana ya kuzungumza juu yenu lakini hatutaki.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nizungumze ni suala hili la viwanda ambalo limeelezwa kwa kiasi kikubwa sana. Miaka ya karibuni Serikali iliweza kupitisha sera kwamba ajira zote hivi sasa ziweze kusimamiwa na wamiliki wa viwanda na taasisi husika. Hata hivyo, pale Mtwara katika kiwanda cha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na niseme tu kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Muongezee muda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa namna ya pekee nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge aliyeketi kwa kutoa mchango mzuri ambao hauna unafiki wala ubabaishaji.

Ameeleza vizuri kuhusu utawala bora na Wabunge wa namna hii ndiyo wanaotakiwa ili kuijenga Tanzania kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyofafanua mambo mengi ya msingi kuhusu kilimo, afya, maji na maendeleo mbalimbali ya nchi yetu. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa upande wa afya mmefanya kazi kubwa lakini bado zipo changamoto nyingi sana. Changamoto kwenye majimbo ya vijijini ni kubwa mno. Tukija mijini huku tunawakuta madaktari bingwa wa akinamama na magonjwa mbalimbali lakini vijijini tunakuwa na daktari mmoja halafu huyo ndiyo bingwa wa magonjwa yote. Kwa hiyo, nataka nichukue fursa hii kuwapongeza sana madaktari wanao-*save* katika vijiji vyetu, wanafanya kazi kubwa sana kwa sababu magonjwa ya akinamama ni yao, ya watoto ni yao na ya akinababa ni yao. Hawa ndiyo ambao nataka kuwatambua leo kwenye Bunge kwamba ni madaktari bingwa kwelikweli kwa sababu wanashughulika na matatizo makubwa sana ya wananchi vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa uamuzi sahihi wa kuamua kujenga baadhi ya vituo vya afya kwenye maeneo yaliyotengwa sana na maeneo makubwa ya kupata huduma nzuri za afya. Kwa mfano, ukitazama Tarafa yangu ya Mpwayungu, pale usiponipa kituo kikubwa cha afya ni hatari sana kwa akinamama wajawazito, kwa sababu kutoka Mpwayungu mpaka kuja Hospitali Teule ya Wilaya pana kilometa kama 85 niambie barabara ya vumbi, mama mjamzito anafikaje hapo kuja kuwahi operesheni. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa uamuzi wenu sahihi na nina hakika hili mtaliangalia kwa jicho la huruma kwenye majimbo mengi ya vijijini hasa yaliyokosa huduma za msingi za kiwango hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia habari ya Wizara ya ujenzi, itazame vilevile barabara za vijijini. Tunazungumza sana ujenzi wa barabara za mijini lakini za

vijijini tunaacha. Barabara za vijijini zikipitika kwa kiwango kizuri zitarahisisha sana huduma za maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumie kwa haraka haraka Wizara ya Maji. Maji ni Wizara mtambuka. Tukipata maji safi na salama tutapunguza kwa kiasi kikubwa sana matumizi kwenye Wizara ya afya kwa sababu magonjwa mbalimbali ambayo yanaweza kutibika kwa kupata maji safi na salama yatakuwa yameji-*solve* yenyewe na kuruhusu wananchi wafanye shughuli zingine za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na pongezi zangu kwa Wizara zote ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameziwasilisha katika hotuba yake hii, nataka nizungumzie vile vile suala la ulinzi na usalama. Suala la ulinzi na usalama limezungumzwa hapa kwa mapana na marefu lakini nataka nizungumze kwenye kipengele kimoja. Nichukue fursa hii kusema watu wanaotuhumiwa, unajua Wabunge tunachanganya kuna wengine wanasema kuna kikundi kidogo ndani ya Usalama wa Taifa wengine wanasema Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwapongeze sana watu wanaofanya kazi kwenye idara hiyo. Idara ya Usalama wa Taifa inafanya kazi kubwa sana, inafanya kazi nyeti sana na kuna baadhi ya watu nitawataja hapa bila kuwepo ulinzi na usalama kwenye maeneo yao wasingekuwepo hapa. Mnakumbuka wakati wa msiba wa Chacha Zakayo Wangwe, ni watu wa Usalama wa Taifa ndiyo walimuokoa Mbowe pale Tarime nani hajui? Kwa hiyo, wakati mwingine tusiwe tunawalaumu tu pale wanapofanya vizuri tuwasifie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme habari ya kupotea watu mimi mwenyewe ni mhanga, wako ndugu zangu walishapotea siku nyingi wengine walipotea mwaka 1980 na hwakuwa wanasiasa. Tanzania hii hata ukitaka kila Mbunge aorodheshe watu waliowahi kupotea wapo.

Hawapotei kwa sababu kuna kikundi kinapoteza watu, hapana! Kupotea kwa wananchi ni jambo la kawaida...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Ila tunaitaka Serikali iendelee kutafuta wananchi waliopotea hata wale ambao hawana majina. Kwa sababu nchi hii tusiseme tu akipotea mtu fulani maarufu ndiyo tunaanza kuzungumza. Upotevu wa wananchi ni jambo la siku nyingi. Kwa hiyo, tuitake Serikali, Idara ya Upelelezi ifanyie kazi mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnazungumza mnasema eti ooh kuna Mkuu wa Mkoa alisema mtu fulani aliyepotea ataonekana kesho mbona Kubenea alisema kwamba huyu Saanane anafahamika na kila siku anaonekana, mbona hamumhoji Kubenea? Kubenea si huyu hapa mhojini? Mbona alisema kwamba Saanane yupo anatafuta kiki tu? Kwa nini msianze na Kubenea mnaanza kuisakama Serikali? Anzeni na Kubenea atuoneshe Saanane yuko wapi, Kubenea anajua.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Alishawahi kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze sana kwenye jambo hili...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Kubenea si usubiri nimalize. *(Kicheko)*

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mbunge anayezungumza...

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Kubenea una haraka gani?

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu Mheshimiwa.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mbunge anayezungumza

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu kwanza.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Ngojea kwanza Kubenea nimalize una haraka ya nini? Wewe umesema Saanane yupo si utamtaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusiichafue Serikali kupitia Kitengo cha Idara ya Usalama, hapana!

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Tuwaache wafanye kazi yao vizuri.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Watu wamekosa kiki, Serikali inafanya kazi nzuri...

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Subiri, Mheshimiwa taarifa.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge anayezungumza kwenye Bunge lako tukufu amenitaja mimi kwa jina langu Saed Kubenea kwamba nimesema Ben Saanane yupo. Kwa maneno hayo amenisingizia, sijawahi kusema jambo hilo mahali popote pale na naomba uamrishe liondolewe kwenye *Hansard* na aniombe radhi vinginevyo alithibitishie Bunge hili kwamba maneno hayo mimi nimeyazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Ulitaka kumpa taarifa, mimi ndiyo maana nimekuruhusu kwa taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Amesema taarifa ndiyo maana nimemwambia taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa siipokei lakini magazeti yake yameandika...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Na yeye mwenyewe anajua.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a) inasema:-

*"Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli". (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hizi vilevile zinaeleza utaratibu ambapo Mbunge atatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli athibitishe. Ni masikitiko sana Bunge linazungumza masuala mazito ya kupotea kwa watu halafu kuna Wabunge wengine wanafanyia mzaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lusinde anasema Mheshimiwa Kubenea kwa maneno yake alisema

Ben Saanane yuko mtaani na anatafuta kiki. Sasa tunaomba Mheshimiwa Lusinde atuthibitishie kama kweli Mheshimiwa Kubenea alisema na kama akishindwa kuthibitisha taratibu za kikanuni zitumike dhidi yake kwa kushindwa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hiyo, nimeomba utaratibu kuhusiana na Kanuni ya 64(1)(a) kutokana na taarifa za uongo ambazo Mheshimiwa Lusinde amezisema.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni utaratibu mbaya wa kupotezeana muda tu, hapo hoja ya msingi haipo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Haujaruhusiwa kuzungumza bwana.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Sasa wewe ndiyo Spika?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mimi nimemwomba Mwenyekiti kuhusiana na utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Wewe Spika?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nasema nimemwomba Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusiana na utaratibu

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Wacha kuleta ubabe wewe, ngoja nikuambie bwana wewe siyo Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge...

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Wewe Siyo Mwenyekiti...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwenyekiti...

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Unajifanya mbabe kwenye Bunge hili, hili Bunge ni la kwako?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna *double standard* tuambizane hapa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lusinde...

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Nakwambiaje wewe kama unavuta na sisi tunavuta.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Tunaelewa tukiomba utaratibu ni Mwenyekiti anatakiwa ajibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde keti chini.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Huyu hapa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, naomba ukae. Umesimama kwa utaratibu umesema Kanuni ya 64 ngapi?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Inawezekana ulikuwa hunisikii vizuri, nimesema.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 64 ngapi?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Jamani...

**MWENYEKITI:** Basi endelea Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Si nili-*quote* mbona ...

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Tunazungumzia habari ya...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Habari ya Wizara ya Nishati na Madini.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiitazama Wizara ya Nishati na Madini...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Yamezungumzwa mambo mengi sana humu...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Lakini huwezi ukapiga marufuku matumizi ya mkaa kama hushushi bei ya gesi.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Tunaitaka Serikali ishushe bei ya gesi.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Bei ya gesi iwe chini halafu ndiyo mpige marufuku matumizi ya mkaa...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Lakini gesi inaongezeka bei...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Halafu huku mnapiga marufuku matumizi ya mkaa inakuwa haiwezekani.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Kwa hiyo, tunaitaka Serikali ishushe bei ya gesi ili watu waweze kutumia gesi.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Waweze kunufaika na kupata maendeleo.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingi sana zimezungumzwa, bado narudi pale pale....

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Kwenye suala la ofisi ya Wabunge...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kitabu chake ameeleza habari ya Bunge...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Wabunge wengi hawana ofisi. Tunaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu kukamilisha ujenzi wa ofisi za Wabunge ili Wabunge waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Tunaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia TAMISEMI isimamie ujenzi wa Ofisi za Wabunge ili Wabunge waweze kupata Ofisi zao na waweze kufanya kazi zao kwa uhakika, waweze kuheshimika kwenye majimbo yao tofauti na sasa ambapo Wabunge wengi wanafanyia kazi zao nyumbani, hili haliwezekani. Ofisi zimejengwa hazijakamilika, kuna maeneo fulani mpaka *frame* zinaanza kung'olewa, kuna maeneo fulani majumba yanaoza kabla hayajamalizika, tunaitaka Serikali ikamilishe ujenzi wa Ofisi za Wabunge ili Wabunge wafanye kazi zao kama sheria inavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kipindi cha mwaka mmoja mmefanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Rais amesimamia maadili, nidhamu na uwajibikaji. Leo tunapozungumza hapa Rais anazindua ujenzi wa reli ya *standard gauge* ambayo itatumia saa moja kufika Morogoro na baadaye watakamilisha Dodoma na kuelekea Mikoa ya Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa sana kwa vitendo na tunamwomba Rais aendelee kusimamia nidhamu ya uwajibikaji, nidhamu ya mapato na matumizi, aendelee kusimamaia amani ya nchi yetu ili watu tuweze kuishi kwa amani na tufanye kazi kwa bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ulinzi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imepata Pato la Taifa 7.0 katika Sekta hii ikiwa inaongoza 2016 -2017 na Mpango wa Serikali inapanga kuziendeleza sekta hii ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iboreshe mazingira wezeshi kwa wachimbaji wadogo hususani mkoa wangu wa Katavi katika migodi ya Kapanda na Ibindi. Wachimbaji waboreshewe huduma za kijamii kama zahanati na miundombinu ya barabara na usalama wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gharama za Leseni za uchimbaji Mkoa wa Katavi una urasimu sana na hivyo kuleta usumbufu kwa wachimbaji (rushwa). Hakuna *coordination* kati ya Wizara ya Ardhi na *Giologist* ili wachimbaji wasaidiwe kujua *potential areas* katika uchimbaji na kuzingatia utunzaji wa mazingira wanapochimba. Madawa ya kusafishia dhahabu ni ghali mno hivyo wachimbaji wadogo ambao ni wengi hawana uwezo wa kununua na hivyo huuza dhahabu zao kwa gharama ndogo huku wanunuzi wakidai madawa ni ghali Serikali ilione hili. Usalama kwa wachimbaji na wanunuzi Mkoa wa Katavi na Tanzania kwa ujumla ni mdogo sana watu wanakuja wanapopigwa risasi katika migodi. Tunaomba polisi na usalama uzingatiwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifugo inayopigwa risasi Serikali ingeona namna ya kuboresha kutumia ng'ombe hao kutoka katika jembe la mkono na kulimia ng'ombe ambao ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza kodi kwa wakulima bado ni tatizo kulipa kodi ya mazao tunaomba Serikali iwangalie wakulima maana wanalima katika mazingira magumu, pembejeo na mbegu feki, itatue tatizo hili. Usambazaji wa pembejeo kuna urasimu na zinachelewa sana. Kuzuia mbegu feki zinazosambazwa na upatikanaji wake.

Ombi kwa Serikali kuzuia mbegu feki mipakani. Iangalie mipaka yote ya Tanzania kuna mbegu feki zinapita na hivyo kuathiri kilimo kwenye mpaka wa Tunduma na Namanga wananchi wanaingiliana katika shughuli na hivyo kuleta upenyo wa kupitisha mbegu feki kutoka nchi za jirani kama Zambia, Malawi na Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato *TRA*. Serikali iangalie kwa jicho la tofauti kwa wafanyabiashara wanapokadiriwa na *TRA* katika maeneo yao ili kulipa kodi, kuna malalamiko biashara zao ndogo na wanakadiriwa kulipa kodi kubwa hivyo kuwafanya washindwe kulipa kodi na kufunga biashara zao na ukizingatia jiografia ya kupata bidhaa kutoka nje ya Katavi na mikoa ambayo iko pembezoni iangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Serikali iboreshe huduma za Wizara Afya na Elimu bure kuhusu *VVU* katika maeneo yenye watu wengi hususani migodini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo na Mifugo naomba Serikali iendelee kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji imekuwa tatizo na hii inaendelea kuleta upungufu wa chakula kutokana na migogoro hii. Wakulima kuchomewa mashamba, mifugo kuuawa au kupigwa risasi.

**MHE. OMAR A. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kutufikisha salama katika Bunge hili. Pia niwape pole wafiwa na majeruhi wa ajali, pia naipongeza Serikali kwa maamuzi yake ya kuhamia Dodoma. Pamoja na juhudi zake za Kasi katika kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumedhamiria kuwa na Tanzania ya viwanda, ni vyema sasa Serikali ikajikita kwa kina katika kuhakikisha kuwa umeme wa kutosha unapatikana ili tuweze kuendesha viwanda vyetu *especially* kwenye umeme wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kujitahidi kutatua changamoto ambazo zinagusa kwa kiasi kikubwa wananchi, mfano maji, afya na elimu, hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kunyanyua jamii yetu na kuifanya jamii yetu ishiriki vyema kwenye maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la maji pamoja na jitihada kubwa za Serikali kuhakikisha tunapata maji safi na salama, bado kuna changamoto kwa upande wa watendaji hususan katika maeneo ya vijijini. Hii inatokana na utendaji wa mazoea kwa wataalam wa Idara husika. Mfano unakuta Mhandisi wa Maji amekaa eneo moja kwa zaidi ya miaka kumi na pamoja na kukaa miaka yote hiyo tatizo la maji bado lipo palepale pamoja na kulipwa mshahara na mahitaji mengine.

Nashauri kuwe na uhamisho kwa watendaji ambao wamekaa sehemu moja kwa muda mrefu na pia ni vizuri wakaangaliwa *performance* yao kila mara ili kuona ni jinsi gani wanafanya kazi ya kutatua kero hii ambayo inagusa kila jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Elimu; ni vizuri Serikali ikatoa mwelekeo mzuri kwa Halmashauri ni jinsi gani wanasaidiwa na wananchi katika ujenzi wa madarasa mfano kuna mkanganyiko kati ya Halmashauri na wananchi. Tunaambiwa kama wananchi tujenge boma na Halmashauri itaezeka juu. kuna maboma mengi yameshajengwa na wananchi lakini bado Halmashauri zinasuasua katika mpango wao wa kumalizia juu na ukizingatia idadi ya wanafunzi inaongezeka kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya, pamoja na jitihada, kubwa kuhakikisha huduma ya afya inaimarika, bado kuna changamoto kwenye ununuaji wa dawa na upungufu wa Madaktari. Nashauri Serikali ihakikishe *MSD* wanapata dawa ya kutosha ili kuepuka kuonekana kulemewa na *order* kwenye hospitali zetu au kuweka utaratibu wa kuziwezesha hospitali kununua dawa maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upungufu wa Madaktari na Wauguzi ni kubwa sana na lipo nchi mzima. Ningependa kuiomba Serikali ifanye haraka kulishughulikia suala hili, mfano katika jimbo langu, kuna upungufu wa karibia asilimia ishirini ya Madaktari na Wauguzi na ukizingatia hospitali yetu inahudumia majimbo manne. Upungufu huu, unasababisha vifo vya mara kwa mara kutokana na kuchelewa kuhudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuyaondoa maduka yote ya watu binafsi (ya dawa) ila iharakishe kuhakikisha maduka ya Serikali yanaanzishwa haraka.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Mgogoro wa ongezeko la vijiji kuingia hifadhi, Mbarali Mbeya. *TANAPA* inaongoza vijiji 21 kuingia katika hifadhi lakini vijiji hivi ni vya wakulima wa mpunga na mgogoro huu umekuwepo kwa zaidi ya miaka nane. Wakati wa kampeni za Urais 2015 Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi kuwatengenezea barabara ya lami ambayo imeanza kutekelezwa na akatoa agizo vijiji vile visichukuliwe na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawa wa mpunga wanazalisha magunia mpaka 1,300,000 sawa na tani 104,000 kwa mwaka. Katika vijiji hivyo vipo viwanda vya kukoboa mpunga vikubwa 42 na magodauni 56 makubwa. Kwa kuvichukua vijiji hivi tayari ajira zitapotea takriban watu 10,000 watakosa ajira. Ukizingatia agizo la Rais ni kuwa Tanzania ya viwanda. Je kwa kutaifisha vijiji hivi na kuvifanya hifadhi Tanzania ya viwanda itatekelezekaje? Serikali isitishe kuvichukua vijiji 21 kwa faida ya maendeleo ya wananchi wanaoishi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni afya na kwa sasa hivi magonjwa yasiyoambukiza kama sukari ya kupanda na kushuka na shinikizo la damu la kupanda na kushuka magonjwa ya moyo magonjwa haya kwa sasa yanawapata

hasa watoto wadogo lakini yanaweza kuzuilika kwa watu kufanya mazoezi na Serikali kupitia Makamu wa Rais, aliagiza watu wafanye mazoezi kwa nia nzuri tu lakini cha kujiuliza watu watafanyia wapi mazoezi. Halmashauri nyingi hazina viwanja vya michezo na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake hajaelezea kabisa mikakati ya kujenga viwanja na ya kupata viwanja hivyo vya mazoezi?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza mchango wangu kwa kuzungumza Sera ya wazee nchini. Sera ya Wazee nchini ilikuwepo tangu mwaka 2003, lakini hadi leo Sheria kwa ajili ya utekelezaji wa Sera hii bado haijaletwa hapa Bungeni ili kukidhi mahitaji ya Sera ya Kitaifa ya wazee kama ilivyopitishwa mwaka 2003. Kumekuwepo kwa ahadi ya muda mrefu ya ulipwaji wa pensheni kwa wazee wote hasa wakulima waliotumikia uchumi wa nchi hii kwa uaminifu mkubwa. Pia kukosekana kwa Sheria hiyo kumefanya ushiriki wa wazee hao kwenye vyombo vya maamuzi kuwa hakuna. Katika ngazi zote za vyombo vya maamuzi, ushiriki wa wazee ni kama hakuna hivyo kuathiri maslahi ya wazee hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kwa mauaji ya vikongwe nchini ni matokeo ya madhara ya kutokuwa na sheria inayowatambua wazee nchini na pia ukosefu wa uwakilishi kwenye vyombo vya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwa Wakala wa Uvunaji wa Mali za Misitu *(TFS)*. Sheria na kanuni zinazotumiwa na Taasisi hii ni bora ikafanyiwa marekebisho kwani kwa kiasi kikubwa imekuwa si shirikishi kwa jamii inayoizunguka au jirani na misitu husika. Mfano ushuru au tozo zinazopatikana katika uvunaji huu. Halmashauri zetu upatiwe kiasi cha asilimia tano tu. Kiasi hiki ni kidogo sana ukilinganisha na uharibifu unaotokana na kazi hii. Vile vile ukizingatia ulinzi shirikishi inakuwa ni vigumu sana kwa jamii kuona faida ya misitu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa *TFS* katika shughuli za maendeleo kwenye vijiji vinavyopakana na misitu midogo

sana kitendo kinachochea jamii kutokuona faida ya moja kwa moja ya uwepo wa misitu hiyo. Kamati za Vijiji za uvunaji wa mali za misitu hazina elimu ya kutosha juu ya uvunaji endelevu. Hivyo kufanya wajanja wachache kutumia mwanya huo kuharibu mali za misitu bila jamii husika kunufaika. Kama ilivyo kwa maliasili, vijiji au Halmashauri upatiwa 25% kwa wawindaji, basi na *TFS* ifikiriwe kutoa kiasi kama hicho cha 25% kwa Halmashauri. Ili Halmashauri iweze kunufaika na uvunaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwa wapiga kura wangu. Wilaya ya Liwale ni wilaya yenye kata 20 lakini wilaya hii hadi leo ina kituo cha Afya kimoja tu. Jambo linaloifanya Hospitali ya Wilaya kubeba mzingo mkubwa sana. Ukizingatia Hospitali yenyewe tangu ilipopandishwa hadhi toka kituo cha afya miundombinu yake haijaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, janga kubwa linaloikumba wilaya hii ni mgao mdogo wa fedha za dawa na *basket fund*. Mfano Mkoa wa Lindi una wilaya tano, wilaya inayopata mgao mdogo ni Liwale ukilinganisha na wilaya zingine. Cha kusikitisha ni kwamba katika Mkoa wa Lindi hospitali za wilaya, Hospitali za Liwale ndio inayoongoza kwa kuhudumia wagonjwa wengi kwa mwezi, lakini ndio inayopata mgao mdogo wa fedha. *Basketi fund*, Liwale milioni 350, Ruangwa bilioni moja, Nachingwea milioni 800, Kilwa milioni 600, hii si haki. Mateso yanayowapata wana Liwale ni matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, hivyo, nashauri Serikali ikafikiria vinginevyo badala ya kuacha watu wakiteseka kwa magonjwa na ukosefu wa madawa. Fedha ya dawa Liwale milioni nane, Ruangwa milioni 21, Kilwa milioni 17 na Nachingwea milioni 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madeni ya Walimu; pamoja na juhudi kubwa inayofanywa na Serikali juu ya kumaliza tatizo hili, lakini kasi yake ni ndogo ukilinganisha na ukubwa wa tatizo. Walimu ni wengi sasa wanaodai nyongeza ya mishahara inayotokana na kupandishwa madaraja na wengine wanaocheleweshwa kupandishwa madaraja ingawa wanakidhi vigezo. Jambo hili linawakatisha tamaa

Walimu wengi na kufanya shule nyingi kuwa na matokeo mabaya. Hali za walimu wetu ni mbaya kwa ujumla wanaishi katika mazingira magumu sana. Uhaba wa ajira tu ndio unaowabakisha huko na si kufurahia ajira yao, kwani walio wengi hawajui hatima yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kuishauri Serikali kuchelewa au kutopeleka Ruzuku ya *OC* kwenye Halmashauri zetu ni kurudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu kwani Halmashauri inashindwa kutekeleza miradi yake ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kutenga fungu la vijana na akinamama. Pengine Halmashauri hutakiwa kutekeleza maagizo ya Kitaifa bila kupewa fungu la fedha za kazi husika ikiwa ni pamoja na michango mbalimbali. Jambo hili hurudisha nyuma mipango ya Halmashauri kwani hulazimika kutekeleza miradi ambayo haikuwa kwenye mpango kazi wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwakilisha.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim M. Majaliwa, kuhusu hatuba ya Bajeti aliyoiwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika kipindi cha mwaka mmoja wa Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mengi yamefanyika. Nampongeza sana juhudi zinazofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi zinazofanywa na Mheshimiwa Rais kuhakikisha Serikali inahamia Dodoma. Bado napenda kukumbusha sheria ya kuhamia Dodoma haijapitishwa katika Bunge lako Tukufu. Je nini kinasababisha ucheleweshaji wa utungaji wa Sheria hii. Pamoja na nia nzuri ya Serikali kuhakikisha Dodoma inakuwa Makao Makuu, kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali mfano

Nkuhungu *Centre,* Kiwanja. P. 639 wanalalamika pamoja na kulipia viwanja vyao lakini wengine wamenyang'anywa kwa madai wameshindwa kuviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaweza kuleta mgogoro mkubwa sana kati ya Serikali na wananchi, hata kama kuna baadhi ya wananchi wameshindwa kuendeleza maeneo ni vema wakapewa taarifa ili ithibitike mapema isiwe Serikali inapokea pesa ya kodi na baadhi ya wananchi wanazo *slip za Bank* ambazo wamekuwa wanazilipia kodi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kuwa Serikali hii ni sikivu ni vema kufuatilia kwa ukaribu jambo hili ili kupata ukweli. Pia Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu hayo inatakiwa itende haki kwa wale wote waliovamia maeneo, hali kadhalika Kamati za Makazi nazo zifuatiliwe kwani kuna baadhi ya Wanakamati hao wanafanya udanganyifu wa kuuza maeneo bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Serikali suala la ukusanyaji mapato unaofanywa na *TRA,* lakini mamlaka inabidi itumie mbinu mbadala ili ulipaji kodi uwe hiyari na wananchi waone ulipaji kodi ni wajibu wa kila Mtanzania. Kwani mtindo unaotumika wa kutumia maaskari na mabunduki mengi inaleta hofu. Ushauri wangu elimu ya mlipa kodi au ulipaji kodi ni kwa ajili ya maendeleo ya nchi katika masuala yote ya kijamii, elimu, afya, miundombinu, kilimo na ufugaji ni kwa maendeleo ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuweka dhamira ya dhati katika kuendeleza kilimo cha biashara, pamoja na kuzalisha mbegu za nafaka ni budi pia kilimo cha biashara cha mbogamboga ambacho kimeanza kuwa na tija na kikitiliwa mkazo kitasaidia kupunguza umaskini kwani kilimo cha mbogamboga mfano matikiti maji, matango, *carrots*, hoho, vitunguu, nyanya na mboga zingine zinaweza kuongeza pato la Taifa, iwapo Taifa litaweka mkazo na kufanya tafiti zaidi na kuzalisha mbegu za mbogamboga. Ili zizalishwe kwa wingi, kwa bei nafuu ili

ikiwezekana mazao ya mbogamboga yaweze kuzalishwa kwa wingi na hatimaye kusafirisha nchi mbalimbali duniani. Kwani uhitaji wa mazao ya mbogamboga ni mkubwa sana na una tija kwa wazalishaji mazao hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukame na njaa, pamoja na wadudu waharibifu nalo ni jambo la kuliangalia kwa jicho tofauti. Kutegemea mvua katika kilimo bado kunasababisha njaa, kwani mvua hazitoshelezi kutokana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, hivyo ni budi Serikali ijikita katika kilimo cha umwagiliaji na pia uvunaji maji ya mvua ili yatumike kumwagilia kipindi cha kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo ikiwemo kanda ya Kati, Mikoa ya Dodoma na Singida, pia baadhi ya mikoa inayolima mazao ya mtama, mfano Shinyanga kumekuwa na tatizo la ndege waharibifu ushauri wangu Serikali ifanye utaratibu wa kupata ndege yake ili inapotokea uharibifu wa ndege iwe rahisi kutekelezwa kwa haraka kuliko kusubiri ndege ya kutoka Nairobi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa vita dhidi ya rushwa na madawa ya kulevya. Bado mkazo utiliwe na Serikali kutoa elimu kwa jamii waone ubaya wa rushwa, pia kwa vijana kujihusisha na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uchumi na viwanda na kuimarisha viwanda vyetu bado naendelea kushauri, wananchi wa Tanzania wahamasishwe kuzalisha malighafi kwa ajili ya kuhudumia viwanda. Kwani tukiwa na viwanda halafu malighafi ikaletwa kutoka nje haitakuwa na maana. Ni budi Serikali ikaweka mkakati wa makusudi ili kuhakikisha malighafi zaidi zinazalishwa nchini ili ziweze kukidhi mahitaji ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza ujenzi wa miundombinu vijijini unaotekelezwa na kampuni ya *Viettel,* je, ni ofisi ngapi za Wakuu wa Wilaya zimepatiwa miundombinu ya mitandao ya *Internet* nauliza jambo hili kwa

sababu baadhi ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya hazina huduma za *Internet.* Nahitimisha kwa kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo heshima kuipongeza Serikali ya CCM kwa kazi nzuri. Kipekee kumpongeza Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoijenga Serikali na kuwafanya Watanzania wajisikie vizuri. Naomba nitoe ushauri ufuatao ili kuongeza ufanisi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa kada mbalimbali kwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Makatibu Tawala na Wakurugenzi uzingatie faida ya wateuliwa hao na ni vizuri wafanyiwe usaili *(interview)* ili kujiridhisha uwezo wao. Mfano Katibu Tawala Mkoa au Wilaya ni wakuu wa Watumishi wote wa Umma katika maeneo yao. Watendaji wa nafasi hizo ni lazima au vizuri, wawe na ueledi na uamuzi unaoashiria kuwa wao ni Wakuu wa Watumishi wa Umma. Mheshimiwa Waziri Mkuu, *DAS* wa Makete alikuwa mtunza fedha (*cashier*) kampuni ya *TiGO*, ndiye sasa Mkuu wa Watumishi wa Umma wote wa Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, yapo madhara hasi kwa kuteua wateule ambao watumishi wa mahali pale wanaona kiongozi wao hatoshi. Morali wa watumishi wa umma inakuwa chini kwa maana wanakuwa hawaungi mkono Serikali. Hili ni kubwa sana kwa kuwa Serikali yoyote lazima iangalie madhara ya kutoungwa mkono. Pamoja na nia nzuri ya Rais wetu na wewe mwenyewe Waziri Mkuu, wateuliwa wanaotoka nje ya mfumo wa Serikali, nachukua muda mrefu kujifunza na hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya Taifa letu na kuipunguzia kukubalika Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wateuliwa kama Wakuu wa Mikoa na Wilaya, wanajikuta wanakosa weledi katika kutumikia nafasi zao. Kwa bahati mbaya kila ubaya unaofanywa na viongozi wa Serikali anayeadhibiwa ni CCM.

Jambo la pili. ninaomba ofisi yako Mheshimiwa Waziri Mkuu au Ofisi ya Rais iunde timu ya watu waliopewa neema ya kufikiri. Nakumbuka wakati mzee Malecela akiwa Waziri Mkuu mwaka 1991-1994 aliunda Kamati ya Mipango ambayo kazi yake ilikuwa ni kuisaidia Serikali kufikiri. Kufikiri ni kipawa haimaanishi kuwa mtu akiwa na elimu kubwa basi uwezo wake wa kufikiri unaongezeka. Bali ujuzi wa eneo alilojifunza ndio unaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii inaweza kujumuisha watu mbalimbali hata baadhi ya Mawaziri (kama wana zawadi ya kufikiri) ili kuisaidia Serikali kutoa ushauri wa kiuweledi bila kusukumwa na maneno yasiyo na mashiko. Timu hii itasaidia kutoa weledi kwenye uwekezaji, siasa na kadhalika. Jambo kubwa ni kuwa, moja kati ya changamoto ambazo Serikali karibu zote duniani zinapata, ni uhakika wa taarifa inazozipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naipongeza sana Serikali yetu ya CCM kwa kuangalia vipaumbele ikiwa ni pamoja na ujenzi wa reli ya kati na barabara mbalimbali katika nchi yetu Tanzania. Nami nawaombea viongozi wote mpate kuwa na afya njema na utashi mkuu. Ahsante.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yenye mwelekeo na dira ya utekelezaji wa maendeleo ya Serikali yetu. Katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Maeneo ya huduma za Kiuchumi; napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kasi kubwa ya maendeleo inayochukua kasi za maendeleo katika maeneo kadhaa kama vile umeme, barabara, reli na usafiri wa anga ni mkubwa na ni wa kutia moyo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika eneo hili la huduma za kiuchumi ni kwamba, naiomba Serikali kuwa makini kwa kuangalia viwango vya miundombinu hii ili kuepuka hasara za matengenezo ya muda mfupi mara baada ya makabidhiano ya miundombinu hii. Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa matengenezo ya miundombinu ambayo mara nyingine sio ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti Ninamshukuru Mungu kwa rehema na neema yake. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyosheheni taarifa zote muhimu zinazogusa kila sekta ya Serikali. Aidha, nawapongeza Mawaziri walio chini ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Mheshimiwa Anthony Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini kwa kazi nzuri wanayoifanya chini ya uongozi wake mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukuaji wa Uchumi; napenda kuzungumzia masuala kadhaa yahusuyo. Naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kukuza uchumi wa asilimia 7.0 kwa zaidi ya miaka 10 sasa. Haya ni mafanikio makubwa sana kidunia na inaashiria kuweka mikakati na mipango mizuri ya kiuchumi na kimaendeleo ambayo imetekelezwa ukuaji huu. Pomoja na pongezi hizi, naomba niitakie Serikali kuhakikisha kuwa ukuaji huu wa uchumi unatafsiri kuwa maendeleo kwa mwananchi mmoja mmoja na kwa ujumla. Hii inawezekana kwa Serikali kuhakikisha kuwa inaweka miradi ya kimkakati katika sekta na sekta ndogo ambazo zinagusa moja kwa moja maisha na ufanisi wa wananchi wetu wa hali ya chini hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupendekeza kuwa uwepo mpango kazi wa kuhakikisha vikosi vya vijana na wanawake kupitia *SACCOs*, ushirika na makundi mengine na kuwapatia mafunzo ya kuwajengea ujuzi katika kilimo, ufugaji, uvuvi wa kisasa. Sambamba na mafunzo Serikali

iweke mkakati wa kuwapatia mitaji, vitendea kazi na pembejeo, lakini vilevile kuweka mkakati wa kujenga maghala, masoko na miundombinu ya barabara ya kuunganisha uzalishaji na masoko katika mnyororo wote wa thamani kwa kila zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo itakayoweza kufanya haya yote kisayansi na kuyasimamia. Hili haliwezi kuachiwa *NGOs* au watu binafsi kujianzishia vitu kiholela au wananchi wenyewe. Hili ni lazima lisimamiwe na Serikali yenyewe kama mkakati wa kushirikisha wananchi wote katika uchumi *(inclusiveness).* Mkakati tajwa hapo juu utajihakikishia ajira, kipato cha wananchi lakini na pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ni muhimu sana kwenye ufanisi wa nchi. Sekta hii inajumuisha lishe na huduma za afya kwa muda mrefu wananchi wamehamasishwa sana kujenga vituo vya afya na zahanati kwa kujitolea. Nyingi zimekamilika kwa asilimia 80 au zaidi lakini zinahitaji kumaliziwa. Naiomba Serikali ihakikishe kuwa zahanati na miundombinu hii inamaliziwa na kukamilishwa ili zianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la lishe bora bado halijazingatiwa na kuwekewa mkakati mahsusi ya kuhamasisha na kutoa mafunzo ya lishe bora. Kwa kutumia maofisa wa ustawi wa jamii. Vipindi vya redio na televisheni, vituo vya afya na ngoma na michezo ya kuigiza. Hii itasaidia sana kupunguza utapiamlo na huduma kwa watoto wetu takriban asilimia 42. Vyakula vipo ni elimu tu ndiyo inayohitajika kuhakikisha matumizi mazuri ya vyakula mbalimbali ili kupunguza utapia mlo. Huu uwe mkakati mahsusi wa kuboresha lishe ya watoto na wanawake wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Afya masuala ya vifo vya wanawake wakati wa kujifungua na vifo vya watoto wachanga na wale wa chini ya miaka mitano. Bajeti ya afya itenge fungu maalum la kuhakikisha vifaa tiba na

huduma muhimu za wazazi zinakuwepo. Wahakikishe kuwa vifaa vya kupokelea watoto wanapozaliwa hospitali vinapatiakana ikiwa ni pamoja na maji, wodi, wauguzi na vyumba vya kupumzikia wanawake wanapojifungua-pamoja na vyumba vya upasuaji. Haya yatapunguza kwa kiasi kikubwa sana vifo vya wazazi na watoto wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu UKIMWI na watu wanaoishi na VVU changamoto kubwa ni mashine za kupima *viral load* na fedha ya dawa za kurefusha maisha lakini vile vile uhamasishaji kwa wananchi. Wazee bado hawajawekewa mkakati wa kitaifa kwa kuhakikisha matibabu, kupimwa afya, kuelimishwa juu ya maradhi yanayowasibu, lakini pia wazee waingizwe kwenye *TASAF* wote kupunguza hoja ya kuwapa kipaumbele.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napongeza sana kwa hutuba nzuri sana. Pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia haya yafuatayo:-

*CDA* ni chombo cha Serikali Kuu na chombo hiki kipo ndani ya Manispaa ya Dodoma, Manispaa ya Dodoma ni chombo cha mamlaka ya Serikali za Mitaa. *CDA* wanapima viwanja na kuchukua mapato ya ardhi kodi ya ardhi ambayo ipo chini ya Manispaa ya Dodoma na Manispaa wanapima viwanja na kuchukua kodi ya viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Waziri Mkuu huu sio mgogoro kati ya *CDA* na Manispaa ya Dodoma kwa kuwa Kisheria ardhi yote ni mali ya Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na ndiyo wenye haki ya kupima viwanja na kupata kodi ya viwanja (ardhi) na sio *CDA*. Sheria iliyoanzisha *CDA* iangaliwe upya, *CDA* ilianzishwa kwa ajili ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma na tayari Makao Makuu Dodoma yameanza.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na kuunga mkono hoja na nachangia katika masuala yafuatayo:-

Kilimo, umuhimu wa Sekta ya Kilimo katika uchumi uko wazi; naishauri Serikali kuweka dhamira na mikakati kuongeza uzalishaji tija kuwa kilimo chetu kiwe cha kibiashara. Hivyo yafuatayo yazingatiwe.

(a) Kilimo cha umwagiliaji kwa kuongeza mabanio yaliyopo sasa hususan katika maeneo ambayo yana fursa za uhakika wa mito ya kudumu kwa Mkoa wa Morogoro, Wilaya za Malinyi, Ulanga na Kilombero.

(b) Uwepo wa Soko la kuhakikiwa kwa mazao ya kilimo. Wakulima katika kero kuu zinazowakabili wakulima ni soko la uhakika kwa mazao hususan mazao ya nafaka kama mpunga au mahindi.

Mifugo; mwendelezo/ongezeko kubwa la mifugo na ufugaji kiholela wa mifugo aina ya ng'ombe nchini inahatarisha uchumi wa nchi huko siku za usoni. Nashauri Serikali kusimamia na kutekeleza zoezi la matumizi bora ya ardhi ili yatengewe maeneo mahsusi kwa malisho ya mifugo. Aidha, Serikali kuweka miundombinu rafiki wa mifugo kama marambo ya maji na visima katika maeneo ya malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa hili utasaidia kwa kiasi kikubwa sana kumaliza changamoto katika mifugo, migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Aidha, itainusuru nchi katika kuelekea nchi kuwa jangwa kama tutaendeleza ufugaji/uchungaji wa ng'ombe kiholela. Ahsante.

**MHE. TWAHIR AWESU MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kuandika maelezo yangu haya na

kuyawasilisha mbele ya Bunge lako hili. Nazungumzia kipengele cha siasa ukurasa wa kumi (10) cha kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukamilika kwa uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 hata haiwezekani kuweka siasa pembeni kwa baadhi ya vyama vya siasa kuwa na uhuru wa kufanya shughuli za kisiasa na vyama vingine kumnyima fursa ya kufanya shughuli zake za kisiasa. Kauli ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuzuia vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara hadi mwaka 2020 jambo ambalo ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, demokrasia ina uwanja mpana sana ukiwemo uhuru wa kujieleza, uhuru wa kupata habari haki ya kukosoa na kukosolewa na mengineo. Leo hii Taifa linashuhudia jinsi wananchi wanavyokosa fursa ya kuhoji ama kuwakosoa viongozi wao. Pia vyombo vya habari vinavyoshindwa kufanya kazi zake kwa uhuru na uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siasa za amani na utulivu ni za muhimu sana kwa wakati huu katika Taifa letu ili maendeleo yaweze kupatikana. Siasa ya amani na utulivu haziwezi kustawi hapa nchini kwa taasisi zilizojengwa kuvilea vyama vya siasa kugeuka na kuanza kuvihujumu vyama vya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msajili wa Vyama vya Siasa nchini alipaswa abadilike na achane kabisa na dhamira aliyonayo ya kutaka kukisambaratisha Chama cha Wananchi *CUF* na aache kulazimisha kuwachagua viongozi wa kukiongoza kwani vyama vina Katiba na Kanuni zake Aviachie vyama vifanye maamuzi yake na asiviamulie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amani ya nchi ni muhimu sana kwa Muungano wetu una maslahi mapana kwa wananchi wa pande zote mbili za Jamhuri na ni jambo la hatari; huyu Msajili wa Vyama vya Siasa asiachiwe

akaliendeleza jambo hili litaleta mtafaruku mkubwa. Kwa upande wa pili wa Muungano wetu, hautariridhia hali ambayo amani ya nchi yetu itarudi kule kule tunakotoka katika siasa za chuki na uhasama baina ya wana *CUF* na wana CCM kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu:-

(i) Ili kudumisha mfumo wa Vyama vingi nchini Msajili wa vyama vya siasa afanye kazi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa na aachane kabisa kuvipangia ama kuviamulia Vyama vya Siasa.

(ii) Asaidie kutatua migogoro na sio kupandikiza migogoro.

(iii) Awe karibu na vyama vya siasa ache kujenga uadui na baadhi ya vyama vya Siasa.

(iv) Yeye ni mlezi kama baba atoe haki sawa kwa vyama asionyeshe ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nianze kwa kupongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanya kwa kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu, nampongeza sana kwa kufika na kutatua changamoto sugu jimboni na Mkoani Manyara. Pamoja na pongezi hizi tunazo changamoto na ahadi tulizopewa na Serikali kupita viongozi wetu wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miundombinu; tunaomba kujengewa barabara ya kutoka Karatu –Mbulu, Haydom Singida/Sibiti maana inasaidia ikiwa itajengwa kwa lami. Barabara hii inapita katika majimbo matano na hata itasaidia sana wananchi kufika katika Hospitali ya Kilutheri ya Haydom ili kupata matibabu na pili itasaidia wananchi kiuchumi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekjiti, kupandishwa hadhi hospitali ya Kilutheri ya Haydom iwe ya Kanda kama ulivyoahidi. Jambo hili la kupandishwa hadhi itasaidia sana kuhudumia jamii inayozunguka. Mikoa ya Simiyu, Manyara, Arusha, Singida, Tabora na sehemu ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa la miradi ya maji ambayo imekwama kutokana na kutopata fedha kwa wakandarasi. Hoja, mradi wa maji Hydom- Tumati, tunaomba Serikali ifanye mkakati wa kuwasaidia wakandarasi. Mifugo/Kilimo katika jimbo langu kuna wizi wa mifugo ambao umepelekea kufariki kwa kuuawa zaidi ya wananchi wanne na zaidi ya mifugo 500 kuibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iimarishe usalama katika Bonde la Yaeda Chini/Eskesh Kilimo. Tunaomba sasa mbegu na mbolea zinazotolewa kwa wakulima zije kwa muda muafaka yaani kabla kunyesha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ipo katika ilani ya CCM kujenga zahanati kila kijiji. Naomba nitoe ushauri ni bora Serikali kutoa maelekezo mahususi kujikita katika kujenga kituo kimoja cha afya kila Halmashauri kwa mwaka wa fedha ili baada ya miaka mitatu tutakuwa tuna vituo ziadi ya 500 hapo ndipo tutaona matokeo ya haraka katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawapongeza sana, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri, Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwa kazi nzuri.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana hotuba ya Waziri Mkuu kwa sababu imetaja maeneo ambayo Serikali inafanya kazi zake. Kwa kuwa maji ni muhimu kwa maisha ya binadamu Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba sana kuishauri Serikali kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji ambayo imeharibika na wananchi wanashindwa kupata maji safi na salama.

Jimbo la Mufindi Kusini tuna tatizo kubwa la maji Serikali iliweza kujenga matanki ya kutosha katika Jimbo la Mufindi Kusini lakini matanki hayo hayafanyi kazi sababu ya miundombinu kuharibika katika Kata za Nyololo, Idunda, Itandula, Mtambula, Ihomasa, Igowole, Kibao na Sawala. Wananchi wanapata shida kubwa ya maji kutokana na kuwa na matanki ambayo hayawezi kuhifadhi maji kutokana na miundombinu mibovu. Nitashukuru sana kama Serikali itafanya ukarabati wa miundombinu hiyo ili wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini waondokane na tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umeme, naiomba sana Serikali kupeleka umeme katika Jimbo la Mufindi Kusini vijiji vingi bado havina umeme. Kata ya Idunda ina vijiji vitatu navyo havina umeme. Kata ya Itandula vijiji sita havina umeme, Kata ya kiyowela vijiji vinne havina umeme, Kata ya Maduma vijiji vitatu havina umeme Kata ya Kasanga vijiji vitatu havina umeme, Kata ya Nyololo vijiji vinne havina umeme. Jumla ya vijiji 48 katika jimbo la Mufindi Kusini havina umeme. Naibu wa Nishati na madini alikuja na kuahidi kuwa Serikali itapeleka umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afya, naomba sana Serikali kujenga kituo cha Afya katika Kata ya Makungu, Idete, Kiyowela, Luhanga, Mtambula, na Mtwango. Katika kata hizi wananchi wanapata shida kubwa ya kukosa vituo vya afya. Pia tuliomba gari la wagonjwa ambalo litahudumia kata tatu, Makungu, Kiyowela na Idete. Bado hilo gari hatujapata na Serikali iliahidi kutoa hilo gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuweza kunifikisha mahali hapa na mimi leo hii niweze kuchangia hoja hii muhimu iliyopo mbele yetu. Napenda vilevile kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuandaa hotuba nzuri ya bajeti yenye mlengo chanya kwa mafanikio, maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inatupa mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge, hakika ni mwelekeo mzuri na wa kupongezwa sana, kwani imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kufanya ziara maeneo mbalimbali na nimshukuru pia kwa kufanya ziara jimboni kwangu Kibaha Vijijini, ziara zake zimekuwa na tija kubwa sana kwa maendelo ya wananchi, na kufungua fursa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa hii kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali ilizochukua kwa maendeleo ya Taifa letu, hatua ya kuhamia Dodoma na kuwa Mji Mkuu wa nchi yetu ni hatua nzuri na ya kuthubutu, kwani maamuzi yalishafanywa hapo awali na ilikuwa bado utekelzaji tu. Yatupasa kuunga mkono jitihada hizi na kuishauri Serikali kwa namna yoyote katika uboreshaji wa mkakati huu ambao tayari umeshaanza kwa Wizara mbalimbali kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kila mpango huja na changamoto zake, vivyo hivyo katika mpango huu wa kuhamisha Makao Makuu ya nchi yetu kuja Dodoma unachangamoto mbalimbali, changamoto hizi ni pamoja na mipango miji, barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam na miji mingine leo hii tunaona kwa namna gani tulichelewa katika kupanga miji yetu na leo hii miji haijapangika, tumekuwa na changamoto mbalimbali ambazo ni wajibu wetu kuzichukua kama fursa na kuja nazo Dodoma na kuziboresha hivyo kuepuka makosa yaliyofanyika katika miji mingine hususan mji wetu wa Dar es Salaam hayana budi kutokutokea katika Mji wetu wa Dodoma. Mipango Miji ipangwe vizuri, kutengwe maeneo ya viwanda, makazi ya watu, ibada, vituo vya mafuta, shule, hospitali, viwanja vya michezo na kadhalika, pia barabara zitengwe maeneo makubwa na ya kutosha ili kuepuka bomoa bomoa za kila mara ambazo tumekuwa tukizishuhudia katika miji mbalimbali, mji wa Dodoma uwe

ni mji wa mfano na wa kihistoria, mitaro ya kupitisha maji *(drainage system)* iboreshwe kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa kufanikiwa kwa kiasi kikubwa mpango wa kutoa elimu bure wenye tija kubwa kwa wananchi wetu ili kila mtoto wa Kitanzania aweze kupata elimu. Uwajibikaji na nidhamu katika utumishi wa umma umekua kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na hapo awali ingawa bado zinahitajika juhudi zaidi kufanywa na Serikali ili hii dhana ya uwajibikaji iwe endelevu na yenye tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado tuna changamoto ya upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi. Napenda kuishauri Serikali yangu sikivu kuzichukua changamoto hizi kama fursa kwa kuboresha maeneo hayo kwa maendeleo ya wananchi wetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kugusia suala zima la ukuaji wa uchumi nchini. Serikali imeainisha ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2016/2017 unaonesha uchumi wetu unazidi kuimarika. Kwa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu, ukuaji halisi wa Pato la Taifa ulifika 7.0% mwaka 2016, pongezi kwa Serikali ila kuna changamoto nyingi sana katika ukuaji wa uchumi kwa ujumla na ukilinganisha na uchumi wa mtu mmoja mmoja, wananchi wengi ambao vipato vyao ni vidogo na maskini wamekuwa wakiendelea kulalamika hali ngumu ya maisha, mifumuko ya bei za bidhaa muhimu kama chakula na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ikiwaumiza sana wananchi na hivyo kutokuona umuhimu wa hizi takwimu za ukuaji ama nafuu ya maisha. Naomba kuishauri Serikali kuwajengea uwezo wananchi ili waweze kukabiliana na changamoto hizi wanazokumbana nazo, Serikali iweze kusimamia vyema mifumuko ya bei isiyokuwa na tija na yenye kumuumiza mwananchi wa kawaida. Serikali isimamie kikamilifu bei za mazao ya wakulima ambao ndio nguvu kazi kubwa hapa nchini, wauze mazao yao kwa faida ya bila vipingamizi vyovyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo ni Serikali ilipoamua kusimamia bei la zao la korosho na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa wakulima kuuza mazao yao kwa faida nzuri. Hivyo naiomba Serikali ifanye pia katika mazao mengine nchi nzima ili wakulima wetu ambao kitakwimu ndio wengi waweze kufaidika na kilimo, waondokane na umaskini na kuona faida hizi za ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishazungumza sana na kuchangia humu Bungeni kwa umakini mkubwa na kuishauri Serikali kuwa viwanda ndio msingi mkubwa wa ukuaji wa uchumi na kumaliza kama si kupunguza tatizo la ajira. Naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano ikiongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli kuja na kipaumbele hiki cha Tanzania ya viwanda. Na mimi nasema Tanzania ya viwanda inawezekana kwa kuungana sote na kuunga mkono jitihada hizi kwa manufaa ya nchi yetu ili tuondokane na changamoto nyingi tunazokabiliana nazo za ajira kwa vijana wetu ni lazima tuwekeze katika viwanda kwani malighafi mbalimbali tunazo hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi tajiri kiuchumi duniani ni maamuzi ya uwekezaji wao katika viwanda kwa muda mrefu. Mkoa wetu wa Pwani una viwanda takriban 89, viwanda hivyo viko katika maeneo mbalimbali ya mkoa lakini mpango kazi wetu ni kuzidi kutafuta wawekezaji ili waje kuwekeza katika mkoa wetu hususan Kibaha vijijini kwani tuna maeneo makubwa yametengwa kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto mbalimbali katika sekta ya viwanda hususan katika utoaji wa vibali vya mazingira. Nashauri vibali hivyo vya mazingira viwe vinatolewa kwa eneo zima ili kuepuka usumbufu wa mtu mmoja mmoja kufanya maombi ya vibali hivyo. Kibaha Vijijini kama nilivyosema hapo awali tuna maeneo ya kutosha ambayo tayari yameshatengwa kwa shughuli husika. Niliishauri Serikali humu humu Bungeni kuhusu suala la bandari kavu iliyopo Kwala, bandari hii iwe maalum kuegesha magari yote *(used),* kwa maana kuziondoa *yard* za kuuzia magari *(used)* ambazo zimezagaa kila kona ya Jijini Dar es

Salaam na hivyo kuwepo sehemu maalum ya mtu akitaka magari *(used)* anajua wapi pa kwenda hili limefanyika katika nchi nyingi sana zilizoendelea kama Dubai na kadhalika, huwezi kukuta kila kona ya mji kuna *yard* ya kuuzia magari. Hizi *yard* zimekuwa zikiharibu mandhari ya miji yetu na uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hilo pia la bandari kavu kuwepo na upatikanaji wa *spare* tofauti tofauti za magari pamoja na mashine mbalimbali. Hiyo itapelekea kuondokana na maeneo ya mijini kutapakaa maduka ya *spare* hovyo kama ilivyo hivi sasa mtaa wa Shaurimoyo. Hatua hii ikikamilika watu watajua wakitaka magari yaliyotumika yote ama *spare* zote basi wanakwenda Kwala Kibaha Vijijini na kufanya manunuzi. Itasaidia kuwa na sehemu moja tu ambayo utapata hitaji lako ama gari au *spare.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili, Serikali tayari imeshaonyesha nia kwa kutenga maeneo kama ilivyo jimboni kwangu. Kilichobaki ni utolewaji wa elimu na uhamasishaji kwa sekta binafsi kuziona fursa hizi na kuzifanyia kazi. Hatua hii ikishakamilika Serikali itapata fursa ya kuanzisha njia ya treni kutoka Dar es Salaam mpaka Kibaha kuwarahisishia wananchi watakaokuwa wakienda bandari kavu hiyo. Serikali kupata fedha za uendeshaji, vilevile Mkoa wa Pwani hivi sasa umekuwa na watu wengi sana. Kupatikana kwa usafiri wa treni hiyo kutawasaidia watu wengi sana kutatua changamoto ya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio changu cha muda mrefu ni miundombinu ya barabara na mambo mengine mengi, ila kuna hii barabara ya Makofia, Mlandizi na Mzenga ina miaka sita sasa tunazungumzia ujenzi wa barabara hii. Wananchi wamekuwa wakipata shida sana katika shughuli zao za kila siku kutokana na hii barabara, shughuli zao za kiuchumi zimekuwa zikizorota. Naiomba Serikali hii sikivu sasa katika bajeti hii wakamilishe ujenzi wa barabara hii. Wananchi wale na wao waone faraja na kuanza kutumia barabara nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii tunaomba fedha zitengwe na barabara hiyo iweze kukamilika. Hata hivyo, niipongeze Serikali kwa jitihada kubwa zinazoendelea kuzifanya kwa kuleta miradi mikubwa ya barabara za juu makutano ya TAZARA, daraja jipya la Salender, ujenzi wa barabara Dar es Salaam – Chalinze kiwango cha *express way* bila kusahau ujenzi wa barabara za juu *(interchange)* kwenye makutano ya barabara ya Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni hatua muhimu za kimaendeleo katika kukabiliana na changamoto ya msongamano wa magari. Vilevile Mji wa Mlandizi kutokana na kukua kwa kasi, kuna uhitaji wa makutano ya barabara ili kurahisisha watumiaji na kuufanya uwe wa kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa jitihada kubwa inazochukua katika kulinda na kufuatilia sekta nzima ya madini. Hatujachelewa bado na jitihada zilizoanzishwa na Mheshimiwa Rais ni mwanga tosha kwa sasa. Kazi imeanza na kama kulikuwa na upotevu wowote wa madini yetu au ukwepaji wa kodi sasa kila kitu kitakuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuunda Tume Maalum ya kufuatilia suala zima katika sekta ya madini. Kama tutaitumia vizuri, basi Taifa litanufaika sana na kupata maendeleo katika nyanja mbalimbali hapa nchini. Madini ni kitu ambacho hakipatikani kila sehemu au nchi madini ni bidhaa adimu sana, hivyo tukifanya maamuzi katika utulivu wenye tija basi hatua stahiki zichujuliwe na hizo changamoto tuzichukue kama fursa na kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusimamie madini yetu yote kwa uadilifu mkubwa, zaidi madini ambayo hayapatikani sehemu yoyote duniani zaidi ya hapa kwetu tuyape thamani na kuyasimamia kwa faida ya Taifa letu ili pato la kodi liweze kuongezeka na kuleta maendeleo kwa wananchi. Vivyo hivyo, tuwawezeshe wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwatolea kodi kwa vifaa watavyoagiza ili kuwapa motisha katika kazi zao za uchimbaji. Tuwathamini wazawa ambao

ni wachimbaji wadogo kwani wametengeneza ajira hivyo kutokuwapa kipaumbele wao na kuwapa wageni tunawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wafugaji na wakulima imeendelea kuibuka maeneo mbalimbali nchini na chanzo cha migogoro hiyo ni ardhi ambayo imekuwa ikigombaniwa. Naipongeza Serikali kwa jitihada zake katika kutatua na kupambana na migogoro hiyo, ila naishauri Serikali kupitia watumishi wake, maafisa mifugo kuanza kutoa elimu kwa wafugaji kufanya ufugaji wa kisasa ambao hauhitaji kuwa na kundi kubwa la ng'ombe ambao baadaye madhara yake mfugaji anashindwa kuwa na chakula cha kujitosheleza na hivyo kupelekea migogoro kuibuka, kutoa elimu kwa wafugaji kulima nyasi zao wenyewe na kuzihifadhi vizuri ili kipindi cha kiangazi waweze kuzitumia nyasi hizo. Kufanya hivyo kutapunguza sana hii migogoro na kurudisha hali ya kuaminiana na kupendana baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa umepita tangu kuomba kuwekewa kivuko cha kuvukia watu na usafiri, *Ruvu Station,* Soga, Mpiji, Kwala, Magindu, kukosekana kwa vivuko hivyo kunapeleka wananchi kuwa katika hali ya hatari sana kwani maeneo hayo hayana alama yoyote. Kwa kuwa kikwazo kwa wananchi kufanya shughuli zao za kila siku pindi wanapotaka kuvuka ama kuvusha vitu mbalimbali.

Naomba katika bajeti hii sasa tupewe kipaumbele kwa maeneo hayo kuwekewa vivuko, vilevile kuna uhitaji mkubwa sana kwa maeneo tajwa hapo kuwa na vituo vya treni ili kuwarahisishia wananchi hawa pindi kukiwa na vituo kutakuwepo na fursa mbalimbali maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya mawasiliano bado imekuwa kubwa hapa nchini kwetu. Jimboni kwangu Kibaha Vijijini ni wahanga wa changamoto hii kwani kuna maeneo mengi hakuna kabisa mawasiliano ya simu kwa kuwa hakuna hata kampuni moja ya simu

inayopatikana maeneo hayo. Dutumi, Mpelamumbi, Miyombo, Gwata, Msua hakuna mawasiliano kabisa. Tunaomba minara ya Tigo, Vodacom na Airtel, hakika kwa wananchi wangu hii imekuwa ni kero ya muda mrefu sana. Hata hivyo, naipongeza Serikali kwa hatua yake nzuri ya kukamilisha kituo kimoja cha kuhifadhia taarifa na mifumo ya Serikali *(Government Data Centre)* na Serikali haina budi kuzihamasisha Ofisi za Serikali kutumia mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu zote nilizokuwepo humu Bungeni, nimekuwa nikilisema hili la Kituo cha Afya Mlandizi kupandishwa hadhi. Sifa na vigezo tunavyo. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Awamu ya Tano walitoa ahadi ya kukipandisha hadhi kituo hiki na kuwa hospitali. Lakini Awamu ya Nne imepita bila kituo hiki kupandishwa hadhi. Sasa tuko Awamu ya Tano, naomba ahadi hii sasa itekelezwe kwani Mheshimiwa Rais akitoa ahadi, kinachofuata ni utekelezaji kwa mamlaka husika. Hivyo, mimi na wananchi wangu tungeshukuru sana katika bajeti hii maombi yetu ya muda mrefu na ahadi za Marais wawili zilitekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimeona bajeti ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba imeongezeka kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 251 mwaka 2016/2017. Ni jambo jema na la kupongezwa ila rai yangu kwa Serikali na mamlaka husika kumekuwa na changamoto za upungufu wa dawa katika vituo vyetu vya afya, zaidi dawa kuchelewa kufika kwa wakati. Naamini kwa ongezeko la bajeti basi changamoto hizi hazitakuwepo tena na kuleta nafuu kwa wananchi kupata dawa kwa wakati na kuwaondolea usumbufu wa kukosa dawa pindi wanapoandikiwa dawa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama yetu ya Kibaha Vijijini ina changamoto mbalimbali ila kubwa zaidi ni jengo. Jengo lake haliko katika hali nzuri. Katika michango yangu kila mwaka humu Bungeni, mbali na jitihada zangu binafsi za kuonana na Waziri mhusika nimekuwa nikilizungumzia takriban miaka sita bila matumaini yoyote. Naomba Serikali

katika bajeti hii basi ituangalie kwa jicho la huruma na sisi tupate jengo la Mahakama. Napenda pia kuikumbusha Serikali kufikisha fedha za bajeti kwa wakati katika Halmashauri zetu kwani bajeti inapita lakini fedha zinachelewa na kuzorotesha shughuli za kimaendeleo. Fedha zikifika kwa wakati na miradi ya kimaendeleo itawafikia wananchi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, napenda kugusia kidogo suala zima la vita dhidi ya dawa za kulevya. Hili ni janga kubwa kitaifa na duniani kote. Dawa za kulevya zimekuwa zikiwaathiri hasa vijana wetu, nguvu kazi ya Taifa. Ndoto za vijana hawa zimekuwa zikisitishwa na kujiingiza katika kutumia dawa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza na kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuonyesha dhamira ya dhati kabisa ya kupambana na vita hii. Kwanza kwa kuteua watendaji wakuu watakaosimamia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Mamlaka hii ina nguvu ya kukamata, kupeleleza na kushtaki watuhumiwa wanaohusika na biashara ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe na Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kunipa nafasi ya kusimama na kutoa mchango wangu katika hoja hii muhimu ya mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza Serikali ya CCM kwa kutimiza mwaka mmoja kwa mafanikio makubwa katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ikiwa ni pamoja na Serikali kuhamia Dodoma. Naungana na mpango wa Serikali kuufanya Mji wa Dodoma kuwa mji wa kisasa uliopangwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake kwa kuandaa hotuba nzuri iliyogusa nyanja zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimejielekeza katika kutoa mchango wangu katika mambo matatu yafuatayo:-

(i) Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi;
(ii) Maji; na
(iii) Afya, elimu na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa15 – 17 wa hotuba ya Waziri Mkuu taarifa inaonyesha jitihada zilizofanywa na Serikali katika kuwezesha wananchi kupitia mipango na programu mbalimbali kwa kuwekeza nguvu zaidi kwa wanawake na vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupongeza Serikali nina ushauri katika maeneo yafuatayo; wanawake ndio nguvu kazi, wanawake ndio walezi wa familia, unapomkomboa mwanamke kiuchumi unakomboa familia na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shilingi milioni 50 kwa kila kijiji; katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka wa fedha uliopita 2016/2017 Bunge lilipitisha fedha ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa kupeleka shilingi milioni 50 kila kijiji katika baadhi ya mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua ni kiasi gani cha fedha kilitolewa na kilipelekwa katika mikoa ipi, na ni vikundi vingapi vilikopeshwa vikiwemo vya wanawake na Vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kujua ni kiasi gani cha fedha kimetengwa na ni mikoa gani na mingapi itapelekewa fedha hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ningependa kujua ni mamlaka gani imepewa jukumu la kusimamia mpango wa shilingi milioni 50 kila kijiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kutoka Serikali Kuu umekuwa ni mkombozi. Kwa vipindi vya miaka ya hivi karibuni na hata bajeti ya mwaka 2017/2018 mfuko huu haukutengewa fedha, naishauri Serikali itenge na kutoa fedha kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya vikundi vya wanawake kama ilivyofanyika kwa vijana, kutotenga fedha kwa ajili ya wanawake ni kurudisha nyuma jitihada za wanawake katika kujikomboa kiuchumi kwa sababu mfuko huu unaotolewa na Wizara ulikuwa ni ukombozi kwa vikundi vya wanawake badala ya kutengewa asilimia 10 ya mfuko wa wanawake na Halmashauri tu ambao pia hakuna uhakika kwa sababu Halmashauri nyingi hazitengi na kutoa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo katika Halmashauri kutotenga asilimia 10 kwa ajili ya mfuko wa vikundi vya maendeleo ya wanawake na vijana katika Halmashauri zetu. Naomba kutoa ushauri kwamba kwa kuwa utaratibu wa kutoa fedha hizo asilimia 10 ya vikundi vya wanawake na vijana ni maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu miaka zaidi ya 20 iliyopita, naishauri Serikali kuleta muswada ili Bunge litunge sheria itakayoweka utaratibu wa kutenga, kutoa na kurudisha fedha hizo kwa vikundi vya maendeleo ya wanawake na vijana kuliko ilivyo sasa, kwani jambo la kutoa fedha hizo limebaki kama ni jambo la hisani na si jambo la lazima kwa sababu hakuna sheria inayotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kila unapofanyika ukaguzi linatokea tatizo la kutotoa fedha vikundi vya wanawake na vijana na katika Halmashauri zilizo nyingi zimeonyesha yapo madeni makubwa. Hapa ningependa kusikia kauli yako Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya ulipaji wa madeni haya ili fedha hizi zielekezwe katika kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, riba katika taasisi zinazotoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na wananchi; pamoja na kuzipongeza taasisi za fedha kwa kutoa mikopo midogo na mikubwa kwa vikundi vya wanawake na vijana. Lipo tatizo katika baadhi ya taasisi za fedha viwango vyao vya riba ni vikubwa sana mpaka kufikia asilimia 35 jambo ambalo husababisha wanawake na vijana kushindwa kujikomboa kiuchumi, badala yake wameambulia kufanya kazi za uzalishaji na kuwanufaisha waliowapa mikopo na wao kuambulia kutaifishiwa mali zao kwa mfano vifaa vya nyumbani kama vitanda, magodoro, vyombo na kuuziwa mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba naiomba Serikali itoe riba elekezi kwa taasisi zote zinazotoa mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana lengo likiwa ni wanawake na vijana wanufaike na mikopo hiyo kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake ilianzishwa kuwakomboa wanawake waishio vijijini na mijini ambao hawana fursa za kufika taasisi nyingine za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, naomba Serikali itoe fedha kwa Benki hii ili ipate mtaji wa kufungua matawi katika mikoa yote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake pia yaangaliwe upya kwa sababu masharti hayatofautiani na masharti ya benki zingine, hivyo wanawake walio wengi hasa waliolengwa na kuanzishwa kwa benki ni wanawake wanyonge ambao hawana mali za kuweka kama dhamana wanashindwa kukopa katika benki hii. Hivyo malengo ya kuanzishwa kwa benki hii bado hayajafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali irejee upya masharti ya kutoa na kurudisha mikopo ili benki hii ya wanawake iwe ni mkombozi kwa wanawake na Watanzania kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maji, katika ukurasa 38 – 39 Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kwa kina jitihada zinazofanywa na Serikali za kujenga miundombinu ya maji. Naipongeza Serikali kwa kazi kubwa ya kujenga miundombinu ya maji katika miji mbalimbali hapa nchini. Pia katika ukurasa wa 38 – 39 taarifa inaonyesha kuwa kufikia mwezi Julai na Desemba, 2016, miradi 90 ya miundombinu ya maji vijijini ilikamilika na kufanya mradi iliyokamilika kuwa 1,301 na kubakia miradi 509.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, suala la maji bado ni tatizo kubwa sana, wanawake bado wanatembea umbali mrefu kwenda kutafuta maji, wanawake bado wameshindwa kushiriki shughuli za kiuchumi kwa sababu wanatumia muda mrefu kwenda kutafuta maji, bado dhamira ya CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwatua wanawake ndoo kichwani bado haijafikiwa kiwango kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali yafuatayo:-

(a) Kutafuta fedha za kutosha hata kama ni kwa mkopo kwa ajili ya utekelezaji wa miundombinu ya maji hasa vijijini.

(b) Serikali na Bunge likubali kuongeza tozo ya mafuta ya petroli na dizeli kutoka shilingi 50 kila lita ya mafuta hadi shilingi 100 katika kila lita ya mafuta. Fedha zitakazopatikana zielekezwe katika ujenzi wa miundombinu ya maji hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo baadhi ya miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji iliyopangwa kutekelezwa kwa fedha za nje mfano, ujenzi wa mradi wa maji Mwanga, Same hadi Korogwe, ujenzi wa mradi wa maji Mgango, Kiabakari, Butiama, ningepeda kujua fedha za kutekeleza miradi hii zimekwishapatikana na mradi wa Mwanga, Same na Korogwe upo katika hatua gani? Je, mradi wa Mgango, Kiabakari na Butiama unaanza lini? Kwa sababu mpango wa mradi huu ni wa muda mrefu sana. Mradi wa Muyayango,

Sokoni Butiama ni miradi ya muda mrefu lakini mpaka sasa miradi hii ya Mgango, Kiabakari Butiama haijaanza na Mwanga, Same na Korogwe ni wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya katika ukurasa wa 39 Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kazi inayofanywa na Serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata afya bora kwa kuboresha miundombinu na upatikanaji wa vifaa tiba pamoja na kuimarisha huduma ya mama na mtoto ili kupunguza vifo vya wanawake na watoto pamoja na kazi nzuri ya Serikali, naomba kuishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka mikakati itakayopunguza vifo vya wanawake wanaofariki kwa kujifungua kwa mujibu wa utafiti uliofanyika unaonyesha kuwa kila saa moja mwanamke mmoja anafariki kwa tatizo la kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi vituo vya afya ambavyo havijakamilika Serikali ijitahidi kukamilisha vituo vya afya vilivyojengwa ambavyo havijakamilika. Serikali ijitahidi kutafuta fedha na kukamilisha miundombinu ya vituo hivyo ili viweze kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vituo vipya vya afya kila Kata; naishauri Serikali itafute fedha na kujenga vituo vya afya kila mwaka tuwe na vituo vya afya kila Halmashauri za Wilaya vinavyojengwa ikiwa ni hatua muhimu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu; naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kutoa elimu isiyo na malipo pamoja na pongezi, nashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuongeza madarasa katika kila shule ya msingi kwa sababu ongezeko la wanafunzi limeleta tatizo la ukosefu wa madarasa ya kutosha.

(ii) Ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari kwa sababu watoto wetu na hasa watoto wa kike wanapata adha kuishi mtaani, kutembea umbali mrefu jambo linasababisha pia mimba za utotoni.

(iii) Kuongeza nyumba za walimu na maslahi ya walimu.

(iv) Upungufu wa walimu wa sayansi, hapa ningependa kujua Serikali kwa sasa ina mkakati gani wa kuongeza walimu hao wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, nashauri Serikali iongeza wigo kwa kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yanayozungukwa na maziwa na mito na maeneo yenye ukame ili kuongeza upatikanaji wa chakula kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi wa lini uwanja wa ndege wa Lindi utakarabatiwa na kutoa huduma za ndege kama ilivyokuwa kwa hapo awali? Uwanja huu ni miongoni mwa viwanja vya ndege vya zamani hapa nchini lakini pia ni uwanja mkubwa wenye barabara nyingi za kurushia ndege. Uwanja huu umechakaa sana kiasi cha kufanya ndege kuacha kutua jambo ambalo linasababisha usumbufu mkubwa kwa wakazi wa Lindi ikizingatiwa kuwa hivi sasa Lindi iko mbioni kuanza mradi wa *LNG* hivyo kuna haja ya kuboresha uwanja huu ili kurahisisha usafirishaji kwa njia ya anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu ombi la Mfuko wa Maafa ulio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuweza kusaidia katika maeneo mbalimbali ya jimboni kwangu ambapo miundombinu ya madaraja yamebomolewa na mafuriko yaliyotokea mwezi wa tatu mwaka huu wa 2017. Madaraja na barabara zilizoharibiwa na mafuriko ni barabara ya Mkwajuni - Namkongo; barabara ya Milola - Nangaru; pamoja na barabara ya Kitomanga - Mvuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli kabisa barabara hizo zimeharibika sana na fedha kidogo zinazotolewa na mfuko wa barabara haziwezi kujenga madaraja hayo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana mfuko wako wa maafa usaidie kujenga walau madaraja yaliyopo katika barabara tajwa hapo juu.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa uwezo walau wa kukamata kalamu na kuandika haya machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianzie mchango wangu wa bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika ukurasa wa 10 wa kitabu chake kwenye mada ndogo ya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki tumeelekezwa kuwa hali ya siasa nchini ni shwari ambapo ukiangalia kwa umakini unaona kuwa kauli hiyo haina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2015 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizuia Vyama vya Siasa kutofanya kazi zake kama ilivyoelekezwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Vyama vya Siasa vina viongozi wake waliochaguliwa kwa mujibu wa Katiba zao ukiachia mbali na Wabunge. Unapomruhusu Mbunge kufanya mikutano ya hadhara katika Jimbo lake lakini ukamzuia Mwenyekiti au Katibu Mkuu kutofanya mikutano katika maeneo yaliyomo ndani ya nchi ni kinyume na Katiba na kwa maana hiyo hatuwezi kusema kuwa hali ya siasa ni shwari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la demokrasia ambalo limeelezewa ukurasa 11 wa kitabu cha bajeti ni kweli kwamba nchi yetu inajenga demokrasia lakini demokrasia kama tunavyojua ina uwanja mpana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, demokrasia ni pamoja na uhuru wa watu wa kutoa maoni yao, uhuru wa vyombo vya

habari, uhuru wa kukosoa na kukosolewa kwa Serikali iliyo madarakani na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nchi hii inashuhudia jinsi raia wanavyoishi kwa woga na hofu, kosa ni kuisema Serikali. Vyombo vya habari navyo vinashindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi huku vikijua kwamba kukosoa mamlaka ya dola ni kujitafutia balaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vielelezo vyote hivyo ni uthibitisho tosha kwamba suala la demokrasia tunalihubiri tu, lakini kivitendo halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Msajili wa Vyama vya Siasa nchini ni kwamba tunaelewa fika kwamba yeye si muamuzi wa kuwachagulia vyama vya siasa viongozi wa kuwaongoza. Ofisi hii ipo kwa mujibu wa Katiba kwa lengo la kusajili vyama vya siasa na pia kuvishauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msajili wa Vyama vya Siasa hana mamlaka ya kuwachagulia wala kuwapangia vyama vya siasa viongozi ambao kwa mujibu wa Katiba za vyama hivyo si viongozi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vya siasa vinaongozwa na Katiba zao, lakini mbali na Katiba zao, pia kuna Katiba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Msajili wa Vyama vya Siasa atuelekeze ni Katiba ipi kati ya hizo tatu inayotoa uhuru wa kiongozi kujiuzuru na baadaye akarejea kwenye nafasi yake hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo ambayo Lipumba alijiuzulu na baadaye Ofisi ya Msajili ikamtambua kama Mwenyekiti halali wa chama, tunamuomba Msajili wa Vyama kama vile ambavyo anaheshimu maamuzi ya vyama vingine kwani vyote ni sawa kwa matakwa ya Katiba zao.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi, aidha nipende kuchangia katika Wizara hii ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi, ninaipongeza Serikali yangu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa mipango mizuri ya kuinua uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba ya Waziri Mkuu, kimsingi inaonyesha ukusanyaji wa mapato umepanda toka shilingi bilioni 850 mpaka trilioni 1.2, hii ni hatua nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze udhibiti na usimamizi bora katika haya yafuatayo:-

(i) Matumizi bora ya fedha inayopatikana;

(ii) Kuziba mianya ya rushwa ambayo ilikuwa imekithiri;

(iii) Kukomesha ubadhirifu wa mali ya umma kwa kuchukua hatua stahiki; na

(iv) Wizi wa mali ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo imeleta imani kubwa sana kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kubwa sana katika afya, elimu, miundombinu, kilimo. Katika mkoa wangu wa Ruvuma ambao unajumuisha Wilaya sita zenye jumla ya majimbo tisa ambayo ni kama ifuatavyo; Songea Mjini, Peramiho, Madaba, Namtumbo, Tunduru Kusini, Tunduru Kaskazini, Mbinga, Mjini, Mbinga Vijijini, Nyasa.

(i) Upungufu wa madarasa baada ya sera ya elimu bure kutekelezwa;

(ii) Vifaa vya kufundishia;

(iii) Madeni ya walimu; na

(iv) Nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya ndipo penye changamoto lukuki, hapa nitaeleza chache na nyingine nitachangia kwenye Wizara ya Afya:-

(i) Kuna kituo cha afya cha Mjimwema katika Manispaa ya Songea kinahudumia wananchi wengi sana lakini mgao wa dawa wanaopata ni mdogo sana, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mgao wa dawa ikiwa ni pamoja na kukamilisha vifaa vya chumba cha upasuaji ili akinamama ambao wanakufa kwa kukosa huduma za upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hicho cha Mjimwema kipo kwenye mchakato wa kupandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya tangu mwaka jana, ni lini mchakato huo utakamilika?

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kituo cha afya cha Lusewa (Mji Mdogo) Wilayani Namtumbo ambacho hakina gari la wagonjwa wala vifaa vya upasuaji. Kituo hicho kiko katika jiografia ifuatayo:-

(a) Kutoka Lusewa - Namtumbo - kilometa 80;
(b) Kutoka Lusewa - Songea Mjini - kilometa 150; na
(c) Kutoka Lusewa - Mbesa Wilayani Tunduru - kilometa 150

Mheshimiwa Mwenyekiti, adha wanayoipata wananchi wa Lusewa ni kubwa mno na inatia huruma sana, nimeshuhudia mama anayejifungua akibebwa katika tenga mithiri ya nyanya katika pikipiki akiwa anasafirishwa kilometa 150 toka Lusewa. Pata picha halisi ni maumivu kiasi gani anayopata mama huyo, hivyo basi akina mama wengi sana wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba yafuatayo kupitia kituo hicho cha afya cha Lusewa; gari ya wagonjwa, vifaa vya upasuaji, dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya miundombinu katika Mkoa wa Ruvuma bado ni tete. Barabara ya kilometa 124 - Lokujufusi - Mkenda bado haijaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami, barabara ya Lumecha - Londo Morogoro bado haijaanza, barabara ya Minga -Nyasa kilometa 66 bado haijaanza, bara bara ya Kitahi - Lituhi bado haijaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mpainduzi kupitia *ATCL* imenunua ndege sita, kati ya hizo mbili zimeshawasili na zimeshaanza usafirishaji kwa abiria katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini ndege (usafiri wa anga) utaanza kutoa huduma katika Mkoa wangu wa Ruvuma? Ikumbumbwe kuwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma nao pia ni miongoni mwa Watanzania ambao wanahitaji usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa usafiri huu wa anga kupitia shirika letu la ndani la *ATCL* lianze safari Ruvuma kabla hizo ndege hazijachakaa au kabla ya Bunge hili la bajeti kuisha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo pia kuna changamoto zituatazo; upungufu wa mbolea ya ruzuku, mbegu zinazoletwa nyingine ni *fake,* pembejeo za kilimo kutokufika kwa wakati katika vituo vinavyotoa huduma, masoko ya uhakika na upungufu wa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisimama mara kwa mara kuomba Wizara ya Kilimo kuleta huduma ya kibenki kwa maana ya Benki ya Kilimo ili kukuza mitaji ya wakulima wa Ruvuma ili waweze kupata fursa ya kukopa na kukuza mitaji yao na kufanya kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaimani unatambua kuwa Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa yenye mvua ya uhakika hivyo hitaji la benki ni muhimu ili kusaidia wananchi waweze kuzalisha kwa wingi kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania, kwa sababu wakizalisha kwa wingi itakuwa neema kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya maji katika Mkoa wa Ruvuma ni kubwa sana, wananchi bado wanakosa maji safi na salama. Kuna miradi ya maji ambayo ilijengwa na *World Bank,* miradi hii kwa taarifa za maandishi inaonekana imekamilika lakini kiuhalisia maji hayatoki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya maji ya *World Bank* imetumia fedha nyingi sana lakini haijazaa matunda. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha miradi hii inakamilika na inatoa maji? Miradi hii ipo katika Wilaya ya Namtumbo, Mbinga Vijijini na Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali yangu iendelee kuangalia vipaumbele kwa wananchi ikiwemo maji na kwenye maeneo ya vijijini vichimbwe visima virefu wakati mchakato wa maji ya mtiririko unaendelea basi wananchi waanze kutumia maji ya visima virefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali yangu haya yafuatavyo; zahanati na vituo vya afya vikamilishwe, vifaa tiba na dawa katika vituo vya afya vizingatiwe, pembejeo za kilimo zifike kwa wakati katika vituo vya kusambazia pembejeo, utafiti wa mbegu bora uzingatiwe ili kuleta tija kwa wakulima, ujenzi wa barabara zote nilizoainisha kwa kiwango cha lami, mawasiliano ya simu katika tarafa ya Wino kupitia Halotel ufanyiwe kazi haraka, vita dhidi ya dawa za kulevya uendelee, kulipa stahiki za walimu na madeni ya ndani yalipwe kwa watoa huduma za ndani (wazabuni).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaomba pia mchango wangu huu wote uingie kwenye *Hansard.*

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri na hasa ya ziara zake mikoani na busara anazozitumia katika utatuzi wa changomoto mbalimbali. Pia niwapongeze Mawaziri Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Antony Mavunde na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nianze mchango kwa mambo yafuatayo; ucheleweshaji wa pesa za maendeleo katika miradi ya maendeleo. Kutokana na pesa za miradi kucheleweshwa katika Halmashauri zetu kunasababisha miradi mingi kutokamilika kwa wakati na pia kuongezeka kwa gharama za miradi *variation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Manispaa yetu ya Iringa iliyopo katika Jimbo la Iringa Mjini kuna mradi wa machinjio ya Ngerewala. Mradi huu mzuri lakini umeanza toka mwaka 2007. Mradi huu ukikamilika ungeweza kutoa ajira kwa wananchi wa Iringa zaidi ya 200.

Mheshimwa Spika, nashauri ni vema Serikali ingetoa pesa katika mradi huu kiasi cha shilingi bilioni moja ili Halmashauri isiingie kwenye mkataba mbovu wa miaka 25. Pia atafutwe mtaalam mshauri ili asaidie mradi huu uendeshwe kwa faida kwa sababu hiki ni chanzo kizuri sana cha mapato. Mfadhili akipata atapandisha bei ya uchinjaji na kusababisha wachinjaji kuchinjia mtaani na inaweza pia kusababisha bei ya nyama kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Jamii, nipongeze jitihada zinaofanywa na mifuko ya jamii ya *NSSF, LAPF, PPF, GEPF, PSPF* na *NHIF* kwa kukubali wito wa kuanza kujenga viwanda ikiwemo ufufuaji wa kinu cha kusaga mahindi. Lakini niiombe Serikali iweze kulipa madeni inayodaiwa na mifuko hiyo ili viwanda vijengwe ambavyo vitasaidia kukuza uchumi na kuongeza ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fao la kujitoa, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kujali wafanyakazi pale

wanapostaafu au wanapoacha kazi, lakini sheria ya kuzuia wafanyakazi kujitoa kwenye mifuko pale ajira zao zinapokomaa hadi mfanyakazi atimize miaka 60 hili ni tatizo kubwa sana kwa sababu ajira za wafanyakazi zimetofautiana. Mfano sekta ya ujenzi, sekta ya kilimo na sekta ya kazi za majumbani si rahisi wafanyakazi wa sekta hizo kufikisha miaka 60 tunashauri sheria hiyo itofautishe sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watu wenye ulemavu, niipongeze Serikali kwa kuwatambua watu wenye ulemavu nchini lakini bado wanachangamoto hasa katika suala la usafiri, bado vyombo vya usafiri sio rafiki, ni lini Serikali italiangalia hili? Pia ni kwa nini katika ile mikopo ya Halmashauri na wao wasitambulike kutengewa asilimia zao katika asilimia tano ya vijana na akina mama? Walemavu wengi ni wajasiriamali lakini hawakopeshwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumza kuhusu kumtua ndoo kichwani mwanamke. Katika Mkoa wetu wa Iringa limekuwa ni tatizo kubwa sana hasa katika maeneo ya vijijini. Kinachosikitisha Serikali imekuwa ikitumia pesa nyingi sana kwa miradi ya maji lakini maji hayatoki kama miradi ya Ilindi, Ng'uruhe, Ihimbo, Iparamwa Ruaha Mbuyuni na Mkosi. Lakini mkoa wetu una Mto Ruaha, Lukosi na Mtitu na chanzo cha Mto Mgombezi. Ni kwa nini mito hii isitumike katika kusambaza maji kuliko hiyo miradi ya visima iliyotengwa. Je, Serikali inawachukulia hatua gani hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii ya hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu umeme wa *REA* Awamu ya Tatu, naomba Serikali inieleze ni lini mradi huo wa *REA* Awamu ya Tatu utafika Kigoma? Na ninaomba utakapofika Kigoma uweze kufika Kasulu hasa katika vijijji vyote vilivyopo katika barabara kuu ya Kigoma - Nyakanazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/2018 unaonyesha kwa kiwango kikubwa Serikali inategemea kukopa fedha katika mifuko hii ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, kukopa sio dhambi, lakini mikopo ambayo inazidi uwezo na kupelekea hatari ya kuua/kufifisha uwezo na kupeleka hatari na lazima Serikali ituambie imejipanga vipi kuhakikisha mifuko hii haifi/kupunguza uwezo wake?

(a) Je, *return on investment* kwa miradi ya namna hii ambayo inachukua muda mrefu kurudisha faida imetazamwa kwa kiwango gani?

(b) Je, *foreseeable risk* kwenye *operation* za viwanda na miradi inayowekezwa imefanyika *assessment* kina?

(c) *SSRA* ambaye ni mdhibiti na msimamizi wa mifuko hii inaweka ukomo/kiwango kwa mifuko kutokopa zaidi ya 20%. Hata hivyo kwa taarifa ya Benki Kuu ya mwaka 2016 inaonyesha kuwa *proportion* ya mifuko kwenye deni la ndani ni 26% kutoka 16% na imechukua nafasi ya mabenki ya biashara. Uhai wa mifuko hii upoje? Kwa nini Serikali iendelee kukopa zaidi kinyume na sheria zilizopo?

(d) Kumekuwa na hoja ya muda mrefu wa kuunganisha mifuko hii ya hifadhi ya jamii. Je, lini Serikali itaanza machako wa kuunganisha mifuko?

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa kuja na hotuba nzuri. Naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira kwa vijana. Hivi sasa kuna vijana wengi ambao wamehitimu katika vyuo mbalimbali vya ngazi zote lakini kuna tatizo la vijana kukosa kazi za kuajiriwa ama kujiajiri wenyewe. Tatizo la

ajira lina athari kubwa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Lazima Serikali ije na mpango mahususi wa kuwaajiri au kuwawezesha kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo; hivi sasa kilimo kinaajiri watu zaidi ya asilimia 75; ili nchi iendelee lazima kutoa pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu. Ahadi ya Waziri Mkuu kuwa na bei elekezi ni muhimu sana. Lakini pia mbegu nzuri, kilimo cha kisasa na umwagiliaji ni lazima kwa kipindi hiki. Baadhi ya maeneo tuanzishe mashamba makubwa ya kuanzia kilimo na kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa za kulevya; naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali za kupambana na dawa za kulevya. Ni muhimu vita hii iendelee kwa nguvu zote ili kuiokoa nchi, vijana na Taifa kwa ujumla. Naomba Serikali iongeze nguvu zaidi kuwakamata wauzaji, wasambazaji na watumiaji. Tungependa kusikia Kamishina wa Kupambana na Dawa aongeze kasi na kutupatia taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa; hivi sasa kuna rushwa sana katika maeneo ya Serikali za Mitaa kwa mfano Mbozi hali ni mbaya sana. Naomba vyombo vinavyohusika vichukue hatua za haraka kwani wananchi wanateseka sana.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Kamati ya Bajeti kutambua Mfuko wa Bunge kukabiliwa na changamoto za kutopata fedha za Bajeti kwa wakati na mara nyingine hutolewa zikiwa pungufu jambo ambalo linasababisha shughuli za Bunge kuendeshwa kwa kusuasua ama kubahatisha. Niishauri Serikali iangalie upya utoaji wa fedha za Mfuko wa Bunge kwa wakati na kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 (kifungu na 48). Hata hivyo ni vyema hata kama watatoa kwa kila mwezi basi fedha hiyo itolewe yote ili Ofisi ya Bunge iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; yapo majengo yaliyotelekezwa miaka 10 mfululizo hayajatengewa fedha hususani jengo la Chuo cha Uuguzi Korogwe. Niiombe Serikali (Wizara ya Afya) iangalie upya namna itakavyokamilisha jengo hilo hata kwa kutengewa fedha kidogo kidogo hadi kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi zinazofanywa na hii Wizara ya Ujenzi lakini niishauri Serikali fedha zinazotolewa kwa ajili ya barabara za changarawe hususani maeneo ya mjini kama vile Halmashauri ya Mji wa Korogwe Wizara ianze kuona uwezekano wa kutenga Bajeti kila mwaka angalau kilometa 1 - 2 kupitia bajeti ya *Road Fund*. Aidha, kama haiwezekani basi fedha za barabara za changarawe mijini zitengwe na za kutengeneza mifereji kwa kiwango cha mawe ili kuweka uimara wa barabara hizi.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ya bajeti imegusa kila nyanja ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu, pamoja na kazi inayofanywa na Serikali kwenye sekta hii zipo changamoto nyingi lakini niiombe Serikali kuja na mpango mahsusi wa kuondokana na madeni ya walimu. Niiombe Serikali kuja na mpango wa *teaching allowance* ili iwe motisha kwa walimu kama inavyotoa kwa viongozi yaani *responsibility allowance.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji; naishukuru Serikali kwa kuendelea kuwajali wananchi wa Jimbo la Singida Mjini. Naomba nizungumzie miradi ya vijijini 10 inayofadhiliwa na Benki ya Dunia changamoto kubwa inayojitokeza katika Jimbo la Singida Mjini ni kuwa miradi yote imekamilika akini wananchi hawapati maji tatizo kubwa ni kwamba umefanyika uchakachuzi mkubwa katika ujenzi wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida Mjini tumejaliwa rasilimali ya vyanzo vya umeme:-

(i) Umeme wa upepo na makampuni mawili yaliyojitokeza ni:-

(a) *Power pool*

*(b) Wind East African Company.*

(ii) Umeme wa jua *(solar power)* na kampuni ya *Synohydro* ya China wamejitokeza kuzalisha umeme huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba *TANESCO* ipunguze urasimu katika kutoa *PPA* na pia *TANESCO* inapaswa kuyaacha makampuni kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi milioni 50 kila kijiji, naiomba Serikali yafuatayo; kwanza isomeke shilingi milioni 50 kila kijiji na kila mtaa ili kutoa fursa kwa majimbo ambayo hayana vijiji bali ni mitaa kama Singida Mjini na pia fedha hiyo itoke mapema.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa utekelezaji na usimamiaji mzuri wa mipango ya Serikali iliyoandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya CCM. Hata hivyo napenda kuchangia katika maeneo yafuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama; Ofisi ya Waziri Mkuu itambue kuwa Wilaya ya Mkalama ni moja kati ya Wilaya mpya na huduma za mahakama zinazopatikana katika Wilaya ya Iramba (Kiomboi) na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa na haki kupotea kwa wananchi wa Wilaya hii. Ninaomba katika bajeti ya mwaka 2017/18 Wilaya ya Mkalama ijengewe Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkalama wanajihusisha na kilimo kinachotegemea mvua za msimu lakini kwa bahati mbaya mvua hizo zimenyesha chini ya wastani katika msimu wa mwaka 2016/2017 unaomalizika sasa na ofisi ya Waziri Mkuu imefanya tathimini na kubaini kwamba Halmashauri 55 zimeathirika na ukame. Hivyo

napenda Ofisi ya Waziri Mkuu itambue na kuingiza Wilaya ya Mkalama katika Halmashauri zilizoathirika na ukame kwani kata zifuatazo mvua haijanyesha, Mpambala, Mwangeza, Gemenga na Mafongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya madini inatoa mwongozo wa usimamiaji vizuri wa sekta hii lakini uzoefu unaonyesha kuwa uratibu wa sekta hii ikiwemo utaratibu wa utoaji leseni hauendani na sera iliyopo mfano. Leseni za kuchimba madini ya *gypsum* katika eneo la Dominiku - Mkalama bila wananchi kuhusishwa na hivyo kuzua migogoro kati ya wananchi na waliopewa leseni. Tunashauri Serikali ichukue hatua na kufuta leseni hizo au kuhakikisha wananchi wanapata fidia stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya mipaka na ardhi napenda kuweka bayana kuwa migogoro ya mipaka kati ya Mkoa na Mkoa na Wilaya kwa Wilaya haijapatiwa ufumbuzi ama kama zipo juhudi basi zinaenda kwa mwendo wa kinyonga yaani polepole. Tangu niingie Bungeni nimetoa taarifa za kuwepo mgogoro katika maeneo yafuatayo; mgogoro wa Singida - Manyara na Singida – Simiyu. Migogoro hii ya mipaka inasababisha migogoro na mapigano kati ya Wilaya zifuatazo; Mkalama - Mbulu, Eshijeshi - Iranoto, Mkalama - Mbulu, Singida A – Singida B, Mkalama - Singida Vijijini, Mkarama - Iramba na Mkalama - Nyahaa – Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume iliyoundwa naamini haina taarifa hizi na wapo wananchi wameumizwa kwa mapanga. Nashauri suala hili litolewe maagizo maalum lishughulikiwe.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu katika bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu na hususani kuhusu maendeleo ya vijana nchini ofisi ya Waziri Mkuu imepewa jukumu la kusimamia maendeleo na ustawi wa vijana lakini kundi hili la vijana halipewi kipaumbele na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa randama ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 20017/2018 Serikali imefanya shughuli tatu tu ambazo inadai kuwa ndizo shughuli za kusimamia na kuratibu maendeleo ya vijana, hizo ni za mbio za mwenge, mafunzo na kutoa mikopo katika mifuko ya vijana na wanawake katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika randama hiyo, Serikali imekiri kuwa kwa upande wa mfuko wa maendeleo ya vijana hakuna fedha yoyote iliyotolewa hadi kufikia 31 Februari, 2017. Hii inadhihirisha kuwa Serikali haina mpango wala mkakati wa maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Taifa ambalo kiwango cha ukosefu wa ajira ni asilimia 11.7 lakini leo hii Ofisi ya Waziri Mkuu inakuja kusema maendeleo ya vijana ni kusimamia mbio za mwenge na uzinduzi wa miradi 1,387 yenye thamani ya shilingi 498,892,879,808 bila kutoa mchanganuo wa fedha hizo na kuonyesha ni vijana wa ngapi kutoka mikoa ipi walifanikiwa na miradi ya mbio za mwenge. Aidha, Serikali imesema kuwa inaratibu mafunzo ya vijana hao wametoka mkoa gani na wamepatiwa mafunzo gani na mafunzo hayo yamewasaidiaje kupata ajira na kujikwamua na umaskini.

Mheshimu Mwenyekiti, ni aibu kubwa kwa Taifa letu kukosa kabisa dira mahsusi ya maendeleo ya vijana na kudhani kuwa miradi ya mbio za mwenge ndio maendeleo ya vijana, kitendo hiki ni kuwahadaa vijana na kuwapa matumaini hewa juu ya uwezeshwaji wa kimitaji kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali kuacha mara moja kuwahadaa vijana kuwa inawajali wakati vijana wa nchi hii wako hoi hawana ajira na ndio wahanga wakubwa wa dawa za kulevya, UKIMWI na kila aina ya jambo baya. Serikali ichukue suala la vijana kwa uzito unaostaahili kwa kubuni mpango mahsusi wa kushughulikia utekelezaji wa sera ya maendeleo ya vijana na kuweka mkakati wa kuongeza ajira miongoni mwa kundi hili kwani

kuendelea kuwabagua vijana kunawezaa kuliingiza Taifa katika machafuko kutokana na vijana kukata tama ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya katika kusimamia shughuli za kila siku za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii mambo mengi yaliyomo ndani ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mengi ni mazuri, lakini ningependa kuchangia baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa walimu wa shule za msingi na sekondari, baadhi ya maeneo mengi hasa katika Halmashauri zetu hayana walimu wa kutosha; uwiano wa mwalimu mmoja kufundisha idadi ya watoto inatofautiana. Mfano Mkoa wa Tabora mwalimu mmoja anafundisha watoto 40 uwiano huo unaonyesha dhahiri kuna ugawaji mbaya wa watumishi hususani katika kada ya walimu naomba suala hili litazamwe kwa umakini na kurekebishwa kwa sababu inarudisha juhudi za Serikali za kutoa huduma sawa kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la usimamizi wa miradi ya maji katika miji yote na Halmashauri zetu kunakuwa na mapungufu mengi. Serikali haina utaratibu ulio imara wa kukagua mradi mingi ya maji ambayo imegharimu Serikali fedha nyingi hali inayopelekea miradi mingi kutoa huduma chini ya kiwango au kuharibika kwa muda mfupi naishauri kuanzia sasa Wizara ya Maji na TAMISEMI waweke utaratibu wa shughuli zao kila siku ziwe zinafuatilia miradi hii yote ilete matokeo yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali imuongezee *CAG* uwezo wa kifedha ili afanye kazi ya ukaguzi kwa ufanisi

(*performance auditing)* kwa sababu ukaguzi huu umeonyesha kwa kiasi kikubwa namna gani Serikali inaweza kuufanyia kazi ushauri unaotolewa na *CAG.* Ukaguzi huu ni muhimu sana kwa sababu unalenga katika kuonyesha je, miradi imetekelezwa kwa ufanisi au la. Je, wakandarasi wa miradi mbalimbali wanatimiza wajibu wao? Na Wizara au Halmashauri nazo zinatimiza utaratibu wao? Kupitia ukaguzi kwa ufanisi Ofisi ya *CAG* imefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishauri Wizara ya Elimu iimarishe ukaguzi katika shule zote, kitengo hiki hakifanyi kazi sawasawa ndio maana hata baadhi ya shule zote zinafanya vibaya katika matokeo ya mitihani yao, zamani kiwango cha ukaguzi wa shule zetu zilikuwa zikitoa taarifa za shule leo hii wakaguzi hawana vyombo vya usafiri ambavyo vinaweza kuwasaidia kutembelea shule zote. Wakaguzi hawa wapewe magari, ofisi pamoja na kuwezeshwa posho za mazingira magumu kuwapa moyo na kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuchangia eneo la migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima. Serikali wakati inafikiria kuleta sheria na mabadiliko juu ya ufugaji wa kisasa idadi ya wafugaji imeongezeka, wananchi wanaongezeka lakini ardhi haiongezeki.

Nashauri sasa ukifuga mifugo michache kwa njia bora kabisa ya kisasa hii itapunguza migogoro. Lakini vilevile ione kuwa ufugaji bora wa mifugo utasaidia Serikali kuongeza pato lake la Taifa ikijikita katika kutoa elimu ya ufugaji bora. Vilevile elimu itolewe kwa wananchi wafugaji lakini Serikali iandae miundombinu bora ya *zero grazing* hii italeta mapinduzi makubwa lakini itapunguza migogoro ya mara kwa mara ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utunzaji wa vyanzo vya maji ni eneo lenye matatizo makubwa wananchi wamekuwa wakilima katika vyanzo vya maji lakini pia wananchi wengi kulima katika maeneo ya milima, ulimaji huu unaleta athari kubwa katika kuharibu mazingira. Lakini

mbaya zaidi ukosefu wa mvua maeneo mengi umesababishwa na shughuli zisizo rasmi katika maeneo ya mabonde na milima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kulima mita 60 kutoka vyanzo vya maji usimamiwe kwa dhati ikiwezekana iwe ni sheria kamili kulinda maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza hotuba ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa imegusa maisha ya wananchi wa aina zote katika nchi hii yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, Mheshimiwa Jenista Mhagama katika Wizara yake anafanya kazi kubwa na yenye tija kwa Taifa letu kwa ujumla na Naibu wake Mheshimiwa Antony Mavunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu la Kibiti zipo changamoto nyingi katika suala zima la afya. Sina budi kushukru Serikali yangu inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kutuletea mradi wa *BRF* kwa kupata kila zahanati shilingi 10,000,000 kwa ajili ya kuboresha zahanati zetu na kununua baadhi ya vifaa vya tiba kama vitanda na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kila penye mafanikio hapakosi changamoto, katika Jimbo la Kibiti changamoto kubwa katika idara ya afya ni moja ambayo ni upungufu wa watumishi, ikama ni 630 waliopo 152 upungufu ni 478; naomba Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi watuangalie kwa jicho la huruma pamoja na upungufu wa watumishi lakini zipo changamoto zingine kama umaliziaji wa majengo, maboma yaliyoachwa kwa muda mrefu. Kituo cha Afya Kibiti kimezidiwa katika utoaji wake wa huduma,

naomba iangaliwe kwa jicho la huruma kwani ndio inayobeba Kibiti kwa ujumla katika idara ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu ka Kibiti zipo changamoto nyingi katika sekta ya kilimo kama maafisa ugani wapo wachache, kwa hiyo husababisha wananchi wangu wa Jimbo la Kibiti kushindwa kulima kilimo chenye tija. Hata hao wachache waliopo nao wana changamoto ya uhaba wa vifaa vya kufanyia kazi kama magari na pikipiki, upatikanaji wa pembejeo kwa wakati nalo ni tatizo kubwa linalowakabili katika sekta hii ya kilimo katika jimbo langu la Kibiti, kwani pembejeo haziji kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi hizi pembejeo ambazo tunaletewa kwa ruzuku naomba mfumo huu ubadilishwe kwa kuondolewa kodi ambazo si lazima ili pembejeo hizi ziwe kama vocha na kwa bei nafuu.

Kuhusu mashamba darasa njia hii ni nzuri sana kwa wakulima wangu wa jimbo la Kibiti kuwapa elimu ili waweze kulima kilimo chenye tija; aidha, stakabadhi ghalani ni mfumo ambao nao katika uuzaji wa mazoa ni mzuri lakini unachangamoto kubwa kama chama kikuu cha *CORECO* – Pwani kina matatizo makubwa na moja ni kufanya minada kiujanja, pili kuchelewesha malipo ya minada na vilevile vyanzo vya msingi navyo ni tatizo tuna kila sababu ya kupitia upya mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu, sina budi kuishukuru Serikali yangu kwa kuanzisha elimu bure. Lakini kila penye mafanikio hapakosi changamoto, moja upungufu wa walimu, vyumba vya madarasa, vyumba vya walimu na baadhi ya maeneo watoto hutembea umbali mrefu kwenda kwenye shule. Katika jimbo langu la Kibiti kuna maeneo ambayo yapo kwenye delta, walimu wanafanyakazi kwa hali ngumu kabisa. Naomba wafanyakazi hawa wa maeneo haya ya delta wapewe hata posho ya kujikimu ya mazingira magumu.

Mwisho namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu mama yetu Joyce Ndalichako kwa kufanya ziara katika jimbo langu la Kibiti hasa maeneo ya delta, maeneo ya Nyamisati, Salale, Mfisini na tunashukuru sana kwa kutuletea pesa za ujenzi wa mabweni shule ya sekondari Nyamisati shilingi 261,000,000 na Mtanga delta shilingi 256,084,461.25 tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika sekta hii ya miundombinu kama barabara ya Bungu - Nyamisati tunaomba barabara ijengwe kwa kiwango cha lami kwani kipindi cha mvua huwa inapitika kwa taabu sana ukizingatika barabara hii inatumika kwa majimbo mawili, wananchi wa Kibiti na Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ujenzi wa gati la Nyamasati nalo ni muhimu sana kwa wananchi waishio maeneo ya delta. Kwa ujumla barabara ya kutoka Muhoro – Mbwera barabara hii nayo ni muhimu sana kwa wananchi waishio maeneo ya Mbuchi, Mbwera, Kipoka Maparoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na kuendelea kutupatia amani kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali yangu kwa juhudi zake katika kuboresha miundombinu, huduma muhimu kwa wananchi wake, vyote hivyo vikiwa chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Kutokana na juhudi zote hizo tunaona jinsi gani Pato la Taifa lilipo ambapo ni asilimia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Mkoa wa Pwani, tunashukuru kwa mkoa wetu ambao tumebahatika kuwa na viwanda ambavyo tayari vinazalisha na vingine viko kwenye hatua za ujenzi au taratibu za kuanzishwa.

Pamoja na manufaa hayo kwa mkoa wetu kuna mambo muhimu ambayo tunapaswa yapewe vipaumbele ili viwanda hivyo viweze kuwa na uzalishaji ambao hautakuwa na vikwazo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Pwani tuna tatizo kubwa la upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali pamoja na neema tuliyopewa ya kuwa na mito mingi tena mikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya barabara zetu sio nzuri, Wilaya ya Kisarawe imetenga eneo mahususi kwa ajili ya viwanda, lakini tatizo ni barabara. Hivyo basi naiomba Serikali inipe majibu ni vipi tutatokana na matatizo hayo ili kuweza kuvutia wawekezaji ambao wako tayari kuja kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni kwa kiasi gani Serikali imejipanga kwa kuhakikisha ajira za vijana hasa kwenye viwanda vinazalisha na vinatarajiwa kuwa kuna baadhi wanatoa ajira lakini mshahara ni mdogo sana (shilingi 5,000) kwa siku. Hii nilishawahi kuuliza hapa Bungeni kwenye kipindi cha maswali na majibu. Mipango mizuri ndio faida ya Watanzania ambapo ni Serikali yetu inavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa gesi utasaidia sana kupunguza gharama za uzalishaji viwandani, lakini pia utaratibu wa kupeleka umeme huo majumbani uongezewe *speed.*

Mheshimwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na pongezi kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu wake Mheshimiwa Antony Mavunde.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Waziri Mkuu kwa kufanya ziara ya kihistoria mwishoni mwa mwaka jana Wilayani Karatu. Ziara hiyo ilileta matumaini mapya ya maisha kwa wakulima wadogo wadogo wa Bonde la Ziwa Eyasi wanaotumia kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia chemchem zilizoko Qangded.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu kwa kusikiliza malalamiko ya wananchi wa bonde hilo kupitia mabango waliyomwandikia na kwa kuzingatia misingi bora ya uhifadhi wa vyanzo vya maji, Waziri Mkuu aliagiza mashine zote zilizoko mtoni ziondolewe na mipaka ya chanzo ihifadhiwe kwa mita 500 kila upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kauli hiyo ya kiongozi mkubwa ambayo pia imezingatia sheria; viongozi wa chini yake waliopaswa kusimamia maagizo hayo wameshindwa kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea baadhi ya mashine bado ziko mtoni kabisa. Upimaji wa mipaka ya chanzo ulifanyika hivi karibuni lakini bado mipaka hiyo haizingatiwi na watu wanalima ndani ya eneo lililopimwa. Uhifadhi wa vyanzo vya maji ndiyo njia pekee ya kuinusuru nchi hii kugeuka kuwa jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri Mkuu akamilishe kazi hii njema aliyoianza kule Karatu kwa kutoa tena tamko kwa uongozi wa chini yake wasimamie kauli yake ambayo ni kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi wanajishughulisha na kilimo ili kupata chakula na pia mazao ya biashara. Kilimo chetu kimekuwa tegemezi kwa mvua jambo ambalo limepunguza mapato na mavuno pindi tunapokuwa na mvua chache. Niishauri Serikali kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga mabwawa makubwa ambayo yatakinga maji nyakati za mvua. Nchi kadhaa duniani na hata hapa Afrika wamefanikiwa kwa kuwekeza katika miradi ya aina hiyo.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika mjadala huu wa kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya, uzima na uhai na kuwa hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu Majaliwa Kasim Majaliwa kwa kazi kubwa anayofanya ya kusimamia shughuli za Serikali kwa weledi, maarifa na utulivu wa hali ya juu. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayofanya ya kumsaidia Waziri Mkuu na wao wenyewe kufika katika Jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki kwa nyakati tofauti katika kusukuma maendeleo ya watu wa jimbo langu na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa ni mnyimi wa shukrani kama sitamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayofanya ya kuwatumikia Watanzania na hasa kwa kutuletea maendeleo katika Jimbo langu kama vile Kiwanda cha Sukari katika Kata ya Mkulazi, barabara ya lami toka Ubena Zomozi mpaka katika kambi yetu ya Jeshi la Ulinzi na Usalama, Kambi ya Kizuka na mradi wa maji katika Kijiji cha Fulwe Mikese na mengine mengi katika kipindi kifupi cha mwaka mmoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na cha kupewa hakina nyongeza na kwa kuwa katika kijiji na Kata hii ya Ngerengere kuna kambi tatu za Jeshi kwa maana ya Kizuka na kikosi namba 23 na Sangasanga na kwa kuwa vyote ni vikosi vyetu na wote ni wapiga kura wangu na hawa wa kikosi cha Sangasanga wasijisikie wanyonge na kubaguliwa na kusahaulika, kwa niaba yao, naiomba Serikali hasa Mheshimiwa Rais kuweka lami pia barabara toka Kizuka mpaka Ngerengere Mjini kupitia Sangasanga mpaka Mdauli ili vikosi vyote vitatu viweze kufikiwa kiurahisi kwa barabara ya lami na walinzi wetu kufaidi matunda ya uhuru kama dhamira njema aliyoonyesha Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuanza kuweka lami katika barabara ya Ubena-

Kizuka. Naomba sana hii barabara ya Mdaula-Sangasanga-Ngerengere-Kizuka nayo kuwekewa lami kilometa kumi na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuanza mchakato wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* ambayo inapita katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki katika Vijiji vya Kidunda, Ngerengere, Kimoko na Mikese ambayo italeta maendeleo makubwa katika eneo la Morogoro Vijijini na Morogoro kwa ujumla ukizingatia sisi Morogoro ndiko inakoishia awamu ya kwanza ya mradi huu. Tunashukuru sana kwa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo naomba kuishauri Serikali na kuiomba itoe ufafanuzi rasmi eneo la hifadhi ya reli ni kiasi gani sababu katika kuandaa utekelezaji wa mradi huu, wataalam wametoa notisi kwa wananchi kubomoa nyumba zao kupisha mradi lakini kila sehemu ina umbali tofauti. Kwa mfano, Ngerengere wameambiwa umbali ni mita 120 kila upande, Mikese mita 90 na Morogoro Mjini mita 30 kila upande. Je, umbali wa hifadhi ni upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kutokana na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, Sheria Namba 4 na 5 na kanuni zake inasema kama mtu amejenga na kukaa zaidi ya miaka 12 bila kubughudhiwa eneo hilo ni halali yake. Je, kwa sheria hiyo Serikali haioni ina wajibu wa kuwalipa wananchi waliojenga na kukaa zaidi ya miaka 12 bila bugudha ili kutowarudisha nyuma kiuchumi wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia muda waliopewa wa mwezi mmoja kuhama ni mdogo sana kwa mwananchi wa kawaida kuhama tena bila ya fidia kupata fedha ya kujenga nyumba mpya. Naomba Serikali kuwapa muda wananchi wa miezi sita ili kupata muda wa kuhama kwa utulivu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni muhimu, michezo ni afya na Bunge linatuhimiza kushiriki mazoezi lakini hatuna uwanja wa kufanya mazoezi kwa timu zetu za Bunge. Kwa

kuwa Serikali imehamia Dodoma na kutakuwa na mahitaji makubwa ya viwanja vya michezo, naomba kuishauri Serikali na Ofisi ya Bunge kuwaona *CDA* na Mamlaka ya Halmashauri kulipatia Bunge eneo la michezo kwa Timu za Bunge badala ya sasa kutangatanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa inazofanya dhidi ya kukwamua kiuchumi wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea suala zima la afya hasa katika Mkoa wangu wa Arusha katika Wilaya ya Longido, wananchi walio mpakani mwa nchi jirani ya Kenya maeneo ya Namanga wamekuwa wakivuka mpaka na kwenda kutibiwa nchi jirani ya Kenya. Jambo hili limekuwa kero sana kwa wananchi wa Wilaya ya Longido. Tunaomba Serikali iwasaidie wananchi wa Longido kuwajengea hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Arumeru Magharibi ni jimbo kubwa sana hali inayopelekea wananchi wengi kutofikiwa na huduma muhimu. Naomba Serikali iangalie upya jinsi ya kugawa jimbo hili ili wananchi wengi waweze kufikiwa na huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo hili kumekuwa na migogoro ya ardhi mara kwa mara na migogoro hii inapelekea wananchi kuishi bila amani. Kuna baadhi ya wawekezaji wamejilimbikizia ardhi kubwa na wanatumia tofauti na ilivyokusudiwa. Wananchi wana shida ya ardhi huku wawekezaji wamejilimbikizia ardhi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo hili la Arumeru Magharibi kuna tatizo kubwa la akinamama ambao wamekuwa wakitembea mwendo mrefu kutafuta maji. Naiomba Serikali iangalie kwa ukaribu changamoto nyingi zilizomo katika jimbo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimbo hili lina changamoto kubwa ya barabara, barabara zake ni mbovu. Naiomba Serikali iliangalie hili ilki wananchi wake wafaidike na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH R.SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo inaajiri wananchi wengi katika nchi yetu. Vilevile katika azma ya Serikali ya kukuza viwanda ipo haja kubwa ya kuimarisha sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao mengi ya biashara yanaelekea kukosa msukumo na wakulima kuyaacha. Hali hii inatokana na Serikali kuweka bajeti ndogo katika kilimo na hivyo kuifanya sekta hii kushindwa kuhudumia kilimo chetu. Hivyo, naomba:-

(i) Taasisi za Kilimo za Utafiti wa Dawa, Pembejeo na Mbolea lazima ziimarishwe kwa kupewa fedha za kutosha.

(ii) Bodi za Mazao haya kama Kahawa, Tumbaku, Pamba na kadhalika ziimarishwe ili kuweza kusimamia vyema mazao haya.

(iii) Tafiti za masoko ambayo yatawanufaisha wakulima kwa kuwapatia bei nzuri zifanyike.

(iv) Uhamasishaji ufanyike ili wakulima waendelee kuzalisha mazao haya kwa kuwa maeneo mengi hasa yanayolima kahawa wananchi wanaelekea kukata tamaa.

(v) Kuhusu mazao mchanganyiko Bodi ya Mazao Mchanganyiko iimarishwe.

(vi) Uhamasishaji ufanyike ili mazao yetu yaongezewe thamani ili kuyaongezea bili na pia kuongeza ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika ni vema sasa kama nchi tuachane na kilimo cha msimu kwa kutegemea mvua na badala yake tuimarishe kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jimbo langu la Rombo wananchi wamekata tamaa sana katika kuzalisha zao la kahawa. Hii ni kutokana na gharama kubwa za uzalishaji na bei kuwa ndogo; hali kadhalika kuyumba kwa Vyama vya Ushirika hasa *KNC*U. Mali na mashamba ya *KNCU* yameuzwa kiholela bila kuwashirikisha wanachama. Naiomba Serikali kuingilia kati ili kunusuru mali na mashamba ya *KNCU* ili kuifanya iwe na nguvu na uwezo wa kulisimamia zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya maji nchini katika majimbo yote ni mbaya sana. Katika Jimbo langu la Rombo wananchi wanateseka sana na ukosefu wa maji. Vyanzo vingi vimekauka na maji yananunuliwa kwa sh. 1000 – 1500 kwa dumu la lita 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi iliyoanzishwa, mfano Mradi wa Shimbi Mashariki na Leto. Miradi hii inasuasua kwa sababu ya fedha kutopelekwa kwa wakati. Kama miradi hii ikikamilika itasaidia kwa kiwango fulani kuatua shida hii katika maeneo ya mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *water table* katika jimbo langu ni zaidi ya mita 300 na kuondoa uwezekano wa visima kuchimbwa katika maeneo mengi, hapa Bungeni Wabunge wote wa Rombo walionitangulia wameleta mapendekezo ya matumizi ya maji ya Ziwa Chala. Tumekuwa tukipata matumaini miaka yote. Tunaomba sasa suala hili lifikie mwisho. Ni lini maji ya Ziwa Chala yataanza kutumika kwa ajili ya wananchi wa Rombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kuhusu maji tuliomba ianzishwe Mamlaka ya Maji ya Wilaya ya Rombo. Tunaomba kujua ni lini mchakato huu utakakamilka ili mgao wa maji kidogo tuliyonayo uwanufaishe wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya, hivi sasa tuna mchakato wa ujenzi wa jengo la *OPD* katika Kituo cha Afya Karume ili kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Hivi sasa ujenzi umesimama kutokana na Mkandarasi kutudai. Tunaiomba Serikali katika bajeti hii kutupatia fedha za kukamilisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuna Mradi wa Ujenzi wa jengo la Halmashauri. Hii ni halmashauri kongwe ambayo ina zaidi ya miaka 30, lakini hatuna jengo la halmashauri. Tunaomba katika bajeti fedha zipatikane ili ujenzi uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu tuna uhaba mkubwa wa Walimu wa sayansi. Tunaiomba Serikali katika mgawo wote wa Walimu wa sayansi tupatiwe kiasi cha kuweza kutusaidia. Zipo shule ambazo tangu zimeanzishwa hadi leo hazina Mwalimu hata mmoja wa somo lolote la sayansi.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pongezi kwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kwa kazi kubwa inayofanyika katika Taifa letu. Wananchi wa Tanzania wanayo imani na matumaini makubwa sana kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wananchi kiuchumi katika eneo hili napenda kuishauri na kutoa msisitizo mkubwa juu ya ahadi ya Rais ya kupeleka milioni hamsini kwa kila kijiji. Serikali katika bajeti ya mwaka 2017/2018 ihakikishe inatenga fedha hizo ili utekelezaji wa ahadi hii uanze kwani wananchi wanategemea fedha hizi katika kuinua uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Madini kazi inayofanyika ni njema hasa utoaji wa ruzuku kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ugani. Kwenye hotuba maeneo yaliyotengwa Mkoani Geita ni Msasa na Matabe tu. Maeneo

haya hayatoshi ukilinganisha na mahitaji makubwa yaliyopo hasa kwa wachimbaji wadogo. Kilio kikubwa ni maeneo ya uchimbaji hasa eneo la *STAMICO* ambalo ni kero ya muda mrefu. Uwekezaji unaofanyika *STAMICO* hauna tija kwa Taifa, hivyo, naomba Serikali itazame upya mikataba hii. Ikiwezekana wananchi (wachimbaji wadogo) wapewe eneo hili la *STAMICO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa ahadi ya Rais ya kujenga kilomita 10 za lami katika Mji Mdogo wa Katoro; naomba ahadi hizi za Rais ziangaliwe na zifanyiwe mkakati wa utekelezaji ikiwemo barabara ya Kahama – Bukoli – Geita ahadi ya Rais Awamu ya Nne Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Hivyo ili wananchi waiamini Serikali yao naomba ahadi hizi zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kwa kuanza kuunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ione haja ya kutangaza Mkoa wa Ulanga ili kusogeza huduma kwa wananchi. Taratibu zote ngazi za Halmashauri na Mkoa (*RCC*) zimeshafanyika. Pia itangaze Halmashauri ya Mlimba ambapo wananchi wa Mlimba wanataabika kumfuata Mkurugenzi kilometa 269 na miundombinu mibovu na kushindwa kupata huduma kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara kutoka Ifakara-Taweta - Madeke - Njombe. Takribani kilometa 269 haipitiki, hivi niandikavyo taarifa hii, barabara hiyo haipitiki hata mabasi ya abiria yaliyokuwa yanatoa huduma yamesitisha kutokana na ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauli zimepanda kutoka sh. 20,000/= hadi sh. 40,000/= kufika Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ambako huduma zote za matibabu, mahakama

na kadhalika zinapatikana. Hali hii ni mbaya, hivyo naomba Serikali ione hitaji kubwa la kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo inategemewa sana na wananchi kusafirisha mazao yao ukizingatia barabara hiyo iko kwenye eneo la ghala la chakula (kilimo kikubwa cha mpunga, mahindi *(KPL)* pia cocoa, ndizi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio kingine kikubwa kwa wananchi wa Mlimba ni maji safi na salama. Hivyo naomba Serikali ianze na kero kubwa hizi mbili, barabara na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha**.**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** nachukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na hewa safi ya *oxygen* ambayo haikati kodi *(TRA)* wala *(ZRB)*. Pia nikushuku wewe kwa kuniruhusu nichangie Ofisi hii ya Waziri Mkuu. Nataka nianze na suala moja dogo akisimama Waziri Mkuu kujibu hoja za Wabunge anipatie jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha aliyotoa Msajili ni fedha ya walipa kodi ambayo hukaguliwa na *(CAG)* Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali. Fedha hii iliyotolewa na Serikali ikaingizwa katika akaunti ya mtu binafsi zitakaguliwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kujua *NMB Bank* nani kawapa ruhusa fedha ya Serikali itolewe kiholelea pasipo kufuata miamala ya kibenki na sheria zake. Inawezekanaje milioni mia tatu na sitini na tisa (369,000,000) zitolewe kwa siku mbili fedha nyingi kama hizi kutoka akaunti ya chama kwenda akaunti ya mtu binafsi au huyu mtu binafsi ana chama chake mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano inapigana vita ya ufisadi na rushwa, suala hili limepigiwa kelele takribani miezi minne sasa, lakini hakuna chombo

chochote cha Serikali mfano, Polisi, Usalama wa Taifa na TAKUKURU na hizi ni fedha za wananchi; je, kuna nini au ugumu gani katika jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya watu wa usafirishaji wa majahazi katika bandari ya Dar es Salaam; wanalalamikia kodi kubwa wanayokatwa kiasi ambacho wao hawapati kitu na wanashindwa kutoa huduma hiyo. Wanakatwa kodi kwa kipimo cha *(CDM)* na *CDM* moja wanalipa Sh. 7,500/=. Gari moja la fuso linapakia *CDM* 80 ni sawa na Sh. 600,000/= ambapo wao wakipakia *CDM* 80 yaani fuso moja mfano wa mbao wanalipwa Sh. 1,000,000/= milioni moja tu. Kama ni kweli na sahihi katika fuso moja Serikali inachukua 600,000 /= wenye Jahazi wanapata 400,000/= tu. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie tatizo hili. Nilimwomba zaidi ya mara tatu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi akutane na watu wa Majahazi ili awasikilize na awasaidie katika hili lakini bahati mbaya shughuli za hapa kazi zilimzidi hakuwahi. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisaidie juu ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizunguzie *(MIVARF)*; mradi huu wa *MIVARF* Mkoa wa Kaskazini Unguja Wilaya ya Kaskazini 'A' tumebahatika kupata mradi wa Soko la Kinyasuni, barabara ya Chaani Donge na barabara ya Lunga Lunga Polisi hadi binti Saidi. Barabara hizi zimesaidia sana wakulima wa maeneo hayo kwa kupata wepesi wa usafiri wa mazao yao. Ushauri wangu barabara hizi zingefanywa endelevu kwa sababu zinajengwa maeneo ya maji hivyo ni rahisi wakati wa mvua kifusi kuondolewa na matatizo kubakia palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko la Kinyasini, naomba Serikali isimamie kwa karibu sana ili limalizike kwa wakati kuondoa adha wanayopata wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Pia kuna watu waliobomolewa kupisha soko hilo na wanalalamika kutolipwa. Nataka kujua nani anawajibika kuwalipa? Naomba nipatiwe majibu; je, wamelipwa, watalipwa au hawalipwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukrani kwa Hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Waziri Mkuu kwa umakini wake na upendo mkubwa alionao anapotekeleza majukumu yake na unapompelekea jambo lolote yuko tayari kulishughulikia mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tena Waziri Mkuu atusaidie kutatua mgogoro unaofukuta juu ya umiliki halali wa majengo ya Halmashauri ya Ushetu yaliyoko Kahama Mjini ambayo bila kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu, Serikali ya Mkoa imeagiza yamilikiwe na Halmashauri ya Mji wa Kahama na kunyima fursa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kupanua wigo wa mapato yake na kuongeza huduma bora kwa wananchi. Vilevile inaiweka katika hatari ngumu kisiasa eneo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maji ya mradi wa Ziwa Viktoria; naishauri Serikali kuangalia *impact* ya upelekaji wa maji yaani kufanya mapitio kiasi gani au idadi gani ya watu wanasambaziwa maji kuliko kuridhika na dhana pekee ya kuwa maji yamefika Makao Makuu ya Wilaya hali maji hayajawafikia wananchi walio wengi. Mfano; maji ya Ziwa Viktoria yamefika katika Makao Makuu ya Wilaya na wananchi wengi hawajasambaziwa maji hayo ikiwemo eneo lote la Jimbo la Ushetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie suala la kutusambazia maji eneo la Jimbo la Ushetu sehemu ambayo ina shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo naiomba Serikali iweke mkazo na kusimamia na kuleta tija katika uzalishaji:-

(i) Suala la pembejeo ipatikane ya kutosha, ipatikane mapema

(ii) Benki ya Kilimo iwezeshwe mtaji wa kutosha na isimamiwe vizuri ili iweze kutekeleza majukumu yake hususani:-

(a) Kutoa mikopo kwa wakulima.

(b) Kufanya utafiti wa kifedha na kiuchumi.

(c) Kutoa elimu kwa wakulima.

(d) Kuwajengea uwezo vijana na kuwawezesha kwenye miradi ya kilimo.

(e) Kuratibu utoaji mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la madini naomba Serikali iwasaidie wachimbaji wadogo wadogo wapate maeneo yao ya uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika eneo la Mwabomba Jimbo la Ushetu kuna hali ya sintofahamu wachimbaji wadogowadogo waliopo watakwenda wapi kufuatia eneo hilo kupewa mwekezaji ambaye anasuasua kuanza shughuli zake wakati huo huo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Magufuli aliwaahidi wananchi kuwa hawatahamishwa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ahadi ya Serikali juu ya hatma ya wachimbaji wadogo wadogo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni suala la kikatiba, Ofisi hii ina jukumu ya kuvisajili Vyama vya Siasa na kuvishauri. Kutokana na majukumu hayo Ofisi

ya Msajili haina mamlaka ya kuingilia maamuzi yaliyofanywa na vyama vya siasa na katiba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msajili wa Vyama vya Siasa kuwapa viongozi wa siasa ambao tayari wameshajiuzulu katika vyama vyao ni kinyume na Katiba ya Vyama na hata Serikali zote mbili. Kwa maana hiyo, tunamwomba Msajili wa Vyama kutekeleza majukumu yake na kuwaachia vyama kutekeleza majukumu katika vyama vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mambo ya kisiasa kama yalivyoelezwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu naomba niseme kwamba, suala hili si shwari ndani ya nchi yetu. Kauli ya Mheshimiwa Rais kuzuia mikutano ya vyama vya siasa ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hali hii inaashiria kutokuwepo na uhuru wa kisiasa wa viongozi mbalimbali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha CCM kina mamlaka pekee ya kufanya siasa katika nchi hii. Kwa mujibu wa Msajili vyama vyote ni sawa, leo iweje Msajili wa Vyama kuviona vyama vingine vina haki na vyama vingine vikawa havina haki; je, hii ni sawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, madawa ya kulevya, kwanza naipongeza Serikali kwa kudhibiti madawa ya kulevya katika nchi hii. Madawa ya kulevya yanaathiri nguvu kazi ya vijana wetu ndani ya nchi yetu. Ndani ya nchi yetu vijana wengi wamejishughulisha na biashara ya madawa ya kulevya kama vile *cocaine*, bangi, mirungi, viroba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeunda Tume ya Kupambana na Madawa ya Kulevya, lakini fedha zilizotengwa ni kidogo kutokana na tatizo hili kuwa kubwa. Hata hivyo, hizi zilizotengwa zitumike vizuri ili lengo lililokusudiwa lifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa anga, Kiwanja cha ndege kilichoko Pemba ni kidogo mno kinahitaji kupanuliwa

kwa sababu ndege zitakazowasili ni nyingi kutokana na abiria wanaingia na kutoka ni wengi hasa watalii wanaokuja kujionea vivutio kama vile nyumba iliyojengwa ndani ya bahari iliyoko, Panga Watoro, katika Kijiji cha Makangale, pamoja na vivutio vilivyoko Meseli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo, naomba nijibiwe.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza na orodha ya Mawaziri hapa wanaanza kuhitimisha kwa kujibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Naanza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango dakika 10, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani dakika 10, halafu Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo dakika 10. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake kwa hotuba nzuri sana na niseme toka mwanzo kabisa kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetolewa hoja nyingi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya nitakutoa nje sasa hivi...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Nimesimama hujanipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Huwezi kunilazimisha nikupe nafasi ya kuongea, nakuomba ukae. Mheshimiwa endelea.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetolewa hoja nyingi ambazo ningependa na mimi nichangie baadhi yake. Moja, ilitolewa hoja kwamba kuna mkanganyiko wa takwimu ambapo kwenye hotuba ya bajeti ya mwaka jana ilionesha mapato na matumizi

shilingi trilioni 29.5, lakini vitabu vya mapato na matumizi vinaonesha namba nyingine. Niwashauri tu Waheshimiwa Wabunge ni vizuri wakaelewa takwimu hizi maana yake nini. Mapato yaliyopo kwenye *Volume (I)* ni mapato ya kodi, yasiyo ya kodi, misaada na mikopo nafuu. Sasa ukichukua matumizi ukatoa mapato kama yalivyo katika *Volume (I)*, ile tofauti ni nakisi ya bajeti. Kwa hiyo, nadhani ni uelewa tu wa kusoma na kuelewa tafsiri ya hizi namba ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lililosemwa ilikuwa ni kuhusiana na uwiano kati ya ukuaji wa uchumi na madai kwamba hali halisi ya wananchi hailingani na ukuaji wa uchumi. Niseme tu kwamba, kwanza, uchumi wa Tanzania hakuna ubishi kwamba unakua, namba hazidanganyi. Ukiangalia *World Economic Data Base,* takwimu za *IMF,* takwimu za *National Bureau of Statistics* zote ziko wazi. Katika Afrika, Tanzania ni moja ya nchi, *the top five* ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tu Benki ya Dunia wametoa taarifa yao pale Dar es Salaam na inaeleza wazi kabisa katika Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo namba moja na hata katika Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu ambazo uchumi wake unakua kwa kasi. Kwa hiyo, hili halina ubishi, tuachane kabisa kubishana na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu uwiano na hali halisi ni kweli bado ile *quality of growth* haijafikia pale ambapo wote tunatamani na sababu ziko wazi. Sababu ya msingi ni *performance* ya sekta ya kilimo ambayo ndiyo inaajiri watu wetu wengi imekua kwa asilimia ndogo sana na wote tunajua, sababu yake kilimo chetu bado kinategemea mvua lakini pia uwekezaji katika sekta ya kilimo ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunajua pia kwamba hali ya maisha ya Watanzania haiwezi kuja mara moja. Ni wazi kabisa kuwa tumeanza kuona mabadiliko katika maisha ya Watanzania. Sababu yake moja ni kwamba baadhi

ya sekta ambazo nazo zinaajiri watu wengi nazo zimeanza kukua kwa kasi. Kwa mfano, uzalishaji viwandani sasa unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.3 kwa mwaka lakini biashara pia asilimia 6.5 kwa mwaka, usafirishaji na uhifadhi wa mizigo asilimia 17 na hizi sekta zinaajiri wananchi wetu wengi, ndiko wanakopatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mkazo wa Serikali uko wazi. Katika mpango wa miaka mitano, tumesema tunataka kujenga uchumi wa viwanda ambao unatumia malighafi ambazo zinazalishwa hapa hapa nchini. Tukiweka jitihada kwenye *agro-processing* na *agri-business,* tukaweka jitihada kwenye elimu na ujuzi kama ilivyo katika mipango yetu, haya ndiyo yatakayofanya ukuaji wa uchumi sasa uweze kuleta matokeo yale ambayo tunatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni ukweli pia, vigezo vingine vya hali ya maisha ya wananchi vinaonekana wazi kabisa vimeboreka. Hali ya nyumba imekuwa bora zaidi, hali ya afya, upatikanaji wa umeme, tumepeleka umeme vijijini, yote haya siyo vitu vya kubishia na vinaongeza ubora wa maisha vijijini. Namshangaa sana Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hivi kweli haya hata kule Hai hayaoni? Mimi naona kama yako wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja kwamba Serikali haina mkakati wa kuinua uchumi vijijini, hii siyo kweli hata kidogo. Someni Mpango wa Miaka Mitano Waheshimiwa Wabunge uko wazi. Tumesema tutaimarisha kilimo cha umwagiliaji, tutaongeza thamani ya mazao na mifugo, tutainua kilimo cha kisasa, tunapeleka umeme vijijni kama nilivyosema, tunaelekeza fedha kwenye utafiti na mafunzo, tunajenga barabara ili mazao ya wakulima na mifugo yaweze kufika kwenye masoko, hii yote ni mikakati ya kuinua uchumi wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na tahadhari kwamba *IMF* mwezi Januari walisema uchumi unaweza kuporomoka kutokana na kubana matumizi kupitiliza. Kwanza niseme tu kwamba, matumizi ambayo Serikali

inabana ni yale ambayo siyo ya lazima siyo kila matumizi. Serikali imekuwa inajitahidi kuhakikisha kwamba uchumi unaendelea kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hii ripoti ya Januari ni kweli ilitoa hiyo *caution* lakini Mheshimiwa Mbowe pia namshangaa maana ripoti hiyo hiyo ya Januari iliweka wazi kabisa, iliipongeza Tanzania kwa kuchukua hatua kusimamia sekta ya fedha vizuri, kudhibiti mfumuko wa bei na kusimamia matumizi. Haya yenyewe hayaoni ila *caution* yenyewe ndiyo anaiona peke yake, kitu cha kushangaza kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunatambua changamoto za kupungua ukwasi katika uchumi wa Taifa letu na tumeanza kuchukua hatua mbalimbali. Hatua ya kwanza tuliyochukua ni kuendelea kulipa madeni baada ya kuyahakiki. Tumelipa shilingi bilioni 631 mpaka mwezi Machi kwa ajili ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri, tumelipa shilingi bilioni 67.5 kwa ajili ya watumishi, shilingi bilioni 78.8 kwa ajili ya wazabuni, shilingi bilioni 17.8 kwa ajili ya watoa huduma. Hii yote ni njia mojawapo ya kuongeza tena ukwasi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni, Benki Kuu imechukua hatua mbili muhimu. Kwanza, imepunguza *discount rate* kutoka asilimia 16 mpaka asilimia 12, lakini imepunguza pia *statutory minimum reserve requirement* kutoka asilimia 10 mpaka asilimia nane. Mheshimiwa Dkt. Chegeni alijaribu kulieleza jana au juzi nafikiri na hatua hizi zinalenga kuongeza uwezo wa *commercial banks* kukopesha sekta binafsi na hivyo kuongeza ukwasi katika uchumi. Pia tunajitahidi kuongeza nguvu sasa kupata fedha za wahisani na mikopo ya kibiashara kwa ajili ya matumizi ya maendeleo na hizi zote ni kwa ajili ya kuinua ukwasi katika Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimekuwepo hoja kuhusu milioni 50 za kila kijiji. Serikali imefanya tathmini na tumeandaa utaratibu wa kupeleka fedha hizo vijijini. Tumefanya hivi ili tuhakikishe kwamba haturudii makosa yale yale

yaliyoambatana na Mfuko wa JK. Imeonekana kulikuwa na matatizo mengi, kuna vikundi ambavyo vililengwa lakini havikusajiliwa, fedha hazifiki kwa walengwa, hakuna elimu ya ujasiriamali, hakuna hata sheria yenyewe ya *microfinance* na kanuni zake lakini hata mfumo wenyewe wa ufuatiliaji ni dhaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inabidi kwanza kurekebisha haya isije ikaonekana ni kama vilevile kwamba hizi fedha zinatolewa ni kama zawadi. Kwa hiyo, muhimu sana hili lifanyike na hatua tuliyofika sasa umeandaliwa Waraka wa Baraza la Mawaziri ili Serikali iweze kufanya maamuzi rasmi kabla ya kuzipeleka hizo fedha vijijini. Kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha, tumetenga shilingi bilioni 60, ziko Fungu la 21, *Subvote* 2001 ni mradi namba 4903 unaitwa *village empowerment. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mwigulu. Siyo lazima umalize dakika kumi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi niongelee vitu vilivyojitokeza kwenye eneo linaloangukia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiwango kikubwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inahusisha Ofisi ya Vitambulisho vya Taifa, Zima Moto, Uhamiaji, Polisi na Magereza. Hata hivyo, kwa kiwango kikubwa masuala yaliyojitokeza zaidi yanahusisha, Polisi, Magereza, Zimamoto na Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, sitasema kwa kirefu kwa sababu tutakuwa na fursa katika Wizara yangu tutakapoongelea suala la bajeti yetu na utekelezaji wa bajeti

katika kipindi kilichopita lakini kwa utangulizi tu kati ya yale yaliyojitokeza toka kwa Wabunge wengi, moja ya hoja ilikuwa ni malipo yanayotakiwa kwenda kwa Askari wa Magereza, Zima Moto pamoja na Uhamiaji ambao bado hawajapata *package* yao kama wanavyoita wenyewe wakijilinganisha na wenzao ambao tayari walishapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge pamoja na vijana wetu kwamba jambo hilo linafanyiwa kazi na watapata kama ambavyo wamepata wenzao na kama ambavyo ilikuwa ahadi ya Serikali. Ni kwamba tu kwa utaratibu wa Wizara yetu ya Fedha na kwa utaratibu wa hali halisi, wanapofanya malipo kuna vitu walivyoviweka kama *first charge.* Wanatoa kwanza mshahara wa watumishi, deni la Taifa na baada ya hapo kinachobaki wanaangalia namna wanavyoweza kugawa katika matumizi mengine haya ambayo tumeyasema. Kwa maana hiyo, ndicho kilichosababisha wagawe kwa mafungu fedha hizo ambazo zilikuwa zinaenda kwenye vyombo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwahakikishie vijana wetu walioko kazini wala wasivunjike moyo na wala wasiwe na hofu. Wale ambao walishapata na wenyewe watapata na mwisho wa siku wote watakuwa wamepata. Ni ahadi ya Serikali na ni jambo ambalo litatekelezwa na ni jambo ambalo ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelisikia sana kwa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mchengerwa alilisema, ndugu yangu Mheshimiwa Ridhiwani alilisema, Mheshimiwa Matiko amelisema na wengine waliochangia. Ni jambo ambalo kama Serikali tunalifanyia kazi kwa ukaribu na tunashirikiana na wenzetu na niwaombe vijana wetu *in particular* askari wetu watambue ni kautaratibu tu wala hatuna maana ya kuweka madaraja, lakini ni utaratibu tu wa utoaji wa fedha kufuatana na upatikanaji wa dirisha la kulipia fedha hizo zinazokwenda kwenye matumizi haya tuliyoyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo liliongelewa sana na Waheshimiwa Wabunge na lilijitokeza kwa kiwango kikubwa ni suala la *treatment* ya Wabunge wanapokuwa hapa Dodoma na wanapokuwa kwenye maeneo yao ya kazi. Waheshimiwa Wabunge, nimelielezea na kama nilivyosema kwenye *briefing,* tuna mambo mawili lazima tukubaliane nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kwamba nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, yale yaliyo ya sheria ni lazima sheria iongoze na ndivyo tulivyokubaliana na sisi ndiyo tuliotunga sheria. Hata hivyo, kuna *mistreatment* inayotokana na mtu mmoja mmoja, tumeyatolea maelekezo ili haki ya Wabunge na ya wananchi wengine iendelee kuzingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kwamba kwa umaskini wetu tulionao tungetamani tuwape watu vitu vingi sana lakini hatuwezi tukawapa kila kitu wananchi wetu. Hata hivyo, kitu kimoja pekee ambacho tunaweza tukawapa wananchi wetu ni haki yao ya msingi, haki ambayo wanastahili na hicho ndicho ambacho na sisi tunakisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukirejea kwa Waheshimiwa Wabunge, nimetolea maelekezo na linapotokea suala la aina hiyo Mheshimiwa Mbunge uko maeneo fulani, uko kazini au hata kwenye mikutano, kwa wale walio wapya ni vizuri tukatambulika na tukajitambulisha na ni vizuri tukatoa hizo taarifa kwamba kutakuwepo na shughuli A, B, C, D kama ni ya mikutano na tukaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wengine wameendelea kuelezea kuhusu mikutano. Tulishasema, Waheshimiwa Wabunge wanaruhusiwa kufanya mikutano yao kwenye majimbo yao. Nilirejee moja ambalo limeelezewa sana kuhusu Wabunge wa Viti Maalum. Wabunge wa Viti Maalum majimbo yao ni kwenye mikoa yao na wenyewe watoe taarifa ili kuondoa usumbufu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine lililojitokeza ambalo na lenyewe nimeona nilitolee taarifa hapa leo, Waheshimiwa Wabunge na hasa katika kipindi hiki ambacho tuko Bungeni, Mheshimiwa Spika alishalisemea alipokuwa akitoa mwongozo kuhusu namna ya ukamatwaji au kufanyiwa mahojiano kwa Waheshimiwa Wabunge, mimi nasisitiza kile kile alichosema Mheshimiwa Spika. Ni mamlaka yake, ameelekeza kama Mheshimiwa Mbunge atatakiwa kwa mahojiano, taarifa itatolewa kwa Mheshimiwa Spika. Hilo lilishasemwa na hivyo ndivyo itakavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wangu kwenye ile inayoangukia kwenye mamlaka yangu, naelekeza, kama suala ni mahojiano angalau kwa kipindi hiki ambacho Wabunge wako Bungeni hapa na wanafanya kazi ya kitaifa, waliyotumwa na wananchi waliowachagua, basi wale watakaokuwa wanataka mahojiano waje wawahojie Wabunge hawa hapa hapa Dodoma. Wachukue hayo maelezo hapa hapa Dodoma na wao warejee katika ofisi zao na yale maelezo waliyowahojia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sababu kubwa tatu. Moja, kazi wanayofanya Waheshimiwa Wabunge hapa Dodoma ni ya kitaifa lakini pili unapunguza *risk* ya kumsafirisha Mbunge umbali mrefu huku unaenda tu kule kuchukua maelezo na tayari ulishafika pale pale na yeye alikuwepo pale pale ungeweza kumhoji kile unachotaka kumhoji na ukaondoka na hayo maelezo. Kama ni vitu vingine ambavyo viko nje ya mhimili wangu kama ni vya kimahakama kwa maana kwamba viko nje ya Wizara yangu, basi hilo litaelekezwa na mamlaka husika kama ni la eneo ambapo anatakiwa akafanyie sio hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mahojiano, yule anayetaka kumhoji Mbunge aje na kumbukumbu zote, aje yule yule ambaye anataka kumhoji. Bahati nzuri Idara yetu imekamilika kila mkoa, kwa hiyo, hata kwa kutuma tu kwamba mhoji kwenye hili na hili inawezekana. Pia yule ambaye ana maelezo aliyetaka kuhoji na yeye anaweza akaja akamhoji Mbunge hapa hapa na hilo likaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini usalama wa raia kwa ujumla wake, naendelea kurudia kusema kwamba, hatutaruhusu na hatutakubali uhalifu uendelee katika nchi yetu. Tunaendelea kupambana kama Serikali, kipaumbele kikubwa ni usalama wa raia wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapooongelea usalama wa raia wetu tunaongelea maisha ya watu wetu. Waheshimiwa Wabunge wengine mlikuwa mnauliza Waziri wa Mambo ya Ndani mbona husemi? Niwaambie kitu kimoja, hii sio Wizara ambayo kila kitu ni habari. Siyo kila habari kwenye Wizara hii ni habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi kwa Waziri wa Mambo ya Ndani siwezi kusema kabla vyombo vyangu havijanipa cha kusema na ni utaratibu wa utendaji kazi katika vyombo hivi. Waziri ukiwa mstari wa mbele kutenda kazi kwenye Wizara ambazo ni za vyombo lazima utoe fursa; moja, ya vyombo kufanya kazi; lakini mbili watu kutendewa haki ili vyombo vifanye kazi kwa mujibu wa sheria, siyo kwa mujibu wa macho ya Waziri yanavyoona kwa sababu taasisi hii inatakiwa ifanye kazi kwa mujibu wa sheria na kwa maslahi ya Taifa na siyo kwa maslahi ya Waziri au vitu binafsi vya Waziri. Ndiyo maana tunatoa fursa ya vyombo vyetu kufanya kazi na Wizara, ndiyo maana tunatoa fursa hii ya kuweka ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mengine tutaendelea kuyapata kwenye Wizara yetu na kwa kuwa hotuba hii ni kubwa basi tutapokea maelekezo kutoka kwa viongozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Umeniomba niongee kwa muda mfupi sana nitajitahidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo machache ambayo yamejitokeza yanahitaji niyatolee majibu. Nianze na la kwanza ambalo ni suala la uelewa tu ambalo Mheshimiwa Nkamia alionesha mshangao hapa kuniona mimi niko pamoja na huyu msanii kwa jina la Roma Mkatoliki anayedaiwa kutekwa pamoja na wenzake watatu siku chache zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati na mimi namsikiliza Mheshimiwa Nkamia Dar es Salaam nilikuwa na kundi kubwa la waandishi wa habari nao walikuwa wanamshangaa kwa nini anashangaa kwa sababu amekuwa kiongozi kwenye Wizara hii anaelewa kabisa Idara ya Habari Maelezo ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa hiyo, ni ofisi yangu ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumehamia Dodoma na Makao Makuu ya Wizara yako hapa *LAPF,* nikiwa Dar es Salaam ofisi yangu iko Maelezo. Sasa mtu akinikuta Maelezo nimemfuata yeye au yeye amenifuata? Ni vitu ambavyo nataka vieleweke. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana huyo alipokuwa amepotea mimi ndiye nilikuwa napigiwa simu na ndugu zake na waandishi wa habari, hakupigiwa Mheshimiwa Nkamia au mtu mwingine, napigiwa mimi. Mimi ndiye mlezi wa hii sekta. Mimi nilikuwa nahangaika na polisi huyu kijana kaenda wapi maana ni vitu ambavyo katika Taifa hili hatujavizoea. Sasa huyu kijana anakuja kuniona ofisini kwangu, kimekuwa kioja tena! Nimekuwa na mkutano naye *for one hour* ofisini kwangu lakini yule kijana ana picha tofauti kabisa kuliko ramli ambazo zinapigwa huko nje na humu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja ananiambia aliyeniteka Mheshimiwa naomba tu upelelezi ufanyike *in detail* kuwa na bastola haina maana mtu lazima atoke Serikalini maana bastola kila mtu anazo. Alichoomba tu alisema tafadhali naomba upelelezi wa kina ufanyike. Kwa hiyo, niliona lazima nimsindikize, ni suala ambalo ni *topic* nchini, *I am the Minister responsible* ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanaacha kupiga ramli tunapata ushahidi wa kutosha, ndiyo upelelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niseme kwamba sasa hivi Sera ya Wizara ni *constructive engagement* na vijana hawa wasanii. Ndiyo maana hata wiki iliyopita alikuja huyu kijana mwingine anaitwa Ney wa Mitego, akaja ofisini kwangu, sasa mlitaka sijui nimkimbie nikae naye kwenye mgahawa, namkaribisha ofisini kwangu ndio hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki ijayo nakaa na Diamond, ni kijana ambaye nimeona wana mfumo mzuri sana wa haki miliki wanauendesha pale katika mfumo wao, *it can be used* hata katika nchi nzima kwa wasanii wengine. Sasa ukinizuia nisikutane nao, ukutane nao wewe ili ufanye nao nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umenipa muda mfupi sana. Kuna suala limejitokeza la lugha za alama, ni Mheshimiwa Ikupa na Mheshimiwa Mollel wameliongelea hili. Ni kweli kabisa, *TV* zetu bado hazijaanza kutoa huo msaada. Kwa kweli siyo kitu kizuri sana kwa sababu hata Mheshimiwa Waziri Mkuu amelikazania suala hilo. Tuna *TV* kama tisa hivi nchini hapa ukiachia zile za *cable* na zote hazijaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hapa ni gharama tu kwamba ukianza kutumia ukalimani lazima kwa siku uwe na wakalimani sio chini ya wanne lakini tumeshaanza majadiliano. Naomba kukuhakikishia kwamba angalau kwa

taarifa za habari tu na sitaki nishinikize *TV* binafsi kabla sijaanza kuhakikisha kwamba *TBC* inaonesha mfano yenyewe katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Kapufi ameongea suala la muhimu sana hapa kwamba hebu tuachane na mipango ya zimamoto katika michezo tuwe na mipango endelevu. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Kapufi. Kwa muda mrefu sana nchi hii, kwa miongo zaidi ya mitatu tumekuwa tunalegalega kwenye michezo. Kwa kweli Mzee wetu, baba yetu Ali Hassan Mwinyi hakukosea kusema tulikuwa kama kichwa cha mwendawazimu, kila mtu alikuwa anakuja kujifunzia kunyoa hapa, lakini yote ni kwa sababu tulikuwa hatuamini katika maandalizi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumebadilika, naomba niliseme hili na ndiyo maana sasa hivi tunaweza kujivunia hata katimu kama Serengeti kwamba *possibility* ni kubwa kakarudi na kombe la dunia hapa nyumbani kwa sababu ya malezi. Vijana wale wamelelewa toka wakiwa na umri wa miaka 12, 13, 14, 15 sasa hivi ni *under seventeen* na hao ndiyo *under nineteen* watakaotuchezea baada ya miaka kadhaa lakini timu nyingine imeandaliwa sasa hivi kuziba nafasi yao. Tumejifunza hilo kwamba tunahitaji kwa kweli kuandaa hizi *talents. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanatumia *academies* lakini sisi kwa uchumi wetu kutokana na sera zetu kwamba tunahitaji kila kijana apate *opportunity,* sisi tumeamua, tena naishukuru sana TAMISEMI, upo hapa Mheshimiwa Waziri kwamba tutumie *peoples academies* ambazo ni shule zetu za msingi na sekondari hizi hizi. Ndiyo maana mwaka huu Mheshimiwa Waziri Mkuu amesisitiza lazima tuwe na michezo ya UMISETA na UMITASHUMTA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimekwenda kupokea kifimbo cha Malkia kuelezea tu kwamba kuna michezo *next*

*year* ya *commonwealth* ambayo tulikuwa tunafanya vibaya. *Can you believe* toka Filbert Bayi avunje rekodi ya dunia miaka 43 bado tuko tu chini sisi. *This time* tutakuja na medali Watanzania kwa sababu tumeanza maandalizi sasa tena ya nguvu kweli kweli kwa ajili ya michezo hiyo inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uliniomba nikuachie dakika chache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, ahsante sana kwa mchango wako. Pia nikushukuru kwa kuniachia muda kidogo kwa sababu nina matangazo mawili, matatu.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza, mmechangia vizuri, orodha ndiyo hiyo na waliopata nafasi ndiyo hao, lakini jioni ataanza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa dakika kumi, halafu Ofisi ya Waziri Mkuu wataingia tukianza na Naibu Waziri halafu Waziri wa Nchi na baadaye mwenye hoja yenyewe halafu tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi.

Waheshimiwa Wabunge, la pili, hii semina yetu waandaaji wanasema saa saba mpaka saa nane maakuli *canteen.* Saa nane na dakika kumi *sharp* muwe humu ndani tuanze semina.

Waheshimiwa Wabunge, la tatu, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Sheikhe Mwongozo wa nini tena, haya tafadhali.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nikupongeze kwa hekima na busara ambayo Mungu amekujalia, Mungu akupe afya njema zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako juu ya taratibu nzuri za uendeshaji wa shughuli za Bunge na kwa kuwa leo kama ratiba inavyosema ni kwamba tunahitimisha.

Naomba mwongozo wako katika shughuli ambayo tunakwenda nayo hii ya Waziri Mkuu na Mawaziri wameanza kujibu, tuna *Vote* karibu tisa. Tuna *Vote* 15, tuna *Vote* 25, tuna *Vote* 27, tuna *Vote* 37, tuna *Vote* 42, tuna *Vote* 61, tuna *Vote* 65, tuna *Vote* 91 na tuna *Vote* 92. Zote hizo tisa ni *Vote* zake Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonekana kwamba wajibu wetu wa kuishauri Serikali na kuisimamia Serikali hatupati nafasi nzuri. Ukiangalia *Vote* 27 ni Msajili wa Vyama vya Siasa, ukiangalia *Vote* 61 kuna Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ukiangalia *Vote* 37 ni Ofisi ya Waziri Mkuu mwenyewe, kwa hiyo kuna mambo ya msingi makubwa. Sasa najiuliza Serikali kwa *Vote* tisa Wabunge leo, muda wa vitabu hivi na ratiba ilikuwa inasema tungeenda mpaka kesho ni kweli Serikali tunataka kweli kuishauri na kuisimamia Serikali au Bunge leo inakuwa kama *rubber stamp* inataka tu twende tumalize hii shughuli?

Mheshimiwa Spika, hasa ukiangalia kilichonitisha nimeangalia kitabu kwenye Ofisi ile Msajili wa Vyama vya

Siasa, nikaangalia kwenye Fungu la ruzuku la Vyama vya Siasa, nikaangalia pale ni sifuri. Sasa kila nikiangaliaangalia na utaratibu tunaokwenda nao na mafungu tisa kwa pamoja yote tunakwenda sisi tu, nikaona Serikali wao watafurahi tu kwa sababu tunakwenda kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako juu ya mafungu tisa kwa pamoja tunakwenda nayo kwa haraka lakini tija inaonekana haipatikani.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Masoud. Tunachukua ushauri wako, lakini tutakapofika wakati huo tutaangalia ni eneo gani ambalo unahitaji hasa kuliangalia kipekee, lakini niseme tu kwamba kama kuna kilichopungua labda ni wale wachangiaji ambao hawakupata nafasi kuchangia kwa Bajeti hii ya Waziri Mkuu, ambao watapata nafasi katika bajeti zinazokuja wala haina wasiwasi. Kwa maana ambao tutautumia kwa kupitia kwenye mafungu mbalimbali ni ule ule ikifanyika kesho, ikifanyika leo muda ni ule ule. Kwa hiyo, tutakwenda vizuri na tutaelezana baadaye namna tunavyoenda. Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atafuatiwa na Naibu Waziri Mheshimiwa Antony Mavunde.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kuchangia. Nikushukuru wewe

mwenyewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna ambavyo mnasimamia uendeshaji wa shughuli za Bunge hili kwa ufanisi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii baada ya kuwa nimesikiliza mjadala huu na mimi nichangie kwa kushauri mambo ambayo yamejitokeza, mambo ya kikatiba na kisheria. Bunge ni taasisi muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa lolote lile, ndiyo maana wanapewa jukumu la kutunga sheria. Kwa sababu ya umuhimu huo mimi nitambue umuhimu wenu ninyi Waheshimiwa Wabunge ni watu muhimu, *your so much very important person,* ndiyo maana mnaitwa Waheshimiwa, lakini Bunge hili nalo lina utaratibu wake wa kufanya kazi; na majukumu ya Bunge yametajwa katika Katiba Ibara ya 63 inaeleza vizuri majukumu ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 63(2) inasema; " Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi, kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza-

(a) kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yapo katika wajibu wake;

(b) kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti;

(c) kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo;

(d) kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo sheria; na

(e) kujadili na kuridhia mikataba yoyote inayohusu Jamhuri ya Muungano ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, pia Bunge limepewa uhuru wa mijadala humu ndani, Ibara ya 100. Lakini Ibara ya 100(2) imeweka masharti kuna mipaka, Ibara ya 100(2) ya Katiba inasema hivi; "Bila kuathiri Katiba hii, au masharti ya sheria nyingine yoyote inayohusika, Mbunge yeyote hatashtakiwa au kufunguliwa sharti la madai mahakamani kutokana na jambo na lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge, au alileta Bunge kwa njia ya maombi, muswada, hoja au vinginevyo." Katiba hii pia imegawa madaraka katika mihimili mitatu ya dola ambayo ni Bunge lenyewe, Mahakama na Utendaji.

Mheshimiwa Spika, Bunge linatunga sheria na kuismamia Serikali utekelezaji wake, Mahakama inatafsiri sheria inatoa haki na Serikali kwa maana ya utendaji, inasimamia utekelezaji wa sheria zilizotungwa na Bunge. Katiba hii inaposema kwamba bila kuathiri masharti haya ina maana kwamba Bunge lazima ifanye kazi zake kwa mujibu wa sheria. Ndiyo maana sasa Ibara ya 26 ya Katiba inaeleza kila mtu ana wajibu wa kuifuata na kuitii Katiba hii na sheria za Jamhuri ya Muungano na kwamba kila mtu ana haki ya kufuata utaratibu uliowekwa na sheria kuchukua hatua za kisheria kuhakikisha hifadhi ya Katiba na sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, moja ya sheria zilizotungwa ni Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, ambayoo inaeleza kitu gani Bunge linaweza kufanya na ambacho hawawezi kufanya na imeweka makosa ya jinai mle ndani. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tunazo Kanuni za Bunge ambazo zinatungwa chini ya Ibara ya 89 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kuendesha shughuli za Bunge hili.

Ibara hii ya 64 inasema hivi; " Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda au kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:

(a) Hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli;

(b) hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala;

(c) hatazungumzia jambo lolote ambalo linahusu uamuzi wa Mahakama au jambo lolote ambalo lilijadiliwa na kutolewa uamuzi kwenye Mkutano uliopo au uliotangulia na ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahsusi. Vilevile hatapinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge isipokuwa kwa kutoa hoja mahususi inayopendekeza kuwa uamuzi huo uangaliwe upya;

(d) Hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani;

(e) Hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia utoaji wa haki, isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahsusi inayohusu jambo husika.

(f) Hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote, hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Spika, nimeona niliseme hili ili kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wajibu wetu kwamba shughuli zetu humu ndani zinaongozwa na masharti ya Katiba, zinaongozwa na masharti ya Kanuni tulizozitunga wenyewe, zinaongozwa na sheria. Tukifanya vile ndipo tutaweza kutekeleza jukumu letu kwa ufanisi ipasavyo la kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, wakati mjadala unaendelea hapa yamejitokeza mambo. Moja yamezungumzwa mambo ambayo yapo Mahakamani, naomba kushauri mambo yote ambayo yako Mahakamani, Katiba imekataza Ibara ya 30(2) ya Katiba imekataza, mambo yaliyopo Mahakamani, inalinda uhuru wa Mahakama na heshima ya watu walioko Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kesi ya mgogoro wa Chama cha CUF yapo Mahakamani. CUF wamepeleka Msajili wa Vyama vya Siasa Mahakamani na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo ushauri kwamba mambo haya tusiyazungumze tena na mambo mengine. Pia mambo ya kutaja jina la Rais hovyo hovyo mambo hayo yote yamekatazwa hapa, kuwaudhi na yamewekewa utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge wote tuna mamlaka lakini mamlaka haya yana mipaka. Ibara ya 100 ya Katiba imeshatafsiriwa na Mahakama Kuu ya Tanzania kwenye katika kesi ya Mheshimiwa Pinda na mimi ndiye niliyeendesha kesi ile, kwa hiyo tuna mipaka yetu. Tunapotekeleza wajibu wetu tuzingatie mipaka hii, hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria na Mheshimiwa Mbowe amesema kwenye taarifa yake. Kwa hiyo, kama hivyo tunavyotambua hivi tufanye hivyo na naomba kushauri.

Mheshimiwa Spika, Kanuni hizi na sheria hizi, zimempa mamlaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwapeleka watu Mahakamani, sitaki kufika huko mimi, kwanza nawapenda sana, nawathamini sana. Hata Waziri Mkuu amesifu utendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali uliohakikisha kwamba hizi kesi zilizokuwa zinawakabili zimekamilika mapema ili mrudi muwawakilishe wananchi wa majimbo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo lazima mlielewe. Kipindi cha bajeti hii Wabunge nawashauri m-*concentrate* sana kwenye mambo yanayohusu wananchi wenu. Kule kuna shida nyingi watu wanataka maji, watu wanataka elimu, watu wanataka umeme, *you would wish to concentrate on those important*

*issues.* Haya mambo mengine yaachieni Serikali itayashughulikia tu yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote wanaohusika na Ofisi yake na timu yake kwa kazi nzuri wanayofanya, wameleta hapa hotuba nzuri sana inayoonyesha mambo makubwa ambayo Serikali hii imefanya mpaka sasa katika kipindi cha mwaka mmoja. Mungu aibariki Serikali hii, Mungu akubariki Waziri Mkuu, Wabunge na wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo kimsingi hayapaswi kuletwa hapa, yamezungumzwa hapa mambo yanayohusu Usalama wa Taifa na mustakabali wa Taifa hili. Wabunge, tumetunga sheria sisi wenyewe hapa, tunayo Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970 na tunayo Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1996. Juzi tumetunga sheria ya *Whistleblower and Witness Protection,* tumeweka masharti ni yapi ambayo yanaweza kuzungumzwa na yapi hayawezi kuzungumzwa na ni makosa ya jinai haya.

Ninawashauri Waheshimiwa Wabunge muda hautoshi, ningekuwa na muda ningesema yote haya, wazisome vizuri hizi sheria ni mambo gani ambayo hayapaswi kuzungumzwa kwa mustakabali wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya ulinzi na usalama yamewekewa utaratibu wake, hata Kamati yako, unayo Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama, mnaona mambo yake yanazungumzwazungumzwa hapa hovyo hovyo? Halafu hatujajua kwamba hapa ni watu wa Usalama tu kama alivyosema Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hivi kila mtu anayebeba bunduki ni mtu wa mambo ya usalama, hatuwezi kufika kule.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuna suala hapa nilitegemea Waheshimiwa Wabunge kwenye *issue* ya usalama watajikita sana kwenye mauaji ya viongozi wa Serikali kule Rufiji, watu wameuawa kule, *and then* tujiulize hii habari ya

kutekateka hivi wameshatekwa watu wangapi? Katika Serikali hii wametekwa wangapi?

**MBUNGE FULANI:** Wawili.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Hakuna hata watu wawili, ni mmoja. Kwa sababu aliyekwisha kutekwa mimi ninayemfahamu ni huyu mwanamuziki anayeitwa Mkatoliki. Huyu wa kwanza anayeitwa Ben Sanane *so far* haijulikani, ameondoka nchini, amejificha, yuko wapi, sasa huwezi kusema ametekwa huyu. Halafu tutofautishe kuteka na kukamatwa na vyombo vya dola kwa ajili ya kuhojiwa. Ukikamatwa na polisi ukaenda kuhojiwa huwezi kusema umetekwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kulishauri Bunge lako Tukufu, kwenye suala hili *we need to be so much serious and strict on enforcement of our rules.* Hatuwezi tukafikia hatua, hivi kwanza mimi nashangaa, hili suala mtu mmoja na muda mfupi tu amepatikana na Waziri ameenda kuangalia pale mna-*challenge*, mlitaka achelewe kupatikana na huyo aliyesema Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, kazi zake zimetajwa kwenye sheria ya Baraza la Usalama wa Taifa. Vyombo vyote vya upelelezi viko pale, kama wamemwambia kwamba mwenendo wetu wa uchunguzi unaelekea tutampata hivi karibuni, mnamhusishaje na utekaji nyara wa watu? Hili suala naomba lisikuzwe, linakuzwa nadhani lina sababu tatu za msingi. *(Makofi)*

Moja, inawezekana matukio haya wanataka kuyatumia watu wasio na nia njema na Taifa hili kufanya uhalifu, waseme kwamba kulikuwa na hii mipango, *if you have any serious information about the crime...* taarifa zote za uhalifu pelekeni kwenye vyombo vya dola. Hatuwezi kufanya hivi. Huyu Ben Sanane hamuwezi kusema kwamba amekufa, Sheria yetu ya Ushahidi inasema ili uweze kuthibitisha kama mtu amekufa baada ya miaka mitano imepita na yule anayedai amekufa ndio ana jukumu la kwenda kuthibitisha

hayo. Someni kifungu cha 117 cha Sheria ya Ushahidi, hatuwezi kufanya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba watu wana vitendo vya uhalifu, labda wanahisi kwamba wakati wote watakamatwa na kuhojiwa inakuwa ni *pre-emptive method...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa hapa mambo ya uchaguzi Zanzibar, uchaguzi Zanzibar umeshapita. Uchaguzi wa Zanzibar unatawaliwa na Katiba ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Novemba ulifutwa Kikatiba wakasema wanarudia mwezi wa tatu, 2016 ukarudiwa na sasa kuna Serikali kule haya yasizungumzwe hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo yanayozungumwa hapa ya mchakato wa Katiba Mpya. Mchakato wa Katiba Mpya tulitunga sheria, ipo Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, ipo Sheria ya Kura ya Maoni, hatua zote zimeshakamilika sasa kimebaki ni kiporo kwa mujibu wa ile sheria, muda muafaka utakaofika ambao mimi siujui mtaenda huko kwenye kupiga kura kama mtaamua hivyo. Kwa sababu kwanza ninyi wenyewe mlikuwa ni *divided* mara mlikuwa hamuitaki wengine mkasusia, eeh! Hata mimi nilivyosema tutunge sheria mkakataa wengine! Kwa hiyo, wakati muafaka hiyo mtapiga Kura ya Maoni *we can not go back to the Constitution whatever.*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, muda hauko upande wako tena, nakushukuru sana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Naibu Waziri Mheshimiwa Antony Mavunde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu wa rehema kwa kutujalia Waheshimiwa Wabunge wote uzima na afya njema. Pia nichukue fursa hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuchangia hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nikiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, ninayeshughulikia masuala ya Kazi, Vijana Ajira na Watu Wenye Ulemavu, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama kwa ushirikiano mkubwa na miongozo wanayonipa inayoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba kutumia fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa kuendelea kuniunga mkono na kushirikiana na mimi katika utekelezaji wa majukumu haya ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba sasa uniruhusu nichangie hoja hii kwa kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge walichangia na kutaka ufafanuzi. Nitatoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja na hoja nyingine zitajibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hoja ambayo ilijotekeza ya kwanza kabisa ilikuwa ni masuala ya Usalama na Afya Pahala Pa Kazi *(OSHA).* Waheshimiwa Wabunge walitamani kusikia kwamba tunaendelea kusimamia afya na usalama wa

wafanyakazi pahala pa kazi na hasa wafanyakazi ambao wanafanya kazi katika maeneo ya migodini na viwandani, na hatua za kisheria zichukuliwe kwa wale wote ambao hawazingatii masuala ya afya na usalama wa wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapokea ushauri wa Kamati wa kuendelea kusimamia afya na usalama pahala pa kazi hususan migodini na Serikali itaendelea kutoa elimu na kuchukua hatua kwa waajiri wote ambao hawatazingatia masuala ya afya na usalama kwa wafanyakazi wao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kila mtu anafahamu na ni dhahiri kwamba falsafa ya Serikali ya Awamu ya Tano ni ya uchumi wa viwanda ambayo itakwenda kuwaajiri Watanzania wengi sana wengi wao wakiwa ni vijana, kwa hiyo, sheria hii sasa itakuwa ni sehemu ya kuweza kui-*protect* nguvukazi ya nchi kutokana na haya ambayo yanaweza kutokea katika migodi na viwandani.

Mheshimiwa Spika, aidha katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Wakala wa Afya na Usalama Pahala Pa Kazi *(OSHA)* umewachukulia hatua waajiri 701 waliokiuka matakwa ya Sheria ya Afya, Usalama Pahala Pa Kazi ikiwemo wamiliki wa migodi mikubwa iliyopo nchini.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilizungumzwa ni Serikali itoe elimu bora kwa watu wenye ulemavu ili wajiondoe katika hali ya utegemezi. Suala la kushughulikia changamoto za watu wenye ulemavu, ikiwemo kuwawezesha kujiondoa katika utegemezi ni moja kati ya vipaumbele ambavyo vimeainishwa kwenye Ilani ya uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015, Ibara ya 166; hivyo, Serikali itaendelea kutoa elimu bora kwa watoto wote nchini, wakiwemo watoto wenye ulemavu kwa kutoa vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali inasambaza vifaa

hivyo kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza ni kwa wanafunzi wasioona na viziwi, awamu ya pili vifaa vitasambazwa kwa watoto wenye ulemavu wa akili na wenye usonji na hatimaye kwa wenye ulemavu wa viungo. Hadi sasa vifaa vilivyosambazwa katika awamu ya kwanza katika shule za msingi na sekondari ni kama ifuatavyo; mashine za nukta nundu *(brail machine)* 932, shime sikio *(hearing aids)* 1,110, karatasi za kuandikia maandishi ya nukta nundu - rimu 2,548, karatasi za kudurufu maandishi ya nukta nundu - rimu 1,000, *universal brail kits* yenye vifaa mchanganyiko 1,495.

Mheshimiwa Spika, katika hoja zilizojitokeza pia hapa, Wabunge walizungumza kuhusu Mfuko wa Watu wenye Ulemavu kwamba haukutengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2016/2017 hivyo Serikali ijitahidi kutenga fedha kwa ajili ya mfuko huu ambao utawezesha Baraza la Watu wenye Ulemavu kutekeleza majukumu yake ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 50 ambazo zitatumika kuandaa mfumo na uratibu wa uendeshaji wa mfuko wa watu wenye ulemavu. Aidha, watu wenye ulemavu wanaendelea kupata huduma mbalimbali, hususan kuwawezesha kiuchumi kupitia mifuko, ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ngazi ya Halmashauri pamoja na programu ya kukuza stadi za kazi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili pamoja na kuwa na programu nyingi sana za uwezeshaji katika kundi hili, lakini pia kila programu ya Wizara hasa katika ukuzaji ujuzi tumekuwa tukitenga asilimia kadhaa kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Mfano wa programu mojawapo ni Programu ya *Youth Economic Empowerment* ambayo iliwahusisha takribani vijana 9,100 katika mikoa mitano ya Mtwara, Lindi, Morogoro, Dar es Salaam na Pwani ambapo walijitokeza watu wengi wenye ulemavu na walipata fursa kushiriki katika mafunzo haya na walikuwa ni kati ya watu ambao walifanya vizuri sana. Kwa hiyo, kama Serikali imekuwa ni sehemu ya msisitizo pia, kuona namna ya kutoa fursa katika kundi hili.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa SHIVYAWATA, Dada Ummy Nderiananga, ambaye amekuwa akifanya kazi kubwa sana pamoja na Serikali katika kuhakikisha kwamba tunaongeza uelewa katika kundi hili la watu wenye ulemavu ili wengi zaidi wajitokeze kushiriki katika programu mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ilijitokeza pia, hoja ya kwamba watoto wenye ulemavu wa macho kutokuwa na uwezo wa kurejea nyumbani nyakati za likizo kutokana na kutokuwa na wasindikizaji. Niliarifu tu Bunge lako kwamba Serikali tumeliona hili na tunalichukua na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kuitaka Serikali iwasilishe takwimu za hukumu zilizotolewa kwenye kesi zinazowahusu waliohukumiwa kwa makosa ya jinai, kuhusiana na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, takribani kesi 28 za ukatili wa jinai kwa watu wenye ulemavu zimetolewa hukumu na kesi 37 ziko Mahakamani. Nichukue fursa hii kuwashukuru sana mhimili wa Mahakama kwa kuendelea kutoa msisitizo mkubwa wa usikilizaji na umalizaji kesi hizi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilikuja pia hoja nyingine ya Wabunge walichangia uanzishwaji wa kambi za kilimo kwa ajili ya vijana ili iwasaidie vijana kuweza kujiajiri. Serikali kupitia Programu za Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi inalenga kuwawezesha vijana kujiajiri katika sekta za uzalishaji mali, ikiwemo kilimo. Aidha, wadau mbalimbali wakiwemo *FAO, Techno Serve*, *World Vision Tanzania, Heifer International, Swiss Contact, Planning International* na *ILO,* wameendelea kutekeleza programu mbalimbali kuwawezesha vijana kujiajiri katika sekta ya kilimo pamoja na mnyororo wake wa thamani. Serikali pia kupitia Vituo vya Vijana vya Ilonga na Sasanda inaendesha programu za kilimo katika mfumo wa mashamba darasa ambapo vijana wanaojishughulisha na kilimo kutoka maeneo mbalimbali wanafika na kupata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, mafunzo yanayotolewa ni pamoja na kitalu nyumba kwa mazao ya mbogamboga, mazao ya biashara kama vile kahawa, mazao ya chakula, ufugaji wa ng'ombe, samaki na nyuki. Aidha, Serikali imezindua mkakati wa kuwawezesha vijana kujiajiri kwenye sekta ya kilimo pamoja na mnyororo wa thamani.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu tunaufanya pamoja na Wizara ya Kilimo ambapo tuna mkakati wa Kitaifa wa kuwaingiza vijana kwenye kilimo, moja kati ya maeneo ambayo tunaanza nayo ni katika eneo la Morogoro - Mkulazi, ambapo kitajengwa kiwanda cha sukari chini ya mifuko ya *PPF* na *NSSf.* Katika eneo lile zimetengwa takribani ekari elfu 63. moja kati ya eneo ambalo tulilichukua kubwa tutapatengeneza *blocks* za mashamba kwa ajili ya vikundi vya vijana na tunategemea kutoa ajira kupitia mashamba haya, ajira takribani 100,000.

Mheshimiwa Spika, vilevile siyo kwa wananchi wa Morogoro tu mashamba haya yanaweza pia yakatawanywa pembezoni mwa Morogoro, hasa katika Mkoa ambao miwa ile ikilimwa inaweza kufika kiwandani ndani ya saa 24. Kwa hiyo, vijana wote waliopo nje ya Morogoro lakini wenye uwezo wa kufanya shughuli ya kilimo, wana uwezo wa kulima mua huu na soko lake liko *assured* kwamba viwanda hivi vitachukua miwa hii. Kwa hiyo, naendelea kutoa wito kwa vijana wote nchi nzima kuona fursa hii na kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, ilijitokeza pia hoja ya pongezi, Wabunge walipongeza kwa programu mbalimbali ikiwemo ya ukuzaji ujuzi, hasa kupitia viwanda vya *Tooku Garments* cha Dar es Salaam na *Mazava Fabrics* Morogoro. Vilevile walishauri kwamba programu hizi zipanuliwe na ziweze kuwafikia vijana wengi zaidi. Pongezi zimepokelewa na Serikali itaendelea kupanua wigo wa utekelezaji wa programu ya kukuza ujuzi na stadi za kazi ili kuwafikia vijana wengi zaidi nchini.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 vijana zaidi ya 17,350 watanufaika na mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi

yatakayotolewa sehemu mbalimbali nchini, ukilinganisha na vijana zaidi ya 9,120 ambao watanufaika mwaka 2016/2017. Aidha, mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi yatakayotolewa na Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam *(DIT)* Mjini Mwanza mwishoni mwa mwaka huu wa fedha yatawanufaisha pia vijana kutoka Shinyanga walioomba kujiunga na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilijitokeza ni ya mkakati wa uwezeshaji wa vijana na akinamama kiuchumi uendane sambamba na kuwapatia elimu ya kitaalamu katika nyanja za ujasiriamali. Serikali kwa kushirikiana na wadau inaendesha programu mbalimbali za mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana. Programu hizo zinaendelea kuongeza ujuzi kwenye maeneo mbalimbali. Mfano wa programu hizo ni pamoja na ufundi wa stadi za kazi kwa vijana wa Vyuo Vikuu, JKT, wafanyabiashara na waendesha bodaboda. Serikali imeanzisha utaratibu maalum wa majukwaa ya wanawake kwenye Mikoa na Halmashauri zote nchini. Katika majukwaa hayo wanawake wanapata fursa ya kupata elimu ya ujasiriamali, taarifa za mitaji na masuala mengine ya kuboresha shughuli zao za kiuchumi. Serikali pia inaendelea kuzisimamia kwa karibu Halmashauri zote nchini kulenga na kutoa fursa za mikopo kwa wanawake na vijana kwa asilimia tano kama ilivyoelekezwa.

Mheshimiwa Spika, ilizungumzwa pia hoja ya mikataba kwa wafanyakazi. Wabunge waliishauri Serikali kuendelea kusimamia sheria ili wafanyakazi wengi zaidi waweze kupata mikataba.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili ninataka nikiri kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kufanya kaguzi mbalimbali kuhakikisha kwamba Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya mwaka 2004, inafuatwa kwa waajiri wote kutoa mikataba, kama ambavyo kifungu Namba 14 kinavyosema. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya kaguzi mbalimbali ili basi kuweza kuwabaini wale waajiri wote ambao wanakiuka Sheria hii na tunaendelea kuchukua hatua kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa nchi hii

wanapata mikataba yao na wafanye kazi wakiwa na mikataba.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia katika hoja ambazo zimesemwa, baadhi ya wachangiaji walikuwa wanahoji mipango ya Serikali kama kweli ina nia thabiti ya kuwasaidia vijana wa nchi hii. Nataka niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge ya kwamba hata ukiangalia *trend,* katika kipindi hiki cha muda wa mwaka mmoja kazi nyingi sana za vijana zimefanyika, mafunzo mengi sana yamefanyika na kwa kweli, ukiangalia kazi ambazo zimefanyika zimewagusa vijana moja kwa moja na imewasaidia sana kuwafanya vijana hawa waondokane na utegemezi. Sasa tunawatengenezea utaratibu ili vijana wengi zaidi waweze kujiajiri kupitia katika programu zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika kushughulikia masuala ya vijana jambo la kwanza kabisa ambalo tunalifanya ni kuwatambua kwanza vijana, tunafanya *identification* ya vijana kwa makundi yao. Tuna vijana wa aina tofauti, tuna *graduates,* lakini tuna vijana ambao hawakupata fursa ya kupata elimu ya juu. Vilevile hatua ya pili tunayoifanya ni ya kuwarasimisha *(formalization),* hapa tunawaweka vijana katika vikundi kupitia *SACCOS* na kampuni vilevile.

Mheshimiwa Spika, ninao huu mfano wa vijana ambao wanafanya vizuri sana, ambao ni vijana kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine ambao wao walihitimu pale chuoni na baadaye wakatengenezewa utaratibu na wakapewa mikopo. Vijana hawa wanaitwa *SUGECO* ambao wanafanya shughuli za kilimo na hivi sasa ni kati ya vijana ambao wanafanya vizuri sana na wameanza kuwasaidia vijana wenzao nchini kwa kuwasaidia mitaji, vilevile na kuwapa mafunzo mbalimbali hasa katika maeneo ya kilimo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanahoji namna ya uwezeshaji wa vijana. Katika Ofisi ya Waziri Mkuu tunayo mifuko mingi sana, lakini mifuko hii pia tunaratibu pamoja na Wizara zingine. Lakini huu mfuko mkubwa ambao

tunautumia ni Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao mpaka ninavyozungumza hivi sasa tayari umeshakopesha takribani vikundi 297 kiasi cha shilingi bilioni 1.5 na vijana wamenufaika na tumeanza kuona matokeo na mabadiliko miongoni mwa vijana. Siyo hivyo tu, tuna Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, vilevile tunao Mfuko wa Nishati ya Umeme Vijijini. Katika hili pia tunao mfuko wa kutoka *BOT (SME)* unaitwa *Small and Medium Enterprises Credit Guarantee Scheme,* hii yote inafanya kazi za kusaidia kuwawezesha vijana.

Mheshimiwa Spika, ilikuja hoja hapa ya kwamba kama Serikali tumejiandaaje? Inavyoonekana katika takwimu vijana wanaokwenda katika soko la ajira kila mwaka ni takribani vijana 800,000 mpaka 1,600,000, lakini nafasi za ajira zinazotengenezwa ni chache sana. Serikali tuliona jambo la kwanza la kufanya ili kumfanya kijana wa Kitanzania ajitegemee cha kwanza kabisa ilikuwa ni kuanza kuwabadilisha mtizamo, kuwabadilisha mtizamo vijana ilianza katika kuwapa elimu na kufafanua kwamba ajira maana yake ni nini. Kwa sababu mtazamo uliopo hivi sasa ni kwamba ili mtu aonekane ana ajira ni lazima awe tu ana ofisi yake, anavaa shati jeupe, ana tai, ana kiti cha kuzunguka, hiyo ndiyo ajira. Kwa mujibu wa Sera ya Ajira ya Taifa, inasema ajira ni shughuli yoyote halali ambayo inampatia mtu kipato.

Kwa hiyo, tumeanza kuwaondoa vijana kimtazamo kuamini kwamba siyo wote lazima waajiriwe, kuna shughuli za kilimo, kuna shughuli za ufugaji, shughuli za ujasiriamali. Ninavyozungumza hivi sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, malizia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza hivi sasa tumetenga takribani ekari 85,000 nchi nzima kwa ajili ya shughuli hizi za vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri. Sasa naomba nimuite Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuweza kutufikisha tena siku hii ya leo tukiwa wazima na salama. Ninakushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu utendaji kazi wa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amekuwa ni kiongozi mahiri, imara na shujaa katika kusimamia maendeleo ya nchi yetu. Naomba nichukue nafasi hii pia nimpongeze Makamu wa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya na vilevile kwa nafasi ya pekee kabisa, nimpongeze sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwangu binafsi naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyoniongoza, kwa jinsi anavyonisaidia kumsaidia kazi katika Ofisi yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nikushukuru sana. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mchapakazi, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni jembe hasa linalotosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwapongeza Viongozi Wakuu hao niliowataja, nichukue nafasi ya pekee nimpongeze sana Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Antony Mavunde amekuwa ni msaada mkubwa sana katika kazi zangu, naomba nimshukuru sana. Kwa nafasi ya pekee

nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Antony Mavunde kwa sababu leo amepata *baby girl, first born* wake, Mungu ampe maisha marefu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumkumbuka pia Balozi Dkt. Abdallah Possi ambaye alifanya kazi nzuri ya kunisaidia. Nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amekuwa ni mshirika wangu mkubwa katika kuhakikisha shughuli za Bunge na shughuli za Serikali zinakwenda vizuri. Siwezi kuendelea na majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge bila kutambua mchango mkubwa wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania linaloongozwa na Rais wao Ndugu Tumaini Nyamhokya na Katibu Mkuu, Dkt. Yahaya Msigwa, pamoja na Shirikisho la Waajiri Tanzania linaloongozwa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Almasi Maige na Mtendaji Mkuu Ndugu Aggrey Mlimuka, wamekuwa wakitupa ushirikiano mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu nawashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Peramiho, Hapa Kazi Tu, tutaendelea na mwaka 2020 ni mambo vilevile, Hapa Kazi Tu, ushindi kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu hoja hizi za Kamati nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na Makamu wake, ndugu yetu Mheshimiwa Najma Giga, lakini na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa ushurikiano mkubwa. Niwashukuru pia, Wajumbe wa Kamati ya UKIMWI inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na Makamu wake Mheshimiwa Dkt. Tiisekwa na Wajumbe wote. Nichukue nafasi ya pekee kumshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Ndugu yangu Mheshimiwa Josephat Kandege na Wajumbe wote kwa ushirikiano mkubwa waliotupa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru sana Shirikisho la Vyama vya Wenye Ulemavu Tanzania, vikingozwa na dada Ummy. Naomba nitambue mchango

wa pekee wa Wabunge wawili ndani ya Bunge hili wenye ulemavu, dada yangu Mheshimiwa Stella Ikupa Alex na dada yangu Mheshimiwa Amina Mollel, wanafanya kazi nzuri sana na tunashirikiana nao vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge na wafanyakazi wote wa Bunge kwa jinsi wanavyotusaidia ndani ya Serikali kutekeleza majukumu yetu hapa Bungeni sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(2) naomba sasa kwa heshima kubwa nitoe majumuisho ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Ninaomba kwanza hotuba yangu hii iingie yote kwenye *Hansard,* vilevile tutaleta kitabu cha majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu muda ni mfupi hatutaweza kuyajibu yote. Kabla ya kujibu hoja naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Nsanzugwanko alisema sana hapa, tuendelee kama waratibu wa Serikali kuangalia kuleta maendeleo kwa kuzingatia uwiano wa mikoa yetu na jinsi maendeleo yalivyo ndani ya mikoa yetu. Kwa hiyo, ndani ya Serikali tutaangalia kwa sababu, lengo letu ni kuhakikisha Watanzania nchi nzima wanaendelea bila kujali ukabila wala ukanda wala nini, lakini ni lazima wote wapate maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na hoja ya Makao Makuu Dodoma. Kulikuwa na hoja nyingi zinazohusu Serikali kuhamia hapa Dodoma. Hii ilikuwa ni ndoto ya Marehemu Baba wa Taifa, lazima niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge. Tarehe 30 Agosti, 1973 mpaka tarehe 9 Septemba, 1973 Halmashauri Kuu ya chama cha *TANU* ambacho ni baba ni Chama cha Mapinduzi, iliketi Dar es Salaam na kuridhia kwamba Makao Makuu ya nchi yatakuwa Dodoma na mwaka1973 Chama cha *TANU* kiliamua na kupitisha maazimio hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa uhamiaji tunaohamia nao kwenye Serikali ya Awamu ya Tano, wote tunakumbuka kwamba, tarehe 23 Julai, 2016 Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa anahutubia kwa mara ya

kwanza kwenye Mkutano wa CCM kama Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, aliwatangazia Watanzania kupitia Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Tano itahamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Serikali hii imeshakwishakuhamia hapa Dodoma na tumehamia hapa watendaji wakuu wote, Mheshimiwa Waziri Mkuu akituongoza, Mawaziri, Naibu Mawaziri wote, Makatibu Wakuu wote, Naibu Makatibu Wakuu wote na baadhi ya Watumishi ambao tumehamia nao hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengi walifikiri hili ni suala la kisiasa na kuna watu wamechangia wanasema Serikali haina dhamira ya dhati. Naomba niwakumbushe huu ni utekelezaji wa Ibara ya 151 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, faida za kuhamia Dodoma, Wabunge wamechangia kuuliza ni zipi? Pamoja na kutusaidia kwamba Makao Makuu kuwa katikati ya nchi yetu, lakini tunaona kabisa kwamba Serikali itapunguza gharama kubwa sana za matumizi ya uendeshaji wa Serikali na hasa inapokuwa vipindi vya Bunge, kuhamisha Serikali kutoka Dar es Salaam kuja kushughulika na shughuli za Bunge. Vilevile tutaenda kuchachua uchumi wa nchi kwa kuhakikisha kwamba tunatoa nafasi ya maeneo mengine kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kuleta Bungeni Sheria ya Makao Makuu, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba mchakato wa maandalizi ya sheria hiyo uko tayari na mara tu tutakapokuwa tumefikia hatua ya mwisho tutaomba ridhaa yako na wewe umetuagiza sana na umetuambia hapa hakieleweki mpaka sheria mwaka huu iingie Bungeni. Tupo tayari tutawasiliana na Ofisi yako na tutaleta sheria hii humu ndani. Mpaka sasa tunaendelea kuhamia Dodoma kwa kutumia *GN* Na. 230 ya mwaka 1973 na hiyo nayo ni tamko la kisheria la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipokea hoja nyingine ya kuhakikisha kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza katika ujenzi wa viwanda kama ni tija na inaweza ikawa na faida gani. Kwanza niseme kabisa kwamba uwekezaji katika sera hii ya viwanda unatokana pia na mpango wetu wa maendeleo wa miaka mitano. Hivyo basi, Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii imeamua kuwekeza kwenye miradi ya viwanda 25 yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 153 mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulichokifanya kama Serikali ni kuhakikisha kwamba uwekezaji huo unakuwa na tija na tija ya kwanza utakwenda kuzalisha ajira za watoto wa Kitanzania 310,000 kwenye viwanda hivyo 25. Kwa hiyo, ni jambo la kupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vipo baadhi ya viwanda vimeshaanza kufanyakazi tutatoa orodha kwa Wabunge muda ni mfupi tungeweza kuvisoma hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri ameweza kutaja baadhi ya viwanda hivyo. Tumesema pia viwanda hivyo vitasaidia pia kutengeneza soko la mazao yetu na kuongeza thamani ya mazao ya wakulima katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na hoja kuhusu mradi wa *MIVARF,* huu ni mradi wa miundombinu ya masoko na uongezaji wa thamani na huduma za fedha vijijini. Mradi huu Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati walitaka kujua maendeleo ya ujenzi wa ukarabati wa barabara na ukarabati wa masoko Pemba na Unguja. Mradi huu ulianza kufanyiwa kazi mwaka 2014 na ulikamilika katika maeneo kadhaa na hasa kwenye eneo la barabara mwaka 2015 kule Pemba na Unguja. Kwa sasa tunaendelea na mradi wa kukamilisha maeneo ya masoko. Jumla ya kilometa za barabara 148.5 zimejengwa na masoko manne makubwa yameweza kujengwa kule Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema mradi huu unazo faida nyingi na umekuwa ni mradi shirikishi, mradi huu umekuwa ni kichocheo kikubwa cha muonekano wa

mashirikiano yetu ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ninaomba tu niseme kwamba pamoja na mafunzo yanayotolewa kwa wananchi, jamii kushirikishwa kuweza kubadilisha mfumo mzima wa uzalishaji mazao na masoko yao, nawapongeza Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na hasa Mheshimiwa Ally Saleh. Mheshimiwa Ally Saleh alikiri kabisa kwamba mradi huu ni kiashirio kizuri cha Muungano kati ya Tanzania Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono na mawazo ya Mheshimiwa Ally Saleh, lakini tujue kabisa kwamba Muungano wetu una faida kubwa na ni lazima tuendelee kuuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja iliyohusu Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Mfuko huu umeanzishwa kwa Sheria Namba 20 ya mwaka 2008. Mfuko huu umeweka mfumo mzuri ambao ni wa kidijitali wa kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazotokana na watu ama wafanyakazi wanaopata ajali kazini zinapatikana kwa haraka na malipo kwa watu hao wanaopata ajali kazini yanafanyika kwa haraka. Sheria hii iliyoanzisha huu mfuko imeweza kuwakomboa wafanyakazi wengi sana katika nchi yetu ya Tanzania na tunategemea itafanya kazi nzuri ya kutoa fidia kwa magonjwa, vifo na ajali zinazotokea maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Wabunge walitaka kujua kazi zilizofanywa mpaka sasa. Mpaka sasa tumeshafundisha madaktari kama 359 nchini ambao wamepewa uwezo wa kubaini magonjwa na namna ya kutathmini athari na ulemavu unaotokana na ajali kazini. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa kazi za mfuko huu kwa kuwa sasa zimeshaanza basi malalamiko ya wafanyakazi katika sekta ambazo zimeainishwa kwenye mfuko na Sheria ya Mfuko hatutakuwa tena matatizo ya kutoa fidia kwa wafanyakazi wote nchini. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kuwaeleza taasisi mbalimbali ambazo zinawaajiri katika maeneo yenu ili

watambue sasa tuna mfuko huu wa fidia kwa wafanyakazi ambao umeshaanza kutoa fidia kwa wafanyakazi na wajisajili waajiri wote.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia mfuko wa fidia kwa wafanyazi uzingatie sera na miongozo ya uwekezaji. Naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba agizo hilo linasimamiwa vizuri na Serikali, vilevile linasimamiwa vizuri na *SSRA* ambaye ni mdhibiti wa sekta ya hifadhi ya jamii pamoja na Benki Kuu ambao ndio wamepewa kazi ya kusimamia uendeshaji na uwekezaji unaofanywa na mifuko ya hifadhi ya jamii katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia mfuko huu wa fidia kwa wafanyakazi uchukue jitihada za kutosha katika kupambana na kudhibiti mianya yote ya rushwa. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba mfuko unazingatia maagizo ya Serikali na umeweza kuweka miongozo ambayo inaongozwa na sheria iliyoanzishwa ya mapambano dhidi ya rushwa katika nchi yetu ya Tanzania hivyo, mfuko unaendelea kutekeleza agizo hilo vizuri.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuboresha kiwanda cha Mpigachapa Mkuu wa Serikali na Waheshimiwa Wabunge na Kamati walituagiza tuhakikishe kwamba tunaboresha mazingira ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi hiyo tuliianza kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 na tulitenga fedha za Kitanzania milioni 150 za kuanza mchakato wa zoezi hilo. Fedha hizo zimetumika mpaka sasa kumuweka Mshauri Elekezi ambayo ni Taasisi ya Viwanda na Ujenzi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wao wameshaanza utafiti wa awali wa kuweza kuboresha Ofisi ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali na Kiwanda chetu cha Uchapaji cha Serikali. Tayari taarifa ya awali tumeshaipokea na mwishoni mwa mwezi Aprili tutapokea taarifa kamili ya jinsi tunavyoweza kufanya kazi hiyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshafanya mazungumzo na Benki ya Rasilimali *(TIB)* kuona ni namna gani wanaweza

kutusaidia fedha sasa za kuweza kujenga kiwanda kipya kizuri, kikubwa hapa Dodoma ili kuweza kusaidia shughuli hizo za Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Tayari tumeshapata kiwanja na tumeshakilipia na umiliki wa kiwanja hicho umeshahamia kwenye Serikali tayari kwa kuanza kazi hiyo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala Sheria ya Maafa, tuliagizwa Serikali kupitia Sheria ya Maafa nchini, naomba niwaambie na niliarifu Bunge lako tukufu kwamba tayari Bunge lilishatunga Sheria ya Usimamizi wa Maafa Namba 7 ya mwaka 2015. Aidha, Kanuni za utekelezaji wa sheria hii zimeshakamilishwa na zinangoja tu muda ufike ili ziweze kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na ziweze kutumika inavyotikiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kutoka Kambi ya Upinzani kwamba kumekuwa na ukimya kuhusu matumizi ya fedha zilizokusanywa wakati wa tetemeko la ardhi na pendekezo la kumwagiza *CAG* kufanya ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha hizo. Ofisi ya Waziri Mkuu ilishaunda kikosi kazi maalum ili kufanya ukaguzi kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli aliyoyatoa alipofanya ziara Mkoani Kagera tarehe 2 Januari, 2017. Jambo hili lilishaagizwa na Rais na tulishaanza kulitekeleza, kwa hiyo nadhani tutaendelea na maagizo yale Mheshimiwa Rais aliyokwishakuyatoa na tutaendelea kuyatekeleza. Hata hivyo, zipo kazi nzuri ambazo zimeshafanywa katika kurudisha miundombinu na hasa ya taasisi za Serikali kule Kagera. Mfano mzuri ni ujenzi wa shule ya Ihungo, pia tumeboresha kwa kiasi kikubwa zahanati ya Ishozi na imeboreshwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeboresha sana makazi ya wazee ya Kilima na vilevile tumeshatoa fedha za Kitanzania zisizopungua bilioni mbili kwa ajili ya kuanza ujenzi wa shule ya sekondari ya Nyakato. Kwa hiyo, nimuombe sana na kumshawishi tu Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni aliyetoa hoja hii atembelee shule hizo na maeneo hayo ataona kazi nzuri iliyokwisha kufanyika mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Serikali kudhibiti Wabunge wa Upinzani wawapo Bungeni. Naomba niseme kwamba Serikali haina uwezo wa kufanya udhibiti wowote wa Wabunge wa Upinzani wawapo Bungeni ama hata Wabunge wa Kambi ya Chama Tawala. Majukumu ya Bunge yametajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Uendeshwaji wa shughuli za Bunge unaongozwa na Kanuni za Bunge na pale maamuzi yanapokuwa hayamridhishi Mbunge yeyote, Kanuni za Bunge zinamruhusu Mbunge huyo kuchukua hatua zaidi kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, ninaomba nilithibitishie Bunge lako kuwa Serikali haina mkono wowote wa kumkandamiza Mbunge yeyote.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja Serikali kutimiza ahadi ya milioni 50 nadhani Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameijibu vizuri sana leo hapa ndani asubuhi. Ofisi ya Waziri Mkuu tunaendelea na maandalizi ya pensheni kwa wazee, tumeshakamilisha *documents* zote na taratibu sasa za kuwasilisha maandiko yetu katika vikao vya maamuzi Serikalini yanaendelea ili hatimaye tuweze kutekeleza Ilani ya Uchaguzi Ibara ya 165(e) kuhusu pensheni kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kutuuliza tumefikia wapi kuunganisha mifuko ya pensheni. Tumeshafika hatua nzuri, tathmini imefanyika, andiko la mapendekezo ya kuunganisha mifuko limeshaboreshwa na tunasubiri maamuzi ya Serikali. Tutaendelea kutoa fedha kwenye Mfuko wa UKIMWI lakini vilevile tutaendelea kutoa fedha za kutosha ili Mamlaka ya Kupambana Dawa za Kulevya nchini iweze kufanya kazi zake vizuri. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge mapambano dhidi ya UKIMWI na dawa za kulevya ni ya kwetu wote pamoja na ninaomba tushirikiane kwa pamoja kama Watanzania ili kupiga vita dawa za kulevya na UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tulipewa ushauri kuhusu kuboresha mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa ahadi za Serikali za viongozi na Ilani ya Uchaguzi. Tumepokea ushauri huo na mfumo huu siku moja tutakuja kuwaonesha

Waheshimiwa Wabunge ni mfumo mzuri ambao nadhani watatuunga mkono na watatusaidia ili kazi hii ifanyike sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na hoja ya kuhakikisha kwamba Serikali inashughulikia tatizo la fao la kujitoa. Naomba tu niwambie Waheshimiwa Wabunge katika mafao ambayo yanaorodheshwa kama ni mafao yatolewayo kwenye sekta ya hifadhi ya jamii fao la kujitoa halipo. Ibara ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatueleza na inatupa mwongozo wa jinsi ya kuwakinga Watanzania na hasa siku za uzee na majanga yoyote yanayoweza kuwapata. Hata hivyo, kulingana na mabadiliko ya uchumi na Sera ya Hifadhi ya Jamii ibara ya 3(8) inatupa mwongozo wa kushughulikia namna nzuri ya kuona ni namna gani tunaweza kuwakinga Watanzania wanaokosa kazi ili waweze kumudu maisha yao.

Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tumeanza mazungumzo na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini na hivyo basi tunataka tumalize mzizi wa fitna wa fao la kujitoa ili wafanyakazi waweze kufanya kazi zao wakiwa na amani na suala la fao la kujitoa isijekuwa ni ajenda tena ya kuwasumbua katika shughuli na mifumo yao mbalimbali ya ajira*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema kwamba kwa sababu muda wangu umepita, ninaiunga mkono sana hoja hii na ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuiunge mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu mafanikio haya yote ambayo yamekuwa yakionekana dhahiri ni mafanikio ambayo yamekuwa yakiratibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu na ndugu yetu Kassim Majaliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba niwahakikishie Wabunge tutaendelea kuheshimu michango na ushauri wao na Serikali tupo tayari kufanya kazi kwa weledi mkubwa na uaminifu mkubwa kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele kwa maendeleo, Hapa Kazi Tu, hatutalala

na hivyo basi tunaamini baada ya miaka mitano tutakuwa tumepiga hatua ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kengele karibu inagonga, naomba niunge mkono hoja hii, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Jenista Mhagama. Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba nimuite mtoa hoja ili aweze kuhitimisha hoja yake ikiwa ni pamoja na kujibu masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa mjadala, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye rehema ambaye leo ameweza kutupa afya na kupata nafasi ya kuja kuhitimisha majadiliano ya bajeti yetu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, naomba niwakumbushe Watanzania kwamba leo ni siku ya kumbukumbu ya hayati Edward Moringe Sokoine aliyekuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Kwanza alizaliwa tarehe 1 Agosti, 1938 na kufariki tarehe 12 April, 1984 takribani miaka 23. Naamini Watanzania wote tutaendelea kuungana pamoja kumuombea Kiongozi wetu aliyetutangulia mbele za haki ili Mungu aweze kuiweka roho yake mahali pema, amina.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba ya Sheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge UKIMWI na Kamati ya Kudumu ya Bajeti kwa michango yao mizuri kwenye hoja ambayo niliwasilisha mbele yako.

Mheshimiwa Spika, kipekee nakushukuru sana wewe mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kusimamia kwa umahiri mkubwa majadiliano ya hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa

pamoja. Pia ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa pongezi zenu kwa Serikali na kwa michango yenye dhamira yenye kuboresha mipango na kazi zilizokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, mjadala huu umedhihirisha namna ambavyo Bunge linaendelea kuimarika na kutekeleza wajibu wake wa kikatiba kuishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu. Nawashukuru tena Makatibu Wakuu wangu, Wakurugenzi, Makamishna, watumishi na watendaji wote ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa waliyoifanya kipindi chote cha bajeti hii katika kuratibu mambo yote muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mjadala huu leo ulichangiwa na Waheshimiwa Wabunge 148, ambapo Waheshimiwa Wabunge 99 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 49 wamechangia kwa njia ya maandishi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja yangu, hata hivyo kutokana na muda naomba mridhie nisiwataje kwa majina lakini majina ninayo na ninaomba yote yaingie kwenye *Hansard* ili iweze kuwa kumbukumbu muhimu siku za baadae.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, leo hii niko mbele yenu hapa sasa kuja kuomba ridhaa yenu mtupitishie bajeti yetu tufanye kazi za pamoja kwenye maeneo yenu ya kuboresha maendeleo na kusimamia maendeleo na watendaji wetu walioko kule ili tuweze kupata matarajio ambayo tumeyakusudia. Serikali imejibu hoja hizo kupitia Mawaziri pia Mwanasheria Mkuu namshukuru sana, Naibu Mawaziri na hoja zilizosalia zitajibiwa kwa maandishi.

Aidha, kama ambavyo mnajua kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo ofisi ambayo inafanya shughuli zote za Serikali kwa hiyo, mambo mengi ambayo mmekuwa mkichangia Waheshimiwa Wabunge yalikuwa yanagusa sana kwenye Wizara za kisekta na kwa hiyo, zipo hoja

ambazo sitazijibu hapa lakini zitakuja kuzungumzwa kwa kina na Wizara husika ili muweze pia kupata mwelekeo wa utekelezaji wa jambo ambalo mmeshauri.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema tu kwamba utendaji wa jumla wa Serikali ni mzuri, kabla ya kuanza hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba uniruhusu nibainishe baadhi ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nianze kwa kumpongeza sana yeye Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa namna wanavyoendelea kuiongoza nchi yetu kwa uzalendo uliotukuka na kwa dhamira njema isiyotiliwa shaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina hakika Watanzania wote ni mashuhuda wa kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais pamoja na timu yake katika kuongoza nchi yetu kwa weledi mkubwa na kwa mipango iliyo imara ili kuboresha maisha ya Watanzania. Katika kipindi cha mwaka mmoja ambacho nimeingia madarakani tumeushuhudia uongozi wake kuanza kwa miradi mikubwa na yenye tija kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kueleza moja kati ya hiyo kati ya mambo ambayo yalikuwa yamechangiwa ni elimu bure isiyokuwa na malipo. Chini ya Serikali ya Awamu ya Tano ambapo watoto wote wa Tanzania wanapata elimu ya msingi na sekondari bila malipo, kila mwezi Serikali inapeleka shilingi bilioni 18.77 kwenye shule zote za Serikali nchini. Aidha, chini ya Serikali hii kiasi cha shilingi bilioni 3.3 zinatolewa kila mwezi kwa walimu wakuu, wakuu wa shule kama motisha ya Viongozi hao na kufanya jumla ya shilingi bilioni 22.7 kila mwezi ambazo tunazipeleka ikiwa ni utekelezaji wa eneo hili. Tunajua zipo changamoto ambazo zimejitokeza pamoja na idadi kubwa ya vijana walioandikishwa na kusababisha upungufu wa madawati.

Nataka nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Wabunge wenzangu, mlijitokeza sana baada ya Serikali kutoa wito wa

kuchangia madawati kwenye shule zetu, mmetumia fedha zenu, mmetumia muda wenu, mmeshauri Halmashauri zenu kuweza kuchangia na leo hii tunaweza kusema tatizo la madawati limepungua sana kwenye shule zetu za sekondari na msingi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, tuende pamoja kwa ajili ya maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia sekta ya afya imeboreshwa sana sasa hivi baada ya mwaka mmoja huu. Bajeti yetu pia ime-*reflect* hilo, kwamba bajeti ya mwaka 2015/2016 zilitengwa shilingi bilioni 31 lakini leo hii tuna shilingi bilioni 251 ambazo zinapelekwa kwenye Halmashauri zetu na kufikia leo hii kila Halmashauri imeshapokea zaidi ya asilimia 75 ya fedha hii ya bajeti kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwenye maeneo yetu, lakini tumeona pia ujenzi wa maduka ya madawa, mpaka sasa tumejenga maduka nane tunajenga maduka mengine katika kila mkoa ili kuweza kutoa huduma kwa karibu. Tumenunua magari ya *ambulance* 67 ambayo tunayapeleka kwenye vituo vya afya na tumeanza na Kanda ya Ziwa ili kuanza kutoa huduma na kadri tunavyokuwa tunanunua tutajihakikishia kwamba tunapeleka kila Halmashauri kwenye vituo vya afya ili huduma iendelee.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kutoa huduma za mama na mtoto, tunajenga katika kila Halmashauri, tunaanza na Halmashauri 140 kwa kujenga wodi ya watoto, maabara ya damu, nyumba moja ya mganga na chumba cha upasuaji. Hiyo ndiyo kazi ambayo inaendelea kwa sasa kwenye maeneo yetu. Pia jana Mheshimiwa Rais kama ambavyo mmepata kwenye vyombo vya habari ameshagawa vifaa vifuatavyo katika kila Halmashauri nchini. Ametoa vitanda 25 kwenye kila Halmashauri, vitanda vitano kati ya hivyo ni vile ambavyo vinatumika katika kujifungulia, magodoro 25, mashuka 50 na vifaa tiba seti tano kila Halmashauri, huu ni mkakati wa kuboresha sekta ya afya. Tutaendelea vizuri, nataka tuwahakikishie sekta ya afya pamoja na changamoto zake tutafikia hatua nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya uzalishaji, ujenzi wa reli ya kati, Serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha reli ya

kati kwa lengo la kurahisisha usafiri wa usafirishaji wa mizigo na abiria ndani ya nchi na sasa kupitia fedha tuliyotenga, trilioni moja, tumeanza utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, leo hii, tarehe 12 Aprili Mheshimiwa Rais ameweka jiwe la msingi saa tatu zilizopita tayari kwa ujenzi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge.* Hii ni sehemu ya mkakati wa kuchochea maendeleo kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwenye ujenzi wa viwanda; leo hii tumeshasajili viwanda 2,169 nchini, viwanda hivi katika sekta mbalimbali na tunaamini kupitia michango yenu kwamba tuimarishe kilimo ili viwanda vifanye kazi ni wazo ambalo tumelichukua, tutalifanyia kazi ili viwanda vyetu viweze kufanya kazi. Bado tumefungua milango viwanda vije na tunaendelea kufanya hivyo. Mkoa wa Pwani kwa sasa unaongoza kuwa na viwanda vingi sana, tuna viwanda vikubwa 83 na vidogo zaidi ya 200. Tunatoa wito Halmashauri na mikoa zitenge maeneo kwa ajili ya viwanda, mikakati ambayo mmetushauri Waheshimiwa Wabunge tutaizingatia ili viwanda vyetu hivi tuweze kuvifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, tumeboresha sana sekta ya usafiri wa anga kama ambavyo tulieleza kwenye taarifa yangu ya awali nilipokuwa nawasilisha taarifa yangu kwamba tumenunua ndege mbili na nne zinakuja, lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunaboresha usafiri wa njia ya ndege, pia tunakamilisha *Terminal III* uwanja wa ndege ikiwa ni mpango wa uimarishaji wa viwanja vya ndege. Tunaendelea kukamilisha Uwanja wa Mwanza, ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro *(KIA),* Uwanja wa Songwe - Mbeya, vilevile Serikali inaendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege pale Geita, Tabora, Kigoma, Sumbawanga, tutajenga pia Lindi na Shinyanga.

Serikali imeanza maandalizi kwa ajili ya ukarabati wa ujenzi wa viwanja vya ndege vya Musoma, Mtwara, Lindi na Songea. Kazi hii itaendelea kwenye viwanja ili ndege zile tulizonunua ziweze kusafiri kwenye maeneo yote ambayo

tumeyataja ndani ya nchi lakini lengo letu hasa ni kuimarisha utalii wa wageni wa kutoka nje na watalii wa ndani ambao ni sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tumeimarisha pia barabara na Serikali inaendelea na kukarabati na kuboresha barabara ili kuunganisha nchi nzima. Kwa sasa tunakamilisha barabara za ngazi ya mikoa na maeneo yote sasa tunajenga barabara za ngazi ya mikoa na ninyi wote ni mashahidi, kule upande wa Magharibi, Kigoma, Kasulu mpaka Nyakanazi kazi zinaendelea, lakini pia Tabora – Kaliua kwenda kutokea Malagarasi – Uvinza kazi inaendelea, Rukwa kupitia Mpanda kwenda kutokea Uvinza kazi inaendelea, lakini pia hapa katikati Iringa – Dodoma mpaka Babati tumebakiza kilometa 20, 30 kazi inakamilika na huko Kusini tumejenga barabara kutoka Tunduru – Songea na tunakwenda mpaka Mbinga tunashuka mpaka Mbamba bay ili kudhihirisha kwamba kazi hizi zinafanywa maeneo yote nchini, naomba mtuunge mkono ili tuendelee na tufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamejadili sana kuhusu suala la madeni ya wakandarasi, wazabuni, watumishi na watoa huduma. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, hawa wakandarasi na watoa huduma wote ndugu zetu, makampuni ya nje, tunaendelea kulipa na wakandarasi wengine ambao wametoa huduma tunaendelea kuhakiki madeni yao, tunataka tuhakikishe kwamba tunalipa huduma zote. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge muendelee kutuunga mkono ili tuhakikishe kwamba jambo hili hatupati tena lawama kutoka kwa wenzetu ambao wanatoa huduma Serikalini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine Bunge lako tumetoa fedha, najua Waheshimiwa Wabunge walikuwa na mashaka juu ya huduma za Bunge. Bunge hili tumeliongezea fedha, shilingi bilioni 21 ili liweze kufikia tarehe 30 Juni, kwa hiyo, Bunge hili halina mashaka litafika. Lakini maombi ya bajeti mpya tumepandisha mpaka bilioni 121 ambazo pia zitafanya Bunge lijalo liweze kuendelea kwa mwaka ujao wa fedha.

Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwamba Serikali yetu ni sikivu, tumewasikia vilio vyenu, ushauri wenu na sasa tunatekeleza. Tunaomba ridhaa yenu leo ili fedha hii tuweze kuitoa na Bunge letu liweze kufanya kazi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kujibu hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuzitoa na nianze na ya kiongozi mwenzangu, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge lakini pia Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Najua swali lake la kwanza limejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nataka niongeze pale aliposhauri kwamba sasa Serikali itoe maelekezo kwa Halmashauri ili kuongeza ajira angalau 20,000 kila mwaka katika miradi mbalimbali ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, nataka kukuambia kwamba tayari natoa maelekezo na kwa maelekezo haya sasa nataka Halmashauri zote zizingatie mwongozo wa bajeti ya Serikali unaotolewa na Hazina kila mwaka unaozitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara na taasisi zote kubainisha fursa za ajira zinazotarajiwa kupatikana kila mwaka kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vilevie mwongozo huo unazitaka sana taasisi hizo kutoa taarifa za ajira zinazozalishwa kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo ili pia na sisi tuweze kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge wajue kinachoendelea kupitia Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na hoja ya pili ya hali ya upatikanaji wa chakula nchini. Kama ambavyo nilisema kwenye Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2017/2018 ipo ukurasa wa 21. Katika msimu wa kilimo uliopita wa mwaka 2016/2017 hali ya upatikanaji wa mvua haikuwa nzuri kwenye mikoa, hasa ile ambayo inapata mvua wakati wa vuli na hali ya mavuno katika baadhi ya maeneo hayo iliyumba kwa sababu hakukuwa na mvua za vuli, leo hii tunaendelea kupata mvua, tulichokifanya ni kusisitiza wafanyabiashara wetu wa ndani waendelee kusafirisha vyakula kutoka vinapopatikana mpaka eneo ambalo lina upungufu mkubwa na tulibaini zile Wilaya zetu 55, taratibu zinaendelea

na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anasimamia upatikanaji wa chakula kwenye maeneo hayo kupitia wafanyabiashara wetu wa ndani.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa mvua zinazoendelea sasa, maeneo mengi mvua zinanyesha tujitahidi basi kupanda mazao ya muda mfupi ili yaweze kuiva katika kipindi kifupi ili msimu ujao wa mavuno tuweze kufanya tathmini, je, tumepata chakula cha kutosha, tuna upungufu wapi, ile akiba tuliyonayo tutaona namna ambavyo tunaweza tukaisambaza kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge ambaye alitoa hoja hii, Serikali imejipanga kwa utaratibu huo na tutaisimamia kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ilikuwa ni kuwa na mipaka mingi yenye vipenyo vingi pamoja na ukanda mrefu wa bahari ambao umefanya udhibiti wa uingizaji wa dawa za kulevya kuwa mgumu sana. Serikali imeshauriwa kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa kutoa elimu kwa jamii zinazoishi mipakani ili zishirikiane na vyombo vya dola kwenye maeneo hayo ili kudhibiti hali hiyo. Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeshaanza kutoa elimu kwa Kamati za Ulinzi na Usalama katika maeneo ya mipaka ya Tunduma, Kasumulo, Namanga, Horohoro na Mtukura ili kuweza kutoa elimu ya juu ya athari za dawa za kulevya kwa jamii inayoishi mipakani.

Aidha, elimu hii itatolewa kwa wananchi kadri hali inavyoruhusu ili wananchi wote kwa pamoja washiriki katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya badala ya kuviachia vyombo vya dola peke yake. Kwa hiyo, kazi hiyo inaendelea ili tuweze kuimarisha maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya ili kulinda watoa taarifa na pendekezo la kutaifisha mashamba ya bangi. Tatizo la dawa za kulevya ni janga kubwa, tumelizungumza mara nyingi na linaathiri sana ustawi wa nchi yetu. Serikali imedhamiria kwa dhati kabisa kupambana na mtandao wa dawa za kulevya nchini. Mafanikio katika mapambano ya dawa za kulevya

yanahitaji sana ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wananchi, hivyo napenda sana kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba watoa taarifa za wahusika wa dawa za kulevya watalindwa na wanaendelea kulindwa kwa mujibu wa sheria za kulinda watoa taarifa na mashahidi ambao wanatoa ushahidi wa kesi hizi na kwa mujibu wa sheria ile ya mwaka 2015 *(Whistleblowers and Witness Protection Act, 2015)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalipokea pendekezo hili kutaifisha mashamba ya bangi na litaendelea kutafakari utekelezaji wake vilevile. Pale ambapo tutajiridhisha kuwa adhabu hii itatosha inaweza kutoa fundisho kwa wananchi wanaojihusisha na kilimo cha bangi, Serikali haitasita kuleta Bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ili pia tuweze kupata mwongozo mwingine zaidi kutoka kwako.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya tano ya kuongeza kituo cha tiba za *methadone* na *sober houses* za Serikali angalau moja kila mkoa. Uanzishwaji wa vituo vya tiba kwa kutumia *methadone* unategemea ukubwa wa tatizo la matumizi ya dawa za kulevya na uwepo wa miundombinu ya msingi katika mkoa husika. Hadi sasa kuna vituo vya *methadone* katika Hospitali za Muhimbili, Mwananyamala na Temeke Mkoani Dar es Salaam, vilevile Serikali inakusudia kufungua vituo kama hivyo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani na Tanga. Kwa kuwa matibabu ya *methadone* yanasaidia sana watumiaji wa dawa za kulevya aina ya *heroin* tu pekee, Serikali inatarajia kuanzisha nyumba ya upataji nafuu *(sober house)* kila mkoa, huduma hii itakuwa ni kwa ajili ya kuwasaidia warahibu wengine wa aina zote za dawa za kulevya badala ya kuwaachia watu binafsi ambao mpaka sasa wanaendesha nyumba 17 za upataji nafuu nchini.

Hata hivyo, niwasihi sasa wale wote waendelee na kazi hiyo na kama wapo wadau wengine wataendelea kutuandalia nyumba za aina hiyo, tutazipokea na tutazisajili lakini Serikali inaendelea kuandaa mwongozo wenye lengo la kusimamia na kuratibu hizo nyumba zote za watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na hoja nyingine ambayo Serikali ilishauriwa iongeze vituo vya afya, vifaa tiba, wahudumu wa afya wenye weledi wa kupunguza umbali wa kupata huduma za wanaoishi na virusi vya UKIMWI; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Sera ya Maendeleo ya Afya ya Msingi inaelekeza Serikali kuboresha huduma za afya ya msingi kwa kjenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata na Hospitali ya Wilaya kila Wilaya.

Aidha, Serikali ina mkakati wa kuongeza idadi ya wataalam wa afya nchini kote. Jambo hili limezungumzwa na Wabunge wengi wakiuliza maendeleo ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya, zahanati na vituo vya afya. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kadri tunavyopata fedha na kuzitenga katika bajeti tutaendelea pia kuhamasisha wananchi kuanzisha miradi ya ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na Serikali itaendelea kuunga mkono kwa lengo la kila kijiji kuwa na zahanati yake, kila kata iwe na kituo cha afya na Wilaya ziweze kuwa na Hospitali za Wilaya na yale majukumu yote ya Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI yataendelea kuimarishwa ili maeneo yote yawe yanapata huduma ikiwemo na uwepo wa watumishi wa afya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ushauri wenu kwenye eneo hili tumeupokea, nataka niwahakikishie kwamba tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine ambayo inataka Serikali itoe elimu ya kujikinga na VVU kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo elimu kwa njia ya sinema na kuanzisha vilabu vya mapambano dhidi ya VVU katika shule zote kuanzia msingi hadi sekondari na kuandaa mitaala ya elimu ya UKIMWI katika ngazi zote za elimu ya msingi hadi Vyuo Vikuu. Nia ya Serikali katika hili ni kuona elimu ya UKIMWI inawafikia wote wanaostahili nchini. Serikali ina magari ya sinema katika mikoa yote 20 ya Tanzania Bara ambayo pia hutoa elimu ya UKIMWI kwa njia ya sinema. Mkakati tulionao sasa pia na mikoa mitano ya Tanzania Visiwani nayo itapata magari ya sinema ili kuendelea kutoa huduma nchini kote.

Wizara ya Elimu kwa pamoja na Wizara ya Elimu ya Zanzibar imetoa mitaala kufundisha wanafunzi kuhusiana na elimu ya UKIMWI kwenye shule zetu. Serikali inatoa wito pia kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri kuyatumia ipasavyo magari hayo na kuhakikisha kwamba walimu wapya wanapitishwa vema katika mitaala hiyo pamoja na kuanzisha *clubs* za kuhamasisha mapambano dhidi ya UKIMWI katika shule, vyuo vyote nchini na mahali pote ambapo kuna mikusanyiko ya watu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na ushauri unaosema Serikali ibuni chanzo mahsusi cha kutunisha Mfuko wa UKIMWI *(Aids Trust Fund)* kama ilivyo kwa mifuko mingine mfano *REA* na maji ili kufanikisha mapambano dhidi ya UKIMWI. Kupitia Bunge lako napenda kuwahakikishia kwamba ushauri huu uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge umepokelewa na Serikali itaufanyia kazi. Malengo yetu ni kuhakikisha kwamba mfuko huu tukiuanzisha, tukiutunisha huduma zote zinaweza kuwafikia mpaka walioko vijijini, kwa hiyo, jambo hili Waheshimiwa Wabunge tumelipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na hoja pia ya kuweka utaratibu wa kufuatilia fedha zinazotolewa na wafadhili kwenye Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali zinazojihusisha na masuala ya UKIMWI. Utaratibu wa kufuatilia fedha zinazotolewa kwenye *NGO's* upo na tumekuwa tukisisitiza ufuatwe vizuri. Mathalani nilipofanya ziara mkoani Arusha hivi karibuni nilirudia wito wa kuzifanyia kaguzi za mara kwa mara *NGO's* zinazofanya kazi nchini. Hivyo, ushauri wangu wa Kamati kuhusu hitaji la kufanya ukaguzi kwenye *NGOs* zinazoshughulikia UKIMWI utaendelea kuzingatiwa kama ambavyo tumetoa maelekezo. Natoa wito kwa wakurugenzi wote wa Halmashauri zetu za Wilaya nchini waendelee kuhakikisha wadau wa UKIMWI wanaofanya kazi kwenye maeneo yao wanakaguliwa kulingana na Sheria ya UKIMWI ya mwaka 2008 na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002, ili tuweze kujiridhisha wanapata nini kwa ajili ya huduma gani, kiasi gani kinatumika ili wanufaika waweze kuridhika kwenye huduma hii.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilikuwa imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni juu ya Serikali kujiridhisha kuhusu masuala ya kitaalam ya kufanya mapitio na maboresho ya sheria stahiki katika kutekeleza mpango wa kuunganisha mifuko ya pensheni; hili limezungumzwa vizuri sana na Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Lakini zoezi la kuunganisha mifuko ya pensheni linafanyika kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam. Katika kutekeleza jukumu hilo mifuko yote ya pensheni imefanyiwa tathmini ambayo pamoja na mambo mengine imebainisha kuwa kuunganisha mifuko ya pensheni ndiyo njia bora ya kuimarisha sekta ya hifadhi ya jamii nchini.

Aidha, Serikali imeandaa andiko la mapendekezo ya kuuunganisha mifuko, kazi hii imefanyika kwa kushirikisha wadau muhimu katika sekta husika. Serikali itaendelea kutoa taarifa za mara kwa mara juu ya hatua iliyofikiwa kwenye mpango huo wa kuunganisha mifuko.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na ushauri mwingine kwamba mifuko ya hifadhi ya jamii inayojishughulisha kuwekeza kwenye uchumi iweze kuendelea na uwekezaji huo hasa kwenye maeneo ya viwanda. Uwekezaji ni kazi mojawapo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na lengo la uwezeshaji ni kulinda thamani ya michango ya mwanachama pamoja na kukuza uwezo wa mifuko, kupitia na kulipa mafao kwa wanachama wake pamoja na wanapopatwa na majanga mbalimbali yanayowasababishia kukosa kipato. Majanga hayo ni kama vile maradhi, uzee na kifo, kwa msingi huo uwekezaji kwenye viwanda unavyofanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii sasa una manufaa makubwa sana kwani pamoja na kulinda thamani ya fedha za michango ya wanachama, uwekezaji huu unakuza mapato ya Serikali, unatoa fursa za ajira na hivyo kusaidia kuongeza idadi ya wanachama watakaoweza kuongeza michango yao kwenye mfuko husika.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Serikali kwa pamoja vitaendelea kuhakikisha kwamba

uwekezaji unaofanywa na mifuko ya hifadhi ya jamii unazingatia miongozo ya uwekezaji ili mifuko hiyo isiweze kupata hasara kubwa, tunashukuru jambo hili linaendelea na tutakuja kuwapa mrejesho.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na hoja ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura na utoaji wa elimu ya kupiga kura. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inayo jukumu la kuboresha daftari la kudumu la kupiga kura. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Tume ya Taifa ya Uchaguzi itaweka kipaumbele katika uboreshaji wa daftari la wapiga kura na Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura nchini kote na kusimamia na kuratibu asasi, taasisi na watu wanaotoa elimu kwa mpiga kura. Tume pia imeendelea kutoa elimu ya mpiga kura kwa njia mbalimbali ikiwemo kutumia redio, *television,* kukutana na wadau, kupitia maonyesho mbalimbali pamoja na kushiriki mikutano katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ambayo ilizungumzia suala la mgogoro wa uongozi ndani ya Chama cha CUF. Jambo hili limezungumzwa kwa hisia kali na sisi tumelipokea lakini nataka niseme tu kwamba hoja hii kwa namna ambavyo imejadiliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wameweza kuijadili sana. Serikali haifurahishwi na migogoro ndani ya vyama vya siasa kwani inadumaza demokrasia nchini na kusababisha mifarakano isiyokuwa na tija. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kama mlezi wa vyama vya siasa imekuwa ikishiriki sana kikamilifu katika kuhakikisha kwamba migogoro ndani ya vyama vya sisa inatatuliwa kwa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, katika hili mgogoro uliopo ndani ya Chama cha CUF, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilitoa ushauri kulingana na taratibu zilizopo, hata hivyo wakati usuluhishi ukiendelea, baadhi ya wanachama wa CUF ambao hawakuridhika na usuluhishi uliofanywa na Msajili walipeleka shauri Mahakamani ili kudai haki yao kwenye

mhimili ya Mahakama ikiwa ni pamoja na suala la ruzuku ambalo Mahakama imetoa zuio la muda mpaka shauri la msingi lililoko Mahakamani litakapotolewa uamuzi. Kwa kuwa masuala haya yapo Mahakamani na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge mnataka jambo hili lingepata nafasi ya kuzungumzwa basi ni vizuri tukaiacha Mahakama ifanye kazi yake halafu tuje tulizungumze. Hiyo ni rai yangu na namna nzuri ya kuweza kutatua mgogoro *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa jambo ambalo limezungumzwa sana hapa ndani, suala la usalama na kutokuwa na uhakika wetu Waheshimiwa Wabunge. Jambo hili kama ambavyo Mwanasheria amelieleza, Serikali inalifanyia kazi na hapo baadae tutakuja kutoa taarifa ya Serikali kwenu kwa sasa tunawasihi Waheshimiwa Wabunge tuache vyombo vyetu vifanye kazi, vifuatilie ni nini hiki kinaendela, nani anaendelea nacho, malengo ni nini ili tuje tujiridhishe kama je, matendo haya yanayozagaa huko ni matendo ambayo yanakubalika? Kimsingi hayakubaliki, lakini taarifa rasmi tutakuja kuileta Bungeni Waheshimiwa Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ulinipunguzia muda na niliona nitumie muda huu kuzungumza haya machache, nashukuru nimefika mwisho wa maelezo yangu ili nirudi tena kwa Waheshimiwa Wabunge kuomba ridhaa yao ya fedha tuweze kutekeleza na yale ambayo mliyasema ambayo sijayajibu lakini nina uhakika kwa maelekezo ninayoyatoa kwa Wizara ni lazima waje wafafanue vizuri ya hoja zote ambazo mlizitoa Waheshimiwa Wabunge ili tupate mwelekeo. Nataka niwahakikishie kwamba ushauri wenu tumeuchukua ili tuufanyie kazi katika kipindi cha mwaka mmoja wa fedha kinachokuja baada ya ninyi kuridhia maombi yetu ambayo tunayo hapa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, muda usingeweza kutosha kujibu hoja zote zilizotolewa, Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja, tumejifunza mengi sana kutoka kwenu, kwenye kupitia michango yenu na tuko tayari kuendelea kujifunza zaidi kutoka

kwenu Waheshimiwa Wabunge na ni jukumu letu kuwasikiliza na kupokea ushauri wenu.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni yetu sote na kila mmoja wetu anaowajibu wa kulisukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu, kila mchango wa Mheshimiwa Mbunge una thamani kubwa sana kwetu na ninawashukuru sana kwa ushauri, maangalizo na mafunzo mliyotupa. Nataka niwahakikishie ushauri huu wakati mwingine tunautekeleza tunapokuja kwenye Majimbo yenu, nitaendelea na ziara zangu kwenye maeneo yenu ili kutekeleza na haya ambayo mmetushauri. Bado tuko pamoja, nataka niwahakikishie ushirikiano ambao tutawapa wakati wote katika kipindi cha mwaka wa fedha ujao. Endeleeni kutoa ushauri kwa Serikali hata kwa maandishi tu wakati wowote siyo lazima Bungeni, popote ili tuweze kufikia hatua nzuri ya maendeleo, na sisi tutapokea ushauri huo na kuona namna bora ya kuufanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila Mtanzania mkiwemo Waheshimiwa Wabunge mnawajibika kuiacha Tanzania ikiwa ni nchi bora zaidi ya tulivyoikuta. Ili kuifikisha azma hiyo inabidi tuanze kuwa tayari kujinyima mambo mazuri tuliyoyazoea angalau kwa muda ili kuimarisha misingi ya ujenzi wa Tanzania yetu. Ninawasihi sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu muielewe dhamira ya Serikali na mtuamini katika kusimamia rasilimali ya nchi yetu kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo. Serikali imejipanga vizuri katika kulinda maslahi ya nchi hii na wananchi wake. Hivyo nawaomba muendelee kutuunga mkono kwa kupitisha bajeti yetu ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo leo hii iko mbele yenu na tunaomba ridhaa yenu ili tufanye kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha hoja yangu tena katika siku ambayo Taifa letu kama ambavyo nimeeleza ninalazimika kuwakumbusha Watanzania wote tuendelee kumuenzi mpambanaji huyo wa haki za wanyonge kwa kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano za kupambana na rushwa na ubadhirifu wa mali za umma. Tumuombe tena Mwenyezi Mungu aendelee kumpumzisha

Hayati Edward Moringe Sokoine aliyekuwa Waziri Mkuu Awamu ya Tatu. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, amin.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, niko chini yenu kuomba ridhaa yenu kwenye mpango ambao tutauleta.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelezo hayo mazuri ya kuhitimisha hoja yako ikiwa ni pamoja na kujibu masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati Waheshimiwa Wabunge wakiwa katika mjadala wa bajeti ya ofisi yako.

**MAELEZO YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU AKITOA UFAFANUZI NA MAJIBU YA HOJA ZA WAHESHIMIWA WABUNGE NA KUHITIMISHA HOJA YA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU NA TAASISI ZAKE NA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**

- Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutupa Afya njema hadi leo ninapohitimisha Majadiliano ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2017/2018.

- Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha hoja yangu, katika siku ambayo Taifa letu liliondokewa na aliyekuwa Waziri Mkuu,

Hayati Edward Moringe Sokoine, aliyezaliwa tarehe 1 Agosti 1938 na kufariki kwa ajli ya gari siku kama ya leo mwaka 1984. Ninalazimika kuwakumbusha Watanzania wote kumuenzi mpambanaji huyo wa haki za wanyonge kwa kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano za kupambana na rushwa na ubadhilifu wa mali za umma. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpumzisha kwa amani Edward Moringe Sokoine. Amen.

- Natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa michango yao mizuri kwenye Hoja yangu.

- Kipekee ninakushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kusimamia kwa umahiri mkubwa majadiliano ya Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge.

- Ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi zenu kwa Serikali na kwa michango yenye dhamira njema ya kuboresha mipango na kazi zilizokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Mjadala huu umedhihirisha namna ambavyo Bunge linaendelea kuimarika na kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba kuishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu.

- Ninawashukuru Makatibu Wakuu wote, Makamishna na watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara nyingine walioshiriki kuandaa taarifa hii.

## 2.0. WACHANGIAJI

**Mheshimiwa Spika,**

- Mjadala huu, ulichangiwa na Waheshimiwa Wabunge **148,** ambapo Waheshimiwa Wabunge **99** walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge **49** wamechangia kwa njia ya maandishi.

- Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Hoja yangu. Hata hivyo, kutokana na muda naomba uridhie nisiwataje na majina yao yaingizwe katika *Hansard*.

## WABUNGE WALIOCHANGIA KWA KUONGEA NDANI YA BUNGE

Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi, Mheshimiwa Edward F. Mwalongo, Mheshimiwa Godbless J. Lema, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Amina S. Molel, Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus B. Kamala, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mheshimiwa Stephen J. Masele, Mheshimiwa Kunti Y. Majala, Mheshimiwa Godfrey W. Mgimwa, Mheshimiwa Janet Z. Mbene, Mheshimiwa Sebastian S. Kapufi, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Hussein M. Bashe, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Zuberi M. Kuchauka, Mheshimiwa Joseph G. Kakunda, Mheshimiwa Abdallah A. Mtolea, Mheshimiwa Riziki S. Ngwali, Mheshimiwa Raphael J. Michael, Mheshimiwa Cecilia D. Paresso, Mheshimiwa Deo K. Sanga, Mheshimiwa Ikupa S. Alex, Mheshimiwa Magreth S. Sitta, Mheshimiwa Jumaa H. Aweso, Mheshimiwa Anna K. Malecela, Mheshimiwa Emmanuel P. John na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah.

Pia Mheshimiwa Hassan E. Masala, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Mary P. Chatanda, Mheshimiwa Neema W. Mgaya, Mheshimiwa Shaban O. Shekilindi, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Richard P. Mbogo, Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mheshimiwa Lucy S. Magereli, Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa John P. Kadutu, Mheshimiwa Daimu I. Mpakate, Mheshimiwa Mashimba M. Ndaki, Mheshimiwa Anatropia L. Theonest na Mheshimiwa Mwl. Kasuku S. Bilago.

Wengine ni Mheshimiwa Musa R. Ntimizi, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Munde A. Tambwe, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Abdallah D. Chikota, Mheshimiwa Juma S. Nkamia, Mheshimiwa Mheshimiwa Ridhiwani J. Kikwete, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Zitto Z. Kabwe, Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Kiteto Z. Koshuma, Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, Mheshimiwa Khalfan H. Aeshi, Mheshimiwa Cosato D. Chumi, Mheshimiwa Benardetha K. Mushashu, Mheshimiwa Constantine J. Kanyasu, Mheshimiwa Zubeda H. Sakuru, Mheshimiwa Joyce J. Mukya na Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba.

Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mheshimiwa Joram I. Hongoli, Mheshimiwa Dalaly P. Kafumu, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Ally S. Ungando, Mheshimiwa Yussuf Kaiza Makame, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali na Mheshimiwa Paschal Y. Haonga.

Wengine ni Mheshimiwa Joyce B. Sokombi, Mheshimiwa Dkt. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Ally K. Mohamed, Mheshimiwa Innocent L. Bashungwa, Mheshimiwa Roman J. Selasini, Mheshimiwa Amina N. Mikilagi, Mheshimiwa Njalu D. Silanga, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Joseph K. Mhagama, Mheshimiwa Rashidi A. Shangazi, Mheshimiwa Maftaha A. Nachuma Mheshimiwa Livingstone J. Lusinde, Mheshimiwa Philip I. Mpango, Mheshimiwa Mwigulu L. Nchemba, Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa George M. Masaju, Mheshimiwa Antony P. Mavunde na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama

**ORODHA YA WABUNGE WALIOCHANGIA KWA MAANDISHI**

Mheshimiwa Rhoda E. Kunchela, Mheshimiwa Omar A. Kigoda, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Zuberi M. Kuchauka, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mheshimiwa Prof. Norman A. S. King, Mheshimiwa Mbaraka K. Dau, Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mheshimiwa Janet

Z. Mbene, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Cecilia D. Paresso na Mheshimiwa Japhet N. Hasunga.

Wengine ni Mheshimiwa Mary P. Chatanda, Mheshimiwa Mussa R. Sima, Mheshimiwa Allan J. Kiula, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa Omari M. Kigua, Mheshimiwa Massay F. Gregory, Mheshimiwa Gimbi D. Masaba, Mheshimiwa Twahir Awesu Mohamed, Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mheshimiwa Dkt. Hadji H. Mponda, Mheshimiwa Jacqueline K. N. Msongozi, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke na Mheshimiwa Ritta E. Kabati.

Mheshimiwa Zainab M. Vullu, Mheshimiwa Qambalo W. Qulwi, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Hamid H. Bobali, Mheshimiwa Lolesia J. Bukwimba, Mheshimiwa Susan L. Kiwanga, Mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mheshimiwa Elias J. Kwandikwa, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mheshimiwa Hamoud A. Jumaa, Mheshimiwa Ally S. Ungando, Mheshimiwa Omary T. Mgumbo, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Miza Bakari Haji, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mheshimiwa Devota M. Minja Mheshimiwa Zubeda H. Sakuru na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana W. Kikwembe.

- Niko mbele yenu kuomba ridhaa yenu ili tupitishe bajeti hii tuweze kufanya kazi katika maeneo mbalimbali nchini.

- Serikali imejibu hoja hizo kupitia Mawaziri na Naibu Mawaziri. Hoja zilizosalia zitajibiwa kwa maandishi. Aidha, baadhi ya hoja zitajibiwa na Mawaziri wa sekta husika watakapowasilisha bajeti zao.

## 3.0. UTENDAJI WA SERIKALI KWA UJUMLA

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuanza kujibu Hoja za

Waheshimiwa Wabunge, naomba uniruhusu nibainishe baadhi ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa namna wanavyoendelea kuiongoza nchi yetu kwa uzalendo uliotukuka na dhamira njema isiyotiliwa shaka.

**Mheshimiwa Spika**, nina hakika Watanzania wote ni mashuhuda wa kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli katika kuiongoza Nchi yetu kwa weledi mkubwa na kwa mipango iliyo imara ili kuboresha maisha ya Watanzania. Katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wake tumeshuhudia kuanza kwa miradi mikubwa na yenye tija kwa nchi yetu.

## A: HUDUMA ZA KIJAMII

***Elimu bila malipo***

**Mheshimiwa Spika,** chini ya Serikali ya Awamu ya Tano ambapo watoto wote wa Tanzania wanapata elimu ya Msingi na Sekondari bila malipo. Kila mwezi Serikali inapeleka shilingi bilioni **18.77** kwenye shule zote za Serikali nchini Tanzania. Aidha, ni chini ya Serikali hii, kiasi cha shilingi bilioni **3.3** zinatolewa kila mwezi kwa Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule kama motisha kwa viongozi hao na kufanya kila mwezi kutuma shilingi bilioni **22.7**. Tunajua zipo changamoto zilizojitokeza, hasa uandikishaji mkubwa uliosababisha uhaba wa madawati. Kipekee, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kujitolea kusimamia suala hili kwa dhati.

**Mheshimiwa Spika,** huu ni utekelezaji wa Ilani ya CCM wenye lengo la kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata urithi ulio bora, ambao ni elimu.

***Maboresho kwenye Sekta ya Afya***

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Tano inatoa kipaumbele kikubwa kwenye sekta ya afya. Tunatambua

kwamba jamii yenye afya njema ndiyo inayoweza kuzalisha kwa tija. Kutokana na ukweli huo, Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya kwa kuongeza bajeti ya kununua vifaa tiba na dawa kutoka **shilingi bilioni 31** mwaka 2015/2016 hadi **shilingi bilioni 251** mwaka 2016/2017. Hadi leo, tumenunua *ambulance* 67, tumeanza kuzigawa kwenye Kanda ya Ziwa. Pia tumeagiza kila Halmashauri hapa nchini, zitenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba moja ya mganga, nyumba ya muuguzi na maabara ya damu.

Aidha, Serikali imebuni utaratibu wa kununua dawa na vifaa tiba moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji badala ya kununua kutoka kwa wasambazaji. Pia, Serikali imeanzisha utaratibu wa kujenga maduka ya madawa ya MSD kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa bei nafuu kwa wananchi. Tayari maduka manane (8) yamejengwa na mengine yanaendelea kujengwa kote nchini.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kuboresha huduma za afya nchini, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya uamuzi wa kusambaza magodoro 25, mashuka 50 na vitanda 25 vya hospitali katika Halmashauri zote 184 nchini. Kati ya vitanda hivyo, 5 ni kwa ajili ya wajawazito. Pia Serikali imetoa seti tano za vifaa tiba katika kila Halmashauri. Serikali itaendelea kuboresha huduma za afya nchini, ikiwemo kusambaza watumishi katika sekta ya afya.

## B: SEKTA ZA UZALISHAJI

### *Ujenzi wa Reli ya Kati*

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha reli ya kati kwa lengo la kurahisisha usafiri na usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilitenga **shilingi trilioni moja** kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa reli hiyo. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, leo hii tarehe 12 Aprili, 2017 Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameweka jiwe la msingi kwa ajili ya

ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*. Ujenzi wa reli ya kati ambayo ni mradi wa kipaumbele katika Dira ya Taifa ya Maendeleo, kuchochea ukuaji wa uchumi na ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini.

***Ujenzi wa Viwanda***

**Mheshimiwa Spika,** Serikali pia inaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda na kuvutia uwekezaji nchini. Ndani ya mwaka mmoja jumla ya **viwanda 2,169** vimesajiliwa, ikiwa ni pamoja na viwanda vya mbolea, saruji, chuma na usindikaji wa mazao. Uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda nchini ni dhahiri na tayari tumeanza kuona matokeo. Kwa mfano, Mkoa wa Pwani pekee una viwanda **vikubwa 83** na vingine vidogo vidogo **zaidi ya 200**. Huu ndio mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano.

***Maboresho kwenye Sekta ya Usafiri wa Anga***

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea na jitihada za kulifufua Shirika la Ndege la Tanzania kwa kununua ndege mpya sita, ambazo zinawasili kwa awamu mbalimbali. Serikali imekamilisha upanuzi wa uwanja wa ndege wa Dodoma pamoja na kuendelea kujenga jengo la tatu la abiria (Terminal III) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza na ukarabati wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro na Uwanja wa Songwe – Mbeya. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mkoa wa Geita na kukamilisha maandalizi kwa ajili ya upanuzi na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Tabora, Kigoma, Sumbawanga, Lindi na Shinyanga. Serikali imeanza maandalizi kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Musoma, Mtwara, Iringa na Songea.

Jitihada hizi ni kudhihirisha dhamira ya dhati ya kuboresha usafiri wa anga ili kurahisisha usafiri kwa wananchi pamoja na kuchochea utalii nchini.

***Miradi ya Barabara***

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kukarabati na kuboresha barabara zinazounganisha mikoa nchini. Aidha,

Serikali inaendelea kuimarisha barabara kote nchini ikiwa ni pamoja na kujenga barabara zitakazofungua fursa za kiuchumi katika maeneo mbalimbali. Baadhi ya barabara hizo ambazo ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi ni **Barabara ya Itoni – Mkiu – Ludewa – Manda (km 211); Barabara ya Tabora – Sikonge - Ipole- Koga – Mpanda (km 259); Barabara ya Mbeya – Makongorosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (km 528); Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7); Barabara ya Dodoma – Babati (km 261);** Barabara ya **Iringa – Dodoma (km 260); Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 866.7); Barabara ya Makutano – Nata – Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu (km 338); na Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza- Kaliua – Tabora (km 491);**

***Madeni ya makandarasi, wazabuni, watumishi na watoa huduma:***

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wamejadili kuhusu madeni ya makandarasi, wazabuni, watumishi na watoa huduma wanaoidai Serikali kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali inatambua umuhimu wa kuwalipa wakandarasi na wadeni wote wa Serikali. Hata hivyo, kabla ya kufanya malipo hayo, Serikali inabidi kujiridhisha kuhusu uhalali wa madeni hayo, na mara moja tunapokuwa tumejiridhisha kuhusu uhalali wa madeni hayo tumekuwa tukilipa bila kusita. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2016 jumla ya **shilingi bilioni 2,934.2** zilikuwa zimehakikiwa, ambapo **shilingi bilioni 555.2** zililipwa. Ninawaomba makandarasi, wazabuni, watumishi na watoa huduma wote wanaoidai Serikali, watuwie radhi na watuvumilie wakati tunapojiridhisha kuhusu madeni yao. Serikali isingependa mdeni wake apunjwe lakini pia ingependa Serikali ilipe madeni halali.

Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imeongeza shilingi bilioni 21 kwa shughuli za Bunge ili liweze kufika tarehe 30 Juni, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** niliona ni vyema nianze mjadala huu kwa kubainisha masuala muhimu yaliyofanywa na Serikali ili kuweka kumbukumbu vizuri kutokana na baadhi yetu kuchangia kana kwamba hakuna jambo lolote lililofanywa na Serikali tangu iingie madarakani.

## 4.0. MAJIBU YA HOJA

**Mheshimiwa Spika,**

- Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99 (13) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba nitumie nafasi hii kujibu na kufafanua baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:

**1. HOJA:** Serikali itoe maagizo kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri kutengeneza ajira angalau 20,000 kila mwaka katika miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Halmashauri zao, na taarifa ya utekelezaji wa agizo hilo iwe inatolewa kila mwaka kwenye Bunge la Bajeti.

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni); Mheshimiwa Juma Hamidu Aweso (Pangani)**

**JIBU:**

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda, kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 **Ibara ya 59** inazielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa zote nchini kuzingatia viashiria vya ukuzaji ajira katika mipango ya maendeleo ya ngazi husika pamoja na kutoa taarifa za mwenendo wa ajira kila robo mwaka.

Aidha, maelekezo haya, yanazingatiwa katika Mwongozo wa kuandaa Bajeti ya Serikali unaotelewa na HAZINA kila mwaka unaozitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara na Taasisi zote kubainisha fursa za ajira zinazotarajiwa kupatikana kila mwaka kutokana na utekelezaji wa miradi

ya maendeleo. Vilevile Mwongozo huo unazitaka Taasisi hizo kutoa taarifa za ajira zinazozalishwa kutokana na utekelezaji wa Miradi hiyo kila robo mwaka. Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wizara na Taasisi zote ziendelee kuzingatia maelekezo haya.

**2. HOJA:** Kuhusu hali ya upatikanaji wa chakula nchini.

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Kunti Yusuph Kajala (Viti Maalum); Mheshimiwa Zuberi Zitto Kabwe (Kigoma Mjini); Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete (Chalinze)**

**JIBU**

**Mheshimiwa Spika**, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu ya Bajeti ya 2017/18 ukurasa wa 21, katika msimu wa kilimo 2016/17 hali ya upatikanaji wa mvua katika Mikoa inayopata mvua za vuli haikuwa ya kuridhisha na hivyo kusababisha ukame na upungufu wa mavuno katika baadhi ya maeneo. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali inahamasisha sekta binafsi kununua mazao ya chakula kutoka maeneo yenye ziada na kuyauza katika maeneo yenye uhaba hasa kwenye wilaya 55 tulizozibaini.

Aidha, wafanyabiashara waliohifadhi nafaka katika maghala, wazisambaze katika masoko ya ndani. Katika kuunga mkono juhudi hizo, Serikali imesambaza tani 1,969 za mbegu bora za mazao yanayostahimili ukame kwenye Halmashauri mbalimbali. Natoa wito kwa wakulima kuendelea kutumia vizuri mvua zinazonyesha katika msimu huu wa masika kwa kupanda mazao yanayokomaa kwa muda mfupi na kutumia mbegu bora za mazao ya kilimo zinazostahimili ukame.

**3. HOJA:** Kutokana nchi yetu kuwa na mipaka mingi yenye vipenyo vingi pamoja na ukanda mrefu wa bahari ambavyo hufanya udhibiti wa uingizaji wa dawa za kulevya kuwa mgumu, Serikali imeshauriwa kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa kutoa elimu kwa jamii zinazoishi mipakani ili zishirikiane na vyombo vya dola hatua ambayo itasaidia udhibiti wa uingizwaji wa dawa hizo hatari nchini.

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda (Kamati ya Kudumu ya Bunge, Masuala ya UKIMWI)**
**JIBU**

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeshaanza kutoa elimu kwa Kamati za Ulinzi na Usalama katika maeneo ya mipaka ya Tunduma, Kasumulo, Namanga, Horohoro na Mtukula ili kuweza kutoa elimu juu ya athari za dawa za kulevya kwa jamii inayoishi mipakani. Aidha, elimu hii itatolewa kwa wananchi kadri hali itakavyo ruhusu ili wananchi wote kwa pamoja washiriki katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya badala ya kuviachia vyombo vya dola pekee.

**4. HOJA:** Mapambano dhidi ya dawa za kulevya, kulinda watoa taarifa na pendekezo la kutaifisha mashamba ya bangi.

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda (Kamati ya Kudumu ya Bunge, Masuala ya UKIMWI); Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq (Viti Maalum)**

**JIBU**
**Mheshimiwa Spika,** tatizo la dawa za kulevya ni janga kubwa la kitaifa linaloathiri ustawi wa Nchi yetu. Serikali imedhamiria kwa dhati kupambana na mtandao wa dawa za kulevya nchini. Mafanikio katika mapambano ya dawa za kulevya yanahitaji ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wananchi. Hivyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, watoa taarifa za wahusika wa dawa za kulevya wanaendelea kulindwa na watalindwa kwa mujibu wa Sheria ya Kulinda Watoa Taarifa na Mashahidi ya Mwaka 2015 (*Whistleblower and Witness Protection Act of 2015*).

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inalipokea pendekezo la kutaifisha mashamba ya bangi na itaendelea kutafakari utekelezaji wake. Pale tutakapojiridhisha kuwa adhabu hii itatoa fundisho kwa wananchi wanaojihusisha na kilimo cha bangi, Serikali haitasita kuleta Bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria ili kuongeza suala hilo.

**5. HOJA:** Kuongeza vituo vya tiba ya *Methadone* na *Sober Houses* za Serikali angalau moja kila Mkoa.

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda (Kamati ya Kudumu ya Bunge, Masuala ya UKIMWI); Mheshimiwa Abdallah Ali Mtolela (Temeke)**

**JIBU**

**Mheshimiwa Spika,** uanzishwaji wa vituo vya tiba kwa kutumia *Methadone* unategemea ukubwa wa tatizo la matumizi ya dawa za kulevya na uwepo wa miundombinu ya msingi katika Mkoa husika. Hadi sasa kuna vituo vya *Methadone* katika hospitali za Muhimbili, Mwananyamala na Temeke - Dar es Salaam. Vilevile, Serikali inakusudia kufungua vituo kama hivyo katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani naTanga.

Kwa kuwa matibabu ya *Methadone* yanawasaidia watumiaji wa dawa za kulevya aina ya *Heroin* pekee, Serikali inatarajia kuanzisha nyumba za upataji nafuu (*Sober Houses*) kila Mkoa. Huduma hii itakuwa ni kwa ajili ya kuwasaidia waraibu (*addicts*) wengine wa aina zote za dawa za kulevya, badala ya kuwaachia watu binafsi ambao mpaka sasa wanaendesha nyumba 17 za upataji nafuu nchini. Vilevile, Serikali imeandaa Mwongozo wenye lengo la kusimamia na kuratibu *Sober Houses* za watu binafsi.

**6. HOJA:** Serikali iongeze vituo vya afya, vifaa tiba, wahudumu wa afya wenye weledi na kupunguza umbali wa kupata huduma kwa Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU).

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda (Kamati ya Kudumu ya Bunge, Masuala ya UKIMWI);**

**JIBU**

**Mheshimiwa Spika,** Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Sera ya Maendeleo ya Afya ya Msingi vinaelekeza Serikali kuboresha huduma za afya ya msingi kwa kujenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata na Hospitali kila Wilaya. Aidha, Serikali ina mkakati wa kuongeza idadi ya wataalam wa afya nchini

kote. Kupitia mikakati hii, wananchi wakiwemo WAVIU watapata huduma karibu na maeneo wanayoishi.

**7. HOJA:** Serikali itoe elimu ya kujikinga na VVU kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo elimu kwa njia ya Sinema na kuanzisha vilabu vya mapambano dhidi ya VVU katika shule zote kuanzia msingi pamoja na kuandaa mitaala ya elimu ya UKIMWI katika ngazi zote za elimu (elimu ya msingi hadi vyuo vikuu).

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda (Kamati ya Kudumu ya Bunge, Masuala ya UKIMWI);**

**JIBU:**
**Mheshimiwa Spika,**
Nia ya Serikali ni kuona elimu ya UKIMWI inawafikia wote wanaostahili. Serikali ina magari ya Sinema katika mikoa ishirini ya Tanzania Bara ambayo hutoa elimu ya UKIMWI kwa njia ya sinema. Tanzania Visiwani nayo sasa inapatamagari ya sinema katika mikoa yake yote. Wizara ya elimu imetoa mitaala ya kufundisha wanafunzi kuhusiana na elimu ya UKIMWI shuleni.
Serikali inatoa wito kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri kuyatumia ipasavyo magari hayo na kuhakikisha Walimu wapya wanapitishwa vyema katika mitaala hiyo pamoja na kuanzisha klabu za kuhamasisha mapambano dhidi ya UKIMWI katika shule na vyuo vyote nchini.

**8. HOJA:** Serikali ibuni chanzo mahususi cha kutunisha Mfuko wa UKIMWI (AIDS TRUST FUND) kama ilivyo kwa mifuko mingine kama vile REA na maji, ili kufanikisha mapambano dhidi ya UKIMWI.

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda (Kamati ya Kudumu ya Bunge, Masuala ya UKIMWI);**

**JIBU:**
**Mheshimiwa Spika,**
Ushauri uliotolewa umepokelewa na Serikali itaufanyia kazi.

**9. HOJA:** Kuweka utaratibu wa kufuatilia fedha zinazotolewa na wafadhili kwenye Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) zinazojihusisha na masuala ya UKIMWI.

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda (Kamati ya Kudumu ya Bunge, Masuala ya UKIMWI);**

**JIBU**

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu wa kufuatilia fedha zinazotolewa kwenye NGOs upo na tumekuwa tukisisitiza ufuatwe. Mathalan, nilipofanya ziara Mkoani Arusha hivi karibuni nilirudia wito wa kuzifanyia kaguzi za mara kwa mara NGOs zinazofanya kazi nchini. Hivyo, ushauri wa Kamati kuhusu hitaji la kufanya ukaguzi kwenye NGOs zinazoshughulikia UKIMWI utaendelea kuzingatiwa.

Natoa wito kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri waendelee kuhakikisha wadau wa UKIMWI wanaofanya kazi kwenye maeneo yao wanakaguliwa kulingana na Sheria ya UKIMWI ya mwaka 2008 na Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002. Nia yetu ni kujua wanapata nini, kwa ajili ya huduma zipi ili wanufaika waweze kujulishwa.

**10. HOJA:** Serikali ijiridhishe kuhusu masuala ya kitaalam na kufanya mapitio na maboresho ya Sheria stahiki katika kutekeleza Mpango wa kuunganisha Mifuko ya Pensheni.

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama (Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria)**

**JIBU**

**Mheshimiwa Spika,** zoezi la kuunganisha Mifuko ya Pensheni linafanyika kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mifuko yote ya Pesheni imefanyiwa tathmini (Actuarial Valuation), ambayo pamoja na mambo mengine, imebainisha kuwa kuunganisha Mifuko ya Pensheni ndio njia bora ya kuimarisha Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini.

Aidha, Serikali imeandaa Andiko la mapendekezo ya kuunganisha Mifuko. Kazi hii imefanyika kwa kushirikisha

wadau muhimu katika Sekta husika. Serikali itaendelea kutoa taarifa za mara kwa mara kwa hatua zinazofikiwa.

**11. HOJA:** Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza kwenye uchumi wa viwanda.

**MTOA HOJA: Mheshimwia Zuberi Kuchauka (Liwale)**

**JIBU**

**Mheshimiwa Spika**, uwekezaji ni kazi mojawapo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Lengo la uwekezaji ni kulinda thamani ya michango ya wanachama pamoja na kukuza uwezo wa Mifuko kulipa mafao kwa wanachama wake pale wanapopatwa na majanga mbalimbali yanayowasababishia kukosa kipato. Majanga hayo ni kama vile maradhi, uzee na kifo. Kwa msingi huo, uwekezaji kwenye viwanda unaofanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii sasa una manufaa mtambuka kwani pamoja na kulinda thamani ya fedha za michango ya wanachama, uwekezaji huu unakuza mapato ya Serikali, unatoa fursa za ajira na hivyo kusaidia kuongeza idadi ya wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba uwekezaji unaofanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii unazingatia Miongozo ya Uwekezaji ili mifuko hiyo isiweze kupata hasara.

**12. HOJA:** Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura.

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama (Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria)**

**JIBU**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jukumu la kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Tume ya Taifa ya Uchaguzi itaweka kipaumbele katika uboreshaji wa Daftari la Wapiga kura.

Aidha, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa jukumu la kutoa

elimu ya mpiga kura Nchi nzima na kusimamia na kuratibu Asasi, Taasisi au watu wanaotoa elimu ya mpiga kura. Tume imeendelea kutoa elimu ya Mpiga Kura kwa njia mbalimbali ikiwemo kutumia Redio, Televisheni, kukutana na wadau kupitia maonyesho mbalimbali, pamoja na kushiriki mikutano katika ngazi za Mikoa na Halmashauri.

**13. HOJA:** Mgogoro wa Uongozi ndani ya CUF

**MTOA HOJA: Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama (Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria) Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni); Mheshimiwa Cecilia Danel Paresso (Viti Maalum); Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah (Tumbe); Mheshimiwa Khatibu Said Haji (Konde); Mheshimiwa Juma Kombo Hamad (Wingwi); Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum (Mtambile)**

**JIBU**

**Mheshimiwa Spika,** Hoja hii imejadiliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali.
Serikali haifurahishwi na migogoro ndani ya vyama vya siasa, kwani inadumaza demokrasia nchini na kusababisha mifarakano isiyokuwa na tija. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kama mlezi wa vyama vya Siasa imekuwa ikishiriki kikamilifu katika kuhakikisha migogoro ndani ya vyama vya siasa inatatuliwa kwa majadiliano.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mgogoro uliopo ndani ya chama cha CUF, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilitoa ushauri kulingana na taratibu zilizopo. Hata hivyo, wakati usuluhishi ukiendelea baadhi ya wanachama wa CUF ambao hawakuridhika na usuluhishi uliofanywa na Msajili walipeleka shauri Mahakamani, ili kudai haki kwenye Mhimili wa Mahakama ikiwa ni pamoja na suala la ruzuku ambalo Mahakama imetoa zuio la muda mpaka shauri la msingi lililoko mahakama itakapolitolewa uamuzi. Kwa kuwa masuala hayo yapo Mahakamani, ni vizuri tukaiacha Mahakama ifanye kazi yake. Hiyo ni rai yangu.

## 5.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kama nilivyosema hapo awali, muda usingeweza kutosha kujibu hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja. Tumejifunza mambo mengi kutoka kwenye michango yenu, na tupo tayari kuendelea kujifunza zaidi kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge.

**Mheshimiwa Spika,** Nchi hii ni yetu sote, na kila mmoja wetu anao wajibu wa kulisukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu. Kila mchango wa Mheshimiwa Mbunge una thamani kubwa sana kwetu, na ninawashukuru sana kwa ushauri, maangalizo na mafunzo. Endeleeni kutoa ushauri kwa Serikali, hata kwa maandishi siyo lazima kusubiri Bungeni, nasi tutaupokea na kuona namna bora ya kufanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika,** kila Mtanzania ikiwemo Waheshimiwa Wabunge, anawajibika kuiacha Tanzania ikiwa ni nchi bora zaidi ya alivyoikuta. Ili kuifikia azma hiyo, inabidi tuanze kuwa tayari kujinyima mambo mazuri tuliyoyazoea, angalau kwa muda, ili kuimarisha misingi ya ujenzi wa Tanzania yetu. Ninawasihi waheshimiwa Wabunge wenzangu muielewe dhamira ya Serikali na mtuamini katika kusimamia rasilimali za nchi yetu kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo. Serikali imejipanga vizuri katika kulinda maslahi ya nchi hii na wananchi wake, hivyo nawaomba muendelee kutuunga mkono kwa kupitisha Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Fungu 37 Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama alivyosema Katibu ukurasa wa 233. Natumaini wote wenye vitabu tumefika hapo na hapa ni mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tunaenda ka utaratibu wetu ule tuliojiwekea ambapo waulizaji wa eneo hili ni wale ambao majina ninakuwa nimeshaletewa na Kambi zenu mbalimbali.

Kif.1001 *Admn. and HR Mgt* .................... Sh. 3,909,749,907/=

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Hapa kulikuwa kuna hoja ilitolewa kuhusiana na mgawanyiko wa vyama vya siasa ambavyo vimepelekea kuwa vipande vipande na makundi ambavyo hoja hii Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye alisema kwamba pia Serikali nayo haifurahishwi na hili. Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa rai kwamba tuache Mahakama ifanye kazi yake. Sasa kwa kuwa Mahakama inaweza ikafanya kazi yake lakini bado kwa tunavyofahamu mgogoro huo unaweza ukaletwa humu tena kama ilivyotolewa hoja humu katika Bunge hili.

Kwa nini Ofisi ya Msajili wa Vyama isiwajibike kwa kushindwa kupatanisha pande hizi za mgogoro wa CUF hasa kuhusiana na mgogoro wa ruzuku? Kama sikupata majibu yanayotosha nitaondoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali Hassan King haya si ndiyo ambayo tulipata ushauri kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikal? Labda Mwanasheria Mkuu usimame tena kwa mara nyingine.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili liko Mahakamani na Kanuni zetu nimezisoma hapa, Katiba inakataza kujadili mambo ya huko Mahakamani na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anahitimisha hoja amelisema vizuri hili suala.

Naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba tuliachie suala hili Mahakama ambao ni mhimili tena mwingine huru unaoshughulikia hili suala walishughulikie na Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema vizuri sana, Serikali tungependa mgogoro huu uishe mapema ili shughuli za Vyama vya Siasa ziendele kufanyika kwa ufanisi ipasavyo kwa mustakabali wa Taifa hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ali Hassan King basi swali lako ndiyo limeishia hapo sidhani kama kuna haja ya kuliendeleza.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nieleze wasiwasi wangu pamoja na maelezo mazuri kwamba Mahakama itaamua (a) au (b), sasa hapa bado mgogoro utakuja kuendelea tena. Kwa kuwa maelezo haya kwamba hili suala liko Mahakamani, basi sizuii shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Ali Hassan King kwa kuzingatia ushauri tuliopewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Sub Vote 1001* nitatoa shilingi kama sitapata maelezo ya uhakika kwa sababu ukiangalia sera ya UKIMWI haitofautiani kabisa na Sera ya Dawa za Kulevya, lakini kumekuwa na Kamati ya UKIMWI na nyingine ni Kamati ya Dawa za Kulevya sasa zisifanye kwa pamoja?

**MWENYEKITI:** Uko wapi pale Mheshimiwa au swali lako ni la sera la jumla?

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Ni kwenye mshahara wa Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Kama ni swali la jumla endelea.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Nataka nipate ufafanuzi kwa sababu Kamati zimekuwa nyingi kwanini zisifanywe kwa pamoja kwa sababu zote athari zake zinafanana. Sasa kama sitapata maelezo ya kutosha kwa kweli sitakubali.

**MWENYEKITI:** Ni Kamati ipi na ipi Mheshimiwa Mwamoto?

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya UKIMWI na Kamati ya Dawa za Kulevya.

**MWENYEKITI:** Ungerudia kidogo ili Wabunge wote wawe pamoja na wewe.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zile zimetofautishwa hawafanyi kazi kwa pamoja kwa sababu malengo yanafanana lakini kazi haziendi kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Katika *level* ya Wilaya au katika *level* ya Taifa?

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Katika *level* ya Taifa.

**MWENYEKITI:** Natumaini Mheshimiwa Waziri wa Nchi umemuelewa Mheshimiwa Mbunge, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho ya Sheria ya UKIMWI ya mwaka 2001 na yalifanyika mwaka 2015. Sasa marekebisho yale ya sheria na sheria mama ya mwaka 2001 yana kifungu cha 13(1) na (2). Sasa vifungu hivyo vidogo ndiyo vinaweka mfumo wa Kamati ambazo zinafanya kazi ya

kusimamia tatizo la UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania toka ngazi ya Taifa mpaka kwenye Kata mpaka kule kwenye vijiji.

Mheshimiwa Mbunge anachokisema hapa kama nimemuelewa vizuri ni kwa nini matatizo yote haya mawili la UKIMWI na dawa za kulevya yasiunganishwe na kujadiliwa kwenye Kamati hiyo kama ni UKIMWI Kamati ya Taifa ama mpaka kule kwenye Kamati ndogo ambazo zimeundwa kwa mujibu wa sheria hii. Kama ndivyo hivyo anazungumzia suala hilo, sheria yetu ya mwaka 2015 iliyoanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya kifungu cha 65 kinampa madaraka Kamishna Jenerali anayeshughulikia mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania kum-*co-opt* mdau yeyote ambaye anaona kwamba anaweza na anafaa akasaidia mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia kifungu cha 65 na kwa kutumia kifungu cha 13(1) (2) cha Sheria ya *TACAIDS* tunao uwezo kabisa sasa wa kumuomba Kamishna Jenerali atumie kifungu cha 65 ili Kamati zile za UKIMWI kama ni kuanzia ngazi ya Taifa mpaka kule kwenye vijiji zinaposhughulikia masuala haya ya UKIMWI basi zishughulikie na tatizo la dawa za kulevya nchini.

**MWENYEKITI:** Nashukuru Mheshimiwa Mwamoto umeridhika naona Serikali inawaza katika mstari wako mwenyewe, endelea tu Mheshimiwa Mwamoto kama una la kusema.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi na mimi nimeridhika na narudisha shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwamoto anapendekeza mfumo uwe ni kama Kamati yetu ya Bunge ilivyo, naona Bunge tulishaona mbali inaeleekea. Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakusudia kuzuia shilingi katika hoja hii, nayo inahusu masuala ya usalama wa raia na jambo hili limejadiliwa kwa kina sana katika Bunge hili, katika vyombo vya habari, katika mitandao ya kijamii na limezua sintofahamu na hofu kubwa sana kwa Watanzania, japo katika wakati wa kujibu hoja za awali Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema masuala ya kiusalama hayajadiliwi ndani ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 64 ya Bunge, Kanuni zinazoongoza Bunge nimejaribu kuzipitia kwa umakini sana na nikagundua kwamba hakuna katazo lolote katika Kanuni linalosema masuala ya usalama wa raia ama masuala ya ulinzi na usalama hayawezi kujadiliwa ndani ya Bunge. Hilo katazo katika Kanuni ya 64 halipo.

**MWENYEKITI:** Tusomee Kiongozi ili Waheshimiwa Wabunge waweze kukuelewa.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, Mwanasheria Mkuu alituambia kwamba masuala ya ulinzi na usalama hayajadiliwi ndani ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 64. Kanuni ya 64 inatoa makatazo yafuatayo:-

Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge;

(a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli;

(b) hatazungumzia jambo lolote ambalo haliko kwenye mjadala;

(c) hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama au jambo lolote ambalo lilijadiliwa na kutolewa maamuzi kwenye Mkutano uliopo au uliotanguliwa na ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja

mahsusi na vile vile hatapinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge isipokuwa tu kwa kutoa hoja mahsusi inayopendekeza kuwa uamuzi huo uangaliwe upya;

(d) hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani;

(e) hatazungumzia mwenenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia utoaji wa haki isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahsusi kuhusu jambo husika;

(f) hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote na;

(g) hataumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika vifungu vyote hivyo hakuna katazo lolote linalosema kwamba tusijadili masuala yanayohusu ulinzi na usalama au wahusika katika sekta hizo kama tunafikiri maslahi ya raia wetu yako *jeopardized.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamezungumzwa sana, Wabunge wakiomba miongozo mbalimbali kuhusu hii hoja ya watu kutekwa. Hata Mbunge humu ndani alionesha hofu yake kwamba ana taarifa za uhakika kwamba kuna Wabunge 11 nikiwemo mimi bahati mbaya ambao tuko katika *list* inayotegemewa kutekwa. Sasa hizi habari hazijajadiliwa.

Vilevile hoja ya kutekwa kwa msanii Roma Mkoliki imezungumzwa sana na vilevile wakati Mwanasheria Mkuu anajibu akasema Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Taifa anaweza akawa na taarifa za ziada kuhusu mambo kwa sababu ni ofisi yake na ni wajibu wake na mamlaka hayo amepewa na Sheria ya *Regional Administration.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu ni Mjumbe wa Baraza la Usalama wa Taifa na katika Baraza la Usalama wa Taifa lenye watu watano; Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu ni Wajumbe wa Baraza la Usalama la Taifa. Kuna mambo yamekuwa yanaendelea kwa muda mrefu ya watu kutekwa, watu kuwa *tortured* na tuna taarifa kwamba kuna *torture squad* ambayo ipo inakamata watu mikoani, inawaleta Dar es Salaam wanateswa Mikocheni wengine wanateswa Oysterbay. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo tumelizungumza kwa muda mrefu na hiki kikosi kinachoitwa kikosi kazi kina watu kutoka Usalama wa Taifa, kina watu kutoka Jeshi la Wananchi, Polisi na vikosi vingine. Amepotea Ben Saanane...

**MWENYEKITI:** Naomba umalizie.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ninamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atuambie sasa, atupe ukweli kuhusu kuwapo kwa kikosi kazi hiki, kazi inayofanya na hapo hapo atupe maelezo, Serikali ina mkakati gani basi kushughulika kupotea kwa Ndugu Ben Saanane ambaye amelalamikiwa sana na Serikali haitoi Kauli yeyote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbowe unatakiwa jambo liwe moja mahsusi, sasa umeweka mengi, moja lipi ambalo unataka Mheshimiwa Waziri Mkuu aje a-*adress.*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni moja tu mahsusi, usalama wa raia ambayo huwezi ukai-*discuss in singular* kwa sababu lazima itaungana na watu wanaohusika, watu wanaoshika na mifano ya watu ambao wametekwa, vyote hivyo ni kitu kimoja. Ni usalama wa raia. *(Makofi)*

**MWENYEKTI:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema hizi taarifa zinazosambazwa kwamba kuna orodha ya Wabunge, watu kumi na moja wa kutekwa siyo za kweli ni za mitandao tu. Kwa sababu kama orodha hiyo unayosema kuna *squad* na ina polisi na polisi wako chini yangu, halafu na kwenye orodha na jina langu likawepo nadhani ni yale yale tu ya watu wanaandika orodha zinajitokeza zinakuwepo vile. Hakuna kitu kama hicho na orodha hiyo siyo sahihi. Kama orodha hiyo ingekuwa sahihi nadhani kwa mazingira kama haya wala isingekuwa inatoka kama hivyo inavyotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira hata ya kijijini tu, mtu anayetaka kukuroga wala huwa hasemi anataka kukuroga. Kitu kikubwa kama hicho hawawezi watu wakaorodhesha hivyo kirahisi na ikatoka. Hata ukiangalia hao watu wanaowekwa kwenye orodha ya kutekwa, watekwe ili iweje? Yaani wana kitu gani hasa hicho cha kutisha mpaka useme wanatakiwa watekwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea hoja ya msingi hapa ambayo tunatakiwa kama Bunge kujikita ni suala la usalama. Suala la usalama wa raia ni ajenda kubwa kwa Serikali na kwa Serikali yeyote ile duniani. Waheshimiwa Wabunge kwenye suala la usalama wala hatuna haja ya kutofautiana kwa sababu sisi ni kipaumbele. Tumewahakikishia wananchi kuhusu usalama wao na hapa kama Wabunge tunatakiwa tu kujadiliana namna ya kukabiliana na mambo hayo na ukija ushauri wa namna ya kukabiliana na masuala ya usalama wa raia, Bunge ni kazi yake na Serikali tutajumuika nanyi ili tuweze kuwahakikishia usalama, raia tunaboresha na wananchi wanakaa kufanya kazi katika hali ya usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa wa ajabu sana tukianza kubishana kuhusu usalama wa raia wetu. Hakuna Serikali duniani itaweka rehani usalama wa raia wao. Serikali

tunachukua hatua Waheshimiwa Wabunge, mara kwa mara hata ninyi mtakuwa mashahidi, wakati mwingine tunakuwa katika mazingira yenye utata. Kusingekuwepo na uhakika wa usalama kutoka Serikalini, maisha yetu yangekuwa hatarini.

Kwa hiyo, tusichukue kesi moja moja, kesi moja moja duniani kote zipo za watu kuwa hatarini, lakini hiyo inakuwa siyo ya Serikali inakuwa ya watu waovu na sisi tuko hapa kupambana na watu waovu kuweza kuhakikisha kwamba watu wetu wanakuwana maisha yaliyo na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie duniani kote Serikali inapotangaza mapinduzi ya kiuchumi kunakuwepo na vita ya kiuchumi. Kwa hiyo, inapokuwepo vitu vya aina hiyo kunakuwepo na mbinu nyingi ambazo zinawaondoa watu kwenye malengo na nahisi hicho ndicho ambacho kinafanyika katika mazingira haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tuelewane na tukubaliane kwamba hii ni ajenda yetu sote kuhakikisha kwamba raia wako katika mazingira salama pamoja na mali zao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri anataka kuliaminisha Bunge kwamba hakuna vikosi vya utesaji katika Taifa, sisi tunajua kuna kikosi cha utesaji katika Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo basi naomba Bunge lijadili jambo hili. Hili jambo ni la muhimu naomba nitoe shilingi. Naomba Wabunge waniunge mkono katika suala hili ili tulijadili kwa kidogo tuweze kupata ukweli kuhusu namna ambavyo watu wanahusika na watu ambavyo wameshughulishwa katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shilingi na naomba Wabunge mniunge mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Mawaziri, mnaunga mkono hoja au mnataka kusema kidogo? *(Kicheko)*

Sawa Kiongozi, kaeni ili tusonge mbele. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali unataka kusema kitu, katika uchangiaji eeh? Tuanze mchangiaji wa kwanza Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mojawapo ya mambo ambayo yaliondolewa wakati wa Kiongozi wa Upinzani anawasilisha hoja yake hapa Bungeni. Sasa yatajadiliwaje tena hapa? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, haya ni masuala ya kisheria. Kama mna taarifa hizo, pelekeni huko kwenye vyombo vinavyohusika.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Baraza la Wananchi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Baraza la Wananchi kitu gani? Kwa sababu kwanza....

**MWENYEKITI:** Naomba tusikilizane ndugu zangu, tutafika mahali pazuri.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, hapana. Kwanza Kiongozi wa Upinzani Bungeni amelipotosha, hiyo Kanuni sikuisema kwamba inazuia kujadili.

**MBUNGE FULANI:** Kipi kinazuia sasa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Katiba!

**MBUNGE FULANI:** Wapi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ibara ya 100.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Isome.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Katiba hii hapa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, tuwe na subira. Tupunguze mihemko. Tutafika mahali tutaelewana tu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hiyo Kanuni anayoisema inatu-*subject* kwenye Ibara ya 100. Ibara ya 100 inasema hivi..., ninyi wote hamuwezi kuwa wanasheria. Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali pengine.... *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusoma..... Ibara ya (2) inasema ... bila kuathiri Katiba hii au masharti ya sheria nyingine yoyote inayohusika na sheria zimetungwa nimewasomea hapa wakati nachangia. Moja ni Sheria ya *Whistleblowers* ambayo inakataza kujadili mambo yanayohusu usalama wa ndani na nimeeleza hapa. Sheria ya Usalama wa Taifa.......

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ahsante. Tutarudi kwako baadaye kidogo. Naomba tusikilizane. Tunaendelea kujadili, ataanza Mheshimiwa Tundu Lissu halafu Mheshimiwa Angellah Kairuki, nachukua hao wawili kwanza.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

kwanza kuhusiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Serikali na nchi hii inayumba kwa sababu ya kuwa na Mwanasheria Mkuu wa aina hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu Ibara ya 13(6)(a) imepiga marufuku kuteka watu, kutesa watu, ku-*treat* watu kinyama na inasema:

"Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria, mamlaka ya nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba (a) ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wametekwa, wameteswa, wamedhalilishwa, wamefanyiwa matendo ya kinyama na hili Bunge ndiyo mahali pake pa kuzungumza mambo haya. Kama huwezi ukazungumza kwenye Bunge hutazungumza pengine popote. Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wala siyo vitu vya kufikirika. Fikiria Mheshimiwa Lema aliondolewaje Bungeni hapa kupelekwa Arusha kukaa miezi minne gerezani. *He was abducted* alitekwa nyara. Hakuna *arrest warrant,* hakuna kuambiwa kosa lake. Fikiria mimi niliondolewaje hapa, hauna kuambiwa kosa, hakuna *arrest warrant,* hakuna *nothing. We are being abducted and tortured.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natetea watu 18. Wamekaa *Oysterbay* siku 42 wanapelewa kuna nyumba Mikocheni karibu na wanakokaa Mawaziri wanaenda wanateswa kila usiku, nimewataja majina hadharani. Kuna mtu anaitwa Mohamed Mrutu amekamatiwa Same, kuna mwingine anaitwa Abdallah Bushiri amekamatiwa Kariakoo, wamepigwa, wamevunjwa miguu. Nimekutana nao mahabusu. *This country is torturing people, this government!* Hii Serikali ina-*torture* watu na wala siyo siri, ndiyo maana wananyooshewa bunduki mchana kweupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii leo Mkuu wa Mkoa, *a mere Regional Commisioner* anatembea na Wanajeshi, anavamia vituo vya redio, mnadiriki kutetea ujinga huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema siku moja hapa, mnafikiria mnashughulikia wapinzani, mkumbuke Mheshimiwa Nape, mkumbukeni Mheshimiwa Bashe, mkumbukeni Mheshimiwa Musukuma, kesho ni wewe. Kwa hiyo, hii *ajenda* hii Waziri Mkuu toa kauli iwe ni marufuku kwa hicho kikosi kazi, kwanza kivunjwe. Hakuna Sheria zetu zenye kikosi kazi, hakuna na kinapokea amri kutoka Ikulu. Iwe ni marufuku, toa kauli Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba ni marufuku kwa chombo chochote cha Serikali kutesa watu, kuteka watu nyara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu, kengele imeshalia.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu toa kauli, usipotoa tutajua hii ni Serikali ya watesaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angellah Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi napata taabu tu kuona kwamba suala hili lilishafanyiwa maamuzi lakini limekuwa likienda likirudi na kwa mujibu wa Kanuni sasa niseme tu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme

kwamba chombo hiki ni chombo muhimu. Ni chombo ambacho kiko kisheria, ni chombo ambacho kimeanzishwa kwa majukumu maalum, hivyo basi ni vema tukaweza kukilinda, kukithamini na kukiheshimu.

Kwanza kabisa mtu anaposema kuna *torturing squad*, siyo kweli. Haya ni maneno ya ufitinishi, maneno ya uchochezi na wote tunafahamu nchi hii kuna kosa pia la uchochezi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwasikiliza wakati mnaongea eeh! Wakati unaongea Mheshimiwa Lissu tulikusikiliza kwa hiyo na wewe uwe na uvumilivu usikilize wengine wanapojenga hoja zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika sheria inayoanzisha chombo au Idara ya Usalama wa Taifa katika kifungu cha tano imeeleza majukumu yake. Ukiangalia katika kifungu cha 5(1)(c) wanaruhusiwa ku-*cooperate* au kushirikiana na vyombo vingine vya dola, sasa unapokuja kusema kwamba kuna vikosi kazi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Naomba uniache niseme.. wala hainipi taabu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ongea na mimi tu hutapata taabu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishasema hakuna *torturing squad.* Chombo hiki kimeanzishwa kwa mamlaka yake, majukumu yake yako bayana, lakini hata ukija kuangalia katika kifungu cha 14 kiko wazi kabisa, ni kwa sababu wao wameamua ku-*single out* katika masuala wanayoyataka, wameamua ku-*single out* kuepuka tafsiri yenyewe ya sheria.

Ukiangalia Kifungu cha 14 kiko wazi, imeeleza kabisa mamlaka na majukumu ya chombo hiki katika kukusanya taarifa mbalimbali kwa ajili ya kupata taarifa za kiusalama inapotokea kuna tishio la kiusalama na masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika kifungu cha 15, unaposema kukamata uthibitisho huna. Hauna uthibitisho kwa sababu hauwezi kuwa nao kwa sababu hakuna kitu kama hicho.Ni fikra mnayojijengea ambayo mnataka kuwaaminisha watu kwamba kuna kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima kwenye masuala kama haya ifike mwisho. Tusitake kujenga kukubalika katika jamii kwa kutaka kufitinisha watu. Tunajua ukiangalia katika kifungu cha 15(3) kinaeleza bayana. Ukija katika kifungu cha 16 masuala yote yako wazi mpaka hata kwenye *restrictions* za *publication* na ukiangalia haya masuala yanayofanyika hapa pia ni masuala kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana tumeshafanya maamuzi, ni vema watu wakaelewa, ni vema tukaheshimu chombo lakini pia tusiwadanganye wananchi kwenye masuala mazito kama haya. Ni chombo muhimu sana kinachotegemewa katika Taifa. Unapoanza kukichafua, kwanza unashangaa hivi hata katika nchi zingine za jirani wanawaonaje, wanawaelewaje? Mnapokichanachana chombo chenu kama hiki chombo kizito, ni vema kwa kweli ifike mwisho, ni vema suala hili likemewe, iwe ni fundisho, watu waweze kutambua mipaka na mamlaka ya vyombo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza, uhuru; nimeeleza majukumu; nimeeleza mamlaka ya chombo hiki. Turudi kwenye vifungu vile, turudi kwenye majukumu, turudi kwenye kazi za chombo hiki na tuweze kutafsiri kama sheria ilivyoelezwa. Hata hivyo, cha msingi tufuate ukweli wa mambo, tusipotoshe ukweli na kutaka kuaminisha watu vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, uwe mchangiaji wa mwisho tumrudishie mtoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niunge mkono yale yaliyosemwa na Waziri wa Utawala Bora Mheshimiwa Angelah Kairuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kama Waziri mwenye dhamana ndani ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba niseme jambo lifuatalo. Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akihitimisha hoja yake hapa alisema; kwa kuzingatia misingi hiyo hiyo ya Katiba, misingi ya sheria tulizonazo, misingi ya kupata habari na kuzifanyia kazi kwa kutumia sheria za nchi tulizonazo; amesema hapa ndani ya Bunge lako Tukufu; jambo hili si jambo la kutolea kauli kabla halijafanyiwa kazi kwa kuzingatia taratibu hizo nilizozisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitakuwa busara wala hatutamtendea haki Mheshimiwa Waziri Mkuu kumlazimisha eti atoe kauli hapa ndani kabla hajaweza kutekeleza majukumu yake, yanayozingatia sheria na katiba kulifuatilia jambo hili na kupata taarifa za kina ambazo zitakuwa zimefanyiwa kazi vizuri ndani ya Serikali. Naomba niseme, baada ya kazi hizo zote kufanyika, taarifa kupatikana ambazo ni taarifa sahihi, sheria za nchi tulizonazo zikafuatiliwa kadri zinavyotakiwa, Katiba ya nchi yetu inayolinda mihimili yote

na vyombo hivi vyote ikafuatwa, hapo Serikali itakuwa tayari kusema lolote na kutoa kauli yoyote na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba tuendelee. Bunge lako liheshimu na lielewe kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akihitimisha hoja yake. Anajali, anaelewa, lakini hawezi kutoa kauli hapa kabla ya kauli hiyo haijafanyiwa kazi kupitia vyombo vinavyohusika ndani ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ni bahati mbaya sana kwamba tunafanya jambo hili ni jepesi kwa sababu pengine ninyi hamjaguswa au familia zenu hazijaguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa nyingi na nilitegemea Serikali katika kutoa majibu, ingejipa ujasiri wa kusema nileteeni ushahidi. Maana wangetuambia tuwape ushahidi tungewapa ushahidi. Watu ambao wameteswa chini ya vyombo vya ulinzi na usalama; kwanza naomba tuelewane jambo moja, kambi yetu haina tatizo kabisa na uwepo wa Idara ya Usalama wa Taifa katika kutekeleza majukumu yake, hatuna tatizo na hilo; ila ni pale idara inapotumika vibaya, kugeuka kuwa chombo cha kutesa watu au baadhi ya watu katika idara wanatumika kutesa watu, hapo ndipo mahali ambapo tunalalamika na ndipo tunapotaka Serikali itoe kauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haitoi kauli, wewe kama Spika, bado una nafasi ya ku-*order* liundwe jopo likachunguze, lakini Mheshimiwa Waziri anatuambia sasa hivi kwamba Serikali ikafanyie kazi jambo hili wakati Usalama wa Taifa ni sehemu ya Serikali yaani ni kwamba wao wakajihukumu wenyewe, hilo jambo halipo. Kwa hiyo tunachosema, bado sijaridhika na jambo hili na naomba

sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni suala la *safety* ya nchi yetu, haya mambo yanajenga usalama katika Taifa, yanajenga mshikamano katika Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vyetu hivi vya Ulinzi na Usalama tunavyovi-*subject* kwenye *order* za kwenda ku-*torture* raia ambao hawana makosa au hata kama wana makosa kuna utaratibu wa ku-*handle* makosa yao si ku-*torture.* Watu wanakuwa *tortured* watu wanakuwa *electrified,* watu wanaumizwa na tumesema hapa tuko tayari kutoa ushahidi. Mheshimiwa Lissu amewapa mfano hapa anatetea watu 18 katika jambo hili na wako tayari kwenda kutoa ushahidi kokote unakotakiwa, watu wameuawa Geita, watu wameuawa Sengerema, watu wameuawa maeneo mbalimbali nyie mnasema hamjui labda kwa sababu wanaoteswa ni wapinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo liko *very serious* na likiachwa likaendelea kuota mizizi hatimaye sasa watu watakuwa wanauawa mchana kweupe. Mmeona namna waliokuwa Mawaziri wenu, kwamba wanaweza wakatolewa silaha mchana kweupe, mbele ya kamera na hakuna kauli ya Serikali. Sasa tukiruhusu mambo haya yakaendelea ku-*generate* tukaona ni mambo ya kawaida tu kwa sababu ninyi hamhusiki, hamko salama sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema tunataka nchi yetu irudishiwe amani tuliyoizoea. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vifanye kazi kwa mujibu wa sheria. Hivi vikosi vinavyoundwa kwa sababu eti ya shughuli maalum ambazo haviwekwi wazi, vinashika watu, vinatesa watu, vinaumiza watu, wengine wanauwawa kisirisiri, aah! *No!* Kuna ushahidi wa kutosha na hili jambo halikuanza leo, lakini sasa limeshika kasi sana katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano, ndiyo sababu tunataka Serikali itupe kauli kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mimi naendelea kutoa Shilingi na naomba Wabunge wote waniunge mkono katika hili.

**MWENYEKITI:** Sasa tumefika mahali pa kuhojiana. Kwa hiyo, kilichopo mbele yetu ni hiyo hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Kwa hiyo nitahoji kwanza wanaoafikiana na hoja yake halafu wasioafikiana na hoja yake. Kwa hiyo tutajua suala lipi limevuka katika maamuzi yenu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Mmasi.

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia *vote* 37 ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba ujuzi katika nchi yetu uko chini sana na hatuoni juhudi mahususi za Serikali katika kukuza ujuzi kwa vijana wetu ili waweze kuajirika kirahisi. Sasa, nini msimamo wa Serikali kuhusiana na masuala mazima ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba majibu yanayoridhisha nafsi yangu kwa kuwa suala hili ni ajenda ya Watanzania, ni ajenda ya vijana wahitimu wa nchi ya Tanzania ambao mimi nawawakilisha katika Bunge lako hili Tukufu. Pia ni ajenda ya Wabunge vijana wa Chama cha Mapinduzi katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu yanayoridhisha nafsi yangu, kuhusiana na suala hili kutoka kwa Waziri mwenye dhamana chini ya Wizara hii. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI , OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika kwenda kufikia katika nchi ya uchumi wa viwanda ni lazima kuwa na nguvu kazi ambayo ina ujuzi ambao unaendana na matakwa katika nchi ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ofisi ya Waziri Mkuu tunazo *program* za kusaidia nguvu kazi ya nchi hii iwe na ujuzi. Kwa kutambua kwamba, takwimu zinasema ya kwamba nchi yetu ina ujuzi wa juu wa nguvu kazi kwa asilimia tatu, ujuzi wa kati asilimi 16 na ujuzi wa chini asilimia 79. Hata hivyo, ili kwenda katika nchi ya uchumi wa kati, lazima uwe na nguvu kazi yenye ujuzi wa juu kwa asilimia 12, asilimia 34 ujuzi wa kati na asilimia 54 ujuzi wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu katika bajeti iliyopita ilitengwa kiasi cha shilingi bilioni kumi na tano kwa ajili ya *program* mbalimbali. Moja ya *program* zilizotengwa ni kusaidia kuwarasimisha vijana wa Kitanzania ambao wana ujuzi lakini hawakupitia katika mfumo rasmi. Pia tumekuwa tuna program zaidi ya nne za kuwafikia vijana takribani 9100 kwanza kuwapa ujuzi mbalimbali kupitia masuala ya teknolojia, vilevile masuala ya bidhaa za ngozi, uchomeleaji na masuala ya utalii na ukarimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu pia kiasi hicho hicho kimetengwa, cha zadi ya bilioni ,15 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba nguvu kazi ya nchi yetu inakuwa na ujuzi wa kutosha. Kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge,tunafahamu kwamba huwezi kuwa na nguvu kazi ambayo haina ujuzi. Kwa hiyo, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tumeipa *consideration* kubwa hiyo na hivi sasa tunafikia makundi mengi zaidi ya vijana ili waweze kupata huduma hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Mmasi, nini tena!

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana ndugu yangu, kaka Mavunde, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), lakini tunapoongelea masuala ya ajira kwa kijana wa Kitanzania kiuhalisia tunaongelea masuala yote au mazingira yote wezeshi katika kuona kwamba kijana huyu wa Kitanzania anaweza kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mathalani tunaongelea mitaji. Kwenye Bunge lako Tukufu bajeti iliyopita, ya mwaka 2015/2016 tulisimama hapa kupitia Ofisi ya Waziri wa Kilimo; Dkt. Tizeba alisimama hapa akatupa ahadi kemkem kupitia dirisha la mlango wa kilimo kwa kijana. Ni namna hiyo tu ambapo vijana tunaona wanaweza wakajiwezesha wakaajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zililetwa ahadi nyingi sana, tukasema kwamba kuna bilioni 500 kutoka Benki ya *NMB*, *agro-business loan window* kwamba vijana watakopesheka na wataweza kujiajiri kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini isitoshe kulikuwa pia kunasemwa kwamba zimetengwa bilioni 55 kwa ajili ya Benki ya Kilimo, lakini ni asilimia tatu tu imetumika. Ukija na kwenye lile Baraza la Vijana ilitengwa Shilingi bilioni 1.2; lakini leo hii tumeona tengeo la Baraza la Vijana ni Shilingi bilioni moja tu iliyotengwa. Najiuliza hapa je, mafanikio yamezidi matamanio yetu hata tukaweza kushusha bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kulikuwa na maelekezo ya kisera, kulikuwa na maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu hapa Bungeni mwaka jana, kwa *hansard* zinasoma na Bunge hili lina kumbukumbu...

**MWENYEKITI:** Nakukumbusha Mheshimiwa Esther, ni suala moja tu; si vizuri kuongeza la pili, la tatu; jambo moja mahususi jielekeze ili tupate majibu.

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja huko, najaribu kujenga hoja na kukumbusha tulichokisema hapa Bungeni, najaribu kuweka nyama katika hoja yangu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitashukuru...

**MWENYEKITI:** Sasa nakuelekeza Mheshimiwa Esther jielekeze tu moja kwa moja, ni jambo gani hasa.

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni hii, pamoja na maelekezo mazuri ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Ofisi ya Mipango Miji, kwamba isitokee Ofisi ya Mipango Miji inatoa kibali cha ardhi na matumizi mpaka pale ambapo tumeona vijana wametengewa ardhi kwa ajili ya kilimo, lakini pia tukasema Ofisi za Wakuu wa Mikoa waweze kutenga ardhi kwa ajili ya vijana kujiajiri kwenye suala la kilimo, hakuna waraka uliokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa hawakopesheki, naomba kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, kaka yangu Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde arudi na niridhishe nafsi yangu, tafsiri hii ni nini? Vijana hawa ni lini wataajirika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nadhani umeshaongea ya kutosha, japo mambo mengine haya muwe mnaenda taratibu, yaani watu wasipate ardhi mpaka vijana kwanza, kwani nchi hii ya vijana peke yao? Vijana msiende mbali mpaka mkaanza kudharau wazazi wenu na nini na ninyi mtakuwa watu wazima kesho sijui mtakuwa wageni wa nani! *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI , OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kabisa asilimia kubwa sana ya vijana ambao wangependa kufanya shughuli mbalimbali za biashara, ufugaji na kilimo wanakabiliwa na tatizo la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Novemba, 2014, hapa Dodoma, Ofisi ya Waziri Mkuu ilikutana na Wakuu wa Mikoa wote na madhumuni ya kikao hicho ilikuwa ni kutengeneza maazimio ya kuhakikisha yanatengwa maeneo maalum ya vijana ambayo tuliyapa jina la *Youth Special Economic Zone.* Lengo la kutenga maeneo haya ni kuwapatia fursa ya kujiajiri vijana ambao wako tayari kufanya shughuli za kibiashara na ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, ninavyozungumza hivi sasa zimeshatengwa takribani ekari 85,542 nchi nzima kwa ajili ya vijana. Vivyo hivyo nimezungumza katika majibu yangu hapa wakati nahitimisha hoja. Tukitambua kwamba sekta ya kilimo ni kati ya sekta ambazo zitawaajiri watu kwa wakati mmoja; Serikali ya Awamu ya Tano imetoa msisitizo mkubwa, kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tumekuja na mpango mkakati wa kilimo wa kuwahusisha vijana, ambapo tunafikiria kwenda kuyatenga mashamba makubwa yale ya Serikali, zamani yalikuwa hayatumiki kwa ajili ya shughuli za vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimetoa na mfano hapa Mheshimiwa Esther, pale Morogoro eneo la Mkulazi na Mbigiri vinakwenda kujengwa viwanda viwili vya sukari ambapo katika eneo lile tunazo ekari 63,000, katika hizo ekari tumewachukua vijana kama ndio *outgrowers.* Kwa hiyo, naamini kabisa tuna uwezo wa kutengeneza zaidi ya ajira 100,000 kupitia kilimo na pale Morogoro, hatutawachukua vijana wa Morogoro tu. Tumesema maeneo yote ya karibu ambako vijana wanaweza wakalima muwa na wakaufikisha Morogoro ndani ya masaa 24 sisi tutakuwa tayari kuwasaidia ili wawe na soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hatujawaacha vijana tunawathamini na hiyo ndio *commitment* ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niko kwenye Fungu hilo hilo; lakini naomba uniruhusu niipongeze sana Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa sababu ya kazi nzuri sana iliyofanya wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu ni la Sera. Kwa sababu mwaka 2015 vijana hawakuweza kupiga kura kwa sababu ya takwa la umri; katika uchaguzi ujao mwaka 2020 nina uhakika vijana wengi na hata wale ambao hawakuweza kupiga kura, watapiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, Serikali imejipanga namna gani hasa katika kuboresha daftari la wapiga kura? Kama sitaweza kupata majibu sahihi, kuhusu kuboresha daftari la wapiga kura nitaondoa Shilingi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi kuhusu jambo hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi ya pekee kumpongeza sana Mheshimiwa Ndassa kwa kukumbuka zoezi hili la uchaguzi ambalo ni muhimu sana; ambalo hata sisi Wabunge kupitia Tume ya Uchaguzi ndipo tumeweza kuingia ndani ya Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo ,Tume ya Uchaguzi ni chombo muhimu cha kusimamia uchaguzi katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi Tume ya Uchaguzi inatakiwa ifanye maboresho ya daftari la wapiga kura mara mbili katika kipindi cha miaka mitano tangu uchaguzi mmoja unapofanyika na kabla ya uchaguzi mwingine unapofika. Maana yangu ni nini? Tume ya Uchaguzi inatakiwa iboreshe daftari la wapiga kura kati ya mwaka 2015 na mwaka 2020, liwe limeboreshwa mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha uliopita wa 2016/2017, Serikali haikutenga fedha za uboreshaji wa daftari. Ili kuhakikisha kwamba hao vijana anaowasema Mheshimiwa Ndassa wanaingia kwenye daftari kwa ajili ya kuandaliwa kuwa miongoni mwa watakaopiga kura katika nchi yetu kwa Sheria ya Uchaguzi; mwaka huu wa fedha Serikali imetenga fedha ya kuanza maandalizi ya kuboresha daftari la wapiga kura kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ndassa kwamba tumetenga fedha hiyo, isiyopungua bilioni tisa na fedha hiyo sasa itaanza

kushughulikia maandalizi ya kuboresha daftari letu ili tuweze kukidhi vigezo vya Sheria ya Uchaguzi, ya kuboresha daftari letu na kuwafanya vijana na wale wote ambao kadi zao zimepotea na hawakupata nafasi ya kujiandikisha waweze kuwa kwenye daftari la kupiga kura tayari kwa uchaguzi unaofuata wa nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Ndassa shilingi yangu aniachie tu nikale mshahara wangu na watoto wangu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndasa unamrudishia Shilingi?

**MHE. RICHARD M. NDASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameyasema, basi nimwombe tu kwa sababu ametamka mbele ya Bunge lako Tukufu, mbele yako Mheshimiwa Mwenyekiti, ambaye ni Spika wetu; na ili vijana wetu ambao hawakupata nafasi ya kupiga kura kwa sababu ya umri na sasa wameshafikia umri na kwa sababu ni haki yao ya Kikatiba kupiga kura na kupigiwa kura, naomba basi Serikali hili walilolisema walitekeleze ili vijana wetu hawa waweze kupiga kura katika uchaguzi ujao. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi. Niko kwenye Fungu hilo hilo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, *Vote* hiyo ya 37. Nataka tu nipate ufafanuzi toka kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhusiana na suala la Ofisi za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 70 ya Waheshimiwa Wabunge hawana Ofisi kwenye Majimbo yao. Kitendo cha Waheshimiwa Wabunge kutokuwa na ofisi kinawafanya Wabunge kushindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inasema wazi kabisa kwamba, Serikali ita-*provide* ofisi kwa ajili ya Wabunge na si

Bunge lita-*provide* ofisi. Kwa hiyo, tunaomba tujue, kwamba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambako kuna masuala ya Sera na Uratibu, kwenye masuala ya kupata ofisi, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunawezaje kupatiwa Ofisi ili tuweze kufanya kazi zetu za kuwawakilisha wananchi wetu kwenye Majimbo yetu kwa ufanisi ? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana dada yangu Magdalena Sakaya kwa jinsi anavyowajibika na kufanya kazi vizuri sana za kuwawakilisha wananchi na Watanzania kwa ujumla. Amekuwa mwanamke jasiri miongoni mwetu sisi Wabunge na yeye anafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Sakaya kwamba masharti ya kazi ya Mbunge, kama nitakuwa nina kumbukumbu sawasawa, Kifungu cha 14 kinatutaka Serikali tufanye kazi ya kuhakikisha kwamba, kila Mbunge anapata ofisi ya kufanyia kazi na hasa kazi ya kuwawakilisha wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Ofisi za Waheshimiwa Wabunge hapa katikati limekuwa na mwelekeo wa namna moja na nyingine na hasa katika majadiliano baina ya Tume ya Huduma za Bunge na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa niaba ya Serikali juu ya namna ipi nzuri ambayo itawasaidia Waheshimiwa Wabunge kupata ofisi na ili ofisi zile ziweze kuwasaidia katika kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 2005/2008 kulianzishwa mradi mkubwa sana wa ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge, mradi ule kwa bahati mbaya ulikuwa haujakamilika. Hata hivyo kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge tayari mradi ulishakamilika na ofisi wanazo na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge mpaka sasa hawana ofisi, hivyo takwa la masharti ya kazi ya Mbunge halijatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuliambia Bunge lako Tukufu, kwamba Serikali tumeomba sasa kuwa na mazungumzo ya kina baina yetu sisi na Tume ya Huduma za Bunge ili sasa tufikie muafaka wa kujua nini kifanyike. Je, ofisi hizi zihudumiwe chini ya Tume ya Bunge ama zibaki kwetu Serikalini? Kama zinabaki kwetu Serikalini, basi Serikali iendelee na jukumu lake moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, wakati akijibu hoja mbalimbali zinazohusiana na Ofisi za Waheshimiwa Wabunge hapa ndani ya Bunge lako, aliendelea kusisitiza kwamba kwa sasa Waheshimiwa Wabunge wataendelea kuhudumiwa kwa kupatiwa ofisi kwenye maeneo yao kwa kusimamiwa na Ofisi zetu za Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Kwenye maeneo ambayo hayana ofisi Wakuu hawa wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wataendelea kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge kuona ni namna gani nzuri ya kuwafanya waweze kuendelea na huduma zao na wapatiwe ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tunaendelea kulishughulikia jambo hili na baada ya muda si mrefu tutakuwa tumefikia muafaka na tutakapofikia muafaka basi Ofisi za Waheshimiwa Wabunge zitatolewa kwa kuzingatia masharti yatakayokuwepo, pia na makubaliano ya utendaji wa kazi ndani ya Serikali na Tume ya Huduma za Bunge.

**MWENYEKITI:** Tukushukuru sana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimwambie dada yangu Mheshimiwa Waziri kwamba, Waheshimiwa Wabunge kupatiwa Ofisi kwenye Ofisi za Mikoa haiwezekani. Kwa sababu kwa mfano mimi niko Kaliua, kutoka Kaliua mpaka Mkoa wa Tabora kuna kilometa karibu 120. Kwa hiyo, nikiwa Mkoa wa Tabora kule katikati ya mkoa nikipatiwa ofisi pale ina maana siwezi kuwahudumia vizuri wananchi wa Wilaya ya Kaliua; *same applies* kwa Waheshimiwa Wabunge wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu wa kwamba, mikoa iwapatie Waheshimiwa Wabunge Ofisi haiwezekani kwa utendaji wa kazi ambazo...

**MWENYEKITI:** Yaani mikoa, maana yake ni kwamba kwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo kama utapatiwa ofisi na *DAS,* ndiyo maana ya neno mikoa. Kwa hiyo, si Tabora Mjini, ni Kaliua kulekule.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba tu ni kwamba, Serikali itupatie ofisi kwa sababu, kuwapa lile jukumu Ofisi ya *DAS* ama Mkuu wa Mkoa kiukweli ni kitu ambacho hakiwezekani.

**SPIKA:** Ahsante. Ushauri umefika, ni ushauri wa kufanyiwa kazi. Mheshimiwa Kiteto Koshuma!

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niongelee suala zima la maafa kwa kuwa ni suala la Kisera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maafa mengi yalitokea hapa nchini hususan maeneo ya Kagera ambako kulitokea tetemeko la ardhi, lakini pia hata Mkoa wa Mwanza maeneo ya Ukerewe pia nako kulitokea mafuriko na maeneo mengine mbalimbali; hata hapa tu karibuni ambapo bado hawajasahau, hapo Chalinze kwenye Jimbo la Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete pia, palitokea mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mwaka 2015 ya maafa inataka kuwepo na kituo kikubwa cha kuweza kuangalia haya masuala mazima ya maafa katika nchi hii ya Tanzania. Naomba kupata ufafanuzi wa Serikali, je, ni lini kituo hiki kikubwa cha kuhudumia masuala ya maafa kitaanzishwa ili kuweza kusaidia wananchi wanapopata maafa? Nashukuru.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru na

nimpongeze sana Mheshimiwa Kiteto. Kwa kweli kama mama nadhani anajali sana mambo ya huduma za jamii na hasa pale matatizo makubwa kama ya maafa yanapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, mwaka 2015 tulipitisha hapa sheria mpya ambayo itahudumia masuala yote ya maafa katika nchi yetu ya Tanzania. Sheria ile inaitaka Serikali kuanzisha kituo kikubwa ambacho kitakuwa ni *coordination centre* ambacho kitashughulikia masuala ya maafa katika nchi nzima ya Tanzania. Hiyo *coordination centre* ambayo inatakiwa ianzishwe kwa mujibu wa sheria kazi yake kubwa itakuwa ni kufanya *coordination* ya maafa katika nchi nzima kwa kushirikiana na taasisi ambazo zimetajwa katika Sheria hiyo ya Maafa ya Mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mpango wa Serikali ambao Mheshimiwa Mbunge anausema. Ni kweli mwaka jana tulizungumza hapa Bungeni, kwamba ni lazima sasa Serikali tumefanya maamuzi ya kuhakikisha tunajenga hiyo *centre* kwa ajili ya kufanya *coordination* ya masuala ya maafa makubwa katika nchi yetu. Naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali imeshaanza hatua za awali, tayari tumeshapata eneo la kujenga kituo hicho hapa Dodoma na tayari eneo limeshapimwa na limeshakabidhiwa kwenye mikono ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaanza sasa mazungumzo na *development partners* wetu na tayari wako baadhi yao wameshajitokeza ili tuweze kushirikiana kwa pamoja tuweze kujenga hiyo *centre* kubwa ambayo itakuwa *equiped* na zana zote ambazo zinaweza zikatusaidia kufanya kazi hiyo ya kuhudumia na kutoa huduma ya kukabili na kurudisha hali wakati maafa yanapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye bajeti zetu ukiangalia kwenye *Development Book* yetu tumeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kutoa mafunzo, kwa ajili ya kuimarisha zile Kamati za Maafa kwenye ngazi za wilaya na mikoa. Vilevile tumeendelea kuwaandaa Watanzania wote ili maafa yanapotokea katika hali moja ama nyingine

waweze kujua zile mbinu za awali za kuweza kukabiliana nayo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Koshuma kwamba Serikali imeanza kufanyia kazi agizo hilo la Kisera lakini pia la Kisheria na hivyo basi tutaendelea kutoa taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kila mara jinsi tunavyoweza kuendelea kupiga hatua kufikia lengo hilo jema la Serikali yetu na tuna uhakika kwamba tutafika kule tunakofikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Koshuma bado tu?

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu hayo ya Serikali ambayo yanaonesha namna Serikali inavyotambua suala hili la maafa na jinsi gani linawaathiri wananchi wa Tanzania, naomba tu niseme kwamba, naiomba Serikali iweze kuonesha *seriousness* katika suala zima la kuanzisha kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu, kuanzishwa kwa kituo hiki kutaweza kusaidia hata kuratibu michango ambayo inatolewa na Watanzania pale ambapo maafa yanatokea, lakini tukipanga halafu tusifanye tutakuwa ni kama tunapeleka picha nyingine kabisa kwa Watanzania; kwa sababu maafa yanakuwa yanatokea, Watanzania wengi wanapoteza maisha na watu wanaharibikiwa nyumba. Kule Ukerewe familia karibu mia moja sitini na kitu zilikosa makazi. Hivyo basi, naomba kwamba, japokuwa Serikali imesema, lakini naomba iweke *commitment* kwamba ni lini hasa? Kwa sababu ukiangalia nilipokuwa naanza niliuliza ni lini? Naomba iseme na nisiporidhika basi, mimi nitashikilia shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Koshuma ushike Shilingi kwa ni lini tu? Kifupi sana Mheshimiwa Waziri, tuweze kuvuka!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Mheshimiwa Koshuma aniamini,ini

kwamba, sio ni lini, Serikali imeshaanza tayari, yaani tayari tumeshaanza, tumeshapata eneo Miyuji na kupata tu eneo Miyuji ni kwamba, tayari Serikali imeshaanza. Kwa hiyo kama tumeshapata eneo hiyo ni *commitment* kubwa ya Serikali kwamba, iko *serious* na jambo hili inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tumeshaanza mazungumzo na *development partners,* tumeshakuwa na vikao na Balozi kama mbili. Kwa hiyo, ni tayari kwamba, Serikali imeshaji-*commit* na imeanza kufanya hiyo kazi. Nimwombe dada yangu Mheshimiwa Koshuma akubaliane na mimi kwamba, Serikali inalifanyia kazi jambo hili.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi wa tiba za dawa za kulevya kwa sababu katika nchi yetu ya Tanzania katika mikoa mingi watoto wetu wengi wameathirika na dawa za kulevya. Sasa kuna dawa ambayo Serikali inagawa katika vituo baadhi ya maeneo, ugawaji wa dawa ya *methadone,* sasa mikoani huko watoto hawawezi kupata na wamepata tabu nao vilevile. Je, Serikali imejipangaje kwenye mpango wa kuweka kuweka vituo ndani ya mikoa yetu ili hizo dawa ziweze kupatikana? Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa sana Mheshimiwa dada yangu Anna kwenye eneo hili la waathirika wa dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania. Baada ya kufanya tafiti ambazo tumekuwa tukiendelea nazo tumegundua iko mikoa takribani sita inauathirika mkubwa wa matumizi ya dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Serikali imefanya maamuzi magumu, imeamua sasa tuanze kutoa tiba ya *methadone* katika mikoa mingine; wakati Mkoa wa Dar-es-Salaam ukiendelea. Pia tumeamua kupanua wigo na kupeleka hii tiba ya *methadone* katika hospitali nyingine ndani ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba tunaanza kutoa huduma kwenye mikoa iliyoathirika zaidi na dawa za kulevya tumeandaa miundombinu ambayo ni rafiki kwa ajili ya huduma hiyo. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kushirikiana na Wizara ya Afya tutaanza sasa kutoa tiba ya *methadone* katika Mikoa ya Mbeya, Morogoro na hapa Dodoma, vile vile tutaendelea Mwanza, Kilimanjaro na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo yote ni kusogeza huduma ya tiba hii ya *methadone* ili waathirika hawa wa dawa za kulevya waweze kupata hii tiba inayowasaidia kurudi kwenye kutengemaa na wanaweza wakaacha kabisa matumizi ya dawa za kulevya na wakaendelea kuwa raia wazuri na raia wema kama walivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie dada yangu Mheshimiwa Anna kwamba, kazi hiyo tunaifanya na naomba nimpongeze sana Mheshimiwa dada Anna kwa kazi hii nzuri na yeye amekuwa ni balozi mzuri wa kupambana na dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri kwa majibu mazuri, lakini madawa ya kulevya yameharibu sana watoto wetu na mikoa ambayo wameisema iko katikati na inakaribiana. Sisi kama Rukwa, Katavi, Kigoma, watoto wengi wameathirika sana. Je, Serikali itafanya mpango wowote hata ule wa karibu kwa wale watoto walioathirika katika mikoa ile, maana wengine hawana uwezo wa kufika katika hivyo vituo vikubwa kwa kuwa wazazi wao hawana uwezo na watoto wameathirika? Ni kitu kibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni lazima tuipongeze Serikali kwa jitihada kubwa ambazo wamezifanya kupinga kuhusu masuala ya dawa za kulevya, ni jambo baya, wototo wetu wameathirika sana, wameharibikiwa kabisa kisaikolojia, maisha yao yameshapotea kabisa. Basi Serikali kwa ile mikoa ambayo

iko pembezoni, tunaomba basi wajitahidi wale watoto waweze kupata hata ushauri nasaha ili waweze kuishi maisha ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tiba hii ya *methadone* ni tiba ya namna yake na ni tiba ambayo si rahisi sana, iko *very expensive*, ni ghali kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku tutakuja kuwapa taarifa kamili za tiba hiyo. Kipimo kidogo tu cha *mills* hata moja haifiki lakini gharama yake ni kubwa sana. Kwa hiyo, sisi tumeona kwamba ili kuwasaidia wale wa kwenye mikoa ya pembeni, kama anavyosema Mheshimiwa dada Anna kutoka kule Katavi, ukiweka kituo pale Mbeya wanaweza wakapata huduma pale Mbeya kwa urahisi kuliko ilivyokuwa zamani, watoke Mbeya wapelekwe na wazazi mpaka Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunachotaka kusema ni kwamba hatutaki kutumia tiba hii kama ni kichocheo cha kwamba mtu augue halafu tiba ipo ataenda kupata tiba, hapana! Tunaomba tu tutoe wito kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, kwa Maafisa Ustawi wa Jamii, kwa Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata, Waheshimiwa Madiwani, hata sisi Waheshimiwa Wabunge, kazi kubwa iwe ni ku-*prevent,* iwe ni kuwalinda vijana wetu wasitumie dawa za kulevya kuliko kufikiri kwamba kwa sababu tiba ipo wakiathirika watakwenda kupatiwa matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo, kwa kuzingatia na kuangalia uwezo wa Serikali, tunaweza hiyo *scale up program* tukaiendeleza na tunaweza tukafika katika mikoa yote nchini, lakini itachukua muda kwa sababu ya gharama, uandaaji wa miundombinu na hasa nia ya Serikali

ya kuwafanya vijana wasitumie dawa, kuliko kuwaaminisha kwamba tiba ipo watumie dawa halafu wakapate tiba.

**MWENYEKITI:** Ahsante Sana. Kwanza itabidi kwa mamlaka niliyonayo niongeze muda wa nusu saa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002 - *Finance and Accounts............Sh.* 1,159,401,005/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning................Sh.* 4,586,648,633/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit...................Sh.* 301,489,605/=
Kif. 1005 - *Govt Communication Unit..........Sh.* 178,281,474/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit...Sh.* 310,334,576/=
Kif. 1007 - *Legal Service Unit*...................Sh. 170,121,498/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1008 - *Management Info. System Unit* Shs...232,618,838/=

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwenye *subvote* 1008, *subvote* ndogo 220600 *training – domestic*.

**MWENYEKITI:** Rudia Mheshimiwa Waziri hajakupata.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kifungu 220600.

**MWENYEKITI:** Tuko 1008.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvotes* 1008, kifungu kidogo cha 220800 nina hoja hapo.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa, 220800 mafunzo ya ndani

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, mafunzo ya ndani. Inaonesha kwamba 2016/2017,

kulikuwa na fedha ilitengewa Sh. 1,500,000, lakini ukirudi tena nyuma ilitengwa Sh. 920,000, lakini mwaka huu kuna Shilingi sifuri. Sasa nikataka nijue hii shughuli ambayo ilikuwa inafanyika hapa imeahirishwa au imewekwa shughuli nyingine ndio nahitaji maelezo hapo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu ni kwa ajili ya *training-domestic;* wale ambao walikuwa *trained* kwa kifungu hiki walishamaliza masomo yao. Kwa hiyo, hakuna haja ya kuendelea kutengea watu ambao hawapo shuleni tena*. (Makofi)*

*(kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Civil Affairs and Contingencies*……Sh.146,123,699/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, kifungu gani!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 2001.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihoji kifungu kidogo cha *social assistance benefits in kind.* Kwa uelewa wangu ni fedha kwa ajili ya maafa lakini fedha hizi zimepungua ilhali wananchi wengi kipindi hiki msimu wa kilimo hawakuweza kulima kwa sababu mvua zilichelewa. Tutegemee kwamba hali ya chakula itakuwa si nzuri na *NFRA* wamekuwa wakitengewa fedha chini ya kifungu hiki lakini fedha hizi zimepungua. Nipate ufafanuzi kwa nini fedha hizi zinapungua wakati hali si nzuri?

**MWENYEKITI:** Ilikuwa inanipa tabu kidogo kwa sababu mwaka jana bilioni tatu na laki sita na mwaka huu bilioni tatu na laki sita; japo kuna punguzo lakini punguzo sio *significant.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wewe kwamba punguzo hili si kubwa; lakini naomba tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapotenga fedha kwenye kifungu hiki si kwamba ndiyo tunakuwa tumetenga fedha ya maafa, labda fedha yote ambayo itashughulikia chakula na *rescue* ya chakula na vitu vyote. Sisi tunatenga kwenye kifungu hiki kwa ajili ya misaada ya dharura chini ya idara ya maafa, lakini Wizara ya Kilimo itatenga fedha chini ya *NFRA* kwa ajili ya ununuzi wa mahindi, mtama na mchele kwa ajili ya hifadhi ya chakula kama kutatokea maafa mengine yoyote, tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile zipo taasisi nyingine za Serikali ambazo zote kwa pamoja huwa tunafanya kazi ya kutoa huduma ya dharura maafa yanapotokea. Kwa hiyo, taasisi hizo kwenye Wizara nyingine nazo zinatenga hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia hakuna tofauti kubwa lakini utendaji kazi wa Serikali unategemeana taasisi moja na nyingine. Sisi tunatenga hii, Wizara ya Kilimo watatenga, Wizara nyingine watatenga na mwisho wa siku kwa pamoja tunafanya hiyo kazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *National Festivals* ....................Sh. 304,035,090/=
Kif. 3001 - *Parliamentary and Political Affairs*......................................Sh. 494,836,794/=
Kif. 4001 - *Private Sector Dev't and Eco Emp*.................................Sh. 2,779,805,872/=
Kif. 5001 - *Coordination of Govt Business*......Sh. 700,678,345/=
Kif. 7001 - *Government Printer* ..............Sh. 2,545,358,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 25 - OFISI BINAFSI YA WAZIRI MKUU**

Kif. 1001 - *Admin and HR Management*...Sh. 5,923,228,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 15 – TUME YA USULUHISHI**

Kif. 1001 - *Admin and HR Management*.....Sh. 3,409,750,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud, peke yako.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mshahara wa Waziri sikupata kwa hiyo wacha niaze na hapa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo katika *subvote* 1001, lakini naenda kwenye *item* 410600 *Acquisition of Office and General Equipments.*

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Rudia tena.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 1001, *item* 410600.

**MWENYEKITI**: 410600. Mmm! Endelea.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Randama inaeleza kwamba tangu mwaka 2016/2017 kutoka 5,500,310/= mpaka 119, 000,000/= ni kwa ajili ya ununuzi wa *computer* na *photocopy machine* na *server,* lakini ni kwamba randama zilizopita zilikuwa zinaeleza na ndiyo hoja zaidi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; kwamba ni vyema wataje wanataka kununua *computer* ngapi. Wakasema kwenye manunuzi ndiko kwenye ufisadi. Kwa hiyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mara nyingi huwa

anasema kwamba hata kama fedha imewekwa milioni 119 mnataka kununua *server,* idadi ni kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ya msingi hapa ningependa kufahamu, kwamba kama hautatokea ubadhirifu wa kununua *computer* mbili, tatu au moja kama ambavyo mdhibiti ameliona kwenye ripoti zake mbalimbali. Nataka nipate ufafanuzi, idadi hii mnataka kununua *computer* ngapi tuelewe? Kwa sababu hili jambo limekemewa sana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwamba hamsemi mnaweka mlango wazi. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi na lakini pia kwenye mshahara wa Waziri umeninyima vibaya mno leo. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Hilo swali lako si ungeenda kwenye randama uangalie bwana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama Mheshimiwa Mbunge angekwenda kwenye randama ambazo tuliziwasilisha hapa mezani angeona. Fungu hili la 15 ni Tume ya Usuluhishi na Uamuzi na kifungu hicho anachokizungumzia hicho ndicho kinachotumika kwa ajili ya kugharamia; ukiacha hizo *computer* na mashine za kudurufu, ni kifungu ambacho kinatumika kwa ajili ya kuchapa maamuzi, kushughulikia mwenendo wa kesi na mashauri mbalimbali. Kwa hiyo, ni kifungu ambacho kinatumika kwa ajili ya kusimamia shughuli zote za kesi ambazo zinafanyika kwenye ile Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 27 – MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Kif. 1001 - *Admin and HR Management*.......Sh. 587,169,000/=

**MWENYEKITI:** Ukurasa 115, *subvote* 1001, *administration.* Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niende moja kwa moja kwenye *subvote* 1001, hoja yangu inaenda kwenye *item* 260600.

**MWENYEKITI:** Nimekupata, endelea.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Ningependa kupata maelezo, pamoja na majibu ya Waheshimiwa Mawaziri kwamba fedha imehamishiwa kwenda sehemu nyingine, maana mara nyingi hupata majibu hayo; ningependa kupata maelezo kwa nini sasa hivi imewekwa sifuri? Mbali ya kauli hiyo mnasema kwamba fedha hii imewekwa katika fungu lingine, hapana, nataka hii *specific* mnipe jibu la kweli.

**MWENYEKITI:** Hii si ni ile mnayogombea Mheshimiwa Masoud au hii nyingine? Mheshimiwa Waziri wa Nchi! Wameona mnatoana roho. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Masoud kwa kuona kwamba kumbe kuna umuhimu wa ruzuku ya vyama kutengwa kwenye bajeti ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako sasa naomba nimpeleke Mheshimiwa Masoud ukurasa wa 118, *subvote* 1010, kifungu kidogo cha 260600, ndio kumewekwa ruzuku ya vyama. Sasa nimwombe tu Mheshimiwa Masoud, basi akubali tu kwamba kuna umuhimu wa ruzuku kwenye vyama na sisi tumeona hilo na tumeiweka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Account Unit*.........Sh. 191,894,000/=
Kif. 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*..............................Sh. 70,169,500/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*.....................Sh. 100,248,000/=

Kif. 1005 - *Proc. and Management Unit*......Sh. 92,662,000/=
Kif. 1006 - *Info. and Com. Technology*...........Sh. 78,578,000/=
Kif.1007 - *Govt Communication Unit*...........Sh. 80,103,000/=
Kif. 1008 - *Registration of Political Parties*......Sh. 231,390,000/=
Kif. 1009 - *Election Expenses and Civic Ed*....Sh. 230, 240,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1010 - *Monitoring of Political Parties Unit*...............................Sh. 17,722,277,500/=

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Naomba nipate ufafanuzi wa kina kuhusu kijifungu hicho kidogo 260600 ambacho ni ruzuku ya vyama vya siasa bilioni 17 ambacho kimehamishwa kutoka ukurasa wa 115 kwenda ukurasa wa 118. Kwamba Serikali inatenga fedha hizi na Bunge tunapitisha lakini fedha hizi zinapelekwa kwenye vyama vya siasa ilhali kazi ya vyama vya siasa ambayo ni kazi mahususi imekatazwa na Serikali haijatoa kauli juu ya mikutano ya vyama vya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana miongoni mwa kazi za fedha hizi ni mikutano ya vyama vya siasa. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu alisema mikutano ya Wabunge inaruhusiwa lakini tunatenga fedha za walipa kodi kwa ajili ya ruzuku ya vyama vya siasa. Nipate kauli, hii mikutano inaruhusiwa lini na nisiporidhika nitatoa hoja ya kuondoa shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sijakupata vizuri unavyojaribu ku-*link* fungu hili ni kwa ajili ya ruzuku za vyama vya siasa. Sasa tatizo ni nini? Kwa hiyo, pendekezo lako unashauri kwamba iwe sifuri au unashaurije kwa maana ya fedha hizi? Maana tupo kwenye mafungu hapa, fungu limezidi, limepungua au lipo la kawaida?

**MHE.PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kuondoa shilingi kwa mujibu wa kanuni zetu 102 kama

sikosei ni kwamba unaonesha kutokuridhishwa kama hujapata majibu. Kuondoa Shilingi maana yake unaruhusu Wabunge wenzio wajadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe nijibiwe kama sijaridhika Waheshimiwa Wabunge wenzangu wajadili kwamba fedha hizi zinatolewa kwenye vyama vyetu vya siasa lakini vyama hivi vimezuiliwa kufanya kazi zao. Ni lini wataruhusiwa kufanya kazi zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Maelezo Mheshimiwa Waziri kwamba vyama vimezuiliwa kufanya kazi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza Waheshimiwa Wabunge tuelewane. Tunapofika kwenye fungu hili la ruzuku hatuji kutoa fedha kwa ajili ya vyama vya siasa kufanya mikutano, tunatoa ruzuku kwenye vyama vya siasa kuendesha shughuli zao za kawaida na shughuli ndani ya vyama vya siasa na ziko nyingi tu. Inawezekana ikawa ni shughuli labda za kukodi ofisi za vyama, kujenga uwezo wa viongozi ndani ya chama ama shughuli ya kutatua migogoro iliyopo ndani ya chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii Serikali inajali mfumo wa vyama vingi na ndiyo maana inaweka fedha hii ili kama watu hawana ofisi, kama vyama vingine ambavyo havina ofisi viweze kukodi ofisi zao na viweze kufanya shughuli zao za maendeleo. Sasa kama ni hoja ya mikutano kwenye kifungu hiki hakuna mahali utakapokuta sheria ya kufanya mkutano au ya kutokufanya mkutano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu niseme wewe utatuongoza lakini Serikali inaheshimu mfumo wa vyama vingi, inataka vyama visivyoweza kujenga ofisi vikodi, visivyokuwa na hela ya kusaidia mafunzo vifanye na visivyokuwa na watumishi viweze kuwapata. Kwa hiyo, majibu yangu ni kwamba fungu hili ni muhimu sana katika kuendesha shughuli za vyama. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kabisa kwamba niondoe Shilingi ili Wabunge wenzangu wajadili kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza haki ya vyama vya siasa kufanya mikutano ni haki ya kikatiba na ni sheria yetu ya mwaka 1992 Sheria Na. 5, lakini leo Waziri hawezi akatupangia kwamba tukakodi Ofisi; akatupangia majukumu ambayo yako kisheria na kikatiba. Ndiyo maana tukahoji Bunge tunapopitisha fedha hizi, hizo shughuli zote lazima zikafanyike na ndiyo maana fedha hizi zinakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtuambie Mheshimiwa Waziri, tatizo lililopo ni kwamba mmezuia mikutano ya vyama vya siasa na mmekuwa mkisema kwamba Wabunge mmeruhusiwa kwenda kufanya mikutano; ni Mbunge yupi? Mgombea binafsi humu ndani hayupo, wote tunatokana na vyama vya siasa. Mnapozuia vyama vya siasa visifanye kazi zao ni kosa la kisheria. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mimi sitaki tubishane sana, niombe Wabunge wenzangu wajadili, nitatoa hoja ili tupatiwe majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline, hilo kwanza silikubali na siliruhusu kabisa kwa sababu; kaa kabisa mama uzime hiyo *microphone*. Kwa sababu je vyama vya siasa visipopata ruzuku hii kwa hiyo sasa ndio itakuwa wameruhusiwa kufanya mikutano kwa sababu wao hawapati ruzuku? Yaani ruzuku hii unai-*link* na kitu ambacho... Ingekuwa ruzuku hii ni kwa ajili ya hao na kwa ajili ya vyama vya siasa peke yake hapo ingekuwa sawasawa. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1011 - *Office of Deputy Registrar – Znz* ...Sh. 141,207,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 42 – OFISI YA BUNGE**

**MWENYEKITI:** Hili mtu akipinga namtoa kabisa nje ya Ukumbi kabisa. Katibu soma *(Kicheko)*

Kif. 1001 - *Admin and HR Management*.....Sh. 7,204, 389,000/=

**MWENYEKITI:** Ni Gekul peke yake anayepinga hiki kifungu! Haya Gekul, karibu Pauline.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni cha kwako, mshahara wako.

**MWENYEKITI:** Anataka kushika mshahara wa Spika.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia hiyo; lakini napenda kupata ufafanuzi, pamoja na jitihada ambazo zimefanywa katika Fungu hili la 42 la Bunge kuongeza fedha kwa ajili ya Kamati zetu kutoka milioni 55 mpaka 300, lakini kutujengea lifti kwa zaidi ya bilioni tano katika Jengo la *Administration* na vitu vingine, napenda kufahamu, kuna suala ambalo Wabunge tumekuwa tukilizungumza kuhusu ongezeko la fedha za Mfuko wa Jimbo. Naomba nifahamu tu, kwa sababu ndiyo mahali pake na ni *vote* yake, ongezeko hilo liko wapi, hiyo *review* imeshafanyika? Kuangalia vile vigezo mmeshafanya? Pia kama mnategemea kuongeza, maana nimepitia na kwenye randama nimepita sijaona, nipatiwe ufafanuzi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline, uko kwenye *subvote* ipi?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo hiyo ya kwako.

**MWENYEKITI:** Halafu kifungu kidogo kipi?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 1001.

**MWENYEKITI:** Teremka chini zaidi, kipi sasa ili twende pamoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *total* yake ni bilioni saba. Kwa hiyo ni *subvote* ya kwanza kabisa. Nataka kupata ufafanuzi, fedha za...

**MWENYEKITI:** Ipi Mheshimiwa Pauline?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea hoja mahususi kwa *Vote* ya Bunge, 42, ya kwanza kabisa mshahara wako hapo, hela za Mfuko wa Jimbo zimeongezwa?

**MWENYEKITI:** Iko wapi?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, humo humo.

**MWENYEKITI:** Makatibu kama mnaona hebu niambieni anachosema kiko wapi. Halafu hata hivyo hela za Mfuko wa Jimbo *(CDCF)* si ndiyo? Wala haziwagi huku Bungeni, zinakuwa mahali fulani hivi huko, mtu mwenyewe amenyamaza kimya.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002 - *Library and Research Dep*.............Sh. 289,176,000/=
Kif. 1003 - *Info.and Com. Technology*..........Sh. 546,420,000/=
Kif. 2001 - *Budget Department*...... ..........Sh. 1,641,336,000/=
Kif. 2002 - *Table Office Department*.........Sh. 84,068,746,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 *Parliamentary Committees Dep*..... 10,805,602,000/=

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo katika *Subvote* 2003, *Parliamentary Comittees Department,* hapa ndipo penye Kamati hizi, safi sana kabisa. Nipo katika *item* 221000 *Travel-In-Country,* nimefurahi sana kuona kwamba mwaka wa fedha 2016/2017 kulikuwa na *1.4 billion* mara hii kuna *3.4 billion,* jambo zuri ambalo nimefurahi sana na ukiangalia randama inasema kwamba usafiri wa anga wa ndani kwa Wabunge, magari; lakini wewe mwenyewe ulisema hapa kwamba tatizo kubwa ni upatikanaji wa fedha ili shughuli zetu za Bunge kama Wabunge ziweze kufanikiwa. Napenda kupata uthibitisho kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, fedha hizi kweli zitapatikana tutafanya kazi vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu hayo tu basi.

**MWENYEKITI:** Nikuongezee kidogo, tatizo si upatikanaji wa fedha, fedha tunapata, lakini tunahitaji kupata kwa wakati.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mwenyekiti ambaye ni Spika akisharekebisha swali na kuliweka vizuri ili lieleweke vizuri na Serikali, kwa kweli ni lazima kulijibu kwa ufasaha. Kwa kweli ni *commitment* ya Serikali kuhakikisha tunajitahidi kadiri tunavyoweza kuhakikisha fedha zinalifikia Bunge kwa wakati ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufanya kazi zao bila kupata usumbufu wowote. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2004 - *Hansard Department* ……..….Sh. 1,151,443,000/=
Kif. 2005 - *Legal Counsel Department* ……Sh.1,043,654,000/=
Kif. 3001 - *Private Office of the Speaker* …….Sh. 748, 992,000/=
Kif. 3002 - *Private Office of the Deputy*

*Speaker* ........................................Sh. 410,668,000/=
Kif. 3003 - *Office of the Leader of Opposition*.....................................Sh. 474,456,000/=
Kif. 3004 - *Private Office of the Clerk* .........Sh. 964, 428, 000/=
Kif. 3005 - *Finance and Account Department*.................................Sh. 439, 026,000/=
Kif. 3006 - *Int. Relations and Protocol Department*..............................Sh. 2,129,748,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwisha, sasa Katibu tuendelee na utaratibu wa *guillotine.*

Kif. 3007 - *Information, Education and Communication*............................................Sh. 0/=
Kif. 3008 - *Internal Audit Unit*......................Sh. 237,948,000/=
Kif. 3009 - *Procurement Management Unit*...Sh. 406,328,000/=
Kif. 3010 - *Defense and Security Unit* ...........Sh. 228,912,000/=
Kif. 3011 - *Estate Management Unit*.........Sh. 1,457,786,000/=
Kif. 3012 - *Zanzibar Directorate* .................Sh. 203,204,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 61 – TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

Kif. 1001 - *Admin and HR Management*.....Sh. 2,053,364,359/=
Kif. 1002 - *Planning Monitoring and Evaluation Division*..........................................Sh. 288,928,997/=
Kif. 1003 - *Finance and Accounts Unit*.......Sh. 344,758,042/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*.....................Sh. 285,230,267/=
Kif. 1005 - *Legal Services Unit*.....................Sh. 275,010,267/=
Kif.1006 - *Proc. Mgt & Logistics Unit*............Sh. 370,773,267/=
Kif. 2001- *Election Mgt Division*.....................Sh. 301,178,267/=
Kif. 2002 - *Permanent National Voters Reg Sys Division*.............................Sh. 508,187,267/=
Kif. 2003 - *Voters Educ. & Public Info Division*......................................Sh. 336,863,267/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 65 – KAZI NA AJIRA**

Kif. 1001 - *Admin and HR Management*...Sh. 3,119,736,761/=
Kif.1002 - *Finance and Accounts*................Sh. 220,215,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*...................Sh. 206,555,333/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* ....................Sh.108,160,000/=
Kif. 1005 - *Procurement Mgt Unit*...................Sh.59,535,333/=
Kif.1006 - *Govt Communication Unit* ...........Sh.91,276,667/=
Kif. 1007 - *Info and Communication Tech Unit*.............................................Sh. 20,000,000/=
Kif. 1008 - *Legal Service Unit*........................Sh. 20,000,000/=
Kif. 2001 - *Labour*...............................Sh. 6,258,252,239/=
Kif. 2002 - *Employment Division*...............Sh.1,874,711,580/=
Kif. 2003 - *Registrar of Trade Unions*..............Sh.106,766,667/=
Kif. 2004 - *Arusha Regional Labour Office*.........Sh. 2,955,000/=
Kif. 2005 - *Dodoma Regional Labour Office*.....Sh.2,955,000/=
Kif. 2006 - *Geita Regional Labour Office* ..........Sh.2,955,000/=
Kif. 2007 - *Iringa Regional Labour Office*.........Sh. 2,955,000/=
Kif. 2008 - *Kagera Regional Labour Office*........Sh. 2,955,000/=
Kif. 2009 - *Kigoma Regional Labour Office* ......Sh. 2,955,000/=
Kif. 2010 - *Kilimanjaro Regional Labour Office*...Sh. 2,955,000/=
Kif. 2011 - *Lindi Regional Labour Office*............Sh. 2,955,000/=
Kif. 2012 - *Manyara Regional Labour Office*.....Sh. 2,955,000/=
Kif. 2013 - *Mara Regional Labour Office*.........Sh. 2,955,000/=
Kif. 2014 - *Mbeya Regional Labour Office*........Sh. 2,955,000/=
Kif. 2015 - *Morogoro Regional Labour Office*....Sh. 2,955,000/=
Kif. 2016 - *Mtwara Regional Labour Office* ......Sh.2,955,000/=
Kif. 2017 - *Mwanza Regional Labour Office*......Sh. 2,955,000/=
Kif. 2018 - *Njombe Regional Labour Office*......Sh. 2,955,000/=
Kif. 2019 - *Pwani Regional Labour Office*.........Sh. 2,955,000/=
Kif. 2020 - *Rukwa Regional Labour Office*.........Sh.2,955,000/=
Kif. 2021 - *Katavi Regional Labour Office*..................Sh. 0/=
Kif. 2022 - *Ruvuma Regional Labour Office*.......Sh. 2,955,000/=
Kif. 2023 - *Shinyanga Regional Labour Office*....Sh. 2,955,000/=
Kif. 2024 - *Simiyu Regional Labour Office*..................Sh. 0/=
Kif. 2025 - *Singida Regional Labour Office*......Sh. 2,955,000/=
Kif. 2026 - *Tabora Regional Labour Office*......Sh. 2,955,000/=

Kif. 2027 - *Tanga Regional Labour Office*.........Sh. 2,955,000/=
Kif. 2028 - *Temeke Regional Labour Office*......Sh. 2,955,000/=
Kif. 2029 - *Kinondoni Regional Labour Office*...Sh. 2,955,000/=
Kif. 2030 - *Ilala Regional Labour Office*...........Sh. 2,955,000/=
Kif. 2031 - *Social Security Division*...............Sh. 200,000,000/=
Kif. 2032 - *Youth Development*..................Sh. 300,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 91 – MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Kif. 1001 - *Admin and HR Management*.....Sh. 4,015,912,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 92 – TUME YA KUDHIBITI UKIMWI**

Kif. 1001 - *Policy, Planning and Research*......Sh.176,641,298/=
Kif. 1002 - *Finance, Admn and Resource Mob*...............................Sh. 984,579,441/=
Kif. 1003 - *Monitoring, Evaluation, Research and Mis*.............................Sh.150,000,000/=
Kif. 1004 - *Advocacy, Info, Education and Com.* .......................................Sh.100,780,000/=
Kif. 1005 - *District and Community Response*.......................................Sh. 606,752,000/=
Kif. 1006 - *Procurement Mgt Unit*..................Sh. 87,266,000/=
Kif. 1007 - *Legal Unit*...................................Sh.114,810,000/=
Kif. 1008 - *Management Inform. Systems*.........Sh. 98,412,261/=
Kif. 1009 - *Internal Audit Unit*.........................Sh. 120,933,000/=
Kif. 1010 - *Special Programs*......................Sh. 56,340,000/=
Kif. 1011 - *Government Comm. Unit*..............Sh. 32,090,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### FUNGU 37 – OFISI YA WAZIRI MKUU

Kif. 1001 - *Admin and HR Management*........Sh.5,000,000,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ..............................Sh.0/=
Kif. 2001 - *Civil Affairs and Contingencies*.....Sh.1,461,618,000/=
Kif. 4001 - *Private Sector Dev't and Eco Empowerment*..................Sh. 16,558,594,844/=
Kif. 5001 - *Coordination of Govt Business*....................................Sh. 43,145,159,919/=
Kif. 7001 - *Government Printer*....................................Sh. 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### FUNGU 42 – OFISI YA BUNGE

Kif. 1003 - *Info Com and Technology*..........Sh. 2,800,000,000/=
Kif. 2001 - *Budget Department*..................Sh. 200,000,000/=
Kif. 2004 - *Hansard Department*..............Sh. 1,200,000,000/=
Kif. 3011 - *Estate Management Unit*.........Sh. 3,000,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### FUNGU 61 – TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

Kif. 1001 - *Admin and HR Management*......Sh. 210,428,000/=
Kif. 1002 - *Planning, Monitoring and Evaluation Div*........................................Sh. 7,000/=
Kif. 1003 - *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 10,100/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*..........................Sh. 22,000/=
Kif. 1005 - *Legal Services Unit*....................Sh. 174,683,000/=
Kif. 1006 - *Procurement Mgt & Logistics Unit*.........Sh. 7,300/=
Kif. 2002 - *Permanent National Voters Reg Sys Division*...................................Sh. 9,481,330,600/=

Kif. 2003 - *Voters Educ & Public Info Divison...*Sh. 133,512,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 65 – KAZI NA AJIRA**

Kif. 1003 - *Policy and Planning*...............Sh. 1,400,000,000/=
Kif. 2002 - *Employment Division*..............Sh. 15,000,000,000/=
Kif. 2032 - *Youth Development*...............Sh. 1,000,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 91 – MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*.........Sh. 0/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 92 – TUME YA KUDHIBITI UKIMWI**

Kif. 1001 - *Policy, Planning and Research*.......Sh. 58,554,605/=
Kif. 1002 - *Finance, Admn and Resource Mob*...........................Sh. 3,049,060,440/=
Kif. 1003 - *Monitoring Evaluation Research and Mis*...........................Sh. 79,245,000/=
Kif. 1004 - *Adv, Info, Education and Com*.....Sh. 132,922,955/=
Kif. 1005 - *District and Community Response*...Sh. 25,450,000/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit* ..............Sh. 0/=
Kif. 1007- *Legal Unit*................................................Sh. 0/=
Kif. 1008 - *Management Information Systems*............Sh. 0/=
Kif. 1009 - *Internal Audit Unit*.....................Sh. 47,450,000/=
Kif. 1010 - *Special Programs*.....................Sh. 62,660,000/=
Kif. 1011 - *Government Communication Unit*...........Sh. 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Mtoa Hoja! *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU :** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa Taarifa kwamba Bunge lako lililokaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba sasa kutoa Taarifa ya Kamati ya Matumzi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2017/2018 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Hawa waliosema sio wanapinga mshahara wao wenyewe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana, tunakutakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yako pamoja na wasaidizi wako katika ofisi yako, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na maafisa wote ambao mpo pale Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunawatakia kila la heri katika utendaji wa kazi zenu tunaamini kabisa kwamba kwa uwezesho huu ambao Bunge limewapitishia, safari hii shughuli zenu zitakuwa bora zaidi na tunawatakia kila la heri kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Zitto Kabwe!

## TAARIFA

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 120 ambayo niliitolea Taarifa wakati natoa mchango wangu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusiana na masuala ya utekaji...

**SPIKA:** Subiri kidogo ili Wabunge wenye Kanuni zao waweze kufungua hapo 120.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, niisome?

**SPIKA:** Ngoja kidogo watu watafute hiyo Kanuni ya 120 ili tuwe wengi hapo. Nadhani tuko sawasawa, haya endelea kuisoma.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, niisome yote. Kanuni ya 120(2):-

*'Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya (1) ya Kanuni hii, baada ya kujadili hoja yoyote, Bunge linaweza kuunda Kamati Teule kwa madhumuni ya kushughulikia jambo lolote lililotokana na hoja hiyo kwa utaratibu ufuatao:-*

*(a) Baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa, Mbunge yeyote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya Kanuni hii anaweza kusimama mahali pake na kutoa taarifa ya mdomo kwamba anakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule;*

*(b) Mbunge ambaye anakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule atawasilisha taarifa ya hoja yake kwa kwa maandishi kwa Katibu na hoja hiyo itashughulikiwa wakati unaofaa kwa kuzingatia mpangilio wa shughuli kama ulivyoainishwa chini ya Kanuni ya 30(4)'*

Mheshimiwa Spika, baada ya mjadala wa Hoja ya Waziri Mkuu ambao, pamoja na mambo mengine, ulihusisha hoja mbalimbali kuhusiana na utekaji, uteswaji na mauaji ya raia mbalimbali, nilitoa maelezo kwamba nitaleta hoja ya kuunda Kamati Teule ili Bunge liweze kuchunguza kwa mapana vitendo vya namna hii ambavyo vinaendelea katika nchi yetu na kupendekeza hatua za kuchukua ili kuweza kumaliza vitendo vya aina hiyo. Kwa hiyo natumia Kanuni hiyo sasa kutoa taarifa rasmi ili uweze kuipangia muda tuweze kuileta ndani ya Bunge ijadiliwe na kuweza kuamuliwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Nimewaona Waheshimiwa, lakini kabla Spika hajasema chochote lazima Spika ashauriwe na mnaonishauri ni ninyi wenyewe.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Zitto Kabwe imezingatia utaratibu wa Kanuni zetu. Hata hivyo, bado kuna sintofahamu au kutokukubaliana kama jambo hilo analokusudia kulileta lijadiliwe na Bunge linaruhusiwa kujadiliwa au haliruhusiwi. Kwa sababu tu kwamba nimekuwa nikisikiliza sana na nimejitahidi kusikiliza hasa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani alipokuwa anajaribu kutaka Serikali na hasa akimtaka Waziri Mkuu aeleze kama kikosi hicho kinachodaiwa kwamba kinafanya utekaji kipo na kama kipo Waziri Mkuu atoe *statement* ya kukivunja.

Mheshimiwa Spika, sasa jibu la Serikali tumesema kwanza hakipo, lakini la pili, kama kitu hakipo sasa hatuzungumzi tena kukivunja. Kubwa kuliko haya yote ninayoyasema ni kwamba Serikali ina wananchi wengi sana na yapo matukio nchini hapa mengi sana yanayohusisha

mauaji ya watu. Wanauawa Wenyeviti wa Vijiji, Mkoa wa Pwani, wanauawa watu mipakani, wanauawa watu kwenye mapori na wapo watu wanaopotea. Katika maeneo yangu tu mimi, katika Bwawa la Mtera kuna watu wanaliwa na mamba wanapotea. Wapo watu wanaopotea kimsukule na baadaye wanapatikana, haya yote Serikali inaletewa taarifa kwamba iyachunguze na Serikali ndiyo itakayoambiwa kwa sababu kazi ya Serikali ni kulinda usalama wa nchi na watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanapokuja kuisema, kuiuliza Serikali wala hawakosei; kuiuliza Serikali juu ya usalama wa mtu au mali wala hawakosei. Serikali inapojibu kwamba tupewe muda tufanyie kazi na sisi hatukosei vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama Bunge lako litataka kulichukua jambo hili na kulichunguza hayo maelekezo ya kiusalama mtamwelekeza nani? Nenda kwenye katiba, yaani hayo maelekezo ya kiusalama yanayohusiana na ugaidi na mambo mbalimbali, *what will be the conclusion? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba, Bunge lako lichukue tahadhari. Nimeomba nitoe ushauri kwa Spika na nafanya kazi hiyo ya kutoa ushauri kwa Spika. Ninachotaka kusema ni kwamba, vyovyote itakavyoamuliwa, lakini mimi au sisi upande wa Serikali tunadhani Bunge lijipe muda wa kutafakari jambo hili. Maana sioni *conclusion* yake itakuwa kitu gani na hasa madai yanayodaiwa yana *scenarios* zinazotofautiana na kila mtu anasema lake. Mwingine anasema nilitekwa halafu anarudi mnakunywa nae chai; sasa ulikwenda kusalimia au ulikwenda kutekwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna mambo yana *scenarios* zinazotufautiana, hivyo, huwezi kuweka kwenye *package* moja ukasema Bunge lako lina uwezo wa kwenda kumaliza jambo hili lisipomalizika? Kwa hiyo, nakuomba kwa heshima ya Bunge lako Tukufu tuchukue tahadhari kama Bunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali hebu tupitie kwenye kanuni ya 120(1) halafu ujaribu kutuongoza kidogo pale, kwa ombi langu; kanuni ya 120(1) hebu isome pale na utupe inasemaje.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa nami nichangie hoja hii. Hoja inayozungumzwa hapa na hoja ambayo tumekuwa nayo hapa, yaani hoja inayozungumzwa hapa ilikuwa ni hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2017/2018. Kwa hiyo, hii haikuwa hoja; kama ingekuwa ni hoja hapa ambayo imewekwa mezani kwako... *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mzee tumeshatoka huko.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kama ingekuwa ni hiyo hoja ndiyo imewekwa hapo; kama ingekuwa ni hoja ambayo leo ipo mbele ya meza yako Tukufu basi baada ya kujadiliwa ndipo sasa Mbunge anaweza akaja na hoja hii, lakini hoja iliyo mbele ya kiti chako kitukufu ni hoja ya Serikali ya Makadirio na Mapato. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba ku...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kushauri nikiungana na waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwamba hili suala sio ambalo linaweza kuundiwa tume, haya ni mambo ya kisheria; na kwanza tukiyajadili hapa tu yanaua *process* zote za *investigation.* Nchi hii lazima ibaki na amani na

mshikamano, ina vyombo vilivyopo vinavyofanya kazi na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais hapa amezungumza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali...

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Eee amezungumza hapa kwamba kwa mfano mkiunda inaenda wapi?

**SPIKA:** Naomba jambo moja tu, wewe nenda kwenye kanuni ya 120(1) utuambie inasemaje. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kanuni ya 120 inasema hivi:-

*"Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalumu kwa hoja mahususi itakayotolewa na kuafikiwa."*

**SPIKA:** Na kuafikiwa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Na kuafikiwa, kwa hiyo tupige kura.

**SPIKA:** Ndiko nilikokuwa naelekea huko, kwamba kwa hiyo namba moja ili hoja mahususi iweze kupita si ni lazima iafikiwe? Nilitaka tuelewane hapo, hiyo kanuni ipo sawa au sio sawa hapo? Kanuni ya 120(1), ili aweze kuleta maelezo si inabidi hoja hiyo iafikiwe kwa 120(1)? Tupo pamoja? Haya mtoa hoja tuambie, Mheshimiwa Zitto.

**MHE. ZUBERI Z. R. KABWE:** Mheshimiwa Spika, Bunge hili linaendeshwa kwa Katiba, Sheria, Kanuni, desturi na maamuzi ya Mabunge ya nyuma. Tuna hoja binafsi mbalimbali ambazo zimejadiliwa ndani ya Bunge kwa utaratibu huu. Kulikuwa kuna hoja ya makadirio ya Wizara kwa mfano Ofisi

ya Waziri Mkuu; ndani ya hoja ile kulikuwa na mijadala mbalimbali, Mbunge akatoa taarifa kwamba ataleta hoja, ndipo anasimama kwa ajili ya hoja hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni zetu kuafikiwa ni pale Wabunge wenzake wanaposimama na kuweza kuafiki hoja ile na si kupiga kura ya wengi au hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe umekuwa Mbunge muda mrefu sana; nitakupa mfano wa hoja moja tu, hoja ya Buzwagi. Tulikuwa tunajadili makadirio ya mapato ya Wizara ya Nishati na Madini kukawa kuna hoja ya mikataba; mimi binafsi nikasimama na nikafanya kama hivi. Baadaye nikasimama kwa kanuni hii hii, Spika, Samwel Sitta; Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi; akaagiza hoja hiyo iende ikaandaliwe ili iweze kuja Bungeni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kiweke chombo vizuri kidogo, kikutazame hapo.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Sawa, nafasi ya Wabunge kupiga kura ni kwenye hoja yenyewe kwa sababu hoja italetwa; haina maana kwamba baada ya maelezo haya Kamati Teule inaundwa moja kwa moja, hapana. Hoja italetwa ndani ya Bunge, itajadiliwa na Wabunge kwa pamoja watakubali Kamati Teule iundwe au isiundwe. Kwa hiyo, sasa hivi tunawahisha shughuli za Bunge na kuwahisha shughuli za Bunge kumekatazwa na Kanuni za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeshatoa hoja naomba utupe nafasi tuilete hiyo hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mimi nilichotaka ili nifanye uamuzi ambao ni sahihi, nikataka mnisaidie ile kanuni 120(1), tupate tafsiri yake vizuri ili tuweze kwa sababu muda wetu hauko na sisi, inasema hivi; maana yake wewe uliposimama ulianza na ile (2) ukairuka (1) katika maelezo yako. Niseme katika utaratibu wako uko sahihi mpaka sasa hivi kwamba Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum na

wewe umeeleza madhumuni yako maalum, kwa hoja mahususi itakayotolewa na wewe umetoa hoja mahsusi; kuna neno na kuafikiwa.

Kwa hiyo, maana yake lazima mimi nijue kama mnaafikia au hamuafiki; hapo ndipo tulipo. Mheshimiwa Halima nakupa dakika mbili kwa sababu muda haupo na sisi. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, sheria haisomwi *in isolation;* sheria inasomwa kiujumla wake. Kitu kinachozungumzwa na Kanuni ya 120(1) uliyoisoma wewe kwamba:-

*"Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalumu kwa hoja mahsusi itakayotolewa na kuafikiwa."*

Hiyo hoja mahsusi inayozungumzwa hapa ni hoja ambayo Mheshimiwa Zitto Kabwe ataileta baada ya ku-*notify* kiti chako. Kwa hiyo, Zitto ataleta hoja yake, Bunge litajadili *then* Bunge ndilo litaamua kutokana na uzito wa hoja na mjadala wa hoja kama ipo haja ya kuundwa Kamati Teule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi sioni kuna hofu ya nini kutoka Serikalini wakati wametuambia hicho kikundi hakipo; na jukumu la Bunge ni kuisimamia Serikali Kikatiba. Serikali imetuambia hicho kikundi hakipo, sisi Bunge tunahisi kuna shida ya ulinzi na usalama; sheria na kanuni zinaturuhusu tuunde Kamati Teule pale ambapo italetwa hoja, atafanya uchambuzi wake, ataleta ushahidi wake *then* tutajua kweli hoja ya Zitto ina mashiko ama haina mashiko pale ndio tutaamua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Dakika mbili zimekwisha…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe…

**SPIKA:** Zimeshakwisha dakika mbili

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ndio nafanya *conclusion*. Nikuombe Mheshimiwa wangu ninayekuheshimu sana tukitendee haki kifungu cha 120 cha kanuni (1), (2), (3), (4) na kwenda mbele. Najua unafahamu kanuni vizuri sana, tunaomba ukitendee haki kile ambacho Mheshimiwa Zitto Kabwe amekieleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kama ninyi mnasema ile Kanuni ya 120(2) peke yake inajitegemea sasa kwa nini mmesimama hapa Bungeni? Mnachomwomba Spika ni kipi? Kwa sababu isome ile (2) utaona *role* ya Spika ni nini sasa pale. Kwa nini tunajadili jambo hili hapa? Utakuta kwamba haina chochote. Kwa hiyo, ile inatawaliwa na ile (1) baada ya kuwa imetekelezeka kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na wewe kwamba haiwezi kanuni hiyo ikajitosheleza kama pia hatutarudi kwenye utaratibu wa kufanya maamuzi ndani ya Bunge. Utaratibu wa kufanya maamuzi ndani ya Bunge unatawaliwa na kanuni ya 79(1); na kanuni hiyo inasema kwamba;

"Bila ya kuathiri masharti ya ibara za 46(a), 50(3), 53 na hizo nyingine za Katiba, mambo yote yanayohitaji kuamuliwa na Bunge yataamuliwa kwa kufuata maoni ya Wabunge walio wengi waliohudhuria na kupiga kura Bungeni." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uko sahihi kabisa; kwa hiyo kama hoja imetolewa ni lazima iamuliwe…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Na inapoamuliwa utaratibu wa kufanya maamuzi ndani ya Bunge upo pia kwa mujibu wa kanuni.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Sasa kwa sababu ya muda…

**MHE. ZUBERI Z. R. KABWE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu!

**SPIKA:** Naomba mkae, nimeshawapa demokrasia ya kutosha wote tumezungumza. Hakuna utaratibu katika Bunge hoja ikatolewa, ikaungwa mkono na imeungwa mkono kama ninyi mlivyofanya halafu isiamuliwe, haiwezekani. Kwa hiyo, lazima tuamue kama tunamuunga mkono mwenzetu aendelee sasa kuiandaa hoja kamili na kuileta au vinginevyo, ndio utaratibu wetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa nachukua nafasi hii kuwahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusu hoja ya Mheshimiwa Zitto ambayo mmeisikia wote.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuriwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja yako Mheshimiwa Zitto bado haijapita.

Tangazo, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wetu wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto anawatangazia Wabunge wote kuwa wataalam kutoka Wizarani kwake watakuwepo katika viwanja vya Bunge karibu na Ofisi ya Habari na Mawasiliano ya Bunge kwa ajili ya zoezi la kubadilisha kadi za chanjo *"yellow fever"* kwa kipindi cha wiki moja kuanzia tarehe 2 - 9 Mei, 2017. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa sana tarehe hizo mwende pale nyuma ya jengo la utawala lakini mwende na

kadi zenu za *yellow fever* kati ya tarehe 2 na 9. Na tangazo hili tutalirudia wakati wataalam hawa watakapokuwa wameshafika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo haya, naomba niahirishe sasa shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 13 saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 3.35 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 13, Aprili 2017, Saa Tatu Asubuhi)*